**7 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 7 Mei, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. TUNZA I. MALAPO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jonas Mbunda.

Na. 238

### Kukamilisha Ujenzi wa Maboma Shule za Msingi na Sekondari – Mbinga

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa maboma ya madarasa, nyumba za walimu na vyoo kwenye shule za msingi na sekondari Halmashauri ya Mbinga utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji Mbinga ina jumla ya maboma 88 yakijumuisha maboma ya madarasa 29 na matundu ya vyoo 59 kwa shule za msingi na sekondari ambapo

jumla ya shilingi milioni 329.8 zinahitajika ili kukamilisha maboma haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali ilitenga shilingi 180,000,000 kwa ajili ya kukamilisha maboma tisa ya madarasa na matundu 30 ya vyoo, ambapo hadi Machi, 2025 shilingi milioni 79.98 zimetolewa kukamilisha maboma sita ya madarasa na matundu 30 ya vyoo katika Shule za Msingi Chemka, Kipungu, Kindimba, Torongi na Kitunda shule Shikizi, Masasi, Lusewa Shule Shikizi, Lupilo, Rudisha, Mpepai, Kitete na Lazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetenga shilingi 120,000,000 kwa ajili ya kukamilisha maboma manne ya madarasa na matundu 41 ya vyoo katika Shule za Halmashauri ya Mji wa Mbinga. Aidha, Serikali itaendelea kukamilisha maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kwa awamu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili. Swali la kwanza; pamoja na utekelezaji na ukamilishaji wa maboma, maboma yaliyokamilishwa kwa sehemu kubwa ni yale ya shule za msingi. Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ya shule za sekondari?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ilikuwa na mpango wa kuendelea kujenga maabara kwenye shule mbalimbali za Sekondari za Kata. Ni lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga maabara hizo kwenye shule za sekondari? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ya madarasa katika shule za msingi na pia katika shule

za sekondari. Katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga Serikali imeshapeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, ni kweli fedha nyingi zimetengwa kukamilisha maboma ya shule za msingi kwa sababu yalikuwa mengi zaidi na uhitaji wa madarasa ulikuwa mkubwa zaidi. Hata hivyo, katika bajeti ya kila mwaka Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ya shule za msingi na sekondari. Vivyo hivyo katika Mwaka huu wa Fedha wa 2025/2026, Serikali imetenga bajeti hiyo. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunda kwamba maboma ya shule za sekondari katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga pia yamepangiwa fedha kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu ujenzi wa maabara, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya mapinduzi makubwa katika ujenzi wa maabara. Lengo likiwa ni kuhakikisha watoto wetu wanajifunza kwa vitendo masomo ya sayansi na maabara zimeendelea kujengwa. Katika Mwaka huu wa Fedha 2025/2026, ninamhakikishia Mbunge bajeti ya ujenzi wa maabara imetengwa na tutaendelea kujenga katika halmashauri hiyo na halmashauri zingine kote nchini. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri, Shule ya Sekondari ya Ikuti katika Wilaya ya Rungwe ina upungufu katika mabweni ya wanafunzi hasa vijana. Ni lini Serikali itaongeza nguvu ili kuweza kusaidia mabweni hayo kujengwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia, swali hapa lilikuwa ni ujenzi wa maboma. Mheshimiwa Waziri, jibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba tunahitaji kujenga

mabweni katika shule zetu ikiwemo Shule ya Ikuti na tunafahamu Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Shule ya Sekondari ya Ikuti imepangwa kujengewa mabweni. Serikali itahakikisha inapeleka fedha kwa ajili ya kujenga mabweni na kuboresha huduma za elimu kwa wanafunzi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Njau.

Na. 239

**Hitaji la Uzio - Kituo cha Afya Uru Kusini**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga uzio katika Kituo cha Afya cha Uru Kusini - Moshi Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imepeleka jumla ya shilingi milioni 750 katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha afya cha Uru Kusini ambapo majengo matano ujenzi umekamilika na kituo hicho kinatoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi itatenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa Kituo cha afya Uru Kusini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza. Lakini kabla ya hapo, naomba kutoa pole kwa Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Jimbo la Moshi Vijijini, Kata ya Mbokomu ambao wamepata maafa ya mvua na nyumba zaidi ya 100 haziwezi kukalika tena na vifo vya watu watatu na majeruhi wako katika Hospitali ya *KCMC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ameongelea Kituo cha Uru Kusini, lakini adha hii ipo katika Kituo cha Uru Kaskazini, Uru Mashariki na Okaoni. Ni lini Serikali itakwenda kujenga uzio katika vituo hivi ili kunusuru majengo yasiharibiwe na mvua hizi zinazonyesha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika Kituo hicho hicho cha Uru Kusini kuna shida ya watumishi: watumishi waliopo leo ni 16, lakini wanaohitajika ni watumishi 50, kwa hiyo, kuna shida sana ya watumishi. Ni lini Serikali itaongeza watumishi katika kituo hiki ili kupata ufanisi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na uzio katika vituo vya afya ili kuboresha usalama wa wagonjwa na watumishi, lakini pia mali za Serikali katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa utoaji huduma kwa wananchi, Serikali iliweka kipaumbele katika kukamilisha miundombinu ya vituo ili viweze kuanza kutoa huduma, kabla ya kuendelea na hatua ya ujenzi wa uzio. Kwa hiyo, ninafahamu kwamba tunahitaji uzio katika Kituo cha Afya cha Uru Mashariki, Kaskazini na hicho kingine ambacho amekitaja. Ninapenda kumhakikishia kwamba, Serikali itaendelea kupanga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kujenga uzio katika vituo hivyo na tutahakikisha tunakamilisha pia ujenzi wa miundombinu mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu watumishi, Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa miaka hii minne imeajiri watumishi wa sekta ya afya 34,720. Haijawahi kutokea katika historia ya nchi hii katika miaka minne kuajiri watumishi wengi kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi hawa wanaendelea kuongezeka sambamba na upanuzi wa miundombinu ya sekta ya afya, ikijumuisha ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, na hospitali za halmashauri. Ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutenga bajeti na kutoa vibali vya ajira na kutoa kipaumbele kwenye Kituo cha Afya cha Uru Kusini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, nani Mnzava? Shally? Mheshimiwa Shally.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa, Zahanati ya Rononi kule Uru Kaskazini ina hali mbaya sana na miundombinu aliyosema kwamba Serikali inakamilisha haijawahi kukamilisha kwani haina vyoo kabisa, wala samani za ndani, hakuna mabenchi ya wagonjwa kusubiri. Ni lini sasa Serikali itatoa kipaumbele kwa Zahanati hiyo ya Rononi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Serikali ilifanya mpango mkakati wa ukarabati na upanuzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri kongwe. Tayari tumeanza na hospitali za halmashauri, tutakwenda vituo vya afya kongwe na baadaye tutakwenda zahanati chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kwamba ni wajibu wake suala kama la mabenchi na viti vya ndani ya zahanati viko ndani ya uwezo wa mkurugenzi wa halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa maelekezo haya kwa Mkurugenzi, kwa haraka iwezekanavyo waende kwanza wakafanye tathmini ya uhitaji wa ukarabati wa zahanati hiyo na watenge fedha kupitia mapato ya ndani kwa sababu ipo ndani ya uwezo wao. Wanunue viti na mabenchi kwa ajili ya huduma za wagonjwa ili huduma katika zahanati hiyo ziweze kuboreshwa zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Innocent Kalogeris.

Na. 240

**Hitaji la Gari la Wagonjwa – Morogoro Kusini**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaipatia Gari la Wagonjwa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilinunua magari 594 ya kubebea wagonjwa na usimamizi wa huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ilipokea magari matatu ya kubebea wagonjwa na kupelekwa Vituo vya Afya Duthumi, Mkuyuni na Ngerengere.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa dharura zinazotokea katika Hospitali ya Wilaya ya Morogoro zinashughulikiwa na gari lililopo kwenye Kituo cha Afya cha Duthumi kilichopo takribani umbali wa kilometa 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutenga bajeti ya kununua magari ya wagonjwa kwa ajili ya hospitali za

halmashauri kote nchini ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Morogoro. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kalogeris.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Ni kweli Kituo cha Afya cha Duthumi ndiyo kina *ambulance* inayohudumia zaidi ya kata tano ambazo ni Kata ya Bwakira Juu, Kata ya Mngazi, Kata ya Singisa na kinahudumia pia kwenye vituo vya afya vya Kata ya Kisaki na Kata ya Kasanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kiuhalisia ni kwamba bado tunahitaji *ambulance* kwa ajili ya kusaidia kutoa *referrals* kwenye hospitali ya wilaya kupeleka kwenye hospitali ya mkoa. Kwa sababu hizo kilometa 20 wakati gari iko kwenye maeneo mengine ambayo ni zaidi ya kilometa 40 wagonjwa wanapata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; je, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ina upungufu wa wataalam wa usingizi. Tunaye mtaalam mmoja tu. Ni lini Serikali itatupatia mtaalam mwingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Kata ya Singisa tayari tumeshaandaa eneo kwa ajili ya kituo cha afya cha mkakati kile ambacho tumeahidiwa na wataalam wa afya wilaya wameshafika kukagua eneo. Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili hicho kituo cha afya kijengwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninawapongeza Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Serikali ilinunua magari ya wagonjwa na ilitoa maelekezo kwamba magari hayo yapelekwe kwenye vituo vyenye idadi kubwa zaidi ya wananchi ili huduma za rufaa ziwe na ufanisi mkubwa zaidi. Kwa hiyo, kupeleka katika Kituo cha Afya cha Duthumi ambacho

kinahudumia zaidi ya kata tano zinazokizunguka kituo cha afya ulikuwa ni uamuzi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inatambua kwamba tunahitaji gari lingine la wagonjwa kwa ajili ya hospitali ya halmashauri. Ninamhakikishia Mheshimiwa Kalogeris kwamba, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kunua gari hilo la wagonjwa ili hospitali ya wilaya pia ipate gari kwa ajili ya huduma za rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, tunafahamu Serikali imeweka mkakati wa kujenga vituo vya afya katika kata za kimkakati ikiwemo kata ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja na tayari wataalam wameshafanya tathmini ya ukubwa wa eneo. Ninapenda kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni suala la muda, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo kwa awamu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Hanang ina vituo vya afya nane na hospitali ya wilaya moja. Magari yako mawili kwenye hospitali ya wilaya. Je, ni upi mpango wa Serikali kupeleka gari kwenye vituo hivi vya afya kwa sababu umbali wa kijografia kutoka tarafa hadi tarafa ni mbali na hakuna tarafa yoyote yenye gari la kubebea wagonjwa. Ni upi mpango wa Serikali wa kuongeza gari katika wilaya hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Hanang ina magari mawili ya kubebea wagonjwa kwa maana ya *ambulance*. Pia tunao mpango wa kupeleka magari ya wagonjwa katika vituo vya afya vya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya

Hanang na vituo vyake vya afya ni moja ya vituo ambavyo vimewekwa kwenye mpango wa kupelekewa magari ya wagonjwa ili kuboresha huduma hizo za rufaa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace. Ajiandae Mheshimiwa Kigua.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa niulize swali la nyongeza. Kituo cha Afya cha Kiponzelo ambacho kipo Kata ya Maboga, Jimbo la Kalenga, kinahudumia zaidi ya vijiji saba na wananchi wanapata adha kubwa sana kwa sababu gari lake ni bovu kabisa. Ni lini Serikali itapeleka gari kwa ajili ya kuwahudumia wananchi hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na magari ya wagonjwa kwenye vituo vya afya na ndiyo maana katika mgao wa hivi karibuni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa na Jimbo la Kalenga pia lilipata magari ya wagonjwa na tunafahamu kwamba hayatoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge; kwanza, ninamwelekeza Mkurugenzi na Mganga Mkuu wa Halmashauri kuratibu ipasavyo magari haya ya wagonjwa ili Kituo cha Afya cha Kiponzelo nacho kipate huduma za rufaa pale inapohitajika tena kwa wakati. Pili, napenda kumhakikishia kwamba, Serikali iko kwenye mpango wa kutenga fedha wa ajili ya kununua magari wenye vituo vya afya vya kimkakati vyenye uhitaji mkubwa na Kituo cha Afya cha Kiponzelo pia tutakipa kipaumbele. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kutuingizia shilingi milioni 250 kwenye Kituo cha Afya cha Negero. Nataka kujua ni lini Serikali itatupa gari kwenye Hospitali ya Wilaya ya Kilindi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Hospitali ya Wilaya ya Kilindi ni moja ya hospitali ambazo zinahitaji gari la wagonjwa na Mheshimiwa Omari Kigua amekuwa mara kwa mara akiwasemea wananchi wa Jimbo lake la Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itakaponunua magari ya wagonjwa katika awamu inayofuata, tutahakikisha pia Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi inapelekewa gari hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Aysharose Mattembe, kwa niaba yake Mheshimiwa Flatei.

Na. 241

**Hitaji la Gari la Wagonjwa Kituo cha Afya**
**Mgori - Singida Kaskazini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY K.n.y. MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Gari la Wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Mgori Jimbo la Singida Kaskazini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022, ilinunua magari 594 ya kubebea wagonjwa na usimamizi wa huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Halmashauri ya Wilaya ya Singida imepokea magari mawili ya kubebea wagonjwa na kupelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Singida na Kituo cha Afya cha Mgori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kubebea wagonjwa na kuyapeleka katika halmashauri kote nchini kwa ajili ya kutoa huduma kwenye hospitali na vituo vya afya. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; je, pamoja na magari haya mawili uliyoyasema, Serikali ina mpango gani wa kuongeza gari moja katika ile Wilaya ya Singida kama swali la Mheshimiwa Mbunge linavyosema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Jimbo la Mbulu Vijijini ni kubwa na lina maeneo mengi ambayo hata Wahadzabe hawafikiki kwa magari. Je, ni lini watapeleka gari la wagonjwa katika maeneo haya niliyoyasema? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hoja ya Mheshimiwa Mbunge ilikuwa ni gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Mgori na tayari Serikali imeshapeleka gari hilo katika hicho kituo cha afya cha Mgori, nimhakikishie tu kwamba, tunafahamu bado kuna uhitaji wa magari ya wagonjwa na Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kupeleka hayo magari katika vituo ambavyo vina uhitaji mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na kata na vituo vingine, Serikali imeweka mpango madhubuti wa kufanya

kwanza tathmini ya mahitaji na umbali kutoka kituo kimoja kwenda kingine, ili kuhakikisha wakati tunanunua magari ya wagonjwa tunatoa kipaumbele zaidi kwenye kata au vituo vya afya vyenye idadi kubwa zaidi ya wananchi ambavyo vina umbali mkubwa zaidi kutoka hospitali ya halmashauri. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali itafanyia kazi hoja hizo zote mbili. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tuna Kituo cha Afya cha Mtisi ambacho kiko mbali zaidi ya kilometa 20. Ni lini Serikali itapeleka gari la wagonjwa ili kuwasaidia wananchi wa Kata ya Mtamaa? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Mtisi ambacho kiko umbali wa zaidi ya kilometa 20, tutakwenda kufanya tathmini pia kuona idadi ya wananchi wanaotibiwa katika eneo hilo. Pia, tutaenda kuhakikisha kwamba tunatenga bajeti kwa ajili ya kununua magari ya wagonjwa kwa ajili ya kupeleka katika vituo vyote vya afya ambavyo vina uhitaji mkubwa kikiwemo kituo hiki ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Farkwa ni kipya, tunaishukuru Serikali kwa kutusogezea hiyo huduma kwa wananchi wetu lakini hatuna gari la wagonjwa. Nini mkakati wa Serikali kupeleka gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Farkwa? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri tumefanya ziara na Mheshimiwa Mbunge wa

Viti Maalum na Mbunge wa Jimbo pale Farkwa mwezi mmoja uliopita. Tuliona kweli inahudumia wananchi walio wengi, lakini pia kuna uhitaji wa gari la wagonjwa. Ninaomba nimhakikishie Mbunge kwamba tumeshakiweka Kituo cha Afya cha Farkwa kwenye mpango wa magari yatakayofuata awamu hii kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanapata gari la wagonjwa ili kuboresha huduma za dharura na huduma za rufaa.  Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Litumbandyosi, Kituo cha Afya Matiri na Kituo cha Afya cha Mkumbi pamoja na Hospitali ya Halmashauri hawana gari la wagonjwa. Ni lini sasa tutapeleka gari la wagonjwa katika maeneo hayo? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Kapinga amefuatilia mara kadhaa na tayari kwenye mpango wa magari ya wagonjwa unaofuata kupitia Wizara ya Afya, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambalo ni Jimbo la Mbinga Vijijini tayari limeshawekewa gari moja kwa ajili ya Hospitali ya Halmashauri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, jiandae Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Vunjo lenye wakazi 260,000 lina gari moja tu la kubeba wagonjwa. Je, ni lini watatupatia magari kwenye vituo vya *Magarubu Headquarters*, Kirua Vunjo Magharibi na Kahe Magharibi?  Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Jimbo la Vunjo lina gari moja la wagonjwa

na kwa kweli katika eneo ambalo tumelipa kipaumbele cha hali ya juu katika majimbo ni Jimbo la Vunjo. Nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kimei kwamba, kwenye mgao unaofuata wa magari ya wagonjwa kupitia Wizara ya Afya tayari tumesha-*allocate* gari moja la wagonjwa kwa ajili ya Jimbo la Vunjo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilituahidi gari la wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto. Je, ni lini gari hilo litapelekwa? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kutenga fedha katika kila bajeti ya mwaka kwa ajili ya kupeleka magari ya wagonjwa kwenye hospitali za halmashauri na vituo vya afya vyenye uhitaji mkubwa wa magari ya wagonjwa. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Shekilindi kwamba, Hospitali ya Halmashauri ya Lushoto ni moja ya Hospitali ambazo zitaingizwa kwenye mpango na fedha itatafutwa kwa ajili ya kupeleka gari la wagonjwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Stephen Byabato.

Na. 242

**Watumishi Wanaojitolea Kupangiwa katika Vituo vya Kujitolea**

**MHE. STEPHEN L. BYABATO** aliuliza:-

Je, kwa nini watumishi wanaojitolea wanapoajiriwa wasipangiwe katika Vituo walivyokuwa wakijitolea kama kipaumbele cha kwanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu ya Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo Na.2 la Mwaka 2008, ikisomwa pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298, Ajira katika Utumishi wa Umma hupatikana kwa ushindani na uwazi. Kujitolea katika Utumishi wa Umma huwezesha vijana kujipatia ujuzi wa ziada pamoja na kuwapa uzoefu na uwezo wa kushindana pindi ajira zinapotangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo wanaojitolea wanafaulu usaili, majina yao hupelekwa kwa waajiri ambao huwapangia vituo vya kazi kulingana na mahitaji ya ikama iliyoidhinishwa katika vituo husika. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Byabato.

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina swali moja la nyongeza. Kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza mishahara ya watumishi na kuwafanya wawe na morali na hamu ya kuendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Wabunge wenzangu wameuliza kwenye maswali mengi ya TAMISEMI, ninapenda kufahamu ni upi hasa mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inapunguza ma-*gap* ya ajira ambayo yapo kwenye ikama za Utumishi wa Umma dhidi ya ile ambayo inapatikana kwa sasa. Ni upi mkakati wa Serikali ambao utaondoa kabisa tatizo hili la upungufu wa Watumishi wa Umma? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Byabato kwa kazi nzuri

anazozifanya za uwakilishi wa wananchi wake wa Jimbo la Bukoba Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali lake la jumla; jitihada za Serikali katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ajira mpya zilizokuwa zimejazwa ni takribani ajira 149,000, lakini ajira mbadala ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alizitolea kibali ni 39,963. Pia, hivi juzi katika jitihada ileile, Mheshimiwa Rais ametoa kibali cha ajira nyingine ambazo zinatakiwa zijazwe kabla ya kwisha kwa mwaka huu wa fedha, ajira 33,212. Hii yote ni jitihada na hata hivyo katika bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tayari kuna ikama imetengwa kwa ajili ya ajira mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali ina mpango wa dhati na tutaendelea kujaza mapungufu ya ukosefu wa watumishi kadri ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kutupatia kicheko, furaha na amani watumishi wa Tanzania. Swali langu la nyongeza na nilishauliza mara nyingine hapa; ni lini sasa Serikali itaweka rasmi kigezo cha kujitolea kama sifa ya mtumishi kuajiriwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee tena kumpongeza Mheshimiwa Kamishna Janejelly kwa namna anavyofuatilia masuala ya watumishi. Kama nilivyokwisha kujibu hapa Bungeni ni kwamba tayari tumeandaa mwongozo wa wale wanaojitolea ambao tunaanza kuutumia rasmi tarehe Mosi Julai, mwaka huu. Ndani ya mwongozo huo tumeelekeza namna ambavyo kwanza wanaojitolea watapewa fedha ya kujikimu na namna ambavyo tutaweza kuwapa kipaumbele pale ajira zinavyotangazwa. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwa kuwa tatizo la ukosefu wa walimu wa sayansi nchini limekuwa kubwa sana. Je, ni kwa nini Serikali isione utaratibu wa mfumo rasmi au mfumo maalum wa kuajiri walimu wa sayansi katika shule zetu ili kuondoa tatizo hilo? Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwamba Mheshimiwa Rais ametoa kibali cha ajira 33,212 ambazo zinatakiwa kujazwa kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa fedha. Kati ya hizo ajira, zipo ajira 9,000 ambazo zinaenda kwenye kada ya walimu na wengi waliopo asilimia kubwa ni walimu wa masomo ya sayansi. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika ajira hizi vijana wengi wataarijiwa wa masomo ya sayansi ili kuziba *gap* hilo la upungufu wa walimu wa sayansi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Iringa tulipewa kibali cha kuajiri watendaji 23, lakini baadaye tukaambiwa tusubiri barua ya Katibu Mkuu. Sasa ninaomba kujua ni lini barua hiyo itatoka na wewe kama Naibu Waziri utusaidie ili wale watoto waajiriwe? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nikijibu swali la Mheshimiwa Jesca nitaomba baada ya kumaliza kipindi cha maswali na majibu tukae tufuatilie jambo hilo ili tuone. Ni kweli tulisitisha kupisha zoezi la kuajiri walimu na baadaye sasa tumeendelea na taratibu za kuendelea na ajira nyingine. Kwa hiyo tutakutana pamoja tuone limeishia wapi, kama ni jambo

ambalo limekwama, basi tutamaliza ili muweze kuendelea na utaratibu huo. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Kuchauka.

Na. 243

**Majiko Yanayotumia Gesi Kutumika Shule za Sekondari**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Je, lini majiko yanayotumia gesi yataanza kutumika katika Shule za Sekondari kote Nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2025, Serikali kupitia wadau mbalimbali imewezesha jumla ya shule za sekondari 216 kuhamia katika matumizi ya nishatisafi ya kupikia ambapo kati ya hizo, shule za sekondari 146 zinatumia Gesi ya *LPG*. Aidha, Serikali kupitia *REA* inaendelea kutoa ruzuku ya ujenzi wa miundombinu ya nishati safi ya kupikia kwa shule nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 20 Aprili, 2025, *REA* kupitia Wizara ya Nishati imepokea kibali kutoka TAMISEMI cha kufunga miundombinu ya huduma ya nishati safi ya kupikia katika shule 115 zikiwemo: shule za mikoa za sayansi za wasichana 16; shule za kitaifa za wavulana 7; shule za bweni za kawaida 66; na shule kongwe za sekondari 26. Serikali kupitia *REA* na wadau mbalimbali itaendelea kufunga miundombinu ya nishati ya kupikia katika shule za sekondari kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri na ninaipongeza Serikali kwa kuliona hili. Kutokana na juhudi za kumuunga mkono Mheshimiwa

Rais kuhusiana na nishati safi ya kupikia, Serikali haioni haja ya kupanua wigo kupitia *REA* kutoa majiko haya na kujenga hii miundombinu ya gesi kwenye hospitali, vituo vya afya na magereza kama ilivyofanya katika sekondari na shule za msingi kwa sababu changamoto kubwa kwenye shule za msingi kwa utoaji wa chakula shuleni ni hii miundombinu ya kupikia (mkaa au kuni bei iko juu sana). Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuongea na *REA*, kwamba badala ya kutoa hii mitungi ya gesi kwa wajasiriamali ielekeze kwenye hizi taasisi za Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari inatekeleza mkakati huo. Kama mtakumbuka Mheshimiwa Rais aliagiza taasisi ambazo zinalisha watu zaidi ya 100 ziwezekufungwa mifumo ya nishati safi ya kupikia. Pia tayari Wizara ya Nishati kupitia *REA* tumeanza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi wa kufunga mifumo ya nishati safi ya kupikia kwenye Jeshi la Polisi na Magereza, takribani mikoa 24; Jeshi la Zimamoto pamoja na huduma za Wakimbizi. Hapa tunapoongea tuna mkakati na mradi tayari unaendelea wa kufunga nishati safi ya kupikia katika taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Afya; Hospitali za Mikoa, Rufaa na Kitaifa takribani 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taasisi za Maendeleo ya Jamii vilevile tunafunga mifumo kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Jamii takribani 13. Kwa hiyo, Serikali inatekeleza mkakati huo kuhakikisha kwamba, zile taasisi ambazo zinahudumia kuanzia watu 200 – 100 na zenye watu wengi basi zinafungiwa hiyo mifumo. Tayari tumeshaona matokeo katika baadhi ya magereza, kwa mfano, wameshapunguza gharama ya uendeshaji takribani nusu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mkakati unaendelea na tutaendelea kufanya hivyo hivyo kwa taasisi nyingi zaidi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujua mkakati wa Serikali, kuna mkakati gani wa kuhakikisha

taasisi zote mpya ikiwemo shule, zahanati na vituo vipya vya afya ambavyo vinajengwa wanafunga kabisa mfumo wa gesi badala ya kwenda kuhama baadaye kwa sababu ni gharama? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mkakati wetu wa nishati safi ya kupikia ambao sasa tumeshaanza utekelezaji wake, kwa kweli huo ndio mtazamo ambao hata sisi wenyewe tunautazamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali tumejipanga kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, wenzetu wa Mazingira na taasisi zote ambazo kwa pamoja tunashirikiana katika kutekeleza mkakati huu kuhakikisha yale maeneo ambayo tayari yalishatolewa mwongozo yanayotoa huduma za kijamii na yanayotumia nishati nyingi sana katika kupikia yanafungwa mifumo hii ya nishati safi ya kupikia. Kwa hiyo, tunao mkakati na unatekelezeka vilevile. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Afya, Mheshimiwa Jesca. Mheshimiwa Jesca, mama upo Jimboni? *(Kicheko)*

Na. 244

**Afya ya Akili Kujumuishwa kwenye Bima ya Afya**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, lini *NHIF* itajumuisha huduma za afya ya akili kwenye vifurushi vya bima ya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za matibabu ya afya ya akili, ushauri nasaha na huduma nyingine za kibingwa ikiwemo

huduma za utengamao ni baadhi ya huduma zilizoorodheshwa kama huduma muhimu za afya kwenye mwongozo wa matibabu *(Standard Treatment Guideline)* ambapo hutumika kama kigezo kikuu cha huduma za msingi zinazolipiwa na Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utoaji wa huduma za matibabu kwa wagonjwa wa akili, Mfuko wa Bima *(NHIF)* hugharamia dawa zote kwa kuzingatia aina ya dawa na ngazi ya huduma kwa mujibu wa Mwongozo wa Matibabu *(STG)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, lakini nina maswali mawili ya nyongeza baada ya majibu hayo. Swali la kwanza; Mheshimiwa Naibu Waziri aliahidi hapa kwamba mwezi huu Mei, Baraza la Afya ya Akili litakuwa limeanzishwa nchini. Je, limeshaanzishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri ni daktari, anadhani ni sawa watu wanaotaka kujinyonga kufungwa au kupelekwa hospitali? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze dada yangu ambaye ni mtu wetu mzuri sana katika kupigania matatizo ya afya ya akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama ambavyo amesema kwenye swali lake la kwanza, tulikubaliana hapa Bungeni kwani aliuliza swali na tukakubaliana kufika wakati huu tutajitahidi ili kuweza kuanzisha hili baraza na kwa kweli mchakato bado unaendelea. Tumwombe tu atupe muda, kwa sababu kuna mambo ya muhimu ya kuzingatia kabla ya kuanzisha hilo ili kuweza pia kuyatafakari kwa kina yaliyojitokeza kwenye swali lake la pili, ili wakati tunaenda kuanzisha basi tuwe na miongozo mizuri ambayo itaweza kutufikisha tunapotaka kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kusema ukweli wakati mwingine ni kazi kubwa sana ya kitaalam inahitajika kuweza kujua anayefanya hili ni amefanya kwa makusudi au amefanya kwa sababu ana matatizo ya akili na inahitajika kufanya uchunguzi wa kisayansi ili kuweza kuthibitisha na kuamua sasa mwelekeo ni upi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana ukienda Mirembe utakuta kabisa kuna hawa waliofanya matendo kama hayo kweli ni wafungwa, lakini wako Mirembe wakiendelea kutibiwa na wakihudumiwa na Serikali moja kwa moja wala bila kuhusisha familia zao. Kwa hiyo ninachoweza kukisema, hebu iachie vyombo (vyombo vya ulinzi na wataalamu wa tiba) waweze kuamua hayo yote na sisi tuamini kabisa wanapoamua wanaamua kwa usahihi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Thea.

Na. 245

**Vyuo Vikuu Vyenye Programu ya Afya Kurudishiwa Hospitali Zao za Mafunzo**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa kuzirudishia Hospitali za Mafunzo Vyuo Vikuu vyenye Programu ya Afya kama *UDOM* na *MUHAS* ili kukidhi miongozo ya Kimataifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliipa Wizara ya Afya jukumu la kusimamia Hospitali ya Mloganzila na Benjamin Mkapa ambazo zilikuwa Hospitali za Vyuo Vikuu vya *MUHAS* na *UDOM,* kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi sambamba na kuboresha ubora wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Vyuo Vikuu vya Dodoma na Muhimbili vinaendelea kutumia Hospitali hizi kufundishia wanafunzi wao. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja zito la nyongeza. Kwa sababu amesema kwamba, hizo Hospitali zilikuwa ni Hospitali za Vyuo Vikuu; je, baada ya ripoti ambayo iliongozwa na Profesa Pallangyo, kupelekwa pale kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Serikali haioni haja sasa ya kuifanyia kazi ile ripoti ili kurudisha hizo hospitali zishikiliwe na vyuo kwa 80%? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala ya taaluma na tiba, ninamhakikishia kwamba swali hilo siyo zito kwa sababu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja, Wizara ya Afya ni sehemu ya Serikali pia Wizara ya Elimu ni sehemu ya Serikali, kwa hiyo Serikali inashirikiana na inafanya kazi kama Serikali moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kitu kimoja kwamba leo kwa maana ya *MUHAS* pale Mloganzila wanajenga mabweni, lakini pia wanajenga nyumba za walimu wakishirikiana na Mloganzila kwa maana ya kwamba walimu watakuwa pale na wakati huo huo wanafunzi wanakuwa pale kwa ajili ya kutumia hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusisahau kwamba Wizara ya Afya ina kazi ya kusimamia tiba, lakini Wizara ya Elimu ina kazi ya kusimamia taaluma. Ukianza kuwafanya hawa Maprofesa wakati wanatakiwa kufundisha aanze kuwaza bei za dawa na kuhakikisha anatengeneza faida wakati huo huo aanze kufikiria namna ya kutengeneza kichwa kizuri cha kuweza kusimamia dawa. Ku-*calculate* masuala ya dawa unaweza ukachanganya hiyo habari na ukaleta shida ambayo utapunguza ubora kwenye upande wa tiba, wakati huo huo utapunguza ubora kwa upande

wa taaluma. Kwa hiyo, tunafikiri kila mahali ambapo imetengenezwa elimu wasimamie elimu lakini pia tiba wasimamie tiba na kwa kushirikiana kama Serikali moja tutaleta ubora mzuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato.

Na. 246

**Fursa kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu kufanya Mazoezi kwa Vitendo**

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Taasisi na Mashirika yanatoa fursa kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu kufanya mazoezi kwa vitendo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKINOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha wanafunzi wanapata fursa za kufanya mafunzo kwa vitendo, vyuo vikuu nchini vimekuwa na utaratibu wa kuanzisha ushirikiano na taasisi na mashirika ambayo yanatoa huduma zinazoshabihiana na fani zinazotolewa vyuoni. Hadi sasa taasisi 19 za elimu ya juu zimeanzisha Kamati za Ushauri wa Kitasnia *(Industrial Advisory Commitee)* kama mkakati wa kuongeza nafasi na kuimarisha mafunzo kwa vitendo ambapo jumla ya mikataba 158 imesainiwa kati ya vyuo na taasisi binafsi na viwanda. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Paulina.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kuhusu swali langu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; wanafunzi wanapokwenda kufanya mafunzo kwa vitendo muda unakuwa mfupi kutokana na kukosekana kwa

fedha. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha taasisi zinapata fedha ya kutosha ili muda wa mafunzo kwa vitendo usipungue?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mara nyingi wanafunzi wanapopangwa katika mashirika au taasisi kufanya mafunzo kwa vitendo wanapokuwa kwenye zile taasisi hawapangiwi zile sehemu ambazo ndizo fani zao bali huwepo pale na kupangiwa mambo mengine ambayo hayaendani na fani zao. Je, Serikali inatoa kauli gani katika suala hilo? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Nahato, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na jambo la kwanza kuhusu suala la muda, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba taratibu hizi za kwenda kwenye mafunzo kwa vitendo kwenye vyuo vyetu vikuu kila fani inapangiwa muda wake maalum. Kuna maeneo ambayo wanakwenda mwezi mmoja, kuna maeneo ambayo wanakwenda kwa miezi miwili na wengine wanakwenda kwa miezi mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la muda kuwa mfupi tunaomba tulichukue twende tukalifanyie tathmini ya kina jambo hili ili kuweza kuangalia kwenye mitaala yetu ile, muda ule uliotolewa kwa mujibu wa mitaala kama unatosheleza au la, lakini kimsingi kila fani imepangiwa muda wake na tutakwenda kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili kuhusiana na maeneo ambayo wanafunzi wanakwenda na labda wanapangiwa maeneo mengine tofauti, ninaomba tulichukue nalo jambo hili twende tukalifanyie kazi. Ninachofahamu ni kwamba wanafunzi hawa wanapokwenda maeneo haya ya mafunzo kwa vitendo mara nyingi kunakuwa na *supervisors* ambao wanakwenda kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji vilevile kwenda kufanya upimaji wa kile ambacho wamekwenda

kujifunza katika eneo hilo. Tunashirikiana sasa na hawa *supervisors* na Wakuu wa Taasisi ili kuhakikisha wanafunzi hawa wanapokwenda wanakwenda kwenye yale maeneo ambayo tunayahitaji kwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hiyo nadhani Mheshimiwa Dkt. Nahato unafahamu Serikali yetu ya Awamu ya Sita tumefanya maboresho ya mitaala vilevile tumefanya maboresho ya sera yetu ambayo kwa sasa tunakwenda kuanzisha ule mkondo wa amali, kuanzia katika elimu ya kidato cha kwanza mpaka vyuo vikuu tunaamini kabisa katika elimu hii ya amali itakwenda kuhakikisha kwamba vijana wetu wanakwenda kuwa *hands-on* katika muda wote kuanzia darasani mpaka kule maeneo ya viwanda wanapokwenda. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwinyikondo Rajab.

Na. 247

**Idara ya Uhamiaji Kujenga Hospitali Zanzibar**

**MHE. MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB** aliuliza:-

Je, Idara ya Uhamiaji ina mpango gani wa kujenga hospitali Zanzibar kama ilivyo kwa Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama, Idara ya Uhamiaji ina mpango wa kuwa na zahanati kwa lengo la kutoa huduma za afya kwa watumishi na jamii inayoizunguka. Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji imefanya mawasiliano ya awali na Wizara ya Afya ya Zanzibar ili kupata mwongozo kuhusu namna bora ya uanzishwaji wa zahanati itakayokidhi mahitaji kwa jamii itakayohudumiwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rajab.

**MHE. MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina masuali mawili ya nyongeza. Kwanza ninaipongeza Idara yetu ya Uhamiaji kwa kuwa na majengo mazuri na ya kisasa kwa upande wa Zanzibar. Swali langu la kwanza; ni lini sasa mpango huu utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa tunaanzisha zahanati naamini kwamba kutahitajika wataalam wa kada za afya. Je, Idara ya Uhamiaji ina mpango gani kuwapata wataalam hawa kwa kipindi hiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mustafa Mwinyikondo Rajab, Mheshimiwa Mbunge wa Diwani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi ni kwamba, mara baada ya kupokea mwongozo kutoka Wizara ya Afya Zanzibar ndipo tutakapoanza ujenzi mara moja wa zahanati hii ya kuhudumia Askari pamoja na wananchi wanayoizunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu wataalam, wataalam wapo, lakini Idara pia itaendelea kuajiri hatua kwa hatua kuhakikisha kwamba inakidhi mahitaji ya kutoa huduma katika zahanati ambayo itajengwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Advocate*.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Serikali 2024/2025, iliweka pesa kwa ajili ya vituo vya Polisi vilivyoanzishwa na wananchi vya Magungu – Lengatei – Matui na Chekanao. Je, ni lini pesa hizi zitakwenda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mbunge wa Kiteto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Mwaka huu wa Fedha 2024/2025, vimetengwa vituo vya Polisi kwa Jimbo la Kiteto kama alivyovitaja karibu vituo vinne na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba bado mwaka wa fedha haujakwisha, Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Polisi kama alivyosema. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

Na. 248

**Ujenzi wa Kituo kipya cha Polisi Wilaya ya Micheweni**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kituo kipya cha Polisi cha Wilaya ya Micheweni?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itajenga Kituo Kipya cha Polisi cha Daraja "B" katika Wilaya ya Micheweni, ambacho kitagharimu kiasi cha fedha shilingi 802,926,788, kwa kuwa kituo kilichopo sasa ni chakavu na hakiwezi kufanyiwa ukarabati. Mpango wa ujenzi wa kituo kipya unaanza kwenye mwaka wa fedha 2024/2025 kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kombo.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, uhai wa Bunge la 12 unaenda kwisha sambamba na mwaka wa fedha husika, mpaka sasa katika kituo chetu hakuna mkandarasi wala

hakuna shughuli yoyote inayoendelea tunaomba *commitment* ya Serikali ni lini kituo hiki kinaanza kujengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kipenzi cha Wazanzibari Mheshimiwa Rais Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amepeleka miradi ya kutosha katika Wilaya yetu ya Micheweni. Je, Serikali hamwoni ni muhimu kupeleka nguvu ya ziada katika ujenzi wa mradi huu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Issa Kombo Mheshimiwa Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi *commitment* ya Serikali ni kwamba katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, tunaanza kujenga ujenzi huu. Kwanza tulitenga fedha kwa ajili ya kukarabati jengo lililopo, lakini baada ya kufanya tathmini tukaona jengo limechakaa kabisa halifai kukarabatiwa, ndiyo maana sasa tumeongeza fedha kwa ajili ya kuanza kujenga Kituo Kipya cha Polisi cha Wilaya ya Micheweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba kule Zanzibar kazi kubwa imefanyika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nguvu hiyo hiyo iliyotumika kukamilisha miradi mingine pia itatumika kuhakikisha kwamba Kituo cha Polisi Wilaya ya Micheweni pia inakamilika kwa wakati. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitenga bajeti ya shilingi milioni 115 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kipatimo mwaka huu wa fedha. Je, ni lini fedha hizo zitafika kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Ndulane, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwenye mwaka wa fedha 2024/2025, tulitenga fedha milioni 115 kwa ajili ya Kituo cha Polisi cha Kipatimo ambacho kipo kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Mwaka wa fedha unaendelea na Serikali ipo kazini, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge fedha zitaenda kama zilivyoenda hizi zingine kwa ajili ya kumalizia Kituo cha Polisi alichokitaja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilituahidi kujenga Kituo cha Polisi Kata ya Rundugai kwa sababu wananchi wanatembea umbali mrefu sana kufata huduma Kituo cha Polisi Bomang'ombe ni lini ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Rundugai utaanza? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu la nyongeza ya Mheshimiwa Mafuwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumepanga kujenga ujenzi na Vituo vya Polisi vya Kata na Sheia kwa upande wa Zanzibar awamu kwa awamu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nia ya Serikali ni kuhakikisha kila Kata ya nchi hii inapata Kituo cha Polisi kama ambavyo tayari tumeshapeleka askari katika maeneo hayo. Mheshimiwa Mbunge Serikali itatenga fedha na kujenga kituo cha polisi ulichokijenga kwenye Wilaya ya Hai. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kukikarabati Kituo cha Polisi cha

Maturubai ambacho kinahudumia wakazi wengi wa Jimbo la Mbagala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Chaurembo Mheshimiwa Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya Polisi vya Kata pamoja na Wilaya kama ambavyo ameuliza Mheshimiwa Mbunge. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kituo chake alichokisema cha maturubai tutakichukua tutakiweka kwenye mpango na kukitengea fedha kwa ajili ya kukifanyia ukarabati ili aweze kutoa huduma kwa wananchi wa Mbagala. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Hokororo.

Na. 249

**Ujenzi wa Reli ya Kusini**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza:-

Je, lini ahadi ya ujenzi wa Reli ya Kusini itaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Reli *(TRC)* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa Njia ya Reli ya Mtwara - Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma yenye urefu wa kilomita 1,000. Kwa sasa, Serikali inaendelea na taratibu za kutafuta mwekezaji atakayejenga reli hiyo kwa kiwango cha *Standard Gauge (SGR)* kwa utaratibu wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi *(PPP)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, kuwa na subira wakati Serikali ikiendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi wa reli hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili. Swali la kwanza; je, Serikali inatambua hasa umuhimu na uwezo wa reli ya Kusini katika uchumi wa nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa, katika majibu ya msingi amesema itajengwa kwa utaratibu wa *PPP,* utaratibu huu unapohusisha uwekezaji wa ujenzi wa reli na uendeshaji ninaamini itachukua muda mrefu. Hapa ninaomba nitoe ushauri, ninaishauri Serikali yangu sikivu ifikirie upya badala ya kusubiri ubia ione namna ambavyo itajenga reli ya kusini yenyewe, halafu mwekezaji aje kufanya uendeshaji. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Umeuliza swali la kwanza na pili ni ushauri. Mheshimiwa jibu swali la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge umepokelewa kwa sababu ni jukumu la Bunge kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza ni kwamba, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa reli ya Kusini, hii inatokana na ukweli kwamba upande wa Kusini kwa maana kutoka *Mbamba Bay* mpaka Mtwara na matawi yake kuna fursa kubwa ikiwemo uwepo wa makaa ya mawe zaidi ya tani milioni 426, kuwepo kwa ikiwemo *vanadium, titanium, lithium* pamoja na kwenye eneo la Dangote zaidi ya tani milioni 232 za simenti. Pia umuhimu wa reli hiyo ndiyo unakwenda kuongeza matumizi makubwa ya Bandari yetu ya Mtwara ambayo Serikali imeweka pesa za kutosha pamoja na *Mbamba Bay*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba tukifanikiwa kuanzisha reli hiyo itaweza kusaidia madini ambayo nimeyataja

na hivyo Serikali kupunguza kuagiza madini kutoka nje na chuma kutoka nje. Pamoja na umuhimu huo napenda nimhakikishie Mheshimiwa muuliza swali Mheshimiwa Hokororo kwamba Serikali imeshafanya mambo mengi sana ili kutambua na kuthamini umuhimu wa reli hiyo. Kwanza tumeshaanza maboresho mbalimbali ya bandari tatu, moja hivi ninavyozungumza ujenzi wa Bandari ya Mbamba *Bay* umekwishaanza na zaidi ya bilioni 80 Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amezielekeza pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tumefanya maboresho makubwa Bandari ya Mtwara kwa kuweka zaidi ya bilioni 157. Tatu, kwa sababu tunajua sehemu kubwa ya malighafi zitakazotoka pande wa Liganga na Mchuchuma itakuwa ni pamoja na bidhaa chafu au makaa ya mawe tunajenga bandari mpya ya Kisiwamgao ambapo zaidi ya bilioni 835 zimeelekezwa kwenye bandari mpya kabisa hii yote inadhihirisha na kuthibitisha namna ambavyo Serikali hii ya awamu ya sita inatambua umuhimu wa bandari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishalipa fidia pia kwa zaidi ya wananchi 1000 waliopo kwenye eneo la Liganga na Mchuchuma ili kupisha maeneo yale yote hiyo inaonyesha ni kwa namna gani Serikali inatambua jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaanza kufanya jambo la kwanza tunakuja la pili. Tumeshaanza kujenga reli ya kati kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza mpaka Kigoma na mpaka nje ya nchi ambayo inagharimu zaidi ya dola bilioni 12, zaidi ya takribani trilioni 30 hii inamaanisha nini? Inamaanisha utayari wa Serikali sasa ya Awamu ya Sita kuamua kuwekeza kwenye upande wa reli *especially SGR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoanza maboresho makubwa kwenye reli yetu ya Kusini kwa maana ya *TAZARA* yote hiyo inaonyesha kwamba nchi yetu imeamua kufanya uchumi wake kuwa uchumi na uchukuzi, kwa hiyo nimtoe mashaka nimuombe aendelee kuwa na subira wakati Serikali inakamilisha mambo ambayo imeshaanza kuyafanya na siyo muda mrefu neema ipo mlangoni, watu wa kusini wajiandae Serikali itaanza kujenga reli hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgaya.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru...

*(Mhe. Mwita M. Waitara hakusikia vema jina la Mbunge aliyeitwa kuuliza swali la nyongeza)*

**NAIBU SPIKA:** Wewe ndiyo Mheshimiwa Mgaya? *(Kicheko)*

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Nyanda za Juu Kusini ni wakulima wakubwa wa zao la parachichi na *horticulture* kwa ujumla. Je, ni lini Serikali itaweka mfumo wa *cold-room* katika baadhi ya mabehewa katika Reli ya *TAZARA* ili kuhakikisha kwamba wakulima wakubwa wa mazao hayo wanasafirisha mazao hayo kufika Dar es Salaam kwa ajili ya kupeleka nje ya nchi yakiwa na ubora? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya, kama lilivyoulizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Zambia pamoja na China ilijenga Reli ya *TAZARA* yenye urefu wa kilomita 860. Kwa sasa reli hiyo iliyojengwa ilikuwa na uwezo wa kubeba tani milioni tano, lakini kutokana na sababu mbalimbali hatukuweza kufikia hata 30% ya lengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumeshaanza maboresho mbalimbali kwa ajili ya kuboresha reli yetu hiyo ya *TAZARA,* hivyo ninachukua ushauri wake Mheshimiwa Mbunge tuone namna ya kutazama, siyo tu kuweka *cold room* kwa ajili ya mazao ya parachichi ambayo yapo Mkoa wa Njombe, lakini kuangalia *chain* nzima katika njia nzima kuanzia inapotokea Kapiri Mposhi mpaka Dar es Salaam ili iweze kuwa sehemu ya kuchechemua uchumi wa maeneo ambapo reli hiyo inapita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Mwanzoni kulikuwa na mpango wa kujenga reli kutoka Tanga – Arusha kuelekea Musoma na sasa, badala yake mpango huo umebadilika kwamba, reli inapita Simiyu. Je, ni lini sasa mchakato huo wa ujenzi wa reli hiyo ya kwenda Musoma utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Manyinyi, swali lake alilouliza; Mpango wa Serikali ni kuunganisha Bandari yetu ya Tanga na Mikoa ya Kaskazini kwenda mpaka Ziwa Tanganyika. Mpango huo upo, hatujali sana imepita wapi, lakini tunaangalia kiuchumi ni wapi ipite na kadhalika. Kwa mfano, katika njia hiyo kuna madini mbalimbali, ikiwa ni pamoja na magadi soda, Engaruka kuna madini kule Dutwa, *nickel* na kadhalika. Kwa hiyo, njia *specific* pengine naweza nisizungumzie hapa, lakini kwa maana ya mpango huo ambao Serikali inao itakwenda kujenga baada ya hatua za awali kukamilika, ikiwa ni pamoja na usanifu wa kina.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ameuliza Mheshimiwa Mbunge wa Musoma Mjini. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Florence.

Na. 250

**Ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji, Muhambwe**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati Skimu za Umwagiliaji za Nyendara, Muhambwe, Kumbanga, Mgondogondo na Kigina, Muhambwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini, ikiwemo Skimu za Nyendara, Muhambwe, Kumbanga, Mgondogondo na Kigina zilizopo Jimbo la Muhambwe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, imeanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kwa ajili ya ukarabati wa Skimu za Nyendara, Muhambwe, Kumbanga, Mgondogondo na Kigina zilizopo Jimbo la Muhambwe. Utekelezaji wa kazi za upembuzi yakinifu umefikia 70% na unatarajia kukamilika ifikapo Juni, 2025. Baada ya usanifu kukamilika skimu hizo zitatangazwa mara moja, kwa ajili ya ukarabati. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. Kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, hata hivyo ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, Serikali imethibitisha kwamba, Juni, Mwaka 2025 upembuzi yakinifu utaisha. Nini *commitment* ya Serikali kutenga pesa ya kujenga na kukarabati skimu hizi kwenye bajeti ya mwaka 2025/2026?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Skimu hizi za Jimbo la Muhambwe zina ukubwa wa hekta 1,297 na kati ya hizi ni hekta 582 tu zinazofanya kazi kwa maana ya kulimwa, chini ya 50%. Je, Serikali haioni kwamba, iko sababu ya kuharakisha kutengeneza hizi skimu ili wakulima wa Jimbo la Muhambwe waweze kufaidika na skimu hizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samizi Florence kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Wananchi wake wa Jimbo la Muhambwe,

hususan kufuatilia hii miradi. Jambo moja ambalo nimhakikishie ni kwamba, miradi hii yote ambayo upembuzi yakinifu umekamilika tumeitengea fedha katika Mwaka wa Fedha unaokuja 2025/2026. Kwa hiyo, baada ya hii maana yake ni inaingia katika Mwaka unaokuja, tutazitangaza na zitaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza ukubwa, ili kufanya haraka, ni kwamba, tunatambua kwa sasa ukubwa ni hekta 582 na huu usanifu wa kina umekusudia kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia hizo hekta 1300 kwa hiyo, lipo katika mipango ambayo tunayo. Nimthibitishie tu tutakapozitangaza, tutatangaza katika ukubwa ambao upo kwa sasa. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Sigula.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Umwagiliaji iliyoko Ilemba, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini, kasi ya ujenzi hairidhishi kabisa. Mkataba ulipaswa kukamilika mwaka jana, Disemba, 2024 wameongezewa mwaka mzima, lakini bado kasi hairidhishi. Je, uko tayari kufika *site* kuona namna ambavyo kasi hairidhishi, ili utoe maelekezo kwa mkandarasi huyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sigula, yuko tayari kwenda *site* na wewe au aende peke yake?

Mheshimiwa Waziri, jibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kufika *site* na yeye pamoja na Mbunge wa jimbo. Nimthibitishie tu kwamba, tumepata fedha na tutapeleka ili yule mkandarasi amalizie kazi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Bwawa la Msagali unaenda kwa kusuasua sana. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bwawa la Umwagiliajai la Msagali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Msagali ambalo lipo katika Jimbo la Mpwawa liko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Bahati nzuri eneo hilo nimefika, kusuasua kwake ni kwamba, sisi tulikuwa tumecheleweshea kupeleka fedha ambazo tulikuwa bado hatujazipata, lakini katika mgao huu ambao tumeupata, kwa mwezi ujao, tutaongeza zile fedha, ili mkandarasi aweze kumaliza ile kazi iliyobakia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji za Mwamkulu, Ugawa pamoja na Uwila umekuwa ukisuasua na Serikali imeshatenga fedha nyingi sana, lakini hazijakamilika. Je, upi mpango wa Serikali wa kutenga fedha kukamilisha ujenzi huo, ili kuleta tija kwa wananchi? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, mabwawa yote matatu aliyoyaainisha Mheshimiwa Mbunge tumeyatengea fedha na sisi tumekuwa tukitoa fedha kulingana na tunavyopokea kutoka Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, tutaendelea kupeleka fedha ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Umwagiliaji ya Ruaha Mbuyuni, vifaa vimewekwa pale na mkandarasi, sasa ni miezi miwili, lakini kazi haianzi. Je, ni lini mkandarasi yule ataanza kazi kujenga ile skimu ambayo ilibomoka? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, tulishamkabidhi mkandarasi *site* katika Jimbo la Kilolo, alichotakiwa kukifanya sasa hivi ni kwamba, aanze kazi na sisi kama Serikali tulishamlipa *advance payment* kwa kazi hiyo. Kwa

hiyo, niseme tu kwamba, mimi mwenyewe nitafuatilia kwa kuwaelekeza watu wa *RM* wa Mkoa wa Iringa, ili ahakikishe anamsukuma mkandarasi aanze ile kazi mara moja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Abeid Ramadhan.

Na. 251

**Hitaji la Maji Kijiji cha Sagara, Singida Kaskazini**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itasambaza maji salama katika Kitongoji cha Gairu, Kijiji cha Sagara ambacho wanatumia maji yenye chumvi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha huduma ya majisafi na salama inapatikana kwa wananchi waishio vijijini, ikiwemo Kitongoji cha Gairu, ambacho kwa sasa kwa sehemu kinapata huduma kupitia Skimu ya Maji ya Sagara. Aidha, serikali imechimba visima na kujenga *point sources* katika Jimbo la Singida Kaskazini, kwenye Vijiji vya Mrama, Mwakinchenche, Ikiwu na Mukulu, kama mpango wa muda mfupi wa kuhakikisha huduma ya maji inapatikana. Pia, Serikali inaendelea na uchimbaji wa visima vingine katika Vijiji vya Mangida, Minyenye, Misinko na Kitongoji cha Gairu, ambapo utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea vilevile na Tathimini ya Upanuzi wa Skimu ya Maji ya Sagara kupeleka maji Kitongoji cha Gairu. Mradi utatekelezwa kwa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abeid.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri hayo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye pia, alifika katika Kijiji cha Mrama kuzindua kile kisima, pia, ninaomba nitoe masahihisho kidogo; kwanza Wananchi wa Gairu hawapati huduma katika Mradi wa Sagara kwa sababu, uko mbali na pia, kule ni Bonde la Ufa, Gairu wako Bonde la Ufa na Sagara iko juu kwa hiyo, ni tabu kwao kupanda mlima kwenda kupata maji pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo, sasa ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; badala ya kuchukua maji kwenye *source* au kisima, ule Mradi wa Sagara, kwa nini tusichukue maji kutoka chanzo cha mradi mkubwa wa Kinyamwenda, ambao unatoa maji lita elfu ishirini kwa saa na unaweza kusambaza hata vijiji vitano, ili tupeleke na Kitongoji cha Misuna, ambacho kiko karibu na Kitongoji cha Gairu, ambacho kinapata maji yasiyo salama kwa matumizi ya binadamu na pia, hapohapo tungeweza kuchukua maji ya Sagara tukayapeleka Mangida?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Kitongoji cha Muungano kilichoko Kijiji cha Pambaa hawana maji; kitongoji hicho kina Miradi ya Migodi ya Madini ya Dhahabu, lakini wananchi wanapata taabu, hawana maji. Je, Serikali ina mpango gani kuwapatia wananchi hawa kisima kizuri cha maji ambacho kinaweza kikaondoa tabu hii, lakini pia, kusambaza maji kwenye maeneo ya migodi ya madini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Ighondo kwa kazi nzuri sana ambayo anaendelea kuifanya kwa wananchi wake. Pia, namshukuru sana kwa namna ambavyo ameshirikiana na Serikali kwenye kusimamia upanuzi na uboreshaji wa Mradi huu wa Sagara, lakini pia, kwa kutoa taarifa, kama ambavyo sasa amesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Mradi huu wa Sagara kwenda Gairu kuna umbali na lengo la Serikali ni kwamba, mradi unapokamilika basi maji yawe yanapatikana kwa gharama nafuu. Tunapoyatoa maeneo ya mbali, maana yake ni kwamba, yanapofikishwa kwa watumiaji gharama yake ya kuyalipia inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge nikitambua kwamba, kuna mradi wetu wa shilingi milioni 950 maeneo ya Kinyamwenda. Nitatumia fursa hii kuwaelekeza *RM* upande wa Singida, wakafanye utafiti na kujiridhisha ni namna gani maji haya tunaweza tukayafikisha Gairu, lakini pia, tunaweza tukayapeleka Misuna, katika vijiji na vitongoji vingine ambavyo vimezunguka katika eneo hilo. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kadri anavyoendelea kuwapigania wananchi wake na sisi Serikali tuko pamoja naye kuhakikisha kwamba, tunafikisha huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipengele cha pili, pia, ni kweli kabisa lengo la Serikali ni wananchi kupata huduma ya maji safi na salama. Sisi tumejipanga na kijiji ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja, tunalipokea, tutaenda kufanya utafiti pale tujiridhishe ukubwa wa tatizo, kama ni kuchimba kisima tutachimba kisima na kama ni kupanua skimu nyingine ifikishe maji tufanya hivyo, lengo ni kwamba, wananchi wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na Serikali kupeleka fedha nyingi kwenye miradi ya maji, lakini bado changamoto ya maji kwenye maeneo mengi, hasa maeneo ya vijijini, imeendelea kuwa kubwa. Ninataka nijue, kwa nini sasa Serikali msifanye tathmini ya kujiridhisha maeneo yote, hasa maeneo ya vijijini, ambayo yana changamoto ya maji, waje na mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba, angalau kwenye bajeti ya mwaka 2025/2026 maeneo haya yote, ambayo wananchi wanaathirika waweze kupata mradi wa maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Chege, lakini pia, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025 imeelekeza uhitaji wa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kuwafikishia wananchi huduma ya maji safi na salama kwa kiwango cha 85%, sasa tumeshafikia 80.1% na vilevile kwa mjini kuwafikishia kwa kiwango cha 95% na sasa tumeshafikia kiwango cha 91.6%. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba, Serikali imefanya kazi kubwa sana, lakini bado inatambua kuna maeneo ambayo bado hatujayafikia na tumeweka mikakati ya kuhakikisha kwamba, tunafika katika lengo ambalo tumejiwekea. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wapo Wabunge kama kumi wanaomba maswali ya nyongeza. Naomba maswali yawe mafupi *to the point* na majibu yawe mafupi.

Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Wariku kuna mradi wa shilingi bilioni 1.6 utakaowanufaisha wakazi 3,000, lakini mpaka sasa hivi haijatoka hata shilingi. Ni lini sasa mtatoa pesa ili Wakazi wa Wariku, Kangetutya, Kamkenga, Majago na Rwabu waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi, lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru dada yangu, Mheshimiwa Ester Bulaya na ninafahamu anavyoendelea kupambana kwa ajili ya wananchi hao. Sisi Wizara ya Maji *consumption capacity* yetu ni kubwa na tunaweza kutumia bajeti yetu vizuri sana, lakini pia, madai kama haya sisi tunaendelea kufanya majadiliano mazuri kabisa na wenzetu wa Wizara ya Fedha na tumefikia hatua nzuri. Tunaamini kwamba, muda umefika sasa, tutawalipa hawa wakandarasi, ili

miradi hii iweze kukamilika na watu waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aysharose.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwa kuwa, Vijiji vya Winamila, Tumbi, Dadia, Itetemo na Kitalaro katika Jimbo la Manyoni Mashariki havina kabisa mtandao wa maji. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupeleka maji katika vijiji hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana dada yangu kwa kuendelea kutukumbusha. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, upande wa Manyoni ameweka mradi wa shilingi bilioni 26, Mradi wa Miji 28 na sasa umefikia 40%, lakini pia, tuna programu ya visima 900 ambao unaendelea katika kila jimbo visima vitanovitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kabisa kwamba, miradi hii itakapokamilika kuna visima vina uwezo wa kutengenezewa *extension* na kufikisha katika maeneo mengine ambayo hayana maji. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge avute subira, miradi hii itakapokamilka tutaangalia sehemu ambayo tutakuwa hatujafika, ili tuweze kuona namna gani tutawafikishia wananchi wa maeneo hayo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Wilaya za Meru na Arumeru wana changamoto kubwa ya *floride* kwenye maji, ambayo inawasababishia madhara makubwa ya kupinda viungo na akinamama wajawazito kushindwa kujifungua. Ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha maji haya yanasafishwa kabla ya matumizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijasikia vizuri swali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, hebu rudia tena swali lako. Zungumza polepole *with confidence*.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Wilaya za Meru na Arumeru wana changomoto kubwa ya *floride* kwenye maji, ambayo inawasababishia kupinda kwa viungo na changamoto kubwa kwa akinamama wakati wa kujifungua. Ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha maji haya yanasafishwa kabla ya matumizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vyetu vya maji ambavyo vimekuwa na changamoto za *floride* na *chloride,* kuna vyanzo ambavyo tunaweza kutibu kwa kutumia kemikali tulizonazo ambazo zimepitishwa, lakini kuna maeneo mengine ile *concentration* inakuwa ni kubwa sana kiasi kwamba, gharama ya kuyatibu inakuwa ni kubwa sana. Tunachokifanya ni kubuni miradi mingine mbadala, ambayo inaweza ikatusaidia kufikisha maji katika maeneo ambayo wananchi hao wanaishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba, tunaondokana na gharama kubwa ya kutibu maji, ambayo, *eventually,* gharama hizo zinakwenda kumwangukia mwananchi. Lengo ni kwamba, wapate maji na yawe na gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ni kwamba, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, suala la Meru na Arumeru tayari tumeshalipokea katika ofisi yetu ya Wizara ya Maji na tunalifanyia kazi tukiwa tunaendelea kubuni miradi mbadala ya kuwafikishia huduma ya maji safi na salama. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Noah, jiandae Mheshimiwa Waitara.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali. Je, ni lini Serikali itatoa fedha, kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Oldonyosambu, Tarakwa, Siwandeti, Tiranyi na Kimnya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja; tayari tumeshapokea madai hayo na tumeshawasilisha kwa mchakato wa kulipa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara, jiandae Mheshimiwa Chiristina.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vitano vilielekezwa kwenda Nyabisaga, Kiyongera, Kitenga, Nyakalima na Kubhiterere na wananchi wakawa na matumaini makubwa sana. Ninaomba nijue, ni lini sasa vijiji hivi, ile miradi itakamilika watu wapate maji, kama ambavyo tuliahidi na wakapokea kwa shangwe kubwa sana? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waitara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jana na juzi tuliongea na Mheshimiwa Waitara, kuhusiana na maeneo haya. Nimtoe hofu, Serikali imeshalipokea na inalifanyia kazi. Tutahakikisha kwamba, mkandarasi analipwa, ili vijiji hivyo viweze kukamilika na kuhakikisha kwamba, wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali tuwe na *availability accessibility* na *affordability;* vipengele vitatu lazima tunavizingatia kuhakikisha kwamba gharama ya mradi

unapokamilika basi ikaendane na uwezo wa wananchi kumudu huduma hiyo ya maji ambayo itakuwa inatolewa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yustina ajiandae Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Je, ni lini Serikali itakamilisha zoezi la kusambaza maji kutoka mradi mkubwa wa Laizeri katika Wilaya ya Kiteto, mabomba yako pale na vifaa, uende Vijiji vya Dongo na Ndotoi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibi swali la nyongeza kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameuliza. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, tumekuwa tukishirikiana vizuri sana na ameendelea kuwapambania sana akinamama, tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na kwa ushauri wake ambao umeendelea kutupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utakamilika ndani ya muda wa mkataba, ambapo bado mkataba huo uko *active* na hatujapata changamoto yoyote. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana na sisi ili uweze kukamilika bila kuwa na changamoto yoyote. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia, ajiandae Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Likwidi imekuwa na changamoto ya maji kwa muda mrefu sana tangu tumepata uhuru.  Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inawatua ndoo kichwani  akinamama wa Kata hii ya Likwidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana dada yangu kwa kazi nzuri sana ambayo anaendelea kuifanya. Nilikuwepo Mtwara, tulikuwa naye; lakini pia ni dhamira ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kuendelea kumtua mama ndoo kichwani na pia ni maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vile visima vitano vitano tunatambua kwamba hiyo kata haikuweza kufanikiwa kupata kisima. Ninaomba nimtoe hofu, katika bajeti hii tunakwenda kuweka bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wake wanaenda kupata maji safi na salama katika kata hiyo. Ahsante sana

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba nianze kuishukuru Serikali kwa kuniletea mabomba ya nchi nane kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Mgombasi na pia kutatua tatizo la Mradi wa Mchomola ambao sasa kazi inaendelea. Swali langu; tuna Mradi wa Limamu na Mradi wa Luchiri pale Msufini, je, ni lini Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi huo ambao ipo katika bajeti hii ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2024/2025?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka wiki tatu zilizopita aliuliza swali kuhusu haya mabomba na akaomba kuhusu fedha. Serikali iko kazini na ndiyo maana tayari leo ameongea kwa furaha sana kuonyesha kwamba Serikali imetenda kulingana na jinsi ambavyo alikuwa ameomba. Nimtoe hofu na hili ambalo amelisema, kwa sababu bajeti yetu ya fedha ya mwaka wa fedha 2025/2025 haijapita, nimtoe hofu kwamba tunakwenda kulifanyia kazi ili mradi huo nao uweze kupata fedha kama

ambavyo leo amekiri kabisa kwamba tayari mradi kwanza alioombea pesa Serikali ya Dkt. Samia Saluhu Hassan imekwishapeleka. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali yetu yamekwisha na maswali ya ziada ya maji yatakuja kesho kwenye bajeti ya maji.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni waliokaa Jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Viongozi na Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo; Ndugu Gerson Msigwa, Katibu Mkuu; Ndugu Stephen Kagaigai, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)*; Profesa Saudin Mwakaje, Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA); Ndugu Victor Tesha, Mwenyekiti wa Bodi ya Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (*COSOTA*); na Ndugu Leodger Tenga, Mwenyekiti wa Bodi Baraza la Michezo la Taifa (BMT), karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Mona Mwakalinga, Mwenyekiti wa Bodi ya Filamu Tanzania; Ndugu Asha Dachi, Mhariri Mtendaji wa Shirika la Magazeti ya Serikali; Ndugu Patrick Kipangula, Kaimu Katibu Mtendaji wa Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari; Dkt. Kedmon Mapana, Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa; Dkt. Herbert Makoye, Katibu Mtendaji wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo; na Dkt. Gervas Kasiga, Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Ndugu Neema Msitha, Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa; Ndugu Consolatha Mushi, Katibu Mtendaji Baraza la Kiswahili la Taifa; Ndugu Philemon Kilaka, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu na Msimamizi wa Hakimiliki Ofisi ya Hakimiliki Tanzania; Ndugu Nyakaho Mahemba, Afisa Mtendaji Mkuu Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania; Dkt. Jonas Tiboroa, Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya; na Ndugu Walace Karia, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)*. *(Makofi)*

Sasa ndugu Karia makofi yakiendelea na wewe unasimama. Ahsanteni, hiyo ndiyo heshima ambayo unapewa na Bunge, haya mambo mazuri yanakuja.

Mgeni mwingine ni *Engineer* Hersi Said, Rais wa Yanga *Club*...

**MBUNGE FULANI:** Acheni kelele.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya acha mambo yako hayo.

**MBUNGE FULANI:** Hiyo irudiwe hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Hatuchezi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya, hebu tunza nidhamu zako;

Yupo pia Ndugu Selemani Said, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi *Simba Sports Club*. *(Makofi)*

Ahsanteni, nimemwona Mheshimiwa Lukuvi kapiga makofi kwa viongozi wote wawili; lakini nimewatazama viongozi wengine wakubwa, siwezi kuwataja, wamepiga makofi kwa mmoja, lakini sasa sikuwaona kupiga. Mheshimiwa Waziri nikupongeze, mambo kama haya ndiyo yanayoleta heshima kwenye Taifa. Vilabu hivi viwili vinachangia maendeleo makubwa sana ya nchi yetu. Ni vilabu vinavyoheshimika, viongozi wao wanaheshimika, wanachama wao wanaheshimika na Taifa linaendelea kufanya kazi na wao. Nikuombe panapo majaliwa wakati ukipata fursa nyingine mwalike Mo Dewji aje humu ndani, mwalike na Ghalib Said naye aje humu ndani; basi tuone viongozi wakubwa wa vilabu hivi kwenye furaha ya Taifa letu. *(Makofi)*

Wapo pia Profesa Haruni Mapesa, Mkuu wa Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere; Ndugu Antonia Sangalali, Mwenyekiti wa Umoja wa Machifu (UMT); Ndugu Aron Mikomangwa, Katibu wa Umoja wa Machifu; na Ndugu Joseph Kusaga, Mwanzilishi na Mmiliki wa *Clouds Media*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge napenda kumtambulisha na kumpongeza bwana Joseph Kusaga Mwakilishi na Mkurugenzi

Mtendaji wa *Clouds Media Group* kwa mchango wake, kipekee, katika mendeleo ya Taifa letu. Tangu mwaka 1998 ndugu Kusaga ameongoza mapinduzi katika tasnia ya habari kwa kuanzisha *Clouds FM Redio* iliyoibua vipaji, kutoa elimu, kuburudisha na kuhimiza utambulisho wa Kitanzania. Kupitia *Clouds* TV Malkia *Choice FM*, *Coconut FM* na majukwa mengine amewafikia mamilioni ndani na nje ya nchi. Mchango wake mkubwa zaidi uko katika uwezeshaji wa vijana; maelfu wamepata nafasi kupitia mashindano, vipindi na matamasha aliyoyaasisi. *(Makofi)*

Ndugu Joseph Kusaga *Foundation* amejikita katika kutoa mafunzi zana na mitaji midogo kwa vijana kwenye maeneo ya kilimo, ubunifu na teknolojia. Aidha, Kusaga ametumia vyombo vya habari kuendeleza utamaduni wetu kukuza matumizi ya Kiswahili na kuhamasisha ajenda za maendeleo endelevu kwa kushirikiana na taasisi kama *UNDP*. Kwa mchango huu mpana Joseph Kusaga anastahili kutambuliwa kama shujaa wa kizazi hiki, mlezi wa vipaji mhamasishaji wa maendeleo ya vijana mabalozi wa utamaduni wa Taifa letu. Tunampongeza, tunamtambua. *(Makofi)*

Ninaomba kumtambulisha kwenu Ndugu Rita Paulsen, Mwakilishi wa Mashindano ya Kusaka Vipaji *(Bongo Star Search)*. Ahsanteni. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Kabudi ambao ni Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo kutoka Wizara hiyo, wakiongozwa na Ndugu Savera Salvatory Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge: Mgeni wa Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mwenyekiti Mstaafu wa Mtaa kutoka Moshi Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, mpiga kura wake kutoka Sumbawanga Mkoa wa Rukwa, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Tadayo wapiga kura wake kutoka Mwanga Mkoani Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, watoto wake kutoka Lushoto Mkoa wa Tanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Viongozi wa CCM Kata ya Mkolye, Wilaya ya Sikonge Mkoa wa Tabora. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mwita Waitara, wapiga kura wake kutoka Tarime Vijijini, Mkoani Mara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: Wanafunzi 50 na Walimu sita kutoka Shule ya Sekondari ya Kirinjiko iliyopo Same, Mkoa wa Kilimanjaro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 100 na Walimu saba wa Shule ya *Fountain Gate* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Walimu watano na wanafunzi 75 wa Shule ya Msingi Elizabeth kutoka Wilaya ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Ndugu Theresia Mwageni kutoka Kisasa Jijini Dodoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwite Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Bunge lako Tukufu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96) kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu kwa kuturuzuku uhai, kuendelea kutupatia afya njema na kutuwezesha kukutana tena siku ya leo kujadili ustawi wa sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kwa kuniteua kuwa Waziri wa Wizara muhimu ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hii ni heshima kubwa sana kwangu na ninaichukulia kama chachu ya kuendelea kulitumikia Taifa hili kwa bidii, weledi na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni mhimili muhimu sana kwa maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, ambayo kwa maneno mengine naweza kusema ni Wizara yenye nguvu shawishi (*soft power*) ya nchi inayobeba mtima wa Taifa letu na kuitanabaisha katika kaumu ya Mataifa. Sekta ya Habari imekuwa na mchango mkubwa katika kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa muhimu zinazowawezesha kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha, utamaduni wetu ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Hivyo, kupitia sekta ya utamaduni Serikali imeendelea kujenga uzalendo, kuhifadhi mila na desturi pamoja na maadili ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekta ya Sanaa, imekuwa na nafasi kubwa katika uzalishaji wa ajira hususan kwa

vijana. Aidha, wasanii wetu wameendelea kuwa mabalozi wa nchi yetu ndani na nje ya mipaka yetu. Michezo nayo ni kiungo muhimu katika kujenga fahari ya maendeleo ya Taifa letu. Michezo siyo burudani tu bali pia ni nyenzo ya kuimarisha afya, umoja na mshikamano wa Taifa na ni chanzo cha ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake kubwa na za dhati katika kuendeleza Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Sekta hizi yametokana na uongozi wake mahiri, wenye weledi, umakini na upeo mkubwa unaoendelea kulishamirisha Taifa letu ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia uongozi wake madhubuti tumeona mabadiliko makubwa katika Sekta ya Habari ambapo vyombo vya habari vimeendelea kupata mazingira wezeshi ya kufanya kazi kwa uhuru na uwazi, huku vikizingatia weledi na maadili ya taaluma ya habari. Aidha, katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) limepata mafanikio makubwa ya kujivunia katika nyanja za habari, utangazaji, mifumo, rasilimaliwatu, upanuzi wa usikivu na ujenzi wa Makao Makuu ya *TBC* Jijini Dodoma, uanzishwaji wa chaneli za kimkakati, uboreshaji wa maslahi ya watumishi na upelekaji wa habari za nchi kimataifa. Hivyo, kutimiza lengo kuu la kuitangaza nchi kimataifa pamoja na kukuza lugha adhimu na aushi ya Kiswahili sanifu na fasaha, utalii na utamaduni wa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru na nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa namna alivyo mstari wa mbele kwa kuwa kichocheo cha ukuaji wa Sekta ya Michezo. Mheshimiwa Rais amekuwa akihamashisha timu zetu za Taifa na vilabu vyetu kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa kwa kutoa motisha kwa kila goli linalofungwa katika mashindano ya kimataifa. Ni wazi kuwa mchango wa Mheshimiwa Rais ndiyo chachu ya mafanikio

ya timu zetu za Taifa na vilabu vyetu katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ambapo kwa mara ya kwanza, baada ya miaka 30 jumla ya timu sita za Taifa zimeweza kufuzu katika mashindano makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kama mwenyeji imefuzu katika kombe la Mataifa ya Afrika (*AFCON* 2027) na *CHAN* 2024, Timu ya Taifa ya Wanawake imefuzu katika mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika la Wanawake la *CAF* (*WAFCON*) yatakayofanyika nchini Morocco. Timu ya Taifa ya Vijana chini ya umri wa miaka 17 (Serengeti *Boys*) imefuzu kucheza Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Vijana (*AFCON* U-17), Timu ya Vijana wa Umri wa Chini ya Miaka 20 imefuzu mashindano ya *AFCON* 2025, timu ya Taifa ya mpira wa miguu imefanikiwa kufuzu katika mashindano ya *AFCON* 2024; na Timu ya Taifa ya Wanawake ya Futsal imefanikiwa kufuzu katika fainali za *AFCON (Women's Futsal Cup of Nations 2025)* pamoja na kukata tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuipongeza *Club* ya Simba kwa mafaniko makubwa waliyoyapata kwa kufanikiwa kufika katika hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Mafanikio haya si tu yanatoa heshima kwa *club* hiyo, bali pia yanaitangaza nchi yetu katika ramani ya soka la kimataifa. Kupitia mafanikio haya, Simba, imeweza kushika nafasi ya nne kati ya vilabu bora barani Afrika jambo ambalo ni fahari kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nitoe pongezi kwa mwanariadha mashuhuri na shupavu Alphonce Felix Simbu ambaye hivi karibuni aliipeperusha vema Bendera ya Tanzania kimataifa kwa kushika nafasi ya pili katika Mashindano ya Mbio za Boston zilizofanyika nchini Marekani tarehe 21 Aprili 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yetu imefanikiwa kuwa mwenjeji wa mashindano ya *CHAN 2024*, na *AFCON 2027*. Pia kumekuwa na uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya michezo ikiwamo ujenzi wa viwanja vya mpira wa miguu katika Jiji la Arusha na Dodoma,

ujenzi wa Akademi ya Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na ujenzi wa vituo vya michezo na kupumzikia wananchi katika Majiji ya Dar es Salaam na Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwa bega kwa bega na wasanii wetu kwa kuweka mazingira wezeshi katika maendeleo ya sanaa nchini ambapo wasanii wetu wameendelea kupatiwa mitaji kwa ajili ya kuboresha kazi zao za sanaa. Katika uongozi wake Mheshimiwa Rais amefufua Mfuko wa Utamaduni na Sanaa uliokuwa umekufa kwa zaidi ya miaka 10 na kwa kipindi kifupi, jumla ya miradi 359 ya utamaduni na sanaa imepatiwa mikopo yenye jumla ya thamani ya shilingi 5,250,070,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mheshimiwa Rais amekuwa mshiriki wa moja kwa moja katika matukio na shughuli mbalimbali za sekta zetu, ikiwemo ushiriki wake kama mgeni rasmi katika Tuzo za Ucheshi Tanzania *(Tanzania Comedy Awards)* zilizofanyika tarehe 22 Februari, 2025, na Tamasha la Utamaduni lililofanyika Mkoani Ruvuma, tarehe 20 hadi 23 Septemba na juzi katika Tamasha la Samia Kalamu *Award* lililofanyika Dar es Salaam kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, ninawapongeza sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa katika kumsadia Mheshimiwa Rais. Viongozi hawa wamekuwa chachu na msaada kwa Mheshimiwa Rais kwa kutupatia maelekezo pamoja na ushauri uliosaidia kuboresha sekta hizi. Ninawashukuruni na kuwapongeza sana viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza kwa busara na weledi

Bunge la Kumi la Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelekezo na miongozo yake yamekuwa msingi wa ufanisi mkubwa wa Bunge katika kuisimamia Serikali kutekeleza vema majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakupongeza na wewe kwa kumsaidia na kumshauri vema Spika katika majukumu yake ya kuliongoza Bunge. Ninawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge, kwa kusimamia vema na kwa ustadi mkubwa mijadala ya kibajeti katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko; na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa maelekezo, ushauri, michango na maoni yao kwa Wizara yangu ambayo yametusaidia sana katika kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa maoni, ushauri na maelekezo ambayo yamekuwa yakiisaidia Wizara kuboresha vipaumbele, mikakati yake na pia kuweka msingi imara wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi chote hiki ni kutokana na ushirikiano mzuri miongoni mwa wadau wa Wizara wakiwemo viongozi na watumishi wa Wizara. Ninatambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu wa Wizara wakati wa kufanikisha utekelezaji wa majukumu na mageuzi makubwa tunayoendelea nayo Wizarani na katika sekta zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nimshukuru Bwana Gerson Msigwa, Katibu Mkuu; Bwana Methusela Ntonda, Naibu

Katibu Mkuu; Wakurugenzi; Wakurugenzi Wasaidizi; Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na watumishi wote wanaofanya kazi kwa bidii na wanaohakikisha mipango ya Wizara inatekelezwa kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, ninaomba kutumia nafasi hii kukipongeza Chama Cha Mapinduzi kupitia Mkutano Mkuu Maalum wa Chama uliofanyika tarehe 19 Februari, 2025, kwa hatua ya busara na ya kizalendo ya kumpitisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea wa kiti cha Urais kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika baadaye mwaka huu. Tunapoingia katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, CCM tayari tumekamilisha, kazi iendelee na sasa tunasema 'Kazi na Utu, Tunasonga Mbele,' Mitano tena kwa Mama Samia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kupitishwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar. Vilevile, ninampongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea Mwenza katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Huu ni muunganiko wenye nguvu, uzoefu na uwakilishi bora kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru wapiga kura wangu, wananchi wa Jimbo la Kilosa, kwa kuniamini na kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu; na wakati wa kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazokabili Jimbo letu la Kilosa. Ushirikiano wenu, moyo wa uzalendo na utayari wenu ni nguzo kuu katika mafanikio makubwa tunayoyashuhudia yaliyobadilisha Jimbo letu la Kilosa kuwa na miradi lukuki katika sekta zote. Ninaomba waendelee kuniamini kwani kama wasemavyo wahenga, 'Mwana hasahau mkono uliomlea,' nitaendelea kuwa mtumishi wao mwaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni masikitiko yetu kwamba katika kipindi hiki Bunge lako Tukufu lilipatwa na msiba wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, aliyekuwa Mbunge mwenzetu akiwawakilisha wananchi wa Jimbo la Kigamboni ambaye pia alikuwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)* kwa

Kanda ya Afrika. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile atakumbukwa kama kiongozi shupavu aliyewakilisha Tanzania kwa heshima katika majukwaa ya kitaifa na kimataifa na upande wa michezo hasa kwa kuzingatia kuwa alikuwa mwanamichezo mahiri na shabiki kindakindaki wa klabu ya Simba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu binafsi, Wizara na wadau wetu, tunatoa pole kwako Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, familia ya marehemu, ndugu, jamaa na marafiki na wananchi wote wa Jimbo la Kigamboni. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Taifa letu pia limepoteza wadau mahiri na wa kutegemewa katika sekta zetu, wakiwemo wanahabari, wanamichezo, wanautamaduni na wasanii mbalimbali ikiwemo Profesa Martha Qorro ambaye alikuwa ni Mwenyekiti wa BAKITA na mhamasishaji wa matumizi ya Kiswahili sanifu na fasaha. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia za marehemu wote, ndugu, jamaa, marafiki na kwa Watanzania wote kwa ujumla kwa kuwapoteza wapendwa wao. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azipokee roho za marehemu wote na kuzilaza mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui na maelekezo ya Hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 aliyoiwasilisha hapa tarehe 9 Aprili, 2025. Aidha, hotuba hii imezingatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili 2021; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi; Mpango Mkakati wa Wizara; na Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na maelekezo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu imegawanyika katika Sehemu Nane: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima, Majukumu, Misingi ya Mwelekeo, na Vipaumbele vya Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025; na Sehemu ya Nne inabainisha changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026; Sehemu ya Sita ni Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026; Sehemu ya Saba ni maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza MIpango ya mwaka wa fedha 2025/2026; na Sehemu ya Nane ni Shukurani na Hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majukumu, misingi ya mwelekeo na vipaumbele vya Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara kama nilivyoeleza tumezingatia Dira ya Wizara na maelekezo hayo yote ambayo yametolewa katika nyaraka nilizozieleza. Kwa hiyo, katika hotuba yangu ufafanuzi wa kina wa majukumu, misingi na mwelekeo, dira na dhima ya vipaumbele vya Wizara umebainishwa katika kitabu changu cha hotuba kuanzia ukurasa wa kwanza hadi wa tisa ambacho Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti ya matumizi ya Wizara na mtiririko wa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya shilingi 285,318,387,000. Kati ya fedha hizo, mishahara ni shilingi 11,280,116,000; matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 15,847,483,000 na miradi ya maendeleo ni shilingi 258,190,788,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Wizara ikiwa katika utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya mabadiliko ya kimuundo wa Serikali kwa kuihamisha Idara ya Habari kutoka kwa iliyokuwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na kuihamishia katika iliyokuwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hivyo, kuunda Wizara mpya ya

Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mabadiliko haya yaliongeza majukumu ya Wizara pamoja na bajeti ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, hadi kufikia mwezi Aprili 2025, bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka na kufikia shilingi 310,908,589,567.74, ikiwa ni ongezeko la shilingi 25,590,202,567.74. Hadi Aprili, 2025, Wizara imepokea na kutumia jumla ya shilingi 261,670,322,610.89 sawa na 84.2% ya bajeti yote iliyotengwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kati ya fedha hizo shilingi 12,869,535,407.51 ni mishahara, sawa na 56.0% ya mishahara; shilingi 21,823,654,692.81 ni matumizi mengineyo, sawa na 81.4% ya bajeti ya matumizi mengineyo; na jumla ya shilingi 226,977,132,510.57 ni miradi ya maendeleo, sawa na 86.9% ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2024/2025, Sekta ya Habari. Majukumu ya sekta hii ni pamoja na kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003; Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229; na kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati, programu na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo. Wizara kupitia sekta hii imetekeleza majukumu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Habari, Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 226, imeelekeza uundwaji wa Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari. Ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa tayari Bodi hiyo imekwishaundwa na ilizinduliwa rasmi tarehe 3 Machi, 2025 na kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Msemaji Mkuu wa Serikali, imeendelea kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Serikali ya Awamu ya Sita. Wizara imeratibu na kuandaa mkutano wa mwaka wa Maafisa Habari, Uhusiano na Mawasiliano wa Serikali. Mkutano huo uliofanyika Unguja, Zanzibar kuanzia tarehe 3 Aprili, 2025, uliwakutanisha Maafisa Habari zaidi ya 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeratibu jumla ya taasisi za Serikali 35 kukutana na vyombo vya habari kuelezea mafanikio ya utekelezaji wa Serikali kupitia taasisi hizo na kutoa mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Programu hii imekuwa na mafanikio makubwa kwani wananchi wameweza kuelewa mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Utangazajia la *TBC,* majukumu yake yameelezwa ndani ya hotuba yangu ya bajeti, lakini ningependa kueleza kwamba Serikali ili kuhakikisha kuwa azma yake ya kuuhabarisha umma inafanikiwa kikamilifu *TBC* imeendelea kutekeleza miradi ya upanuzi wa usikivu wa redio katika maeneo zaidi ya 29 nchini. *TBC* inaendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa Makao Makuu ya Shirika eneo la Vikonje, Dodoma ambao unahusisha ujenzi wa jengo la Utawala pamoja na majengo ya studio za redio, televisheni na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC* imeanzisha kampeni zinazohamasisha usafi na utunzaji wa mazingira. Kampeni hizo ni ile ya Pika Kijanja inayoendeshwa na chaneli ya *Bongo FM* ambayo inahusisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Mwezi Agosti, 2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliipa nguvu Kampeni ya Pika Kijanja kwa kuhamasisha na kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi na yeye mwenyewe kupika chakula kwa kutumia nishati safi na matangazo hayo yalirushwa mubashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa utalii wa utamaduni na historia unakidhi mahitaji na maelekezo ya Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *TBC* imeanzisha mchakato wa kipindi maalum kitakachoangazia njia ya biashara ya utumwa na biashara kuanzia Zanzibar, Bagamoyo, Mandela, Morogoro, Mamboya, Kilosa, Ving'hawe Mpwapwa, Kilimatinde Manyoni, Tabora hadi Ujiji Kigoma, inayoitwa Safari *Channel.* Kipindi hiki kitarushwa kupitia vyombo vya *TBC* ikiwemo chaneli ya Utalii ya Safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekamilisha utungwaji wa Sheria ya *TBC* ambayo itakuwa ni jibu la changamoto za *TBC* hasa kutokuwa na chanzo cha uhakika, endelevu na toshelevu cha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kampuni ya Magazeti ya *TSN,* inayouhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi, kwa kuandaa Makala maalum zilizosheheni Shughuli za Bunge na Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, sera, mikakati, miongozo na mipango ya Serikali, *TSN* ilichapisha jumla ya makala maalum 432. *TSN* imeendelea kutekeleza ufungaji wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji. Mradi unahusisha ununuzi wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji, ujenzi wa jengo la kiwanda cha uchapaji, ununuzi wa malighafi za kiwandani na ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari. Mradi huo unategemewa kukamilika ifikapo Septemba, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya maendeleo ya utamaduni; katika kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania wanaendelea kusherehekea, kuenzi, kuthamini na kunufaika na urithi wa utamaduni wao, Wizara iliratibu Tamasha la Tatu la Utamaduni la Kitaifa lililofanyika kuanzia tarehe 20 hadi 23 Septemba 2024 Mkoani Ruvuma lililoongozwa na kaulimbiu, 'Utamaduni Wetu ni Utu Wetu, tuuenzi na Kuuendeleza.' Katika kilele cha Tamasha hilo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na *UNESCO* (Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni), vile vile iliratibu warsha ya wadau ya uteuzi wa muziki wa singeli kuorodheshwa kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia unaoratibiwa na *UNESCO*. Muziki wa Singeli, unatumia vionjo vya ngoma za asili ikiwemo midundo na mikong'oso. Midundo ya Singeli inaendelea kuzalishwa kwa wingi kupitia kivunge cha mtozi kilichotengenezwa na BASATA.

Mheshimiwa Naibu Spika, upekee wa Singeli umeifanya kuwa kivutio kikubwa katika matamasha makubwa ya kimataifa kama vile *Nyege Nyege Festival* Nchini Uganda; *DUO Festival,* Nchini Ubelgiji; *Primavera Sound Festival*, Nchini Hispania; *Apporlibation Festival,* Nchini Ujerumani; na *Cora Festival* Nchini Ufaransa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumalizika kwa warsha hiyo, Wizara iliandaa nyaraka muhimu za uteuzi *(Nomination Dossier)* na kuziwasilishwa *UNESCO* yenye Makao Makuu Ufaransa kwa ajili ya hatua za kuidhinishwa. Hivi sasa kinachosubiriwa ni kukamilika kwa taratibu za *UNESCO* ili hatimaye kutangaza rasmi muziki wa Singeli kuwa sehemu ya Orodha ya Urithi wa Dunia, hatua ambayo itaimarisha zaidi hadhi ya utamaduni wa Tanzania duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia BAKITA iliratibu maadhimisho ya tatu ya Siku ya Lugha ya Kiswahili Duniani yaliyofanyika tarehe 7 Julai, 2024, Jijini Dar es Salaam, yakiwa na kaulimbiu 'Kiswahili Fursa za Maendeleo Duniani.'

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza kasi ya kukiuza na kukieneza Kiswahili kimataifa, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) iliratibu Kongamano la Kiswahili la Kimataifa lililofanyika katika Jiji la Havana, Nchini Cuba kuanzia tarehe 7-10 Novemba, 2024. Kongamano hilo lilijumuisha washiriki zaidi ya 600 kutoka nchi mbalimbali duniani. Lengo la Kongamano hilo lilikuwa kupeleka Kiswahili katika ukanda wa Karibe, Amerika ya Kati na Amerika ya Kusini ambako lugha kuu ya mawasiliano ni Kihispaniola.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mafanikio yaliyopatikana katika Kongamano hilo ni pamoja na kuzinduliwa kwa kitabu cha Misemo ya Kila Siku ya Kihispaniola – Kiswahili kilichoandaliwa na (BAKITA), Kamusi ya Kihispaniola - Kiswahili iliyoandaliwa na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na kitabu cha Jifunze Kihispaniola kwa Kiswahili kilichoandaliwa na Chuo Kikuu cha *SUZA (State University of Zanzibar)*. Kusimikwa rasmi kwa Lugha ya Kiswahili katika Ukanda wa Karibe, Amerika ya Kusini na Amerika ya Kati ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia BAKITA imeandaa kanzidata ya wataalam wa Kiswahili kwa lengo la kubaini uwezo wa nchi kushiriki katika kueneza matumizi na maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya nchi kupitia huduma za ukalimani, tafsiri, ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni pamoja na uandishi wa vitabu. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Baraza limetambua na kusajili wataalam 73 sawa na 61% ya lengo la kusajili wataalam 120, ambapo hadi Aprili, 2025 kanzidata ina jumla ya wataalam 1,897.

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha adhimu na aushi ya Kiswahili ni tunu ya Taifa letu. Pamoja na kazi kubwa inayofanywa kwenye eneo hili la Lugha ya Kiswahili, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa sisi Watanzania tuna wajibu wa kujivunia na kutembea kifua mbele kutokana na mafanikio tuliyoyapata ya Lugha ya Kiswahili na hivyo ni lazima tupigane na maadui watatu wa lugha yaani kufubaza, kubananga na kubagaza Kiswahili na tusikubali mtu yeyote aipuuze au kuibeza lugha yetu kwani imetupa utambulisho wa kipekee duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kituo cha Urithi cha Ukombozi wa Bara la Afrika; baada ya harakati za ukombozi wa Afrika kukamilika Tanzania imekabidhiwa jukumu lingine la kuongoza juhudi za uhifadhi wa urithi wa ukombozi wa Afrika kupitia Azimio la Umoja wa Afrika la mwaka 2011 ikiwa ni ishara ya heshima na kuthaminiwa kwa mchango wa Tanzania katika kuleta uhuru na usawa katika Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo kimeendelea kuratibu ukarabati wa jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya *AU,* ambapo hadi sasa ukarabati umefikia 92%. Mafanikio haya yanadhihirisha juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kutunza na kuenzi historia hii adhimu ambayo ni sehemu muhimu ya urithi wa bara letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine, kituo kimeanza kuratibu ujenzi wa Kituo Kikuu cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kilichopo katika eneo la Kiromo, Bagamoyo,

mkoani Pwani. Ujenzi wa Kituo hiki utakuwa na manufaa mengi kwa Taifa letu, ikiwa ni pamoja na kutumika kama makumbusho ya harakati za ukombozi wa Afrika. Aidha, kituo hiki kitakuwa kivutio kipya cha utalii wa kiukombozi. Vilevile, kituo hiki kitakuwa mfano bora wa uhifadhi wa historia ya ukombozi wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihamie katika maendeleo ya sanaa. Wizara imeratibu kushiriki kwenye matamasha mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa. Wizara imefanikiwa kuandaa Tamasha kubwa la *Samia Serengeti Music Festival* ikiwa ni mwendelezo wa Tamasha la *Serengeti Music Festival* ambalo limekuwa likiandaliwa tangu mwaka 2020. Tamasha hili limechukua jina la *Samia Serengeti Music Festival* kwa heshima ya jitihada kubwa zinazofanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha Sekta ya Sanaa, Michezo na Utamaduni nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tamasha hilo lilihudhuriwa na wananchi takribani 45,000 lilihusu wasanii kutoka kambi mbalimbali kutumbuiza katika jukwaa moja kubwa-jukwaa kubwa zaidi kuwahi kutumika hapa Tanzania na Afrika Mashariki ambalo limeweka viwango vya hali ya juu kabisa, kuongeza thamani ya wasanii wetu dhidi ya wasanii wengine wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kuhakikisha kunakuwa na soko la uhakika la kazi za filamu na muziki nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hatua zilizochukuliwa ili kufikia azma hiyo Wizara inafanya jitihada za kuingia makubaliano na wamiliki wa Kampuni za *Emirates*, ambapo mazungumzo ya awali yalifanyika tarehe 15 Novemba 2024, jijini Dubai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Sanaa la Taifa limeendelea kutekeleza kazi zake na Serikali kupitia BASATA kwa lengo la kuimarisha ubunifu na kuongeza ubora wa sanaa iliratibu utoaji wa tuzo za muziki zilizofanyika Dar es Salaam Oktoba, 2024 katika Ukumbi wa *The S*uper Dome Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuzo hizi kwa mara ya kwanza katika historia ya tuzo zilirushwa na vyombo vikubwa vya kimataifa vya habari vya *BET* na *MTV*. Aidha, jumla ya wanamuziki 180 kutoka ndani na nje ya nchi walishiriki kinyang'anyiro cha tuzo na hatimaye tuzo 36 zilitolewa kwa washindi, huku Mwanamuziki Nguli Steven Hiza aliyeimba wimbo wa Tanzania Yetu akipata Tuzo ya Heshima na zawadi ya shilingi 50,000,000 kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kurahisha utoaji wa huduma kwa wadau Baraza limechukua hatua ya kuunganisha mfumo wa utambuzi wa wasanii *Artists Management Information System (AMIS*) na Mfumo wa Ukusanyaji Mapato wa Serikali za Mitaa (TAUSI) na Mfumo wa Ununuzi (NeST) ili kuwafikia wadau wote wa Sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi ya Filamu Tanzania. Serikali kupitia Bodi ya Filamu imeratibu maandalizi ya Tuzo za Kitaifa za Ucheshi *(Tanzania Comedy Awards)* kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu zilizotolewa mwezi Februari, 2025 ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya tuzo yalikuwa kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya fani ya ucheshi ambavyo vimeendelea kuwa chanzo muhimu cha ajira na kipato kwa wacheshi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Taasisi ya Hakimiliki Tanzania *(COSOTA)* kuhusu masuala ya Hakimiliki ya Wasanii. wizara kupitia *COSOTA* imesimamia ukusanyaji wa mirabaha katika madaraja ya kazi ambazo hazisimamiwi na kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha *(CMO)* ambapo Wizara kupitia *COSOTA*, imekusanya kiasi cha shilingi 847,985,594.26 za mirabaha kutokana na Tozo ya Hakimiliki *(Copyright Levy)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo hizi ni mirabaha inayotokana na matumizi ya kazi za sanaa na zinatarajiwa kugawiwa kwa

mchanganuo ulioainishwa kisheria na ambao umeoneshwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania ulianzishwa kwa lengo la kuinua ubora wa kazi za utamaduni na sanaa ili ziweze kujiendesha kibiashara na kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii tena kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuipatia Mfuko huu fedha kwani umekuwa suluhisho kwa changamoto ya mitaji kwa wadau wa utamaduni na sanaa nchini tangu kuhuishwa kwake. Mfuko huu umewezesha utoaji wa mikopo yenye thamani ya shilingi 5,250,070,500.89 kwa miradi 359 ya utamaduni na sanaa katika mikoa 19 nchini hadi kufikia Aprili 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Mfuko umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 2,692,217,069.89 kwa miradi 143 ya utamaduni na sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa). Hatuwezi kuendelea na sanaa bila kuwekeza katika utaalamu na utafiti. TaSUBa inatoa mafunzo ya aina mbalimbali kuhusiana na masuala ya sanaa na utamaduni nchini. Katika mwaka 2012, TaSUBa iliteuliwa kuwa Kituo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki chenye Ubora Uliotukuka *(Centre of Excellency)* katika ufundishaji wa fani za utamaduni na sanaa, hivyo, ni kituo chenye hadhi ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ninapenda kuitumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi zake kubwa katika kuiwezesha TaSUBa kifedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 TaSUBa imefanikiwa kununua vifaa bora na vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya majengo ya Taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo yanayotolewa na Taasisi hii, ni mengi na yameorodheshwa katika hotuba yangu, lakini kubwa taasisi hii sasa inapanua wigo wa mafunzo na kuongeza udahili kwa kutoa nafasi zaidi za ubunifu. Taasisi iko kwenye hatua za maboresho ya mitaala mipya mitatu ambayo itasababisha kuwepo kwa kozi mpya; ambazo ni Usimamizi wa Sanaa na Masoko katika Sanaa *(Arts Management and Marketing),* ambayo ina lengo la kumwandaa Afisa Masoko kutafuta masoko kwa msanii na kazi yake, ndani na nje ya nchi; nyingine ni Urithi wa Utamaduni na Utalii *(Cultural Heritage and Tourism)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia TaSUBa waliratibu Tamasha la 43 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo lililofanyika Oktoba, 2024 katika Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. Tamasha hili lilikuwa na jumla ya vikundi 78 vikijumuisha vikundi 67 kutoka ndani ya nchi na vikundi 11 kutoka nje ya nchi kama ifuatavyo: Vikundi vitatu kutoka Visiwa vya Mayotte, vikundi vitatu kutoka Zambia, vikundi viwili kutoka Ujerumani, kikundi kimoja kutoka Uhispania, kikundi kimoja kutoka India na kikundi kimoja kutoka Brazili. Tamasha lilihudhuriwa na watazamaji wa ndani na nje zaidi ya 46,326.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Maendeleo ya Michezo ikumbukwe kuwa mwaka 2023 Tanzania ilipata heshima ya kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu Barani Afrika *(AFCON 2027)* kwa kushirikiana na Nchi za Kenya na Uganda. Sambamba na mashindano hayo, Tanzania pia imepata fursa ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya *CHAN 2024* yatakayofanyika katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda mwezi Agosti, 2025 ambayo ni sehemu ya maandalizi ya mashindano ya *AFCON 2027*.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mafanikio makubwa kwa Sekta ya Michezo yaliyotokana na maono na dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungananano wa Tanzania katika kuendeleza Sekta ya Michezo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika kwa ufanisi mkubwa, Serikali kupitia Wizara

imeendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya michezo ikiwamo ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru na ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Arusha na Dodoma. Aidha, Serikali inaendelea na ukarabati na ujenzi wa viwanja vitano vya mazoezi vitakavyotumika wakati wa michuano hiyo vilivyopo Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na ujenzi wa viwanja vya mazoezi na kupumzikia wananchi. Ujenzi wa Viwanja vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi *(Recreational and Sports Centres)* unatekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uwanja wa Benjamini Mkapa ukarabati umefikia 80% na kwa upande wa Uwanja wa Uhuru ukarabati mkubwa umefikia asilimia saba na maboresho yanaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto za uendeshaji wa miundombinu ya michezo nchini, Wizara imeanza mchakato wa kuanzisha chombo maalum cha usimamizi wa miundombinu ya michezo nchini *(Sports Infrastructure Management Agency - SIMA)*. Chombo hiki kitakuwa na mamlaka ya kusimamia uendeshaji, ukarabati na matunzo ya miundombinu yote ya michezo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yetu kwamba uwepo wa chombo hiki utapunguza changamoto za usimamizi wa miundombinu ya michezo na kuongeza thamani ya miundombinu hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Baraza la Michezo la Taifa (BMT); katika kuleta hamasa na mwamko kwa wananchi kushiriki katika maandalizi ya mashindano ya *CHAN* 2024 na *AFCON* 2027. Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) iliratibu kongamano la wadau wa michezo kuhusu kushiriki katika maandalizi ya mashindano ya *CHAN* 2024 na *AFCON* 2027 lililofanyika tarehe 15 Januari, 2025 Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spia, Mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko. Mada kuu ilikuwa ni maandalizi ya Tanzania kuwa mwenyeji katika mashindano ya *CHAN* 2024 pamoja na *AFCON* 2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza tumekuwa na mafanikio mengi ya mashindano ya vijana katika mpira lakini niongeze pia katika timu ambazo zimefanya vizuri ni pamoja na Timu ya Taifa ya Kriketi chini ya miaka 19 imefuzu kucheza kombe la Dunia nchini Zimbabwe. Vilevile, Timu ya Taifa ya *Wheelchair* Tenis imefuzu kombe la Dunia nchini Uturuki, na *Futsal* wanawake wamefuzu kucheza kombe la Dunia nchini Ufilipino. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Klabu zetu za Simba, Yanga, Azam pamoja Coastal Union pia zilifanikiwa kushiriki mashindano makubwa Barani Afrika yaani Kombe la Shirikisho pamoja na kombe la Klabu Bingwa. Tunaendelea kuvipongeza vilabu vya Simba na Yanga kwa kuendelea kuiwakilisha nchi yetu katika mashindano makubwa Barani Afrika. Ambapo imewezesha ligi yetu kushika nafasi ya nne kwa ubora, hii imekuwa chachu kubwa kwa vilabu vingine kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, timu ya Simba na Yanga zina dhima kubwa kwa sababu zinaendeleza diplomasi ya michezo katika Bara la Afrika na Nje ya Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kunakuwa na miundombinu bora ya michezo kwa ajili uibuaji wa vipaji vya wanamichezo nchini, Baraza linatarajia kujenga kituo cha michezo katika Kanda ya Kaskazini katika Mkoa wa Manyara kule Babati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; chuo hiki kimeendelea na ujenzi wa hosteli za wanachuo na katika kuhakikisha michezo inaendeshwa kisasa zaidi Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Daktari Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaendelea na ujenzi wa Akademia ya Michezo ya kitaifa katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Ambacho ni kituo pekee cha uibuaji na ukuzaji wa vipaji katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kituo kuchukua vijana walio katika mfumo rasmi wa elimu, kituo pia kitasaidia kutoa mafunzo kwa vijana wetu walioko katika mfumo usio rasmi wanaopaswa kuendelezwa katika michezo. Maelezo ya kina ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara yametolewa katika kitabu changu katika hotuba kuanzia ukurasa wa 9-77 ambapo Waheshimia Wabunge wamepatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarisha utendaji wa Wizara na rasilimali watu; katika kuhakikisha wizara inakuwa na rasilimali watu endelevu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake, Wizara imeajiri watumishi 20. Halikadhalika, Wizara imeendelea na programu za kuwajengea uwezo watumishi katika maeneo mbalimbali ili kuimarisha utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara yametolewa pia katika ukurasa wa 9-77 ambazo tayari Waheshimiwa Wabunge wanazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka wa fedha 2024/2025, changamoto katika utekelezaji wa majukumu hazikosekani. Changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua zimebainishwa katika kitabu cha hotuba kuanzia ukurasa wa 77.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2025/2026; katika mwaka huo Wizara na Taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia maelekezo ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama nilivyosema na maelekezo yale yote ikiwa ni pamoja na Hotuba ya Mheshimiwa Rais na Dira, Sera na Mipango yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Sekta ya Habari; ni mhimili katika maendeleo ya Taifa letu katika mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia Sekta ya Habari imepanga kutekeleza majukumu mbalimbali ambayo yameainishwa kwenye ukurasa wa 115, 116 na 117. Ikiwa ni pamoja na Wizara kuendelea kuratibu mikutano ya Msemaji Mkuu wa Serikali kupitia *TBC* itakamilisha tathmini ya ufungaji wa mitambo ya masafa mafupi na ya kati

(*Short wave and Medium wave*) kwenye maeneo mahususi ya *TBC* yaliyotengwa na *ITU* kwa ajili ya shughuli za utangazaji, ambayo ni Iwambi (Mbeya), Njiro (Arusha), Kunduchi (Dar es Salaam), Mundemu (Dodoma), Mahembe (Kigoma), Songambele (Nachingwea), Pasiansi (Mwanza) na Bombambili (Songea) ambapo mitambo ya *Digital Radio Mondiale* (DRM) inatarajiwa kufungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu hili litakwenda sambamba na kuanzisha idhaa za redio na chaneli za televisheni za kimataifa (*External Services*) ili kuongeza ushawishi wa Tanzania katika ukanda wa SADC, Afrika na Ulimwenguni katika kuitangaza nchi kupitia Kiswahili na utamaduni wa Mtanzania, pia itatangaza kwa lugha ya Kiingereza ili dunia ipate maudhui ya Tanzania kutoka kwa Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *TSN* itaendelea kuelimisha umma juu ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na kuimarisha matumizi sahihi ya TEHAMA na maelezo hayo yote yako ukurasa wa 118, 119 na 120. Kwenye Sekta ya Utamaduni maelezo pia yako kwenye ukurasa wa 118, 119 na 120. Na mambo muhimui yatafanywa na Wizara ni pamoja na kufanya utafiti wa urithi wa utamaduni usioshikika pamoja na kuandaa Atlasi ya Lugha za Jamii na Atlasi ya Tamaduni Mbalimbali za Makabila ya Tanzania na kuendesha Tamasha la Nne la Utamaduni la Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, itaendelea pia kuandaa Maadhimisho ya Nne ya Kitaifa na Kikanda ya Siku ya Kiswahili Duniani na kuratibu kikao kazi cha Maafisa Utamaduni nchini. Pia itaendelea kuandaa makongamano ya Kimataifa na safari hii itaandaa kongamano la pili la kimataifa la Kiswahili nchini Ufaransa na kufanya usanifishaji mkubwa wa msamiati wa kiswahili kufanya utafiti unaolenga kuongeza maneno milioni 50 katika Kongoo ya Kiswahili ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia kupitia BAKITA imepanga kufungua vituo vya kimkakati vya kufundisha Kiswahili kwa wageni ambavyo vitasimamiwa moja kwa moja na waambata lugha kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano

wa Afrika Mashariki; kuendesha mafunzo kwa wakalimani; kuandaa atlasi ya lahaja za Kiswahili na kusambaza Kamusi ya Kiswahili kwa Shule za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Ukombozi wa Bara la Afrika kutaratibu ujenzi wa kituo kikuu cha urithi wa ukombozi na kukarabati maeneo ya urithi wa ukombozi wa Afrika yaliyomo nchini; kuratibu ziara kwenye maeneo yenye kumbukumbu za historia ya ukombozi wa Afrika kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa urithi wa ukombozi wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Sanaa; ili kuendesha sekta hii pamoja na taasisi zake zinazosimamiwa, imejipanga kutekeleza majukumu ambayo yameainishwa katika ukurasa wa 121 mpaka 125 ya hotuba yangu. Hii ni pamoja na kuratibu maandalizi ya Mkakati wa Miaka Kumi wa Maendeleo ya Sekta ya Sanaa Tanzania ambao utaweka dira ya maendeleo ya sekta ya sanaa nchini. Kuratibu maandalizi ya ujenzi wa vituo vya sanaa katika mikoa 26 ya Tanzania Bara; kulinda na kukuza sanaa ya kipekee ya Kitanzania ya ubunifu ikijumuisha mtindo wa Tingatinga, Muziki wa Singeli na Vinyago vya Kimakonde.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Bodi ya Filamu itafanya mapitio ya Sheria ya Filamu pamoja na kanuni zake ili kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya ukuaji wa maendeleo ya shughuli za filamu na michezo ya kuigiza. Hiyo ni pamoja Wizara kupitia BASATA itaratibu ujenzi wa *National Art Gallery*, Jijini Dodoma. Vilevile itaandaa Atlasi ya Vyombo vya Muziki wa Kiasili kutoka kwenye makundi yote ya kikabila ya Tanzania, pamoja na kuratibu matukio na Tuzo za Muziki Tanzania ili kutambua mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *COSOTA* itasimamia kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha katika makundi ya sanaa na uandishi; kupambana na uharamia wa kazi za wabunifu; kukusanya na kugawa mirabaha kwenye maeneo ambayo hakuna kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia TaSUBa Wizara itaratibu Tamasha la 44 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo;

Kadhalika, kama nilivyoeleza itaanza kozi mpya katika ualimu wa muziki *(Music Education)* na Ualimu wa Sanaa za Ufundi *(Visual Arts Education*) ili kuweza kuandaa walimu wa kufundisha masomo katika fani kuu ya elimu ya amali katika Sanaa Bunifu *(Creative Arts)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa majukumu yatakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 ni pamoja na kuendelea na programu ya mafunzo ya urasimishaji wa kazi za utamaduni na sanaa ambapo wasanii 15,000 wanategemewa kufikiwa. Aidha, Mfuko utaendelea na utoaji wa mikopo kwa wadau wa utamaduni na sanaa waliokidhi vigezo. Kwenye Sekta ya Michezo maelezo yamo kwenye ukurasa wa 126 mpaka 127.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Sekta ya Michezo ni pamoja na kuratibu maandalizi ya *CHAN 2024* na *AFCON* 2027; Kuratibu michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA; pia kuratibu shughuli za Sekretarieti ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV; pamoja na kusimamia uanzishwaji wa chombo cha kusimamia miundombinu ya michezo nchini; pia kusimamia ujenzi wa viwanja vyote unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itagharamia Timu za Taifa 15 kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa. Pia katika mwaka wa fedha ujao yaani 2025/2026, Chuo cha Maendeleo ya Michezo kimepangiwa kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanachuo wapatao 500 kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau wa michezo wapatao 640; kuongeza programu zinazotolewa chuoni hapo kutoka programu tatu hadi sita ikiwamo programu ya uandishi wa habari za michezo, utalii katika michezo na elimu ya masoko ya bidhaa na huduma za michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maendeleo; miradi itakayotekelezwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, inajumuisha Mradi wa Habari kwa Umma, Mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa *TBC*, Mradi wa Ufungaji wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji, Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, Ujenzi wa Jumba Changamani la Filamu (*Film Studio*), Mradi wa Kuimarisha BAKITA

na Kukibidhaisha Kiswahili, Ujenzi wa Akademia ya Michezo Malya, Ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Arusha na Dodoma, Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi (*Recreational Centre*), Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalum za Michezo, Mfuko wa Maendeleo ya Michezo; na Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani na hitimisho; kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2024/2025 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali, taasisi za fedha, vyombo vya habari, Taasisi za hiari Zisizokuwa za Kiserikali na Mashirika ya Kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wasanii, wanamichezo, waandishi wa habari na wananchi kwa ujumla wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wadau siyo rahisi kuwataja wote kwa majina, nitawataja wachache nikianza na wadau wa ndani, ambao ni Kampuni za Azam *Media*; *Multichoice* Tanzania; *Airtel* Tanzania; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* na Benki ya *NMB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni *Tanzania National Parks (TANAPA);* Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro *(NCA);* Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA);* Benki ya *CRDB*; Benki ya *NBC*; Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF);* na Makumbusho ya Taifa. Aidha, wadau wengine ni pamoja na Shirika la Bima la Taifa *(NIC);* Wakala wa Serikali Mtandao *(eGA)*; Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha *(AICC);* Shirika la *Culture and Development East Africa (CDEA);* Taasisi ya *Global Opportunity Youth Network (GOYN);* Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA);* Kampuni ya *Startimes*; Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS);* Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF);* Vituo vya Redio vya *Clouds Media Group, EFM*; Wasafi na *Crown Fm*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wadau wa nje, ninaomba nianze na Balozi zote za Tanzania katika mataifa

mbalimbali, Serikali ya Mji wa Busan nchini Korea ya Kusini; Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea *(KOICA)*; *Bagamoyo Friendship Society* (Ujerumani); *Musicians for a Better Life* (Ujerumani); Kituo cha Sanaa na Utamaduni cha *Alliance Francaise*; Wamiliki wa Kampuni za Emirates; Jamhuri ya Watu wa China na Umoja wa Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nitumie fursa hii kuishukuru familia yangu, hususan mke wangu mpendwa Dkt. Amina Mathew Mwaigusia Kabudi na watoto wetu wapendwa Daktari Tumaini Mwendile Kabudi na Bwana Aidan Imani Kabudi. Wamekuwa nguzo imara ya faraja, matumaini na furaha kwangu. Wamenipa nguvu ya kuendelea mbele kila siku, hata nyakati ambazo changamoto zimekuwa nyingi katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kazi. Kwa mapenzi yao na uvumilivu wao, nimeweza kutekeleza majukumu yangu kwa mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inapatikana kwenye Tovuti ya Wizara ambayo ni *www.michezo.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, ninaomba Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yenye jumla ya shilingi 519,660,073,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo, mishahara ni shilingi 33,403,813,000; matumizi mengineyo ni shilingi 28,065,472,000 na miradi ya maendeleo ni shilingi 458,190,778,000.

**7 MEI, 2025**

**HOTUBA YA MHE. PROF. PALAMAGAMBA JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI (MB), WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Bunge lako Tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96) kwa mwaka wa Fedha 2025/26.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu kwa kuturuzuku uhai, kuendelea kutupatia afya njema na kutuwezesha kukutana tena siku ya leo kujadili ustawi wa sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo. Tunayo kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuijalia nchi yetu amani, usalama, utulivu, mshikamano na upendo. Tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu atuongoze katika kujadili Hotuba hii ya bajeti kwa nia njema ya kuhakikisha Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zinakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kwa kuniteua kuwa Waziri wa Wizara muhimu na nyeti ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hii ni heshima kubwa sana kwangu na naichukulia kama chachu ya kuendelea kulitumikia taifa hili kwa bidii, weledi na uadilifu mkubwa.

4. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara hii ni mhimili muhimu sana kwa maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, ambayo kwa maneno mengine naweza kusema ni Wizara yenye nguvu

shawishi (***soft power***) ya nchi inayobeba mtima wa Taifa letu na kuitanabaisha katika kaumu ya Mataifa. Pia, Wizara hii ndiyo inayolinda mtima wa Taifa hili. Sekta ya habari imekuwa na mchango mkubwa katika kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa muhimu zinazowawezesha kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha, utamaduni wetu ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Hivyo, kupitia sekta ya utamaduni Serikali imeendelea kujenga uzalendo, kuhifadhi mila na desturi pamoja na maadili ya Mtanzania.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa sekta ya sanaa, imekuwa na nafasi kubwa katika uzalishaji wa ajira hususan kwa vijana. Aidha, wasanii wetu wameendelea kuwa mabalozi wa nchi yetu ndani na nje ya mipaka yetu. Michezo nayo ni kiungo muhimu katika kujenga fahari ya maendeleo ya Taifa letu. Michezo siyo burudani tu, bali pia ni nyenzo ya kuimarisha afya, umoja na mshikamano wa taifa na ni chanzo cha ajira kwa vijana wetu.

**6.** ***Mheshimiwa Spika***, *mwenye macho haambiwi tazama*! Kwa heshima kubwa naomba nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake kubwa na za dhati katika kuendeleza sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo. Katika kipindi cha miaka minne (4) ya Serikali ya Awamu ya Sita (6) mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Sekta hizi yametokana na uongozi wake mahiri, wenye weledi, umakini na upeo mkubwa unaoendelea kulishamirisha Taifa letu ndani na nje ya nchi. Sisi na wadau wetu wote wa sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo tunamwahidi kuendelea kumtii, kuchapa kazi kwa bidii na kwa weledi ili kutimiza fikra na maono yake kwa nchi yetu.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia uongozi wake madhubuti tumeona mabadiliko makubwa katika Sekta ya Habari ambapo vyombo vya habari vimeendelea kupata mazingira wezeshi ya kufanya kazi kwa uhuru na uwazi, huku vikizingatia weledi na maadili ya taaluma ya habari. Aidha, katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt.

Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) limepata mafanikio makubwa ya kujivunia. Mafanikio hayo yamejidhihirisha katika nyanja za habari, utangazaji, mifumo, rasilimaliwatu, upanuzi wa usikivu na ujenzi wa makao Makuu ya TBC jijini Dodoma. Aidha, mafanikio mengine ni pamoja na uanzishwaji wa chaneli za kimkakati, uboreshaji wa maslahi ya watumishi na upelekaji wa habari za nchi kimataifa. Hivyo, TBC imetimiza lengo kuu la kuitangaza nchi kimataifa pamoja na kukuza lugha adhimu na aushi ya Kiswahili, utalii na utamaduni wa Mtanzania.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia nimshukuru na nimpongeze **Mheshimiwa Rais** kwa namna alivyo mstari wa mbele katika kuchochea ukuaji wa Sekta ya Michezo. **Mheshimiwa Rais** amekuwa akihamashisha timu zetu za Taifa na vilabu vyetu kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa kwa kutoa motisha kwa kila goli linalofungwa katika mashindano ya kimataifa. Kwa mantiki hiyo, mchango wa **Mheshimiwa Rais** ndiyo chachu ya mafanikio ya timu zetu za Taifa na vilabu vyetu katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ambapo kwa mara ya kwanza, baada ya miaka 30 jumla ya timu Sita (6) za Taifa zimeweza kufuzu katika mashindano makubwa. Kutokana na mchango huu wa **Mheshimiwa Rais** Tanzania imekuwa mwenyeji wa Fainali zaMashindano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN 2024) na Fainali za Mashindano ya Mpira wa Miguu za Mataifa ya Afrika (AFCON 2027). Aidha, timu ya Taifa ya wanawake imefuzu katika mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika la Wanawake la CAF (WAFCON) yatakayofanyika nchini Morocco mwaka 2025 na timu ya Taifa ya vijana chini ya umri wa miaka 17 (Serengeti Boys) imefuzu kucheza Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Vijana (AFCON U-17) za mwaka 2025. Vilevile, timu ya vijana wa umri wa chini ya miaka 20 imefuzu mashindano ya AFCON 2025 na timu ya Taifa ya mpira wa miguu imefanikiwa kufuzu katika mashindano ya AFCON 2024. Pia, timu ya Taifa ya Wanawake ya Futsal imefanikiwa kufuzu katika fainali za AFCON *(Women's Futsal Cup of Nations 2025)* pamoja na kukata tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia 2025.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** *angurumapo simba mcheza nani?* Nitumie fursa hii kuipongeza kilabu ya Simba kwa mafaniko

makubwa waliyoyapata kwa kufanikiwa kufika katika hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Mafanikio haya si tu yanatoa heshima kwa kilabu hiyo, bali pia yanaitangaza nchi yetu katika ramani ya soka la kimataifa. Kupitia mafanikio haya, Simba, imeweza kushika nafasi ya nne kati ya vilabu bora barani Afrika jambo ambalo ni fahari kwa nchi yetu. Aidha, huu ni ushahidi tosha kuwa sekta ya michezo ikipewa kipaumbele na uongozi wa juu wa nchi, inaweza kuwa injini muhimu ya maendeleo ya taifa letu. Pia, nitoe pongezi kwa Mwanariadha mashuhuri na shupavu **Alphonce Felix Simbu** ambaye hivi karibuni aliipeperusha vema bendera ya Tanzania kimataifa kwa kushika nafasi ya pili katika Mashindano ya Mbio za Boston zilizofanyika nchini Marekani tarehe 21 Aprili 2025. Ushindi wake umeitangaza nchi yetu katika tasnia ya michezo Ulimwenguni.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yetu imekuwa na uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya michezo ikiwamo ujenzi wa viwanja vya mpira wa miguu katika Jiji la Arusha na Dodoma, ujenzi wa Akademi ya Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na ujenzi wa vituo vya michezo na kupumzikia wananchi.

**11.** ***Mheshimiwa Spika*****,** pia nitumie nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Rais** kwa kuendelea kuwa bega kwa bega na wasanii wetu kwa kuweka mazingira wezeshi katika maendeleo ya sanaa nchini ambapo wasanii wetu wameendelea kupatiwa mitaji kwa ajili ya kuboresha kazi zao za sanaa. Katika uongozi wake **Mheshimiwa Rais** amefufua Mfuko wa Utamaduni na Sanaa uliokuwa umekufa kwa zaidi ya miaka 10 na kwa kipindi kifupi, jumla ya miradi 359 ya utamaduni na sanaa imepatiwa mikopo yenye jumla ya thamani ya Shilingi **5,250,070,500**. Aidha, **Mheshimiwa Rais** amekuwa mshiriki wa moja kwa moja katika matukio na shughuli mbalimbali za Sekta zetu, ikiwamo ushiriki wake kama mgeni rasmi katika Tuzo za Ucheshi Tanzania (Tanzania Comedy Awards) zilizofanyika tarehe 22 Februari 2025 na Tamasha la Utamaduni lililofanyika mkoani Ruvuma, tarehe 20 hadi 23 Septemba 2024. Hatua hizi zimeongeza hamasa kwa vijana kujiajiri kupitia sanaa na pia imeendelea kuvutia wadau kuwekeza katika Sekta hii. Hakika **Mheshimiwa Rais** anastahili

shukurani na pongezi. Hivi sasa amezibadilisha sekta hizi kuwa fursa ya ajira kwa vijana nchini.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, ninawapongeza sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa katika kumsadia Mheshimiwa Rais. Viongozi hawa wamekuwa chachu na msaada kwa Mheshimiwa Rais kwa kutupatia maelekezo pamoja na ushauri uliosaidia kuboresha sekta hizi. Ninawashukuru na kuwapongeza sana.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** nizidi kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba ya Bajeti yake iliyotoa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2024/25 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2025/26. Pamoja na masuala mengine Hotuba hiyo imetoa maelezo kuhusu Sekta zilizo chini ya Wizara. Wizara yangu inaahidi kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa.

**14.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kipekee naomba nikupongeze wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzani kwa kuliongoza kwa busara na weledi Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelekezo na miongozo yako imekuwa msingi wa ufanisi mkubwa wa Bunge katika kuisimamia Serikali kutekeleza vema majukumu yake. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia na kukushauri vema katika majukumu yako ya kuliongoza Bunge. Nawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.) na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.) kwa kusimamia vema na kwa ustadi mkubwa mijadala ya kibajeti katika Bunge lako Tukufu.

**15. *Mheshimiwa Spika,*** *ukiona vyaelea ujue vimeundwa!* Naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa, Husna Juma Sekiboko (Mb.), na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wote wa Kamati kwa maelekezo, ushauri, michango na maoni yao kwa Wizara yangu ambayo yametusaidia sana katika kuboresha utendaji kazi. Maelekezo yao yamesaidia kwa kiwango kikubwa katika uwasilishaji wa hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Kamati hii imekuwa nguzo muhimu katika usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa bajeti na ukaguzi wa miradi, ambapo imefanikisha kuhakikisha rasilimali za umma zinatumiwa kwa ufanisi na kwa manufaa ya umma. Kama misingi ya nyumba imara inavyowekwa kwa ustawi wa jengo, ndivyo uongozi wa Kamati hii ulivyojenga msingi madhubuti wa maendeleo, unaoleta mafanikio endelevu na mabadiliko chanya katika jamii yetu. Wizara itaendelea kuzingatia ushauri, maoni, mapendekezo na maelekezo yanayotolewa na Kamati kwa maendeleo ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2025/26.

**16. *Mheshimiwa Spika***, pia, nitumie fursa hii kuwashukuru waheshimiwa wabunge wote kwa maoni, ushauri na maelekezo ambayo yamekuwa yakiisaidia Wizara kuboresha vipaumbele, mikakati yake na pia kuweka msingi imara wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ufanisi zaidi.

**17. *Mheshimiwa Spika,*** *kinga na kinga ndipo moto uwakapo!* Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi chote hiki ni kutokana na ushirikiano mzuri miongoni mwa wadau wa Wizara wakiwamo viongozi na watumishi wa Wizara. Natambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu wa Wizara wakati wa kufanikisha utekelezaji wa majukumu na mageuzi makubwa tunayoendelea nayo wizarani na katika sekta zetu. Nianze kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nimshukuru Bw. Gerson Msigwa, Katibu Mkuu; Bw. Methusela Ntonda, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi

zilizo chini ya Wizara na watumishi wote wanaofanya kazi kwa bidii na wanaohakikisha mipango ya Wizara inatekelezwa kama ilivyopangwa. Rai yangu ni kuwa tuendeleze ushirikiano huu kwani *kwa pamoja twaweza, tukitengana twaanguka*.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, niwashukuru Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ikiwa ni pamoja na mashirikisho, vyama, vilabu na kila mdau kwa nafasi yake katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kuhakikisha Sekta hizi zinakua na kufanikisha malengo yaliyokusudiwa kwa mujibu wa Sera.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, naomba kutumia nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi (CCM) kupitia Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama uliofanyika tarehe 19 Februari 2025, kwa hatua ya busara na ya kizalendo ya kumpitisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea wa kiti cha Urais kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika baadaye mwaka huu. Uamuzi huu unaakisi imani kubwa waliyonayo Watanzania kupitia chama chao, kwa uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa muda mfupi amethibitisha kuwa ni kiongozi shupavu, makini, jasiri, na mwenye maono mapana kwa maendeleo ya Taifa letu. Bila shaka, hatua hii itamwezesha kukamilisha kwa mafanikio makubwa, ahadi, mipango na mikakati yote aliyoianzisha, na bila shaka, atayatekeleza kwa kishindo, kwa sababu Tanzania iko kwenye mikono salama. Kama wasemavyo wahenga, *palipo na nia, pana njia*, na kwa uongozi wa Dkt. Samia, tumeona njia hizo zikifunguliwa kwa vitendo, kwa ustawi wa Watanzania wote.

**20.** ***Mheshimiwa Spika***, tunapoingia katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, CCM tayari tumekamilisha na tunasema **"Kazi na Utu, Tunasonga Mbele"**. **Mitano tena kwa Mama Samia!** Watanzania tusidanganyike wala tusihadaike, wale wengine wameanza kugawana fito, tumaini pekee limebaki kwa CCM chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Jemedari wetu.

**21.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kupitishwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar. Uteuzi huu ni

ishara ya kuthamini kazi nzuri aliyofanya na imani kubwa ya wananchi wa Zanzibar. Vilevile, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea Mwenza katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Huu ni muunganiko wenye nguvu, uzoefu, na uwakilishi bora wa Watanzania wote.

**22. *Mheshimiwa Spika*,** *mwenda tezi na omo marejeo ngamani!* Ninawashukuru wapiga kura wangu wananchi wa Jimbo la Kilosa kwa kuniamini na kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu; na wakati wa kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazokabili jimbo letu la Kilosa. Ushirikiano wenu, moyo wa uzalendo, na utayari wenu ni nguzo kuu katika mafanikio makubwa tunayoyashuhudia yaliyobadilisha jimbo letu la Kilosa kuwa na miradi lukuki katika sekta zote. Naomba waendelee kuniamini kwani kama wasemavyo wahenga, "*mwana hasahau mkono uliomlea,*" nitaendelea kuwa mtumishi wao mwaminifu.

**23. *Mheshimiwa Spika*,** ni masikitiko yetu kwamba katika kipindi hiki Bunge lako Tukufu lilipatwa na msiba wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, aliyekuwa Mbunge mwenzetu akiwawakilisha wananchi wa Jimbo la Kigamboni ambaye pia alikuwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa Kanda ya Afrika. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile atakumbukwa kama kiongozi shupavu aliyewakilisha Tanzania kwa heshima katika majukwaa ya kitaifa na kimataifa na upande wa michezo hasa kwa kuzingatia kuwa alikuwa mwanamichezo mahiri na shabiki kindakindaki wa klabu ya Simba. Kwa niaba ya Wizara na wadau wetu, tunatoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, familia ya marehemu, ndugu, jamaa na marafiki na wananchi wote wa Jimbo la Kigamboni. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

**24. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Taifa letu pia limepoteza wadau mahiri na wa kutegemewa katika sekta zetu, wakiwamo wanahabari, wanamichezo, wanautamaduni na wasanii mbalimbali. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia za marehemu wote, ndugu, jamaa, marafiki na kwa Watanzania wote kwa ujumla kwa

kuwapoteza wapendwa wao. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azipokee roho za marehemu wote na kuzilaza mahali pema peponi. Amina.

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui na maelekezo ya Hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2024/25 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2025/26 aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 9 Aprili 2025. Aidha, hotuba hii imezingatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili 2021; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 - 2025); Mpango Mkakati wa Wizara (2021/22 - 2025/26); na sera, sheria na miongozo mbalimbali ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na maelekezo mbalimbali ya viongozi wakuu wa Serikali.

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, hotuba yangu imegawanyika katika sehemu nane: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima, Majukumu, Misingi ya Mwelekeo, na Vipaumbele vya Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Kipindi cha Mwaka 2024/25 na Sehemu ya Nne inabainisha changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2025/26; Sehemu ya Sita ni Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2025/26; Sehemu ya Saba ni Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2025/26; na Sehemu ya Nane ni Shukurani na Hitimisho.

## 2.0 DIRA, DHIMA, MAJUKUMU, MISINGI YA MWELEKEO NA VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, Dira ya Wizara ni "*Kuwa na Taifa linalohabarishwa kikamilifu, linaloshamirika kiutamaduni, lenye kazi bora za sanaa na lenye umahiri katika michezo*" na dhima ni **"***Kuendeleza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji*

*stahiki wa habari, kukuza utamaduni, sanaa na michezo kwa lengo la kuleta maendeleo ya jamii kiuchumi.”*

**28. *Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia Dira ya Wizara, majukumu ya Wizara ni pamoja na: kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango, Miradi na Programu mbalimbali katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuendeleza shughuli za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na kusimamia shughuli za filamu na michezo ya kuigiza. Majukumu mengine ni kuimarisha utendaji na Rasilimaliwatu Wizarani na kusimamia utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kampuni ya Magazeti Tanzania (TSN), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Vilevile, Wizara inaratibu na kusimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, Bodi ya Ithibati Tanzania na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

**29. *Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza na kuimarisha utendaji kazi, Wizara inaongozwa na misingi mitano (5) ya kimkakati na kimageuzi ambayo ni Kuwafikia Wadau *(Outreach Programmes)*; Mageuzi ya Taasisi *(Institutional Reforms)*; Utawala Bora *(Good Governance)*; Ujenzi wa Miundombinu *(Infrastructure Development)*; na Utafutaji wa Rasilimali *(Resources Mobilization)*.

**30. *Mheshimiwa Spika,*** chini ya misingi hiyo, katika mwaka 2025/26 Wizara imejipanga kutekeleza maeneo mbalimbali ya kipaumbele. Maeneo hayo ni pamoja na kukarabati, kuboresha, kujenga na kutunza miundombinu katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuendelea na maandalizi ya CHAN 2024 na AFCON 2027; kukamilisha kutunga na kuhuisha Sera, Sheria, mikakati, miongozo na kanuni mbalimbali katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji katika sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa; kuweka na kuboresha mazingira wezeshi na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza na kuendeleza sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na kuratibu,

kuendesha na kusimamia matamasha, shughuli na matukio makubwa ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**31.** ***Mheshimiwa Spika*****,** maeneo mengine ni kuziimarisha na kuziongezea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kusimamia na kutekeleza majukumu ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuimarisha ushirikiano na Wizara nyingine katika utendaji kazi hususan zile zinazohusika na masuala ya Kazi na Ajira, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Elimu, Afya, Maliasili na Utalii, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ikiwamo Sekta Binafsi katika maendeleo kwa kufadhili na kusukuma mbele gurudumu la Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2024/25

### 3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

#### 3.1.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25 Wizara ilikadiria kukusanya Shilingi Bilioni Moja Milioni Mia Nne Thelathini na Elfu Tatu (Shilingi 1,430,003,000) kutoka kwenye vyanzo saba (7) ambavyo ni mapato yatokanayo na viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, ada za mafunzo na mitihani kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, vitambulisho vya waandishi wa habari, machapisho ya picha, mabango na majarida, usajili wa magazeti na ada ya mwaka ya magazeti. Hadi kufika mwezi Aprili 2025 Shilingi Milioni Mia Sita Ishirini Na Nne Mia Nane Sitini na Moja Elfu na Mia Mbili Kumi na Mbili (Shilingi 624,861,212), sawa na asilimia 43.6 ya lengo la mwaka zilikuwa zimekusanywa. Miongoni mwa sababu za kutofikia lengo ni pamoja na kusimama kwa matukio ya michezo ya Ligi Kuu kutokana na kuwapo kwa ukarabati mkubwa wa viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru jijini Dar es Salaam uliosababisha kufungwa kwa viwanja husika.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo ya mapato ikiwamo kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu katika uwanja, ili kuwezesha kuvutia mashabiki wengi zaidi; kuongeza hamasa katika michezo ikiwamo zawadi mbalimbali kwa washindi ili kuhamasisha matokeo mazuri yatakayochochea ushabiki na hatimaye mapato.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni Shilingi Bilioni Thelathini na Nane, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tisa, Mia Sita Sabini na Tatu Elfu (Shilingi 38,259,673,000), ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2025, Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Moja Arobaini na Nne, Ishirini na Tano Elfu, Mia Tatu Sabini na Nane na Senti Tisini na Nne (Shilingi 17,144,025,378.94), sawa na asilimia 44.8 ya lengo zilikuwa zimekusanywa. Miongoni mwa sababu zilizochangia kutofikiwa kwa malengo ni kutokana na baadhi ya taasisi za serikali kushindwa kulipa kwa wakati huduma za matangazo zilizotolewa na taasisi zilizo chini ya Wizara ikiwamo TSN. Fauka ya hayo, kwa upande wa vyuo, moja ya sababu ni wanavyuo kutokulipa ada kwa wakati kutokana na changamoto mbalimbali.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi inaendelea kutoa elimu kwa wadau na kufanya kampeni mbalimbali ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo. Kampeni hizo ni pamoja na kuhamasisha usajili na kufuata taratibu za uzalishaji na usambazaji wa kazi za sanaa; kuongeza kasi ya kuibua vyanzo vipya vya mapato kwa taasisi; utekelezaji wa mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura ya 218 na kuhamasisha wanavyuo kulipa ada kwa wakati.

### 3.1.2 Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara iliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya Shilingi Bilioni Mia Mbili Themanini na Tano, Milioni Mia Tatu Kumi na Nane na Mia Tatu Themanini na Saba Elfu (Shilingi 285,318,387,000). Kati ya fedha hizo, Mishahara ni Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Mbili

Themanini na Mia Moja Kumi na Sita Elfu (Shilingi 11,280,116,000), Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Nane Arobaini na Saba, Mia Nne Themanini na Tatu Elfu (Shilingi 15,847,483,000) na Miradi ya Maendeleo ni Shilingi Bilioni Mia Mbili Hamsini na Nane, Milioni Mia Moja Tisini na Mia Saba Themanini na Nane Elfu (Shilingi 258,190,788,000).

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, wakati Wizara ikiwa katika utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya mabadiliko ya kimuundo kwa kuihamisha Idara ya Habari (MAELEZO) kutoka kwa iliyokuwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwenda katika iliyokuwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, hivyo kuunda Wizara mpya ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mabadiliko haya yaliongeza majukumu ya Wizara pamoja na bajeti ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muktadha huo, hadi kufikia mwezi Aprili 2025 bajeti ya mwaka 2024/25 imeongezeka na kufikia Shilingi Bilioni Mia Tatu na Kumi, Milioni Mia Tisa na Nane, Mia Tano Themanini na Tisa Elfu na Mia Tano Sitini na Saba na Senti Sabini na Nne (Shilingi 310,908,589,567.74), ikiwa ni ongezeko la Shilingi Bilioni Ishirini na Tano, Milioni Mia Tano Tisini, Mia Mbili na Mbili Elfu na Mia Tano Sitini na Saba na Senti Sabini na Nne (Shilingi 25,590,202,567.74). Hadi Aprili, 2025 Wizara imepokea na kutumia jumla ya Shilingi Bilioni Mia Mbili Sitini na Moja, Milioni Mia Sita Sabini, Mia Tatu Ishirini na Mbili Elfu, Mia Sita na Kumi na Senti Themanini na Tisa (Shilingi 261,670,322,610.89), sawa na asilimia 84.2 ya bajeti yote iliyotengwa mwaka wa fedha 2024/25. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Nane Sitini na Tisa, Mia Tano Thelathini na Tano Elfu, Mia Nne na Saba na Senti Hamsini na Moja (Shilingi 12,869,535,407.51) ni Mishahara, sawa na asilimia 56.0 ya bajeti ya mishahara; Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Mia Nane Ishirini na Tatu, Mia Sita Hamsini na Nne Elfu na Mia Sita Tisini na Mbili na Senti Themanini na Moja (Shilingi 21,823,654,692.81) ni Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia 81.4 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo; na jumla ya Shilingi Bilioni Mia Mbili Ishirini na Sita, Milioni Mia Tisa Sabini na Saba, Mia Moja Thelathini na Mbili Elfu, Mia Tano na Kumi na Senti Hamsini na Saba

(Shilingi 226,977,132,510.57) ni Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 86.9 ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

## 3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25

### 3.2.1 SEKTA YA HABARI

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, Majukumu ya Sekta ya Habari ni pamoja na kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003; Sheria ya Huduma za Habari Sura ya 229 ya mwaka 2016 na kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati, programu na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo. Wizara kupitia sekta hii imetekeleza majukumu yafuatayo:

#### 3.2.1.1 IDARA YA HABARI

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, Sheria ya Huduma za Habari Sura ya 229 inaelekeza uundwaji wa Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa tayari Bodi hiyo imekwishaundwa na ilizinduliwa rasmi tarehe 3 Machi 2025 na kuanza kufanya kazi. Bodi hii inaongozwa na mwandishi wa habari mahiri na mkongwe kwenye tasnia ya habari, Bw. Tido Mhando.

**41.** ***Mheshimiwa Spika***; Wizara kupitia Msemaji Mkuu wa Serikali, imeendelea kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Baadhi ya miradi iliyotolewa taarifa ni pamoja na uzinduzi wa treni ya kisasa ya SGR na maendeleo ya uendeshaji wa treni hiyo; juhudi za Serikali katika kukuza sekta ya utalii; maendeleo ya ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP); maboresho ya utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam baada ya Serikali kuingia mkataba wa uwekezaji; uwekezaji katika maeneo mbalimbali ikiwamo Kongani ya Viwanda na bandari kavu iliyoko Kwala mkoani Pwani, ujenzi wa miundombinu katika Serikali ya Awamu ya Sita. Aidha, mbali na Msemaji Mkuu wa Serikali kuelezea kuhusu mafanikio katika utekelezaji wa miradi, pia amekuwa akitoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayoendelea nchini na kuratibu mawasiliano wakati wa majanga mbalimbali. Fauka ya hayo, Wizara kupitia

Msemaji Mkuu wa Serikali imeratibu ziara za waandishi wa habari kwenda kujionea kwa macho miradi inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ziara hizo zimewafanya wapate picha halisi ya utekelezaji wa Serikali na hivyo kupata uelewa wa kutosha na kutoa taarifa sahihi na za uhakika.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa kikamilifu kuhusu Serikali yao, Wizara imechapisha nakala 5,000 za Jarida la NCHI YETU linalohusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka minne. Jarida hili lina taarifa mbalimbali za miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa tangu Mheshimiwa Rais aingie madarakani hadi mwaka 2025. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO imekusanya zaidi ya habari 10,000 kuhusu utekelezaji wa Serikali na kuzisambaza kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu na kuandaa mkutano wa mwaka wa Maafisa Habari, Uhusiano na Mawasiliano wa Serikali. Mkutano huo uliofanyika Unguja, Zanzibar kuanzia tarehe 3 Aprili 2025 uliwakutanisha Maafisa Habari zaidi ya 500. Katika mkutano huo walijadili masuala mbalimbali ya utendaji kazi na kujengewa uwezo wa namna bora ya kuboresha utoaji wa taarifa za Serikali, changamoto za mabadiliko ya kiteknolojia katika utoaji wa taarifa na kuimarisha mawasiliano kati ya wananchi na Serikali yao.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kuratibu vyombo vya habari katika matukio na mikutano mbalimbali ya kitaifa, mikutano ya kimataifa inayofanyika nchini pamoja na ziara za viongozi ili kuhakikisha vyombo vya habari vinashiriki kikamilifu katika utoaji wa taarifa kwa wananchi.

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeratibu jumla ya taasisi za Serikali 35 kukutana na vyombo vya habari kuelezea mafanikio ya

utekelezaji wa Serikali kupitia taasisi hizo na kutoa mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/26. Programu hii imekuwa na mafanikio makubwa kwani wananchi wameweza kuelewa mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 3.2.1.2 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) lilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 186 la mwaka 2007. Shirika hili lilianzishwa chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma. Sasa TBC imehuishwa na kuanzishwa upya kisheria na Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania Na. 3 ya mwaka 2025. Majukumu ya TBC ni kutoa huduma ya utangazaji kwa kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha. Shirika limetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

### Upanuzi wa Usikivu

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kuhabarisha umma inafikiwa kikamilifu TBC imeendelea kutekeleza miradi ya upanuzi wa usikivu wa redio katika maeneo zaidi ya 29 nchini. Hadi Aprili, 2025 miradi iliyokamilika ni katika eneo la Mwanzi, Wilaya ya Manyoni, Singida (Kilowati 1) na katika eneo la Nyololo, Wilaya ya Mufindi, Iringa (Kilowati 1). Wakati huohuo, ujenzi wa majengo na ufungaji wa mitambo ya kurushia matangazo ya redio unaendelea katika wilaya za Kalambo (Rukwa), Liwale (Lindi), Rufiji (Pwani), Kakonko (Kigoma), Kaliua na Igunga (Tabora) na Karatu (Manyara) na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni 2025.

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC pia imekamilisha ununuzi wa mitambo ya kurushia matangazo ya redio (transmitter) kwa ajili ya wilaya 12 za: Mpwapwa (Dodoma), Tanganyika (Katavi), Gairo (Morogoro), Hanang (Manyara), Siha (Kilimanjaro), Kasulu (Kigoma), Mbulu (Manyara), Kondoa (Dodoma), Kilindi (Tanga), Iramba (Singida), Kilolo (Iringa) na Mahenge (Morogoro). Ujenzi wa majengo na ufungaji wa mitambo katika vituo hivyo unatarajiwa kukamilika Juni 2025.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC imefanya maboresho katika vituo vyake vya redio vya Mabungo (Moshi), Themi Hill (Arusha), Geita, Iringa, Mnyuzi (Tanga) kwa kubadilisha mitambo ya TBC Taifa na Bongo FM pamoja na mifumo ya antena hivyo kuongeza usikivu. Kwa sasa, usikivu wa redio za TBC umefikia Wilaya 139 (asilimia 87) na matarajio ya TBC ni kufikia asilimia 92 Desemba, 2025 baada ya miradi iliyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji itakapokamilika.

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC inaendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa makao makuu ya Shirika eneo la Vikonje, Dodoma ambao unahusisha ujenzi wa jengo la Utawala pamoja na majengo ya studio za redio, televisheni na mitandao ya kijamii. Aidha, awamu ya kwanza (Lot 1) itagharimu Shilingi 54,204,499,116.46. Hadi Aprili 2025, jumla ya shilingi 14,973,158,075.37 zimelipwa. Vilevile, mradi umefikia asilimia 47. Mradi huu ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri Muungano wa Tanzania ya kuzitaka taasisi zake zote zihamishie shughuli zake Jijini Dodoma.

**Maboresho ya Maudhui**

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC katika kutekeleza dhima yake ya kuhabarisha umma imeendelea kuandaa na kurusha vipindi vya kimkakati kwa ajili ya kujenga taswira chanya ya nchi ikiwamo kukuza uzalendo, kulinda utamaduni, kuendeleza tunu za Taifa pamoja na kukuza lugha adhimu ya Kiswahili. Vipindi vilivyoandaliwa kutoka maktaba ni pamoja na "Ndivyo ilivyokuwa" (32), "Mawazo ya kizalendo" (71) na Wosia wa Baba (470). Aidha, vipindi vingine vyenye lengo la kuitangaza nchi kimataifa ni pamoja na "Jicho letu SADC" (30) na "Lulu za Kiswahili" (27). Nitumie fursa hii kupongeza waandaaji wa tamasha la Kiswahili nchini Cuba ambapo TBC ilirusha mbashara matangazo yake pamoja na kuandaa mahojiano katika kipindi chake cha Lulu za Kiswahili.

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC imeanzisha kampeni zinazohamasisha usafi na utunzaji wa mazingira. Kampeni hizo ni ile ya Pika Kijanja inayoendeshwa na chaneli ya Bongo FM ambayo inahusisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Katika

kipindi cha mwezi Julai hadi Machi 2025 jumla ya vipindi saba (7) vilifanyika katika maeneo mbalimbali ya jJiji la Dar es Salaam. Desemba 2024 Bongo FM ilipata heshima ya kuandaa tamasha kubwa Wilayani Ruangwa ikiwa ni sehemu ya Azimio la Kizimkazi ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika tamasha hilo jumla ya mitungi ya gesi 1,000 iligawiwa kwa mama na baba lishe wa Wilaya ya Ruangwa. Bongo FM imejipanga kuipeleka kampeni hii katika kila halmashauri ili wananchi wapate elimu sahihi ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, Mwezi Agosti 2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliipa nguvu Kampeni ya Pika Kijanja kwa kuhamasisha na kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kwenye kipindi hicho, Mheshimiwa Rais alipika chakula kwa kutumia nishati safi. Kipindi hicho kilirushwa mbashara kutokea Ukumbi wa Nkrumah katika Viwanja vya Sabasaba na kuwashirikisha mama na baba lishe zaidi ya 2,000. Kupitia kampeni hii, kufikia Aprili 2025 jumla ya mamalishe na babalishe 5,000 wamefikiwa na jumla ya mitungi ya gesi 3,670 imegawiwa ili kutumika kama nishati mbadala ya kupikia.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** TBC inaendesha kampeni nyingine ya kuhamasisha upandaji wa miti nchi nzima tarehe 27 ya kila mwezi kupitia "Kampeni ya 27 ya Kijani" inayosimamiwa na kipindi cha JAMBO TANZANIA. Kampeni hii ilianza tarehe 27 Januari, 2023 siku ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa ni mwanamazingira namba moja, alifanya mahojiano maalumu na timu ya TBC ikiwa ni kumbukizi ya siku yake ya kuzaliwa. Hadi Aprili 2025 zaidi ya miti milioni 9 imepandwa nchi nzima tangu kampeni hii ianze katika mikoa mbalimbali ikiwamo Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Arusha, Mwanza, Singida, Shinyanga, Simiyu, Manyara, Songwe, Tanga, Tabora pamoja na Zanzibar.



*Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akipanda mti wakati wa kampeni ya mti wa mama (27 ya Kijani) inayoendeshwa na TBC kupitia kipindi cha JAMBO TANZANIA. Tukio hili lilifanyika mjini Unguja (TBC – Digital, 2024).*

**55. *Mheshimiwa Spika***, Kampeni ya Jicho la Mpita Njia ambayo ni mahususi kuhamasisha usafi wa mazingira inatangazwa kupitia kipindi cha ARIDHIO. Kampeni hii kwa sasa imefikia awamu nne (4) katika kipindi cha kati ya mwezi Julai 2024 na mwezi Aprili 2025 ambapo jumla ya makala 180 zimeandaliwa. Kupitia kampeni hii TBC imekuwa ikimulika maeneo yaliyokithiri kwa uchafu na hatimaye kutafuta njia bora za kuondokana na kero hiyo. Matokeo ya kampeni hii ni jamii pamoja na viongozi wa Halmashauri za Wilaya, Jiji na Manispaa kuwa sehemu ya kuunga mkono jitihada za usafi kwenye maeneo yaliyobainishwa na TBC.

**56. *Mheshimiwa Spika*,** TBC imeongeza wigo wa kurusha matangazo mbashara kwa wakati mmoja kwa kutumia *LIVE U*, *Quantum* na *OB Van*. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 TBC ilirusha matangazo mbashara 775 yaliyohusu matukio ya kitaifa na ziara za viongozi yenye thamani ya Shilingi 7,179,494,392.24 na yalitumia jumla ya saa 1,390 na dakika 51. Urushaji mbashara wa matangazo haya umewezesha wananchi kupata habari zinazohusu utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya Serikali. Aidha, TBC imeendelea kuonesha mafanikio ya

Serikali ya Awamu ya Sita, kuibua changamoto zinazowakabili wananchi kupitia vipindi na habari zinazotangazwa pamoja na mafanikio ya Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kimkakati.

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC imeanzisha programu maalumu ya mabadilishano ya maudhui na watendaji na Shirika la Utangazaji la Nigeria (Voice of Nigeria - VON). Kuanzia Julai 5 2024 mwandishi mmoja wa TBC alijiunga na VON kwa kipindi cha miezi sita na mtumishi mmoja kutoka VON anatarajiwa kuja TBC kwa lengo la kujifunza Kiswahili pamoja na kupeleka maudhui katika vyombo vya habari vya VON. Kupitia ushirikiano huu, maudhui ya TBC yamekuwa yakitangazwa katika vyombo vya habari vya VON nchini Nigeria hasa kutangaza lugha adhimu ya Kiswahili.

**58.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC imekamilisha utafiti kuhusu mtazamo wa hadhira na wateja kwa vyombo vyake pamoja na maudhui yanayoandaliwa na kurushwa. Matokeo ya utafiti yanaonesha vyombo vya TBC vinafanya vizuri sokoni kutokana na kuwa na vipindi na maudhui bora. Aidha, watangazaji wa redio, televisheni na mitandao ya kijamii wamekuwa sehemu muhimu katika mafanikio ya TBC katika kuwafikia wasikilizaji, watazamaji na wafuatiliaji wa mitandao ya kijamii. Kupitia utafiti huo, TBC1 na TBC Taifa zinaendelea kuongoza kwa kuwa na maudhui bora yanayopendwa na wananchi. Kutokana na utafiti huo ambao umefanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma - SJMC) vipindi pendwa vya televisheni ni: Aridhio, Jambo Tanzania, Mizani, Zamadamu, na Lulu za Kiswahili na kwa upande wa redio ni: Taarifa ya Habari, Asubuhi hii, Michezo, Jungu Kuu, Wosia wa Baba na Jamvi la Machweo.

**Mafunzo ya kuwajengea umahiri wanahabari**

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC ilitoa mafunzo kwa wanahabari 181 ambapo kati ya hao washiriki 28 walitoka vyombo binafsi vya habari. Mafunzo haya yalilenga kufundisha waandishi wa habari kuhusu namna ya kushiriki katika kuandaa na kutangaza vipindi na matukio yanayohusu chaguzi za Serikali za Mitaa kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Awamu ya kwanza ya mafunzo ilifanyika

tarehe 1 hadi 2 mwezi Oktoba 2024 jijini Dar es Salaam. Washiriki wa mafunzo walikuwa 86 wote wakitokea TBC. Awamu ya pili ya mafunzo ilifanyika tarehe 13 mwezi Novemba 2024 jijini Dodoma. Jumla ya wanahabari 95 walihudhuria ambapo kati ya hao 67 walitoka TBC na 28 walitoka vyombo binafsi vya habari.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, mafunzo mengine yalitolewa kwa wanahabari 327 kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu, 2025 ambapo washiriki 41 walitoka vyombo binafsi, redio jamii na redio zinazomilikiwa na halmashauri. Awamu ya kwanza ya mafunzo ilifanyika tarehe 20 hadi 22 mwezi Machi 2025 mkoani Morogoro. Washiriki wa mafunzo walikuwa 171 ambapo kati ya hao 161 walitoka TBC na wanahabari 10 walitoka vyombo binafsi. Awamu ya pili ya mafunzo ilifanyika tarehe 24 hadi 26 Machi 2025 jijini Dodoma ambapo jumla ya wanahabari 156 walihudhuria, kati ya hao 125 ni waandishi wa habari kutoka TBC na 31 walitoka vyombo binafsi vya habari.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo haya yalilenga kufundisha waandishi wa habari kuhusu namna ya kushiriki katika kuandaa na kutangaza vipindi na matukio yanayohusu uchaguzi kabla, wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu. Vyombo binafsi vya habari vilivyotoa washiriki wa mafunzo kwa awamu zote mbili ni Azam TV, ITV, Channel Ten, TSN, Clouds FM, Zanzibar Leo, Global TV, Wasafi TV, Crown Media na Uhuru Media. Washiriki wengine walitoka Star TV, Dodoma TV, A. FM, Hope Channel, EFM, Full Shangwe, Mwangaza FM na Michuzi Blog. Kwa upande wa redio zinazomilikiwa na halmashauri walishiriki waandishi wa habari kutoka Ruangwa FM, Mpimbwe FM, Mtama FM, City FM, Sengerema FM, Chalinze FM na Newala FM.

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC ilitoa pia mafunzo kwa waandaaji wa vipindi vya elimu kwa umma vya redio, televisheni na mitandao ya kijamii kupitia mikutano ya WASHITIRI ambayo imekuwapo tangu enzi za Redio Tanzania (RTD). Mkutano wa WASHITIRI wa 109 wa mwaka 2025 ulifanyika jijini Mbeya. Jumla ya washiriki 193 walipata mafunzo kuhusu namna bora ya kuandaa vipindi, kuwasiliana kimkakati pamoja na matumizi ya TEHAMA katika kuhabarisha umma. Mkutano huu wa Elimu kwa Umma ulifunguliwa tarehe 17 Februari 2025 na ulifikia kilele tarehe 21

Februari 2025 ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kupitia mkutano huu Makamu wa Rais alikabidhi mitungi ya gesi 2,000 kwa mamalishe na babalishe kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia na utunzaji wa mazingira.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** TBC imefanya maboresho ya kimiundombinu, mifumo na rasilimaliwatu. Katika kipindi hiki watumishi sita (6) wa TBC walipata tuzo za umahiri za uandishi wa habari na utangazaji ndani na nje ya nchi. Tuzo hizi kwa TBC ni ishara wazi kuwa imekuwa na watumishi wenye ushindani katika tasnia ya habari na utangazaji kwa kuandaa vipindi bora vinavyokidhi viwango vya kimataifa.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** TBC imeanzisha chaneli mahususi za kimkakati kwa lengo la kuifikia hadhira ya ndani na nje ya nchi hivyo kuitangaza nchi kimataifa. Katika kipindi hiki TBC imeimarisha chaneli zake kwa lengo la kukidhi dhima ya TBC ikiwamo Tanzania Safari Channel (TSC au Chaneli ya Utalii), ambayo imeendelea kuimarishwa kwa kuandaa maudhui bora yanayohusu utalii na uhifadhi wa mazingira. Katika kipindi hiki jumla ya vipindi 240 vimeandaliwa na kurushwa vikiwa na maudhui mbalimbali. Aidha, Chaneli imetafsiri vipindi 300 katika lugha za Kichina, Kifaransa, Kireno, Kingereza na Kiarabu.

**65.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa utalii wa utamaduni na historia unakidhi mahitaji na maelekezo ya Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TBC imeanzisha mchakato wa kipindi maalumu kitakachoangazia njia ya biashara ya utumwa kuanzia Zanzibar, Bagamoyo, Mamboya, Kilosa, Mpwapwa, Manyoni, Tabora hadi Kigoma (Safari Caravan). Kipindi hiki kitarushwa kupitia vyombo vya TBC ikiwamo chaneli ya Utalii ya Safari. Kupitia kipindi hiki wananchi ndani na nje ya nchi watajifunza njia iliyotumika katika biashara ya utumwa na kitahamasisha utunzaji wa malikale na utamaduni wa Mtanzania. Tayari Tanzania iliashaanza maandalizi ya kuifanya njia hiyo kutambulika kama Urithi wa Dunia kupitia UNESCO.

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa TBC2, katika kipindi hiki watumishi 16 walipata mafunzo kutoka Jamhuri ya Korea kwenye maeneo ya kuhariri, kuandaa maudhui, kupiga picha, kusanifu picha, sauti na ufundi. Aidha, Chaneli ya TBC2 imepokea vifaa na vitendea kazi vya utangazaji vikiwamo *Drone, Microphone, Laptop, Switcher* vyenye thamani ya Shilingi milioni 608 ikiwa ni sehemu ya mradi wa uimarishaji wa chaneli ya vijana ya TBC2 kwa kushirikiana na Jamhuri ya Korea. Vifaa hivi vinaiwezesha TBC2 kuandaa matamasha nje ya studio na kuwafikia vijana wengi zaidi.

**67.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC *digital* imekuwa ni chanzo mahususi cha habari mtandaoni kwa kuhabarisha umma hasa vijana na wapenzi wa habari za mtandaoni. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 wafuasi wa habari mtandaoni wameongezeka kutoka 520,000 hadi 1,800,000 ambapo mitandao ya *Instagram* na *Youtube* imefikisha watazamaji milioni 53.14. Aidha, Chaneli hii imekusanya mapato yanayofikia Shilingi milioni 198 katika kipindi hiki. Pia, kuwapo kwa taarifa ya habari ya Kiingereza kumewezesha kuongeza watazamaji na wafuatiliaji katika majukwaa ya TBC mtandaoni nje ya nchi hivyo kuitangaza nchi kimataifa ambapo habari za Tanzania zimewafikia watu wengi zaidi.

**68.** ***Mheshimiwa Spika***, Bongo FM ni idhaa pendwa ya redio katika kuburudisha na kuelimisha vijana wa rika zote katika jamii kwa kutumia lugha nyepesi ili kuweza kuwasogeza karibu zaidi. Baadhi ya vipindi pendwa vya Bongo FM ni Bao la Asubuhi, Power Bank, Kijora, Fleva, Flyover, Sports Venue, Papaso na Heart Beat. Bongo FM imetimiza mwaka mmoja tarehe 26 Februari 2025 tangu kuzinduliwa kwake. Maboresho yaliyofanyika katika idhaa ya Bongo FM yamewezesha idhaa kuongeza mapato kwa Shirika na ushindani wa kihabari hasa kwa idhaa za vijana hapa nchini.

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imekamilisha utungwaji wa Sheria ya TBC ambayo itakuwa jibu kwa changamoto za TBC hasa kutokuwa na chanzo cha uhakika, endelevu na toshelevu cha mapato. Muswada wa Sheria ya TBC Na. 3 ya mwaka 2025 ulipitishwa na Bunge lako tukufu tarehe 30 Januari 2025 na sasa TBC ina Sheria

yake Na.3 ya Mwaka 2025. Kupitia Sheria hii TBC itakuwa na uwezo wa kuwekeza katika miundombinu ya utangazaji, vipindi, mafunzo na kufanya maboresho ya mara kwa mara ya mifumo ya utangazaji ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

### 3.2.1.3 KAMPUNI YA MAGAZETI YA SERIKALI (TSN)

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ilianzishwa kwa Sheria ya Kampuni Sura ya 212 ikiwa na jukumu la kuelimisha, kuchapa na kusambaza magazeti ya Serikali ambayo kwa sasa ni *Daily News*, *Sunday News*, HabariLEO na SpotiLEO. Aidha, TSN hutoa habari kupitia tovuti na mitandao ya kijamii kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza ikiwamo *Twitter (X), Facebook, Instagram na Youtube*. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Serikali kupitia TSN imefanikiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:

#### Uboreshaji wa Maudhui

**71.** ***Mheshimiwa Spika***, TSN imeuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wakilishi Zanzibar kwa kuandaa makala maalumu zilizosheheni shughuli za Bunge na Baraza la Wawakilishi. Aidha, katika kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, sera, mikakati, miongozo na mipango ya Serikali, TSN ilichapisha jumla ya makala maalumu 432; kati ya makala hizo 194 zilihusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020/25, makala 150 Dira ya Maendeleo ya Taifa, makala 24 Maonesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, makala 12 za maonesho ya kilimo ya Nanenane, Kumbukizi ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, makala 48 kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024, Uhuru wa Tanzania Bara, Maboresho ya Mfumo wa Kodi na fursa za kutangaza na kukuza utalii.

**72.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na mageuzi ya Sayansi na Teknolojia katika sekta ya habari, TSN imefanikiwa kulifikia soko la huduma za habari kidijiti kwa kuanzisha gazeti mtandao (*e-paper*), kuchapisha maudhui katika mitandao ya kijamii na kutoa maudhui ya kidijiti kupitia chaneli ya mkondoni (*Daily News Digital*). Jitihada hizo zimefanikisha kufikia jumla ya wafuasi milioni

80. Kati ya hao tovuti imefuatiliwa na wafuasi milioni 11.1, mitandao ya kijamii wafuasi milioni 42.3, na chaneli ya Youtube wafuasi milioni 26.6.

**Ufungaji wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji**

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, TSN imetekeleza ufungaji wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji. Mradi unahusisha ununuzi wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji, ujenzi wa jengo la kiwanda cha uchapaji, ununuzi wa malighafi za kiwandani na ununuzi wa vitendea kazi ikiwamo magari. Hadi Aprli 2025 utekelezaji wa ujenzi wa jengo la kiwanda cha uchapaji umefikia asilimia 53, ununuzi wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji umefikia asilimia 80 na ununuzi wa vitendea kazi ikiwamo magari umefanyika. Aidha, mpaka kufikia Aprili 2025 TSN imepokea Bilioni 18.2 ambapo mradi huo unategemea kukamilika Septemba 2025.

**74.** ***Mheshimiwa Spika***, TSN katika kuhakikisha habari zinawafikia umma imetekeleza jukumu la kuchapa nakala ngumu za magazeti ya Daily News na HabariLEO ambapo hadi kufikia Aprili 2025 jumla ya nakala za magazeti 1,903,500 zilichapishwa na kusambazwa. Nakala 1,197,000.00 za gazeti la Daily News na nakala 706,500.00 kwa gazeti la HabariLEO. Sambamba na hilo TSN imeendelea kutumia njia ya kidijiti kufikisha habari kwa umma ikiwamo; Gazeti mtandao (*e-Paper*) kwa kuchapa gazeti tepe la Daily News, HabariLEO na SportLEO, Channel ya Online (*Daily News Digital*) na kutumia mitandao ya kijamii.

**3.2.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI**

**75.** ***Mheshimiwa Spika***, utamaduni ndio mtima wa nchi, hakuna Taifa linaloweza kujitambulisha kwa utamaduni wa nchi nyingine. Aidha, Tanzania ni taifa pekee katika Afrika Mashariki na Kati lililofanikiwa kwa kiasi kikubwa kuhimili misukosuko inayotokana na tamaduni za kigeni kwa kudumisha utamaduni wake. Tanzania imefanikiwa kudumisha misingi ya umoja, mshikamano, upendo, amani na utangamano wa kitaifa bila kujali wingi wa jamii tulizonazo.

### 3.2.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya utamaduni imekasimiwa majukumu ya kulinda, kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni wa Taifa ikiwamo lugha, mila, desturi, historia na maadili ya Taifa; kudumisha na kuendeleza utambulisho wa Taifa; kuhimiza na kukuza thamani ya utamaduni wa Taifa kwa wananchi wote hususan watoto na vijana ambao ndio hazina ya Taifa la leo na kesho; kuratibu na kusimamia maendeleo ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi; kuratibu na kufanya tafiti za urithi wa utamaduni usioshikika hususan masimulizi na lugha za kijamii ambazo ni kibebeo kikuu cha urithi wa utamaduni wa Taifa letu. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Utamaduni ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2024 hadi Aprili 2025, Sekta hii imetekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo:

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania wanaendelea kusherehekea, kuenzi, kuthamini na kunufaika na urithi wa utamaduni wao, Wizara iliratibu Tamasha la Tatu la Utamaduni la Kitaifa lililofanyika kuanzia tarehe 20 hadi 23 Septemba 2024 Mkoani Ruvuma. Tamasha hilo lililoongozwa na kaulimbiu, ***"Utamaduni Wetu ni Utu Wetu; Tuuenzi na Kuuendeleza".*** Lengo kuu la Tamasha hilo lilikuwa ni kutoa fursa kwa Watanzania kutambua, kuenzi, kujivunia na kutangaza utajiri anuwai wa urithi wa utamaduni uliopo katika Taifa letu. Katika kilele cha Tamasha hilo, Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tamasha hilo lilifanyika kwa mafanikio makubwa ambapo lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 90,000 wakiwamo viongozi wa Serikali, viongozi wa kimila, viongozi wa kijamii, viongozi wa Chama Tawala na vyama vingine vya kisiasa, pamoja na wananchi.




*Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa na viongozi wa kimila (machifu) katika Tamasha la Utamaduni tarehe 23 Septemba 2024, mjini Songea, Ruvuma***.**

**78.** ***Mheshimiwa Spika***, Tamasha la Utamaduni lilipambwa na shughuli mbalimbali zikiwamo; Mdahalo wa Maadili ya Kitaifa tarehe 14 Septemba 2024 ukijumuisha washiriki 500; mashindano ya ngoma na vyakula vya asili; maonesho ya kazi za sanaa, ubunifu na huduma mbalimbali; burudani za sanaa za maonesho; matembezi ya kiutamaduni; *Songea vibes*, onesho la matumizi mbalimbali ya vazi la kanga katika utamaduni wa Mtanzania ambalo limehudhuriwa na wasanii 200. Vilevile, kulikuwa na mafunzo ya urasimishaji wa kazi za utamaduni na sanaa; mafunzo kuhusu matumizi sanifu na fasaha Kiswahili kwa walimu wa Kiswahili Mkoa wa Ruvuma; mbio za polepole (jogging) na mashindano ya michezo mbalimbali.

**79.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Tamasha hilo, jumla ya vikundi 18 vya ngoma za kiutamaduni kutoka mikoa 17 ya Tanzania Bara na kikundi kimoja (1) kutoka Zanzibar vilishiriki ambapo kila kikundi kilikuwa na washiriki 13 wakiongozwa na Maafisa Utamaduni wa mikoa inayohusika. Aidha, Tamasha hilo

lilishirikisha wasanii wa muziki wa kizazi kipya wakiwamo Sholo Mwamba, Diamond Platinum, na Dulla Makabila.

**80.** ***Mheshimiwa Spika***, miongoni mwa manufaa yaliyopatikana katika Tamasha hilo ni pamoja na kuongeza kipato kwa washiriki kwa kuuza bidhaa zinazotokana na kazi za kiutamaduni na ubunifu na kukuzwa kwa uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kupitia uuzaji wa vyakula; na nyumba za kulala wageni. Aidha, Tamasha lilichochea ari na hamasa ya kuuthamini urithi wa utamaduni wa Mtanzania uliojengwa na Waasisi wa Taifa letu, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume. Waasisi hawa walitujengea misingi ya umoja, upendo, amani, mshikanano, utulivu, moyo wa kuvumiliana na kustahimiliana bila kujali tofauti zetu za kidini, rangi, itikadi, ukanda au kabila. Pia, Tamasha limewezesha kurithisha utamaduni kwa vijana na watoto ambao walishirikishwa katika shughuli za ngoma na maonesho ya kazi za utamaduni na ubunifu. Fauka ya hayo, Tamasha limewezesha kuibuliwa, kukuzwa na kuendelezwa kwa vipaji vya muziki na uchoraji na kutangazwa kwa uanuwai wa urithi wa utamaduni wa jamii mbalimbali nchini.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo; Wizara iliratibu na kushiriki katika matamasha, makongamano na maadhimisho mbalimbali yakiwamo yaliyoandaliwa na wadau wa Sekta ya Utamaduni nchini kama vile Tamasha la 15 la Muziki wa Cigogo lililofanyika tarehe 20-23 Julai 2024 katika Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma chini ya usimamizi wa Kituo cha Sanaa cha Chamwino yaani "Chamwino Arts Centre (CAC)." Zaidi ya Wadau 700 wa utamaduni na sanaa walishiriki katika Tamasha hilo. Pia, Wizara iliratibu Tamasha la Kumbukumbu ya Mashujaa wa Vita vya Majimaji liliofanyika tarehe 25-27 Februari 2025 katika Viwanja vya Mashujaa wa Vita vya Majimaji Songea, mkoani Ruvuma na kujumuisha washiriki zaidi ya 1,000.

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, pia, Wizara ilishiriki katika Tamasha la Utamaduni la Kigoda cha Wamatumbi lililofanyika tarehe 01 Oktoba 2024 mkoani Lindi; Tamasha la Utamaduni la Watu wa Kigoma lililofanyika tarehe 11 hadi 13 Oktoba, 2024 jijini Dar es Salaam; na Maadhimisho ya miaka 60 ya ushirikiano wa

kidiplomasia kati ya China na Tanzania pamoja na Mwaka wa Utalii na Utamaduni yaliyofanyika tarehe 4 Novemba, 2024 jijini Dar es Salaam. Vilevile, Wizara ilishiriki katika Tuzo za uhifadhi na utalii zilizofanyika mkoani Arusha tarehe 20 Desemba 2024; Tamasha la Utamaduni la Ijuka Omuka lililofanyika tarehe 18 hadi 26 Desemba 2024 mkoani Kagera; na Tamasha la Utalii wa Kiutamaduni wa Maasai lililofanyika tarehe 15-16 Februari 2025 jijini Arusha.

**83.** ***Mheshimiwa Spika***, matamasha haya yameendelea kutoa fursa na majukwaa muhimu kwa wananchi wetu katika maeneo mbalimbali nchini kuutambua, kuusherehekea na kuudumisha urithi wa utamaduni wa Taifa letu. Pia yamewezesha kujenga ari ya umoja na mshikamano na hivyo kudhihirisha kwa vitendo pasi na shaka kuwa Tanzania ni Taifa hai ambalo hutoa uhuru kwa wananchi wake kujipambua katika uanuwai wa utamaduni (*diversity of cultural expression*). Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliwahi kusema "**Taifa lisilokuwa na utamaduni wake ni Taifa mfu".** Hivyo, matamasha haya yanauhuisha uhai wa Taifa letu kila uchao. Vilevile, matamasha ya kimataifa yanakuza uhusiano wa kiutamaduni na kidiplomasia baina ya Tanzania na mataifa mengine duniani.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma bora kwa wananchi wa Tanzania kupitia Sekta ya Utamaduni, Wizara iliratibu kikaokazi cha Maafisa Utamaduni nchini kilichofanyika tarehe 22-25 Aprili, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere ambapo jumla ya Maafisa Utamaduni zaidi ya 250 kutoka katika Halmashauri na Mikoa walishiriki. Tofauti na vikaokazi vya miaka ya nyuma, kikaokazi cha mwaka huu kilihusisha Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri nchini. Kikao hicho kilijikita katika kujadili masuala muhimu ya Sekta ya Utamaduni ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; kuchagiza fursa zinazotokana na sekta hii na namna ya kuzichangamkia; kubaini changamoto na kupendekeza njia za kuzitatua na kutoa miongozo mbalimbali ya namna ya kutekeleza shughuli za Wizara katika maeneo yao.




*Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo – Zanzibar wakati wa ufunguzi wa kikaokazi cha Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo tarehe 22 Aprili 2025, jijini Dar es Salaam.*

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa tunaendelea kulinda na kuendeleza maadili ya Mtanzania yanayozingatia mila, desturi na miiko ya Taifa letu, Wizara inaendelea kukusanya maoni kwa wadau kupitia midahalo na makongamano mbalimbali kama ilivyofanya katika mdahalo wa maadili kwa viongozi wa kimila, viongozi wa kisiasa, watendaji wa taasisi za Serikali na binafsi, wanafunzi na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma uliofanyika tarehe 14 Septemba 2024. Mdahalo huo ulishirikisha wadau zaidi ya 500 kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja kuhusu hatua sahihi za kukabiliana na changamoto za mmomonyoko wa maadili nchini ili kuandaa kizazi chenye uwajibikaji na uzalendo kwa Taifa. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu ya maadili kupitia vyombo vya habari ikiwamo redio na televisheni kwa lengo la kulinusuru Taifa dhidi ya changamoto za mmomonyoko wa maadili unaotukabili kwa sasa.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na jitihada za Serikali za kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kulinda maadili ya Mtanzania kwa kukemea vitendo viovu vinavyokiuka maadili yetu kama vile ubakaji, ulawiti, uhusiano wa jinsia moja, ubadhilifu wa mali za

umma, rushwa n.k., naomba nitumie fursa hii kulikumbusha Bunge lako na Watanzania wote, kuwa suala la kukabiliana na mmomonyoko wa maadili ni jukumu la kila Mtanzania. Tunapaswa kuwalinda watoto na vijana wetu dhidi ya vitendo viovu kama vile matumizi ya dawa za kulevya na uhusiano na ndoa za jinsia moja ambavyo vinatokana na uigaji wa tamaduni za kigeni kwa kisingizio cha kuheshimu haki za binadamu. Kabla ya kuiga jambo lolote, tuchuje na kupima endapo linashabihiana na mila, desturi na utamaduni wetu au vinginevyo.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, napenda nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania kwa kuwa kielelezo katika kuhimiza Watanzania kuishi kwa kuzingatia mila na desturi zetu ambazo ndizo msingi wa maadili yetu. Katika hotuba zake anapokutana na makundi mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, Kamati ya Amani ya Kitaifa, wazee na vijana, suala la kuishi kwa kufuata maadili yetu limekuwa moyo wa ujumbe wake. Naomba sote katika majukwaa mbalimbali, tuhimize Watanzania hususan watoto na vijana wetu kuthamini na kuheshimu misingi ya maadili yetu. Natoa rai kwa wazazi na walezi, tufanye kazi ya kufundisha maadili kwa watoto na vijana wetu kwani familia ni msingi wa maadili.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, nitoe wito kwa taasisi, asasi na vyombo vya habari, kubuni na kuanzisha programu zinazohimiza maadili na uzalendo kwa Taifa letu. Makundi ya wasanii wa muziki na filamu nao watumie sanaa zao katika kuhimiza suala la maadili. Kila mmoja akitimiza wajibu wake, tuna uwezo wa kuondokana na hali ya mmomonyoko wa maadili nchini.

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika kuhakikisha kuwa viongozi wa mila na desturi wanasimamia ipasavyo majukumu ya kulinda maeneo ya yanayotumika kwa ajili ya shughuli za kimila, kudumisha maadili ya Mtanzania na kuhamasisha umoja, amani, ustahimilivu, uzalendo na mshikamano miongoni mwa jamii; Wizara iliratibu kikao cha wadau cha kuandaa mwongozo wa utambuzi wa viongozi wa kimila na desturi nchini. Kikao hicho kilijumuisha wadau zaidi 20 kutoka wizara na taasisi mbalimbali za

Serikali. Kikao kilifanyika tarehe 13 Februari 2025 jijini Dodoma. Lengo la kuandaliwa kwa mwongozo wa utambuzi ni kubainisha utaratibu wa kutambua shughuli za viongozi wa kimila nchini kama sehemu muhimu ya kuenzi mila na desturi katika jamii.

**90.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa 2003 wa UNESCO kuhusu kulindwa kwa urithi wa utamaduni usioshikika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Wizara kwa kushirikiana na UNESCO iliandaa ripoti ya miaka minne (4) ya utekelezaji wa Mkataba huo katika Sekta ya Utamaduni kuanzia mwaka 2020 hadi 2024. Ripoti hiyo ilijumuisha masuala mbalimbali ikiwamo; ushirikishwaji wa wananchi katika kulinda urithi wa utamaduni usioshikika; changamoto zinazokwamisha uhifadhi wa urithi wa utamaduni usioshikika; na urithi wa utamaduni kufungamanishwa na maendeleo endelevu. Vilevile, ripoti ilijumuisha utunzaji wa mazingira, kuhamasisha amani na umoja miongoni mwa wanajamii, kuishi pamoja kwa kuvumiliana na kustahimiliana licha ya kuwapo kwa tofauti za mila, desturi, historia na lugha miongoni mwa jamii hizo.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa manufaa ya utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa katika Sekta ya Utamaduni ni pamoja na wataalamu wetu wa ndani kujengewa uwezo katika kuhifadhi urithi wa utamaduni nchini. Kwa msingi huo, Wizara kwa kushirikiana na UNESCO iliratibu warsha ya uandaaji wa mpangokazi wa kulinda urithi wa utamaduni. Jumla ya wataalamu 30 kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar walishiriki katika warsha hiyo kuanzia tarehe 8-16 Julai 2025 mjini Bagamoyo, mkoani Pwani.

**92.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara kwa kushirikiana na UNESCO, iliratibu warsha ya wadau ya uteuzi wa muziki wa singeli kuorodheshwa kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia unaoratibiwa na UNESCO. Warsha hiyo ilifanyika tarehe 24-25 Machi 2025 jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 120 kutoka Wizara, taasisi na wadau wa sekta ya utamaduni wa mikoa mbalimbali nchini. Muziki wa Singeli, unatumia vionjo vya ngoma za asili ikiwamo midundo na mikong'oso. Midundo ya Singeli imeendelea kuzalishwa kwa wingi kupitia kivunge cha mtozi kilichotengenezwa na BASATA. Upekee wa Singeli umeifanya

kuwa kivutio kikubwa katika matamasha makubwa ya kimataifa kama vile "Nyege Nyege" Festival nchini Uganda, DUO Festival nchini Ubelgiji, Primavera Sound Festival Nchini Hispania, Apporlibation Festival nchini Ujerumani na Cora Festival nchini Ufaransa. Baada ya kumalizika kwa warsha hiyo, Wizara iliandaa nyaraka muhimu za uteuzi (Nomination Dossier) na kuziwasilishwa UNESCO Makao Makuu Paris, Ufaransa kwa ajili ya hatua za kuidhinishwa. Hivi sasa kinachosubiriwa ni kukamilika kwa taratibu za UNESCO ili hatimaye kutangaza rasmi muziki wa Singeli kuwa sehemu ya Orodha ya Urithi wa Dunia, hatua ambayo itaimarisha zaidi hadhi ya utamaduni wa Tanzania Duniani.

### 3.2.2.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliundwa kwa Sheria ya Baraza la Kiswahili la Taifa Sura ya 52. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Baraza ni chombo cha Serikali chenye dhamana ya kusimamia matumizi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo la msingi, BAKITA inasimamia matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili na kuzuia upotoshaji wake. Pia, inatoa ithibati ya matumizi sanifu na fasaha ya lugha ya Kiswahili katika vitabu vinavyoandikwa kwa Kiswahili pamoja na kutoa tafsiri rasmi ya lugha ya Kiswahili. Majukumu mengine ni pamoja na kuhakikisha Kiswahili kinatumika kimataifa na kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na umma na kushirikiana na mamlaka zingine zinazohusika katika kuanzisha tafsiri sanifu ya istilahi za Kiswahili katika nyanja mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, BAKITA imetekeleza majukumu mbambali kama ifuatavyo:

**94.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa sasa Kiswahili sio tu lugha ya mawasiliano na kitaaluma miongoni mwa wananchi bali ni fursa kwa Watanzania kupata ajira kitaifa na kimataifa. Suala hili limethibitisha ukweli kuhusu msemo wa Kiswahili, **"Kiswahili ni zaidi ya Lugha".** Hii ina maana kwamba mbali ya kukidhi dhima yake kuu ya kuwezesha na kurahisisha mawasiliano miongoni mwa Watanzania, Kiswahili kwa sasa ni mgodi unaotoa fursa lukuki za ajira kupitia taaluma za ukalimani na tafsiri katika mikutano ya kimataifa, utangazaji kwenye televisheni na idhaa za Kiswahili kimataifa, uuzaji wa machapisho ya Kiswahili na ufundishaji wa

Kiswahili kwa wageni. Pia Kiswahili kinatoa fursa katika utunzi wa nyimbo, filamu, uandishi bunilizi wa kazi za fasihi na uanzishwaji wa vituo vya kufundisha Kiswahili na utamaduni wake ughaibuni.

**95.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na kushamiri kwa maendeleo na matumizi ya lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa, Wizara iliratibu Maadhimisho ya Tatu ya Siku ya Kiswahili Duniani yaliyofanyika kitaifa tarehe 7 Julai 2024 jijini Dar es Salaam. Aidha, Maadhimisho hayo yalianzia jijini Arusha tarehe 01 Julai 2024 kwa Mbio za Kimataifa za Masafa za Kiswahili yaani *Kiswahili International Marathon* na kisha kuendelea katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere kuanzia tarehe 03 hadi 07 Julai 2024 yakiwa na Kaulimbiu, **"Kiswahili na Fursa za Maendeleo Duniani".** Maadhimisho haya ni sehemu ya kuitikia wito wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) la kuitangaza tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani na kufuatiwa na Azimio namba **(A/78/L.83)** la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lililotolewa tarehe 1 Julai 2024 ambapo Baraza hilo liliidhinisha tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani.




*Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani, yaliyofanyika tarehe 7 Julai 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.*

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, tunaendelea kutoa pongezi kwa UNESCO na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa uamuzi wa busara wa kutenga Siku Maalumu ya kusherehekea lugha ya

Kiswahili duniani kwa sababu hii ndiyo lugha ya pekee ya Bara la Afrika iliyopewa hadhi ya kutambuliwa na Shirika hilo la Umoja wa Mataifa.

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Maadhimisho ya Tatu ya Kikanda ya Siku ya Kiswahili Duniani kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika kuanzia tarehe 05 hadi 07 Julai 2024 katika jiji la Mombasa nchini Kenya. Kama ilivyo katika ngazi ya kitaifa, Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) imejiwekea utaratibu wa kufanya Maadhimisho ya Kikanda ya Siku ya Kiswahili Duniani kwa mzunguko katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kuitikia tamko la UNESCO la Siku ya Kiswahili Duniani ambapo nchi zote za Afrika Mashariki hushiriki. Wakati wa Maadhimisho hayo, mada mbalimbali kuhusu maendeleo ya Kiswahili na fursa za kiuchumi zinazotokana na lugha ya Kiswahili ziliwasilishwa na kujadiliwa kwa maslahi mapana ya kukuza na kuendeleza utangamano wa kikanda.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza kasi ya kukiuza na kukieneza Kiswahili kimataifa, Wizara kwa kushirikiana na BAKITA iliratibu Kongamano la Kiswahili la Kimataifa lililofanyika katika Jiji la Havana nchini Kuba kuanzia tarehe 07-10 Novemba 2024. Kongamano hilo lilijumuisha washiriki zaidi ya 600 kutoka nchi mbalimbali duniani. Lengo la Kongamano hilo lilikuwa kupeleka Kiswahili katika ukanda wa Karibe, Amerika ya Kati na Amerika ya Kusini ambako lugha kuu ya mawasiliano ni Kihispaniola. Aidha, mafanikio yaliyopatikana katika Kongamano hilo ni pamoja na kuzinduliwa kwa kitabu cha *Misemo ya Kila Siku ya Kihispaniola – Kiswahili (BAKITA), Kamusi ya Kihispaniola - Kiswahili (TATAKI - UDSM)* pamoja na kitabu cha *Jifunze Kihispania kwa Kiswahili (SUZA).* ; Pia Kongamano hili liliwezesha kutambuliwa kwa lugha ya Kiswahili katika ukanda wa Karibe, Amerika ya Kusini na Amerika ya Kati; kupanuliwa kwa soko la machapisho ya Kiswahili kama vile majarida, vitabu vya kujifunza Kiswahili pamoja na kamusi za Kiswahili.



*Kongamano la Kwanza la Kimataifa la Kiswahili lililofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Havana, Kuba kuanzia tarehe 07 - 10 Novemba 2024.*

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Msumbiji na Shule ya Kimataifa ya Maputo, Msumbiji lilifanya shughuli mbalimbali za maendeleo ya lugha kama vile; kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo diaspora na maafisa wa ubalozi katika kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni ambapo washiriki 43 walihudhuria. Aidha, Baraza lilitambua rasmi na kutoa cheti cha utambuzi kwa kituo cha kufundisha Kiswahili cha ubalozini. Vilevile, Baraza lilipata fursa ya kufanya mazungumzo na Chuo Kikuu cha *Pedagogical de Maputo* kuhusiana na ufundishaji wa Kiswahili chuoni hapo na namna Tanzania inavyoweza kusaidia chuo hicho kwenye ufundishaji wa Kiswahili.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limefundisha na kupima umahiri kwa wageni 113 wakiwamo madaktari 27 waliokuja nchini kwa mafunzo ya vitendo kutoka katika nchi za Zimbabwe, Kenya, Uganda, Nigeria, Eswatini, Kongo, na Sudani. Pia, mheshimiwa Balozi wa Uturuki nchini Tanzania na maafisa wawili (2) wa ubalozi wa Japani nchini Tanzania walifanya mtihani wa kupima umahiri wa Kiswahili. Aidha, wanafunzi 70 wa shule ya Kimataifa ya Braeburn mkoani Arusha nao walifanya mtihani huo.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza hadi sasa katika utoaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo diaspora wa kufundisha Kiswahili

kama lugha ya kigeni tayari imewafikia diaspora 495. Mafanikio yaliyopatikana kupitia diaspora hao ni pamoja na diaspora kufundisha wageni 266 kwa mchanganuo ufuatao: Italia - 68, Ufaransa – 148, Austria - 23 na Nigeria - 27. Aidha, Baraza limesajili vituo 51 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni ambapo vituo 19 viko nje ya nchi na vituo 32 viko ndani ya nchi. Kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 vituo hivi vimefundisha Kiswahili kwa wageni 588.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo Baraza liliwasilisha andiko la ujenzi wa Shule ya Kiswahili na Stadi za Kiafrika Makao Makuu ya UNESCO nchini Ufaransa tarehe 1 Agosti 2024. Andiko hilo linalenga kuomba hisani ya ujenzi wa shule hiyo ambayo itakuwa sehemu muhimu ya kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni, lugha za Kiafrika na lugha mbalimbali za kimataifa. Aidha, masuala ya teknolojia ya michakato ya lugha itafundishwa. Vilevile, Baraza limetoa nakala 250 za vitabu vya Kiingereza – Kiswahili – Kihispaniola, Kiingereza – Kiswahili Kireno, Kiingereza – Kiswahili – Kiarabu na Kiingereza - Kiswahili – Kifaransa kwa viongozi wa vyama rafiki na CCM mwezi Desemba 2024 katika kikao chao kilichofanyika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Kibaha kwa lengo la kuendeleza lugha katika nyanja za kisiasa.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA imeendelea kuuelimisha umma kuhusu kuzingatia matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili. Katika kipindi cha Julai2024 hadi Aprili 2025, BAKITA iliandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 894 kupitia redio na televisheni za Redio One, TBCTaifa, TBC1, Clouds Fm, Kiss FM, U-FM, WAPO Redio, MVIWATA FM, Redio Maria, Redio Idea, Channel 10, na Idhaa ya Kiswahili ya Redio ya Umoja wa Mataifa. Kwa ujumla mada mbalimbali zilizoshughulikiwa zililenga kuelekeza matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili. Hali kadhalika, mada nyingine zilihusisha historia, fasihi na isimu ya Kiswahili kwa ujumla wake. Aidha, Baraza liliandaa maudhui 190 ya mtandaoni ya kutoa elimu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kupitia mitandao ya kijamii ambayo ni *Facebook, YouTube, Twitter (X) na Instagram*. Pia, makala 40 za Kiswahili ziliandaliwa na kutolewa kupitia gazeti la HabariLeo la kila siku ya Ijumaa.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni ni sehemu ya utekelezaji wa *Mkakati wa Taifa wa Kukipeleka Kiswahili Kimataifa*. Baraza limefanikiwa kuimarisha utaalamu kwa makundi mbalimbali ya wataalamu wa Kiswahili ndani na nje ya nchi. Aidha,kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya walimu 216 kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT) Mwanza, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Morogoro (MUM) walipata Mafunzo ya Kuimarisha Stadi za Kufundisha Kiswahili kwa Wageni. Hii inafanya kuwe na jumla ya walimu 1,798 walioimarishwa katika uga wa kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kusimamia matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili kwa kuhakikisha makundi mbalimbali ya watumishi wa umma na binafsi wanapatiwa mafunzo ili lugha inayotumika katika shughuli mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kijamii iwe fasaha na sanifu. Baraza katika kutekeleza jukumu hilo limeendesha mafunzo kwa walimu na wadau wa Kiswahili 220 katika Shule za Sekondari Songea, washereheshaji 205 mjini Songea mkoani Ruvuma na wahudumu wa mapokezi na huduma kwa mteja 41, katika Hoteli ya Morena mjini Morogoro.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo Baraza kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi Waendesha Ofisi (TAPSEA) lilitoa mafunzo kwa Waandishi Waendesha Ofisi (WWO) 1,045 yaliyofanyika mjini Morogoro kuanzia mwezi Septemba hadi Desemba 2024. Mafunzo hayo yalilenga kuwanoa na kuwajengea uwezo wa kuwasiliana na kuandika nyaraka kwa Kiswahili fasaha na sanifu katika mazingira rasmi. Mafunzo hayo yametolewa ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoyatoa mwezi Machi 2024 wakati akifungua Kongamano la Kimataifa la Idhaa za Kiswahili Duniani huko Mbeya. Washiriki wa mafunzo hayo walitoka katika taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi. Halikadhalika, mafunzo hayo yameendelea kwa Maafisa Rasilimali Watu kuanzia tarehe 7 hadi 30 Aprili ambapo jumla ya Maofisa rasilimali 71 walipata mafunzo. Mafunzo haya ni endelevu na yanalenga kufikia kada zote katika utumishi wa umma.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza lilitoa mafunzo ya muda mfupi ya stadi za kukalimani kwa wakalimani 42 yaliyofanyika katika ofisi za Baraza jijini Dar es Salaam na kufanya idadi ya wakalimani waliopatiwa mafunzo kufikia 206. Aidha, Baraza liliratibu na kutoa huduma za ukalimani katika mikutano 17 ya kitaifa na kimataifa. Miongoni mwa mikutano iliyopata huduma hiyo ni pamoja na mkutano wa Nishati wa wakuu wa nchi za Afrika "misheni 300" uliofanyika jijini Dar es Salaam Januari 2025; Mkutano wa Kawaida wa 76 wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu uliofanyika Arusha Tanzania Februari 2025, Mkutano wa Nishati wa wakuu wa nchi za Afrika uliofanyika Arusha Februari 2025; Mkutano wa Uhakiki wa Mkakati wa Umoja wa Afrika wa Utawala wa Bahari uliofanyika Dar es Salaam Aprili, 2025 na Mkutano wa Msaada wa Kitaalamu wa Timu ya Umoja wa Ulaya, kusaidia Utangamano wa Uchumi uliofanyika Dar es Salaam Aprili 2025.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu la kutoa ithibati ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu, BAKITA kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 imetoa ithibati kwa miswada ya vitabu 59 ambapo vitabu vya kiada ni 32 na ziada 27. Vitabu hivi viliwasilishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania, *Room to Read*, Mkuki na Nyota, *E&D Vision*, KIUTA, *Aznas Printing* na waandishi binafsi. Baraza linaendelea kuhamasisha waandishi na wachapishaji wa vitabu kuviwasilisha BAKITA ili viweze kupatiwa ithibati.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA katika kutoa huduma ya tafsiri kwa nyaraka mbalimbali, ilitafsiri jumla ya kazi kubwa na ndogo 1,158 sawa na asilimia 145 ya lengo lilowekwa la kazi 800. Katika tafsiri hiyo kazi kubwa zilikuwa 34 na ndogondogo zilikuwa 1,105. Kazi hizo zilitafsiriwa kutoka na kwenda Kiswahili kwa lugha za Kichina, Kiingereza, Kiarabu, Kihindi, Kigujarati, Kijerumani, Kifaransa, Kireno, Kihispaniola, Kiitaliano, Kifarsi (Kiajemi) na Kikorea. Aidha, hadi Aprili 2025, Baraza lilithibitisha nyaraka kubwa na ndogo 3,364 zilizotafsiriwa sawa na asilimia 112 ya lengo la nyaraka 3,000 lililowekwa.

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BAKITA imeandaa kanzidata ya wataalamu wa Kiswahili kwa lengo la kubaini uwezo

wa nchi kushiriki katika kueneza matumizi na maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya nchi kupitia huduma za ukalimani, tafsiri, ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni pamoja na uandishi wa vitabu. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Baraza limetambua na kusajili wataalamu 73 sawa na asilimia 61 ya lengo la kusajili wataalamu 120, ambapo hadi Aprili 2025 kanzidata ina jumla ya wataalamu 1,897 kati yao wanaume ni 858 na wanawake 1039. Wataalamu hawa ni wale wenye utaalamu wa lugha ya Kiswahili kuanzia ngazi ya Shahada ya Awali, Umahiri, na Uzamivu.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha hakuna nchi inayoachwa nyuma kwenye mkakati wa kitaifa wa kusambaza Kiswahili, BAKITA imeshiriki hafla ya utiaji saini wa hati ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Somalia kupitia Wizara ya Elimu, Utamaduni na Elimu ya Juu. Makubaliano hayo yalihusu kukieneza Kiswahili na utamaduni wake nchini Somalia kwa kutumia mbinu anuwai ikiwamo matumizi ya TEHAMA. Hafla hiyo ilifanyika tarehe 29 Januari 2025 katika Ukumbi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, jijini Dar es Salaam.

**112.** ***Mheshimiwa Spika***, lugha adhimu na aushi ya Kiswahili ni tunu ya Taifa letu, ambapo hadi sasa lugha hii ni miongoni mwa lugha saba (7) zilizotengewa siku ya kuadhimishwa na ina wazungumzaji takribani Milioni Mia Tano (500) duniani. Pamoja na kazi kubwa iliyofanywa kwenye eneo hili la lugha ya Kiswahili, ninapenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa sisi Watanzania tunawajibu wa kujivunia na kutembea kifua mbele kutokana na mafanikio tuliyoyapata ya lugha ya Kiswahili, na hivyo ni lazima tupigane na maadui watatu (3) wa lugha yaani kufubaza, kubananga na kubagaza lugha, na tusikubali mtu yeyote aipuuze au kuibeza lugha yetu kwani imetupa utambulisho wa kipekee duniani.

### 3.2.2.3 KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA

**113.** ***Mheshimiwa Spika***, tunu ya amani, umoja na upendo tuliyonayo Watanzania ilijengwa na waasisi wa Taifa letu na ndiyo iliyosababisha nchi yetu kuwa mstari wa mbele katika ajenda ya kidunia ya kusaidia mapambano ya uhuru kwa nchi za Afrika na duniani kwa ujumla. Baada ya harakati za ukombozi wa Afrika kukamilika, Tanzania imekabidhiwa jukumu jingine la kuongoza juhudi za uhifadhi wa urithi wa ukombozi wa Afrika kupitia azimio la Umoja wa Afrika la mwaka 2011 ikiwa ni ishara ya heshima na kuthaminiwa kwa mchango wa Tanzania katika kuleta uhuru na usawa katika Bara letu la Afrika. Wizara inasimamia Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika ambacho kina jukumu kubwa la kubainisha, kuhifadhi, kulinda na kuendeleza urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

**114.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kimeendelea kutekeleza shughuli muhimu za utafiti wa ubainishaji wa maeneo yenye umuhimu katika historia ya harakati za ukombozi wa Afrika. Katika kipindi hicho, Kituo kimefanya utafiti katika mikoa ya Mwanza, Tabora, Tanga, Pwani, Kagera na Ruvuma, ambapo maeneo 18 yenye historia ya harakati za ukombozi yamebainishwa. Aidha, Kituo kimeendelea kuielimisha na kuihamasisha jamii kuhusu wajibu wa kuhifadhi maeneo hayo ya kihistoria ili kuimarisha urithi wa harakati za ukombozi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

**115.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kufanya tathmini ya uhifadhi wa maeneo muhimu ya kihistoria ikiwamo Kongwa, Dakawa, Mazimbu na Bagamoyo. Maeneo haya ni ushahidi muhimu wa kumbukumbu ya harakati za ukombozi wa Bara la Afrika na yanashikilia urithi adhimu wa historia yetu ya pamoja. Kwa kuyaainisha, kuyahifadhi na kuyaenzi, tunaimarisha msingi wa maarifa kwa vizazi vya sasa na vijavyo, huku tukitambua kuwa utambulisho na maendeleo ya taifa letu hayawezi kutenganishwa na historia yetu. Juhudi hizi zinalenga kuhuisha fahari ya taifa letu na kuendeleza heshima ya mchango wa Tanzania katika historia ya dunia.

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, Kituo kimeendelea kuratibu ukarabati wa jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya O.A.U, ambapo hadi sasa ukarabati umefikia asilimia 92. Mafanikio haya yanadhihirisha juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kutunza na kuenzi historia hii adhimu ambayo ni sehemu muhimu ya urithi wa bara letu la Afrika. Ili kuhakikisha historia hii inaendelea kuhifadhiwa kwa vizazi vya sasa na vijavyo, ushirikiano wa karibu kati ya Serikali na wananchi ni jambo la msingi**.**

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Kituo kimeendea kustawisha ushirikiano wa kidiplomasia na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, ambapo Kituo kilishirikiana na Ubalozi wa Namibia nchini Tanzania kufanya ukarabati wa makaburi matatu (3) ya wapigania uhuru kutoka Namibia waliokuwa wakiishi katika kambi ya kihistoria ya Kongwa. Ushirikiano huu wa kidiplomasia umeimarisha juhudi za pamoja baina ya nchi zetu za kuhifadhi historia ya harakati za ukombozi wa nchi zetu.

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Kituo kimeanza kuratibu ujenzi wa Kituo Kikuu cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kilichopo katika eneo la Kiromo, Bagamoyo, mkoani Pwani. Taratibu za kumpata mshauri elekezi ambaye ataandaa michoro na gharama za ujenzi zinaendelea. Ujenzi wa Kituo hiki utakuwa na manufaa mengi kwa taifa letu, ikiwa ni pamoja na kutumika kama makumbusho ya harakati za ukombozi wa Afrika. Aidha, kituo hiki kitakuwa kivutio kipya cha utalii wa kiukombozi, kitakachochangia katika uzalishaji wa ajira kwa wataalamu mbalimbali, hivyo kukuza uchumi wa taifa letu. Vilevile, kituo kitakuwa mfano bora wa uhifadhi wa historia ya ukombozi wa Bara la Afrika.

**119.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha kuwa vijana na umma kwa ujumla wanapata uelewa mzuri kuhusu harakati za ukombozi wa Bara la Afrika, Kituo kiliratibu Maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika, tarehe 23 Machi 2025. Maadhimisho haya yalilenga kutoa elimu, kuhamasisha umuhimu wa kulinda na kutunza urithi wa ukombozi, kuwaenzi mashujaa wa Afrika, sambamba na kuimarisha mshikamano na umoja wa nchi

za Afrika. Hii ni sehemu ya juhudi endelevu za kuongeza uhamasishaji kuhusu umuhimu wa urithi wa ukombozi wa Afrika kwa jamii nzima, hususan vijana, ili waweze kuelewa, kuthamini, na kulinda michango ya mashujaa wetu. Hivyo, ni muhimu kwa vijana wetu kuwa na ufahamu wa kina kuhusu historia ya mapambano ya ukombozi ili waweze kutambua nguvu za umoja na kuenzi michango ya mashujaa waliopigania uhuru wa Bara letu.

**120.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika zama hizi za kiteknolojia, Kituo kimeanza kuandaa mfumo wa kidijiti wa makumbusho na maktaba. Kazi hii ilihusisha ukusanyaji, uchambuzi, na uhifadhi wa nyaraka, picha, video, na vielelezo vya kihistoria ili vitumike kwa njia ya kidijiti. Lengo ni kuhakikisha kuwa historia ya urithi wa ukombozi inapatikana kirahisi kwa jamii, bila kujali mahali walipo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Kituo kimekusanya na kuchambua jumla ya hotuba 1500, picha mnato 5,000, nyimbo za kiukombozi 150, na mikanda ya sauti 366. Huu ni mfano mzuri wa jinsi gani teknolojia inavyoweza kutumika katika uhifadhi wa historia.

**121.** ***Mheshimiwa Spika***, Kituo kimekuwa jukwaa muhimu la elimu na uhamasishaji kwa wanafunzi, watafiti na jamii kwa ujumla. Kituo kimekuwa chombo cha kufundisha kuhusu historia ya ukombozi wa Afrika, na kuonesha jinsi mataifa ya Afrika yalivyopigania uhuru dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi. Hii inasaidia kuongeza maarifa na kujivunia mchakato wa ukombozi kwa vizazi vya sasa. Kupitia Hati ya Ushirikiano baina ya Kituo na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Kituo kimefanikiwa kuingiza maudhui ya ukombozi katika vitabu vya Historia ya Tanzania na Maadili kuanzia elimu ya msingi hadi sekondari katika mtaala mpya wa masomo. Aidha, kupitia ushirikiano wa Kituo na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kituo kimefanikiwa kutengeneza vipindi vya Ng'ariza Afrika 20 ambavyo vinahamasisha uzalendo kwa umma na kuiendeleza historia ya ukombozi kwa kizazi cha sasa na kijacho.

**122.** ***Mheshimiwa Spika*****,** sanjari na hayo, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa

maelekezo yake katika kuhakikisha urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika unahifadhiwa kwa matumizi ya vizazi vya sasa na vijavyo. Mafanikio haya ni matunda ya juhudi kubwa za Serikali, ambazo zimejikita katika kuhakikisha kwamba historia ya ukombozi inapata hifadhi ya kudumu. Mafanikio haya pia ni matunda ya ushirikiano wa Serikali, mashirika ya kimataifa, wataalamu wa uhifadhi, na jamii kwa ujumla. Aidha, ushirikiano huu umewezesha kuhifadhi urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika, na hivyo tunatoa shukurani za dhati kwa wote waliochangia katika jambo hili la kihistoria.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** upo msemo usemao, **"***Mizizi ya miti ni muhimu kuliko tawi lake***"**. Kupitia msemo huu tunatambua kuwa juhudi za sasa za uhifadhi wa historia ya ukombozi zitakuwa msingi imara kwa vizazi vijavyo katika kuelewa na kuthamini uhuru walioupata kupitia mashujaa wa Afrika. Kwa hiyo, ni muhimu kujivunia mafanikio haya na kuyathamini kama sehemu ya mchakato wa kujenga bara lenye umoja, mshikamano, amani, na maendeleo.

### 3.2.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Maendeleo ya Sanaa nchini ina jukumu la kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sanaa. Sekta hii ni moja ya maeneo muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu kutokana na mchango wake katika kutoa ajira hususan kwa vijana, kukuza utalii na kuitangaza nchi yetu kimataifa. Sekta ya Sanaa inahusisha Idara ya Maendeleo ya Sanaa, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania, Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

#### 3.2.3.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha wasanii wa Tanzania wanaendelezwa na kupatiwa fursa mbalimbali za kutangaza na kuuza kazi zao hatimaye kujipatia kipato, Wizara imeratibu na kushiriki kwenye matamasha mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ambapo katika ngazi ya kitaifa Wizara imefanikiwa kuandaa Tamasha kubwa la *Samia Serengeti Music Festival* ikiwa ni mwendelezo wa Tamasha la Serengeti Music Festival ambalo

limekuwa likiandaliwa tangu mwaka 2020. Tamasha hili limechukua jina la ***Samia Serengeti Music Festival*** kwa heshima ya jitihada kubwa zinazofanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha sekta ya sanaa na utamaduni nchini.

**126.** ***Mheshimiwa Spika***, tamasha hilo lilifanyika katika viwanja vya Tanganyika Packers, Kawe Jijini Dar es Salaam tarehe 26 Aprili 2025 ambapo Mgeni Rasmi ulikuwa wewe, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Malengo ya tamasha hili kwa mwaka 2025 yalikuwa kutoa fursa kwa wasanii wa ndani kuonesha vipaji vyao kwa kutumia sanaa ya muziki ili kuunganishwa na soko la kitaifa na kimataifa, kutangaza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita, kusherehekea Muungano, na kuhamasisha wananchi kushiriki CHAN 2024 na AFCON 2027.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** tamasha hilo lililohudhuriwa na wananchi takribani 45,000 liliruhusu wasanii kutoka 'kambi' mbalimbali kutumbuiza katika jukwa moja kubwa kuwahi kutumika Tanzania na Afrika Mashariki ambalo limeweka viwango vya hali ya juu kabisa, kuongeza thamani ya wasanii wetu dhidi ya wasanii wengine wa mataifa ya Afrika. Aidha, Samia Serengeti Music Festival – 2025 linaweza kuwa ndilo tamasha la kwanza kuandaliwa vema zaidi, kuwa na ushiriki mkubwa wa wasanii na wananchi waliobaki uwanjani kwa wingi wao kwa muda wa zaidi ya saa 20. Kutokana na ukubwa huo, ulishauri lifanyike mara kwa mara badala ya mara moja ili kutoa fursa kwa wasanii wengi zaidi kuonesha vipaji vyao; kufanyika katika mikoa mbalimbali ya Tanzania na kufanyika kwa zaidi ya siku moja kwa kila tukio.Wizara iko tayari kutekeleza ushauri wako huo.

**128.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kurithisha utamaduni wa vazi la kanga, Wizara iliratibu onesho maalumu la kimkakati la matumizi mbalimbali ya vazi la kanga wakati wa Tamasha la Tatu (3) la Utamaduni Kitaifa lililofanyika mwezi Septemba 2024 wilayani Songea mkoani Ruvuma. Miongoni mwa matumizi ya vazi la kanga yaliyobainishwa kupitia onesho hilo ni matumizi ya nyumbani kama vile kata, mbeleko na vazi kwa wanawake; kufikisha ujumbe mbalimbali wa kuelimisha na kuhamasisha.

Tamasha kama hili pia lilifanyika sambamba na Kongamano la Kiswahili lililofanyika Jijini Havana, Kuba mwezi Novemba 2024 ambapo kikundi cha sanaa cha Three Sisters pia kilipata nafasi ya kushiriki na kutoa burudani.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa vazi la kanga litatumika kama nyenzo ya kimkakati ya uhamasishaji katika michuano ya AFCON 2027 itakayofanyika katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda na litaendelea kutumika kukieneza Kiswahili duniani kote.

**130.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika hatua ya kutangaza vivutio vya urithi wa utamaduni wa kitaifa na kimataifa kwa kutumia sanaa, Wizara ilishiriki Maonesho ya Sanaa ya Surajkund Crafts Mela huko New Delhi India tarehe 7 hadi 23 Februari 2025. Katika maonesho hayo, Kikundi cha Magomamoto cha Bagamoyo kutoka Mkoa wa Pwani na washiriki wengine wawili (2) mmoja kutoka Kijiji cha Wasanii Mwenge na mwingine kutoka Kikundi cha Wanawake Wajasiriamali wa Sanaa za Ufundi (WAWAMAKI) cha Kijiji cha Makumbusho Dar es Salaam walipata fursa ya kuonesha kazi zao hususan Michoro ya Tingatinga na Makonde ambayo asili yake ni kutoka nchini Tanzania.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza Sekta ya Sanaa, Serikali kupitia Wizara inaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Miaka Kumi (10) wa Maendeleo ya Sanaa utakaotumika kuanzia mwaka 2026 hadi 2036. Mkakati huu utazingatia malengo ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Utamaduni ya mwaka 1997, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 na Dira ya Maendeleo ya Taifa na Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa Wizara.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita (6) chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuhakikisha kunakuwa na soko la uhakika la kazi za filamu na muziki nchini. Moja ya hatua zilizochukuliwa ili kufikia azma hiyo Wizara inafanya jitihada za kuingia makubaliano na wamiliki wa Kampuni za Emirates, ambapo mazungumzo ya awali yalifanyika tarehe 15 Novemba 2024, jijini Dubai.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imefanikiwa kuandaa Andiko la Ushirikiano baina ya Tanzania na Benki ya Dunia. Ushirikiano huo, pamoja na maeneo mengine, utaiwezesha Serikali kujenga vituo vya Sanaa na Utamaduni katika ngazi ya Mikoa kupitia *Country Partnership Framework 2025 – 2029*. Ujenzi wa vituo hivyo utatoa nafasi kwa wadau kuendesha shughuli za sanaa na utamaduni. Fauka ya hayo, vituo hivyo vitawezesha kufunguliwa kwa ofisi za mikoa za BASATA, BAKITA, Bodi ya Filamu, COSOTA, na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania. Sambamba na ujenzi wa vituo, andiko pia linalenga kuboresha mifumo ya kidijiti ya utendaji kazi wa COSOTA, kutunisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania pamoja na kuanzisha Makao Makuu ya Sanaa kwa Walemavu hapa nchini.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea kushirikiana na wadau wa Sekta ya Sanaa kwa kutoa mafunzo, kushiriki kwenye matukio, mikutano, warsha na vikao mbalimbali yaliyoandaliwa na wadau ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara imeandaa Katiba ya Mfano ambayo ni mwongozo mama utakaotumiwa na Vyama na Mashirikisho yote ya Sanaa Tanzania kwa lengo la kuondoa migogoro ya kikatiba inayozikumba Taasisi hizo na kuimarisha uwazi, usawa na usimamizi bora wa vyama na mashirikisho.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** nina furaha kubwa kutoa taarifa kwa Bunge lako tukufu kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2025 na 2026, mradi wa ujenzi wa ***Film Studio and Multipurpose Entertainment Complex*** wenye thamani ya Shilingi 450,000,000,000 ni mmoja wa miradi itakayojengwa katika mpango wa fedha kutoka Korea Kusini. Mradi huu utakapokamilishwa, sio tu Tanzania itapata fursa ya kuingiza fedha za kigeni kupitia kampuni zitakazokuja kufanya shughuli za filamu na burudani hapa nchini, lakini pia itaongeza thamani kwa wasanii wetu na kuonesha namna ambavyo Tanzania inaithamini Sekta ya Sanaa na burudani katika kuzalisha ajira, kuongeza kipato kwa wadau wake na kuchangia kikamilifu katika Pato la Taifa.

### 3.2.3.2 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**136.** ***Mheshimiwa Spika***, BASATA imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Sura ya 204. Majukumu ya BASATA ni pamoja na kufufua na kukuza sanaa nchini; kufanya tafiti za masuala mbalimbali yahusuyo sanaa; kutoa ushauri na misaada ya kiufundi kwa wasanii na wadau wa sanaa; kupanga na kuratibu shughuli za wasanii na wadau wanaojishughulisha na uzalishaji wa kazi za sanaa nchini; na kutengeneza kanuni za kusimamia ubora wa kazi za sanaa.

**137.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu mengine, ni kuishauri Serikali kuhusu mambo yahusuyo maendeleo ya sanaa nchini; kutoa na kukuza upatikanaji wa miundombinu na vifaa vya mafunzo kwa wasanii, wadau wa sanaa na watu ambao wameajiriwa au wanaotegemea kuajiriwa katika kampuni zinazozalisha kazi za sanaa; na kuchochea maendeleo ya kazi za sanaa kwa kuandaa na kupanga maonesho, warsha, semina na mashindano kwa wasanii mbalimbali.Aidha, BASATA ina jukumu la kuendesha na kusaidia taasisi au watu wanaojishughulisha na kutengeneza, kuingiza, kusafirisha au kuuza nje ya nchi kazi za sanaa.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BASATA kwa lengo la kuimarisha ubunifu na kuongeza ubora wa sanaa, iliratibu utoaji wa Tuzo za Muziki zilizofanyika tarehe 19 Oktoba 2024 katika ukumbi wa "*The S*uper Dome" jijini Dar es Salaam. Tuzo hizi kwa mara ya kwanza katika historia ya tuzo zilirushwa na vyombo vikubwa vya kimataifa vya habari vya BET na MTV. Aidha, jumla ya wanamuziki 180 kutoka ndani na nje ya nchi walishiriki kinyang'anyiro cha tuzo na hatimaye tuzo 36 zilitolewa kwa washindi, huku Mwanamuziki Nguli **Steven Hiza** aliyeimba wimbo wa **Tanzania Yetu** akipata Tuzo ya Heshima na zawadi ya Shilingi 50,000,000 kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kutokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wadau wa tuzo, Baraza limeandaa mwongozo wa tuzo, na vipengele vya tuzo.



*Mheshimiwa Hamis Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo, akitoa tuzo kwa Msanii wa Bongofleva, Omari Ally Mwanga (Marioo) wakati wa hafla za utoaji wa Tuzo za Muziki Tanzania (TMA) zilizofanyika tarehe 19 Oktoba 2024 katika ukumbi wa The Super Dome, jijini Dar es Salaam.*

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kurahisha utoaji wa huduma kwa wadau Baraza limechukua hatua ya kuunganisha mfumo wa utambuzi wa wasanii "Artists Management Information System" (AMIS) na Mfumo wa Ukusanyaji Mapato wa Serikali za Mitaa (TAUSI) na Mfumo wa Ununuzi (NeST) ili kuwafikia wadau wote wa Sanaa. Hatua hii ya kimkakati itaiwezesha BASATA kuwafikia wadau wote wa Sekta ya Sanaa kwa njia rahisi, ya kidijiti na yenye gharama nafuu. Kupitia mfumo huu wa AMIS uliounganishwa, wasanii na vikundi vya sanaa sasa wanaweza kupata huduma mbalimbali kwa urahisi zaidi, zikiwamo, usajili wa wasanii binafsi na vikundi vya sanaa, malipo ya ada za usajili, malipo ya vibali vya wasanii na vibali vya kumbi za burudani. Hadi kufika Aprili 2025, kazi hii ya kuunganisha mifumo imekamilika na tayari mfumo huu umeshaanza kufanya kazi kwa vyanzo 15.

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuimarisha utawala bora katika usimamizi na uongozaji wa vyama na mashirikisho, Baraza lilitoa mafunzo ya uongozi katika sanaa kwa viongozi 63 wa mashirikisho na vyama vya sanaa. Mashirikisho hayo ni; Shirikisho la Sanaa za Ufundi, Shirikisho la Sanaa za Maonesho, Shirikisho la Muziki na Shirikisho la Filamu.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia maslahi ya wasanii, Baraza limefanya vikao vya utatuzi wa migogoro ya wasanii wa muziki kupitia Dawati la Sheria, Maadili na Usuluhishi. Kati ya migogoro 18 iliyopokelewa kati ya Julai 2024 hadi Aprili 2025 migogoro 15 ilitatuliwa na migororo mitatu (3) ipo kwenye hatua tofauti za utatuzi. Mwenendo unaonesha kwamba migogoro ya kimasilahi baina ya wadau wa sanaa imekuwa inapungua kutokana na hatua ambazo Baraza kupitia Dawati hilo, imekuwa inachukua ikiwamo kutoa elimu na ushauri kwa wadau kuhusu masuala ya mikataba ya kazi za sanaa.

**142.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kusimamia dhana ya *"watoto ndio Taifa la kesho",* ni muhimu kuwajengea misingi imara ya sanaa tangu wakiwa wadogo. Katika kutimiza lengo hilo, Baraza liliendesha programu ya sanaa kwa watoto wa shule za msingi na sekondari. Programu hii imeendeshwa katika Shule ya Sekondari ya *Sisters of Marry* na Shule ya Msingi Kauzeni mkoani Pwani, ambapo jumla ya watoto 270 walifikiwa.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** sanaa ni ajira, uchumi na ni burudani. Hivyo, ili kuwa na jamii inayotambua hayo, Baraza limeratibu Programu ya Sanaa Mtaa kwa Mtaa na BASATA *Social Club.* Programu ya Sanaa Mtaa kwa Mtaa imefanyika katika Wilaya ya Kisarawe Mkoa wa Pwani na kuwashirikisha wasanii 402 wa fani za muziki, ngoma za asili, uchoraji na uchongaji wa vinyago. Aidha, programu ya *BASATA Social Club* yenye lengo la kutoa burudani kwa viongozi wa kidiplomasia imefanyika mwezi Julai na Septemba 2024 chini ya uhisani wa Kituo cha Utamaduni cha Ufaransa *(Alliance Francaise)* kilichopo jijini Dar es Salaam.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA kwa kushirikiana na waandaaji wa Tuzo za Kimataifa za "*The Hollywood and African Prestigious Awards (HAPAWARDS)*" kutoka Marekani iliratibu utoaji wa tuzo hizo zilizofanyika tarehe 10 Agosti 2024 katika ukumbi wa *The Super Dome* jijini Dar es Saalam. Jumla ya tuzo 55 zilitolewa kwa wasanii waliofanya vizuri kitaifa na kimataifa kwenye muziki, filamu na ubunifu wa mavazi.

**145.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuchochea maendeleo ya sanaa nchini Baraza limeendelea kuandaa na kuendesha maonesho,

mashindano, matamasha na biashara za sanaa, kufufua na kukuza sanaa kupitia programu mbalimbali za sanaa. Hadi kufika Aprili 2025, Baraza limeratibu matukio ya sanaa 32. Baadhi ya matukio yaliyoratibiwa ni pamoja na Tamasha la 15 la Muziki wa Cigogo lililofanyika Chamwino, Dodoma; Tamasha la Ngoma za Asili la Tulia Trust lililofanyika Mbeya; Wasafi Festival; Nandy Festival; Muziki na Mama; Miaka 60 ya Msondo Ngoma; *Swahili Fashion Week*; *Samia Fashion Show*; *Tanzania Fashion*; na *Anna Fashion Academy*. Vilevile, Baraza limeratibu Tamasha la Muziki wa Dansi " Kadansee la Mama" kwa lengo la kuburudisha umma na kuanzisha kwa mara ya kwanza Tamasha maalumu la muziki huo. Katika usiku wa Tamasha hilo lililofanyika tarehe 01 Februari 2025 jijini Dar es salaam, bendi za muziki wa dansi 11 zilitumbuiza.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na maboresho yaliyofanyika ya kimifumo na rasilimali watu katika kusimamia maadili katika kazi za sanaa, Baraza limeongeza kasi ya kutoa ithibati za nyimbo mbalimbali kwa kuziwekea madaraja. Ongezeko hilo ni kutoka wastani wa nyimbo 200 kwa mwezi hadi nyimbo 800 kwa mwezi ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2025 Baraza limetoa ithibati kwa nyimbo 4,540.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kuhakikisha kazi za sanaa zinaendeshwa kibiashara ikiwa ni pamoja na kukabiliana na changamoto za masoko ambapo, katika kipindi husika wasanii 150 walijengewa uwezo katika kukabiliana na changamoto za masoko na mikataba. Vilevile, Baraza limetoa ushauri na misaada ya kiufundi kwa wasanii na wadau wa sanaa, ushauri wa kitaalamu kuhusu masoko ya kazi za sanaa, usajili na vibali, na matukio ya sanaa umetolewa kwa wasanii binafsi 770, vikundi 54, taasisi 6, kampuni na wadau wengine 21.

### 3.2.3.3 BODI YA FILAMU TANZANIA (TFB)

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Filamu Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura ya 230. Majukumu ya Bodi ya Filamu ni pamoja na kusimamia kazi za filamu na michezo ya kuigiza ikiwamo kuhakiki na kuzipanga katika madaraja; kutoa vibali vya utayarishaji wa filamu; kutoa ithibati za urasimishaji wa shughuli za filamu na michezo ya kuigiza.

Vilevile, Taasisi hii ina jukumu la kuratibu na kuendesha programu mbalimbali za kujenga uwezo na ujuzi wa wadau waliojiajiri/kuajiriwa katika Tasnia ya Filamu nchini kama vile mafunzo ya muda mfupi, matamasha pamoja na tuzo.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliratibu maandalizi ya Tuzo za Kitaifa za Ucheshi *(Tanzania Comedy Awards)* kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu zilizotolewa mwezi Februari 2025 ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Malengo ya tuzo yalikuwa kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya fani ya ucheshi ambavyo vimeendelea kuwa chanzo muhimu cha ajira na kipato kwa wacheshi nchini ambapo jumla ya wasanii wa ucheshi 150 waliingia katika kinyang'anyiro cha tuzo. Kati ya wasanii hao 17 waliibuka washindi na kutwaa tuzo. Aidha, zaidi ya wadau 1,000 walihudhuria katika tuzo hizo




*Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa katika picha ya pamoja na washindi wa Tuzo za Ucheshi Tanzania kwa mwaka 2025 zilizotolewa tarehe 22 Februari 2025 katika Ukumbi wa The Super Dome jijini Dar es Salaam.*

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa vipaji vinaibuliwa na kukuzwa katika Tasnia ya Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini, Bodi ya Filamu iliratibu na kuwezesha uandaaji wa matamasha na tuzo mbalimbali. Matamasha yaliyoandaliwa na tuzo zilizotolewa ni kama ifuatavyo: Tuzo za Filamu kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu (Uni-Awards) ambapo tuzo nne (4) zilitolewa;

Tamasha la Tuzo za Filamu Mkoani Iringa, ambapo tuzo 16 zilitolewa; na Tamasha la Filamu Wilaya ya Kigamboni, ambapo tuzo 41 zilitolewa. Aidha, kulikuwa na Tamasha la Kimataifa la Maendeleo ya Filamu na Sanaa lililofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Desemba 2024 ambapo tuzo 550 zilitolewa.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za kuimarisha weledi na ujuzi kwa wadau wa filamu na michezo ya kuigiza ili waweze kuandaa filamu zenye ubora na shindani ambapo, jumla ya wadau 316 walinufaika kupitia programu hizo ikiwamo warsha ya mafunzo iliyoandaliwa na Bodi ya Filamu mkoani Ruvuma ambapo wadau wa filamu 200 walinufaika. Halikadhalika, Bodi kwa kushirikiana na Taasisi ya *Global Opportunity* Youth *Network* (GOYN) kupitia mradi wa Tanga Yetu iliendesha mafunzo yaliyowanufaisha wanufaika 33 waliopatiwa mafunzo hayo mkoani Tanga. Mafunzo yalilenga kuimarisha ujuzi na weledi katika mnyororo wa utayarishaji wa filamu bora ikiwamo masuala yanayohusu uigizaji, uandishi wa miswada ya filamu, upigaji picha pamoja na Sheria na taratibu zinazosimamia Tasnia ya Filamu.

**152.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, mafunzo mengine yalitolewa kwa mtindo wa Uchambuzi wa Filamu *(Film Screening and Review)* ambayo ni programu inayoratibiwa na Bodi ya Filamu kwa kuwashirikisha waandaaji wa filamu husika ili kuchambua na kutathmini kwa pamoja misingi na ufundi wa utayarishaji wa filamu bora ambapo wadau 18 walinufaika kupitia programu hiyo. Aidha, wasanii 25 wa ucheshi kupitia jukwaa la kibiashara la ucheshi linalojulikana kwa jina la WatuBaki walipatiwa mafunzo yaliyotolewa katika ofisi za Bodi kwa lengo la kuwawezesha kufahamu namna ya kurasimisha kazi zao ili ziwanufaishe zaidi.

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Filamu ilitekeleza Programu ya Filamu Mtaa kwa Mtaa, yenye lengo la kuibua vipaji vya sanaa katika ngazi za mitaa na vijiji kwa kuratibu mchezo wa kuigiza uliofanyika katika Shule ya ekondari ya Vingunguti jijini Dar es Salaam. Mchezo huo ulihusisha wanafunzi 16 na kutazamwa na hadhira ya zaidi ya watu 350. Vilevile, kikundi cha maigizo kiitwacho "Bin Ame Sanaa Group" chenye wadau 24

kilijengewa uwezo wa utayarishaji wa filamu kupitia ziara iliyofanywa na wataalamu wa Bodi wakati wa uaandaaji wa tamthilia yao iitwayo Tajiri Mfupi.

**154.** ***Mheshimiwa Spika***, programu ya kimkakati ya kutetea na kulinda haki za wasanii inayotekelezwa kupitia Kamati ya Haki za Wasanii chini ya uratibu wa Bodi ya Filamu imeendelea kuchukua hatua stahiki za kuhakikisha wasanii wanapata haki zao. Katika kipindi husika, Bodi ya Filamu ilipokea na kushughulikia jumla ya malalamiko matatu (3) kutoka kwa wadau wa sanaa. Kuwapo kwa Kamati hii kumewezesha kupungua kwa malalamiko ya wadau kutoka malalamiko 12 mwaka 2023/24 hadi malalamiko matatu (3) mwaka 2024/25.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bodi ya Filamu imeendelea na hatua za urasimishaji wa shughuli za Filamu na Michezo ya Kuigiza ambapo katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi mwezi Aprili 2025 jumla ya leseni 154 za uendeshaji wa shughuli hizo zimetolewa. Aidha, katika jitihada za kuendelea kuwatambua wasanii wanaojihusisha na shughuli za Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini, Bodi imetoa vitambulisho 168 kwa wasanii hao hatua ambayo inawafanya waingie katika mfumo rasmi wa Serikali.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Wizara kupitia Bodi ya Filamu kwa kushirikiana na BASATA imejenga mfumo wa Wasanii (AMIS) unaowezesha utoaji wa huduma na kuwafikia wadau katika maeneo mengi zaidi nchini ili kuwatambua na kuwarasimisha bila kulazimika kufika ofisi za Bodi. Naomba kutumia fursa hii kuwaelekeza wasanii wote nchini kujisajili kwenye mfumo wa AMIS (*Artist Management Information System)* ambao unatumiwa na Serikali kuwatambua rasmi pamoja na shughuli zao.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika Bodi ilipokea maombi 224 ya utayarishaji wa filamu ambapo yote yalishughulikiwa na kupatiwa vibali. Kati ya maombi hayo, 145 yalikuwa ya waombaji kutoka ndani ya nchi na 79 ya kutoka nje ya nchi. Katika kipindi hicho takribani fursa za ajira 553 zilizalishwa

na kuwanufaisha Watanzania kupitia vibali 79 vya utayarishaji wa filamu vilivyotolewa kwa waombaji kutoka nje ya nchi.

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Bodi ya Filamu ilifanya ukaguzi wa maudhui ya filamu 199 na kuzipanga katika madaraja. Kati ya filamu hizo kulikuwa na filamu ndefu 150 ambapo kati yake filamu 121 zilikuwa za Kitanzania na filamu 29 zilikuwa za kutoka nje ya nchi. Kwa upande wa tamthilia, jumla ya tamthilia 49 zenye jumla ya sehemu *(Episodes)* 1,247 zilihakikiwa ambapo tamthilia 11 zilitayarishwa na Watanzania na tamthilia 38 zilitoka nje ya nchi. Kupitia uzalishaji na uhakiki wa filamu na tamthilia hizo, takribani ajira 4,758 zilizalishwa. Eneo hili pekee limewezesha upatikanaji wa mapato ya moja kwa moja ya zaidi ya Shilingi Bilioni Tatu (Shilingi 3,000,000,000).

### 3.2.3.4 TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) ilianzishwa kwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, Sura ya 218. Majukumu ya Ofisi ya Hakimiliki Tanzania ni pamoja na kukuza na kulinda maslahi ya watunzi, waandishi, wasanii, wafasiri, watayarishaji, wa kurekodi sauti, watangazaji, waongozaji na wachapishaji kwa kulinda haki zao. Aidha, Ofisi hii ina jukumu la kutunza rejista za kazi za usanii na vyama vya watunzi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa sauti zilizorekodiwa, watangazaji na wachapishaji.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COSOTA imesimamia ukusanyaji wa mirabaha katika madaraja ya kazi ambazo hazisimamiwi na kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha (CMO) ambapo Wizara kupitia COSOTA, imekusanya kiasi cha Shilingi 847, 985,594.26 za mirabaha kutokana na Tozo ya Hakimiliki (Copyright Levy). Tozo hii ni mirabaha inayotokana na matumizi ya kazi za sanaa na zinatarajiwa kugawiwa kwa mchanganuo ufuatao: asilimia 10 ambayo ni Shilingi 84,798,559.43 zitagawiwa kwa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania; asilimia 60 sawa na Shilingi 508,791,356.56 zitagawiwa kwa wasanii; asilimia 20 sawa na Shilingi 169,597,118.85 kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za

COSOTA na asilimia 10 sawa na Shilingi 84,798,559.43 ni gawio la Serikali.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Hakimiliki kuhusu ukusanyaji wa mirabaha kwa madaraja ya kazi mbalimbali, COSOTA inakamilisha Kanuni mbalimbali zitakazosaidia ukusanyaji na ugawaji mirabaha. Kanuni hizo ni pamoja na Kanuni za Haki ya Kunufaika na Mauzo Endelevu *(Rights to Benefit from Resale)* ili kuwanufaisha wasanii wa sanaa za ufundi pale kazi zao zinapouzwa nchini au nje ya nchi baada ya mauzo ya kwanza.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia, Ofisi ya Hakimiliki (COSOTA) ilitoa mafunzo kwa wadau wa Sekta za Sanaa na Utamaduni. Mafunzo hayo yalikusudia kuwajengea uwezo kuhusu masuala ya Hakimiliki ambapo wadau milioni moja (1,000,000) walifikiwa. Aidha, mafunzo hayo yaliendeshwa kwa njia mbalimbali ikiwamo Kampeni ya "Hakimiliki Yako Hailiki Kamata Fursa Twenzetu" ambayo ilitekelezwa kupitia vipindi 38 katika redio na televisheni mbalimbali nchini. Baadhi ya vyombo vya habari vilivyotumika ni TBC1, Wasafi FM, Clouds Fm, Times FM, Azam Tv, Sinema Zetu, Mjini FM, Crown Fm, EFM, E TV, Channel 10, EATV, Uhuru Fm, Bongo FM, Singeli Media, Island Fm, Majimaji Fm, Mtwara Fm na Uhuru FM. Vilevile, COSOTA imefanya kampeni za kutoa elimu kupitia mitandao ya kijamii na kushiriki katika maonesho mbalimbali.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kupambana na uharamia wa kazi za ubunifu Wizara kupitia COSOTA imetekeleza operesheni tatu (3) ambapo kazi haramu zenye thamani ya zaidi ya Shilingi 75,000,000 zilikamatwa na kuteketezwa.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha usimamizi wa maslahi ya kazi za wasanii COSOTA imefanikiwa kuanzisha na kusimamia kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha *(Collective Management Organizations – CMOs)* kwa madaraja ya kazi za muziki, sanaa za ufundi, sanaa za maonesho, filamu na kazi za maandishi. Katika kutekeleza jukumu hili COSOTA imetoa leseni kwa kampuni ya *Tanzania Music Rights Society (TAMRISO)*. Aidha,

elimu imeendelea kutolewa kwa wadau mbalimbali ili waweze kuanzisha kampuni nyingine zinazohusiana na kazi hizo.

### 3.2.3.5 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**165.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania ulianzishwa kwa Sheria ya Ujumuisho wa Wadhamini, Sura ya 318 na kupewa Hati ya Usajili Na.1776 mwaka 2020. Lengo la Mfuko ni kuinua ubora wa kazi za utamaduni na sanaa ili ziweze kujiendesha kibiashara na kuchangia katika pato la Taifa. Majukumu ya Mfuko ni: kutoa huduma ya mikopo ya riba nafuu kwa wadau wa utamaduni na sanaa; kutoa mafunzo ya uzalishaji wa kazi bora zinazokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi; kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi iliyowezeshwa na Mfuko.

**166.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuupatia fedha Mfuko huu kwani umekuwa suluhisho kwa changamoto ya mitaji kwa wadau wa utamaduni na sanaa nchini tangu kuhuishwa kwake. Mfuko huu umewezesha utoaji wa mikopo yenye thamani ya Shilingi 5,250,070,500.89 kwa miradi 359 ya utamaduni na sanaa katika mikoa 19 nchini hadi kufikia Aprili 2025.

**167.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Mfuko umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 2,692,217,069.89 kwa miradi 143 ya utamaduni na sanaa. Mikopo hiyo imewanufaisha wadau wanaojihusisha na shughuli mbalimbali za utamaduni na sanaa zikiwamo filamu, muziki, ufundi, maonesho pamoja na lugha na fasihi. Aidha, eneo la filamu limewezeshwa miradi 37 yenye thamani ya Shilingi 645,130,090 ambayo iliwezesha mitaji na ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa studio 21 za utayarishaji wa filamu na tamthilia. Katika eneo la ufundi miradi 59 yenye thamani ya Shilingi 997,129,629.89 imewezeshwa ambapo jumla ya vyuo 5 viliwezeshwa na katika eneo la maonesho miradi 19 yenye thamani ya Shilingi 349,988,000 imewezeshwa ambapo washereheshaji 9 na watoa huduma 10 waliwezeshwa.

**168.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhamasisha uzalishaji wa kazi bora za muziki, miradi 23 yenye thamani ya Shilingi 592,280,750 iliwezeshwa katika kipindi husika. Uwezeshaji huo umesaidia ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kisasa ikiwamo vifaa vya studio 7, vifaa vya bendi 5 za muziki wa injili, vifaa vya bendi 3 za muziki wa dansi na vifaa vya bendi 2 za muziki wa taarabu.

**169.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko unatoa huduma kwa makundi mbalimbali ambapo kupitia miradi 143 iliyowezeshwa, miradi 13 inayomilikiwa na kampuni iliwezeshwa Shilingi 444,747,000; miradi 17 inayomilikiwa na vikundi vya bendi iliwezeshwa Shilingi 325,870,000; miradi 48 inayomilikiwa na wanawake iliwezeshwa Shilingi 715,600,000 na miradi 65 inayomilikiwa na wanaume iliwezeshwa Shilingi 1,206,000,069.89.

**170.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika kuhakikisha wasanii na wadau wa sanaa wanaandaa kazi za sanaa zilizo bora na zitakazomudu ushindani wa soko la kitaifa na kimataifa, Mfuko umetoa mafunzo na kuwajengea uwezo wasanii 3,895 wakiwamo wanawake 2,306, sawa na asilimia 59.2 na wanaume 1,589, sawa na asilimia 40.8. Mafunzo hayo yalilenga mada zifuatazo: Uandishi wa Maandiko ya Miradi, Fursa za Mitaji, Urasimishaji, Biashara na Familia, Sanaa na Afya, Mafao ya Jamii, Fursa za Uchumi na Uwekezaji pamoja na Uwekaji wa Akiba.

**171.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko umekuwa daraja la urasimishaji wa kazi za utamaduni na sanaa katika mamlaka mbalimbali za Serikali ambapo hadi kufikia Aprili 2025 jumla wasanii 8,154 wamefanya urasimishaji wa kazi zao katika maeneo mbalimbali. Kutokana na umuhimu huu, Mfuko umechochea na kuhamasisha urasimishaji wa kazi za utamaduni na sanaa ambapo wasanii 1,963 walifungua akaunti za benki katika Benki za CRDB na NBC, wasanii 117 walijisajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kupata namba za Walipa Kodi (TIN), wasanii 84 wamejisajili BRELA na kupata majina ya biashara, na kampuni 28 zimefunguliwa. Fauka ya hayo, wasanii 235 wamesajaliwa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ili kupata vyeti vya usajili, wasanii 283 walihuisha vibali vya kazi za sanaa, na wasanii 458 walitambuliwa na Bodi ya Filamu Tanzania kuwa wasanii wanaotekeleza kazi mbalimbali katika Sekta ya Filamu.

**172.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko umeimarisha utoaji wa habari kwa umma, mawasiliano na ushawishi kwa kutangaza huduma zake ili wadau wa utamaduni na sanaa waweze kufahamu huduma hizo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Mfuko umechapisha vipeperushi 5000, elimu kwa umma imetolewa kwa njia ya vyombo vya habari 21, ambazo ni redio 9 na runinga 12 pamoja na kufanya mahojiano maalumu katika redio 3 na runinga 2.

**173.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kufuatilia matumizi sahihi ya fedha za miradi ya wanufaika halikadhalika kubaini matokeo ya uwezeshaji kiuchumi kwa mnufaika mwenyewe, jamii na nchi kwa ujumla wake, Mfuko umefanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi ya sanaa 126. Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini hiyo yalibainisha kuwa asilimia 89 ya wanufaika walikamilisha malengo ya fedha walizonufaika nazo ambapo baadhi yao wamefanikiwa kuongeza vifaa vyenye ubora wa kuzalisha kazi za sanaa zenye viwango bora zaidi vya utengenezaji wa filamu na muziki. Aidha, asilimia 27 ya wanufaika wameweza kujiunga na programu za bima za afya, hivyo, kupunguza mzigo wa gharama za matibabu kwao na familia zao. Vilevile, ajira 1987 za moja kwa moja na ajira 8,253 zisizo za moja kwa moja zilizalishwa kupitia miradi ya sanaa iliyowezeshwa na Mfuko.

### 3.2.3.6 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatuwezi kuendeleza sanaa bila kuwekeza katika utaalamu na utafiti. TaSUBa ni miongoni mwa taasisi zinazosimimamiwa na Wizara. Taasisi hii ilianzishwa tarehe 2 Novemba 2007 na Tangazo la Serikali Na. 220 chini ya Sheria ya Wakala Na. 30 ya Mwaka 1997. TaSUBa inatoa mafunzo ya aina mbalimbali kuhusiana na masuala ya sanaa na utamaduni nchini. Katika mwaka 2012, TaSUBa iliteuliwa kuwa Kituo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki chenye Ubora Uliotukuka *(Centre of Excellency)* katika ufundishaji wa fani za utamaduni na sanaa, hivyo, ni kituo chenye hadhi ya kimataifa.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee napenda kuitumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi zake kubwa katika kuiwezesha TaSUBa kifedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Katika mwaka 2024/25 TaSUBa imefanikiwa kununua vifaa bora na vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya majengo ya Taasisi. Hatua hizo zimewezesha kuongeza udahili wa wanachuo kwa kiwango kikubwa na hivyo kuongeza idadi ya wanataaluma kwenye fani ya ubunifu, sanaa na utamaduni ambao wanakwenda kujiajiri na kuajiriwa kama maafisa utamaduni kwenye mikoa, halmashauri za wilaya manispaa na taasisi zetu ili kukuza na kulinda mila, destuli na utamaduni wa Mtanzania.

**176.** ***Mheshimiwa Spika***, mafunzo yanayotolewa na Taasisi hii, yanafundishwa kwa vitendo kwa asilimia 70 na nadharia kwa asilimia 30 katika kozi za Filamu na Uzalishaji wa Vipindi vya Televisheni (Film and TV Production); Uzalishaji wa Muziki na Sauti (Music and Sound Production); na Sanaa za Maonesho na Ufundi (Performing and Visual Arts). Hii inaonesha ni kwa jinsi gani wanachuo wanapohitimu mafunzo yao ni rahisi kuingia kwenye soko la ajira kwa kuajiriwa au kujiajiri wenyewe katika tasnia ya sanaa na utamaduni ndani na nje ya nchi.

**177.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha Taasisi inapanua wigo wa mafunzo na kuongeza udahili kwa kutoa nafasi zaidi kwa vijana wa Kitanzania kujiunga na sekta ya sanaa na ubunifu, Taasisi iko kwenye hatua za maboresho ya mitaala mipya mitatu ambayo itawezesha kuwapo kwa kozi mpya. Kozi hizo ni Usimamizi wa Sanaa na Masoko katika Sanaa (Arts Management and Marketing), ambayo ina lengo la kumwandaa Afisa Masoko kutafuta masoko kwa msanii na kazi yake, ndani na nje ya nchi; Urithi wa Utamaduni na Utalii (Cultural Heritage and Tourism). Kozi hii itamwezesha mhitimu kuingia kwenye soko la utalii wa kiutamaduni ambao kwa sasa unakua kwa kasi kubwa sana duniani. Wizara kupitia TaSUBa itahakikisha mafunzo ya kozi hizi yataanza mara tu baada ya kukamilika kwa mapitio ambayo NACTVET imeshauri ili kupata Ithibati.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo

(TaSUBa) hivyo kuiwezesha taasisi hii kuweka mikakati mbalimbali ambayo imesaidia kuongeza udahili wa wanachuo. Hadi mwezi Aprili 2025 Taasisi imefanikiwa kudahili jumla ya wanachuo 947 wa kozi ndefu sawa na ongezeko la asilimia 118.3 ya lengo lililowekwa la kudahili wanachuo 800. Aidha, Taasisi inaendesha mafunzo ya muda mfupi ambayo hata yule ambaye amekosa vigezo vilivyowekwa na NACTVET vya kuingia kama mwanachuo wa kozi ndefu anayapata. Hii ni njia ya kuwafikia vijana wengi wenye vipaji na kuboresha vipaji vyao. Kwa upande wa mafunzo ya kozi fupi Taasisi ilikuwa na lengo la kupata wanachuo 300 lakini katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 washiriki 289 wamepatiwa mafunzo haya sawa na asilimia 96 ya lengo. Takwimu hizo zimedhihirisha mafaniko makubwa kwa Taasisi hii.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha taasisi inajitangaza na kutambulika kitaifa na kimataifa, TaSUBa imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kutangaza Taasisi (Communication Strategy) ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2025 imefanya ziara 4 katika Vituo vya Habari pamoja na kujitangaza katika vyombo 6 vya habari. Vilevile, TaSUBa imeendelea kutumia kurasa zake za mtandaoni za Instagram (tasuba.bagamoyo), Facebook (Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo), Youtube (TaSUBa TV), na X zamani Twitter (TAASISISANAA) kutoa elimu na taarifa mbalimbali kwa jamii kuhusiana na masuala ya Utamaduni na sanaa. Aidha, TaSUBa imeweza kutumia blogu mbalimbali katika kufikisha taarifa kwa jamii hali iliyowezesha kuongezeka kwa udahili.

**180.** ***Mheshimiwa Spika*****,** TaSUBa imeendelea kuwa kinara katika utoaji wa mafunzo. TaSUBa imeendelea kuwawezesha kitaalamu wadau wa utamaduni na sanaa kwa kuendesha mafunzo maalumu kwa vyama, mashirikisho, asasi zisizo za serikali na taasisi binafsi lengo likiwa ni kuwajengea uwezo katika utekelezaji wa shughuli za utamaduni na sanaa na kuwa mahiri katika tasnia zao ili waweze kukuza pato binafsi na Taifa kwa ujumla. Aidha, TaSUBa kwa kushirikiana na Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Tanzania (TCTA) imeendesha mafunzo kwa maafisa 36 wa Jeshi la Magereza. Vilevile Taasisi iliendesha mafunzo kwa viongozi wa mashirikisho ya sanaa 14 (Ke 4 na Me 10).

**181.** ***Mheshimiwa Spika*,** vilevile, TaSUBa kwa ushirikiano na asasi ya "*Musicians for a Better Life*" kutoka nchini Ujerumani iliendesha mafunzo ya muziki wa kuimba na ala kwa wanachuo na wadau 79 kutoka mikoa mbalimbali. Pia, TaSUBa imeendesha mafunzo ya uimbaji na upigaji wa ala za muziki kwa waumini wa Waadiventista Wasabato ikiwa ni awamu ya 13 iliyofanyika kati ya tarehe 9 Septemba 2024 hadi tarehe 5 Oktoba 2024 ambapo kulikuwa na jumla ya washiriki 42 (Ke 11 na Me 31). Aidha, mafunzo ya awamu ya 14 yalifanyika kuanzia tarehe 10 Februari 2025 hadi tarehe 8 Machi 2025 ambapo kulikuwa na washiriki 40 (Ke 9 na Me 31).

**182.** ***Mheshimiwa Spika***, moja ya jukumu la Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ni kuendesha Tamasha la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 Taasisi iliendesha Tamasha la 43 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo lililofanyika tarehe 23 hadi 26 Oktoba 2024 katika Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. Tamasha hili hufanyika kila mwaka likiwa na lengo la kupima kiwango cha maendeleo ya sanaa na utamaduni, kuibua, kukuza, kuendeleza na kutangaza vipaji na kazi za wasanii. Tamasha lilifunguliwa tarehe 23 Oktoba 2024 ambapo lilikuwa na jumla ya vikundi 78 vikijumuisha vikundi 67 kutoka ndani ya nchi na vikundi 11 kutoka nje ya nchi. Vikundi vya nje vilivyoshiriki ni kutoka nchi zifuatazo;- vikundi 3 kutoka Visiwa vya Mayotte, vikundi 3 kutoka Zambia, vikundi 2 kutoka Ujerumani, kikundi 1 kutoka Uhispania, kikundi 1 kutoka India na kikundi 1 kutoka Brazili. Tamasha lilihusisha maonesho ya sanaa za jukwaani kama vile maigizo na ngoma za asili, sanaa za muziki, maonesho ya filamu, sanaa za ufundi, huduma za biashara, kongamano na mafunzo. Tamasha lilihudhuriwa na watazamaji wa ndani na nje zaidi ya 46,326.



*Kikundi cha ngoma cha wanafunzi kutoka Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) kikitoa burudani wakati wa Tamasha la 43 la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo lililofanyika Bagamoyo tarehe 23 – 26 Oktoba 2024.*

### 3.2.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

#### 3.2.4.1 IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO

**183. *Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Michezo ni nyenzo muhimu ya kuzalisha ajira, kuimarisha afya za wananchi pamoja na kuwaletea furaha Watanzania. Pia, kupitia sekta ya michezo nchi yetu inaendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali kupitia diplomasia ya michezo. Kwa kutambua umuhimu huo Serikali inao wajibu wa kujenga mazingira rafiki kwa ukuaji wa sekta ya michezo. Sekta hii kwa sasa inatekeleza majukumu yake kwa kufuata Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 pamoja na Mkakati wa Maendeleo ya Michezo wa mwaka 2022. Sekta hii ni miongoni mwa mihimili inayotoa ajira na kuchangia katika uchumi wa mtu mmojammoja na Taifa kwa ujumla. Aidha, Sekta hii inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Michezo na taasisi zilizo chini yake ambazo ni Baraza la Michezo la Taifa (BMT), na Chuo cha Maendeleo ya michezo Malya. Katika kutekeleza majukumu yake Wizara kupitia Sekta hii imetekeleza majukumu yafuatayo:

**184. *Mheshimiwa Spika***, ikumbukwe kuwa mwaka 2023 Tanzania ilipata heshima ya kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu Barani Afrika (AFCON2027) kwa kushirikiana na

nchi za Kenya na Uganda ambapo ujio wa mashindano hayo unatarajiwa kuleta fursa mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni nchini. Sambamba na mashindano hayo, Tanzania pia imepata fursa ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya CHAN 2024 yatakayofanyika katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda mwezi Agosti 2025 ambayo ni sehemu ya maandalizi ya mashindano ya AFCON 2027. Ujio wa Mashindano ya CHAN na AFCON yataiIetea nchi yetu fursa lukuki za kiuchumi zikiwamo kuvutia utalii, kuzalisha ajira, kuitangaza Tanzania kimataifa, pamoja na kuwa na miundombinu ya kisasa ya michezo. Haya ni mafanikio makubwa kwa Sekta ya Michezo yaliyotokana na maono na dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muunganano wa Tanzania katika kuendeleza Sekta ya Michezo nchini.

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika kwa ufanisi mkubwa, Serikali kupitia Wizara imeendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya michezo ikiwamo ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru na ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu wa Arusha na Dodoma. Aidha, Serikali inaendelea na ukarabati na ujenzi wa viwanja vitano vya mazoezi vitakavyotumika wakati wa michuano hiyo vilivyopo jijini Dar es Salaam. Serikali pia imejipanga kujenga viwanja vingine vitano (5) vya mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya AFCON 2027 jijini Arusha. Sambamba na hayo Serikali pia inaendelea na ujenzi wa Akademia ya Michezo Malya pamoja na ujenzi wa hosteli ya Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee naomba kupitia Bunge lako tukufu kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa kukubali kutoa fedha za kuwezesha ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu wa Arusha ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua watazamaji (32,000). Uwanja huu si tu utatumika kwa mchezo wa soka bali pia utaweza kutumika kwa ajili ya mashindano ya riadha ya kimataifa. Ujenzi wa Uwanja huu unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Juni 2026 ambapo unatarajiwa kutoa fursa za kiuchumi kwa nchi kwa kuchochea uzalishaji wa ajira, ukuaji wa sekta ya utalii, biashara na uwekezaji katika jiji la Arusha na nchi kwa ujumla.

**187.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na ujenzi wa uwanja wa mpira wa Arusha, Serikali pia imeanza ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu jijini Dodoma katika kata ya Nzuguni ambao ni sehemu ya maandalizi ya AFCON2027 na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020/2025. Kukamilika kwa mradi huu kutakwenda kuchagiza fursa mbalimbali za kimaendeleo kupitia sekta ya michezo, utalii, utamaduni na sanaa na hivyo kuinua uchumi wa nchi na kuongeza idadi ya viwanja vyenye ubora wa viwango vya kimataifa nchini.

**188.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia imeendelea na ujenzi wa viwanja vya mazoezi na kupumzikia wananchi. Ujenzi wa Viwanja vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi *(Recreational and Sports Centres*) unatekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam na Dodoma ambapo kwa upande wa Dar es Salaam mradi umefikia asilimia 46 na Dodoma mradi huu umefikia asilimia 65. Kukamilika kwa mradi huu kutatoa fursa kwa wananchi wa Dar es Salaam, Dodoma na Taifa kwa ujumla kuwa na viwanja vya kutosha vya mazoezi kwa ajili ya michezo mbalimbali ikiwamo, viwanja vya mpira wa mikono, viwanja vya mpira wa miguu, mpira wa wavu, netiboli, mpira wa kikapu, tenisi, na mchezo wa kuogelea.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na ukarabati mkubwa wa kiwanja cha Benjamin Mkapa ambapo ukarabati huu umejumuisha maeneo ya vyumba vya wachezaji *(Dressing room);* na maeneo ya waandishi wa habari **(***Media tribune and Press conference)*. Maeneo mengine ni kufunga viti vipya na kuondoa vya zamani ambapo hadi kufika Aprili 2025 jumla ya viti 40,000 vimewasili na vinaendelea kufungwa; kukarabati eneo la mchezo wa riadha kwa kuondoa na kuweka *tatan* mpya; mifumo ya viyoyozi; mifumo ya mtandao wa intaneti; mifumo ya majitaka ikiwamo vyoo; kupaka rangi sehemu mbalimbali; kuondoa na kufunga taa mpya ambapo jumla ya taa 352 zimefungwa; kuondoa na kufunga milango mipya; kukarabati jukwaa la viongozi; na kuondoa na kupanda nyasi mpya sehemu ya kuchezea. Kwa ujumla ukarabati wa uwanja huu umefikia asilimia 80.

**190.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Uwanja wa Uhuru, ukarabati mkubwa wa uwanja huo umefikia asilimia 7. Maboresho

yanayofanyika katika Uwanja huu yanajumuisha eneo la kuchezea (pitch), kuweka viti, mfumo wa maji, mfumo wa umeme, TEHAMA na upakaji rangi.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi na ukarabati wa viwanja hivi haulengi tu mashindano ya AFCON 2027 na CHAN 2024, bali una faida kubwa kwa Taifa letu katika maeneo mbalimbali. Uimarishaji wa miundombinu ya michezo utasaidia kuendeleza vipaji vya vijana wetu. Tunapokuwa na viwanja bora na vya kisasa, vijana wetu wanapata fursa ya kufanya mazoezi katika mazingira salama na ya kisasa jambo litakalosaidia kukuza vipaji vyao.

**192.** ***Mheshimiwa Spika***, pia Sekta ya Michezo ni chanzo muhimu cha ajira. Kupitia maboresho hayo, vijana wengi watapata nafasi ya kujiajiri kama wanamichezo, wahudumu wa viwanja pamoja na shughuli za ujasiriamali katika maeneo yenye miundombinu ya michezo. Aidha, viwanja hivi vitasadia katika kuimarisha afya na ustawi wa jamii ambapo wananchi watapata sehemu nzuri za kufanyia mazoezi. Vilevile, viwanja vitachangia katika ukuaji wa uchumi kwa kuongeza mapato ya Serikali kupitia utalii wa kimichezo.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu mashindano mbalimbali ya kimataifa yakiwamo mashindano ya Michezo ya Olimpiki yaliyofanyika jijini Paris, Ufaransa mwezi Julai hadi Agosti 2024. Katika mashindano hayo jumla ya wachezaji saba (7) walishiriki ambapo mchezo wa riadha ulihusisha wachezaji wanne (4), mchezo wa kuogelea wachezaji wawili (2) na mchezo wa judo mchezaji mmoja (1). Aidha, nchi inafanya vizuri katika mashindano ya kimataifa. Serikali imeandaa mkakati maalumu wa kuongeza ufanisi katika ushiriki wa michezo ya kimataifa.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuimarisha diplomasia ya michezo, imeweza kushiriki katika mikutano kadhaa kuhusu Sekta ya Michezo ya kitaifa na kimataifa. Baadhi ya mikutano hiyo ni pamoja na; mkutano wa kimataifa wa usalama michezoni uliofanyika jijini Nairobi kuanzia tarehe 02 - 04 Desemba 2024. Ushiriki huo umeiwezesha Serikali kuweka mikakati madhubuti ya kuboresha usalama katika mashindano na matukio ya michezo

yanayofanyika nchini na kuhakikisha michezo inafanyika katika mazingira salama.

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia, imeshiriki katika mafunzo ya uandaaji wa matukio makubwa ya kimichezo yaliyofanyika nchini China mwezi Agosti 2024. Kupitia mafunzo hayo watendaji wa Serikali walijengewa uwezo kuhusu uratibu wa matukio makubwa ya kimichezo yaliyoko mbele yetu yakiwamo ya CHAN 2024 na AFCON 2027.

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha michezo katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara imeratibu kikao kazi cha mwaka cha Maafisa Michezo Tanzania Bara. Kikao hiki kimefanyika sambamba na kikao kazi cha Maafisa Utamaduni nchini kuanzia tarehe 22-26 Aprili 2025 jijini Dar es Salaam. Kikao kazi hiki kimejadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya michezo nchini yakiwamo utendaji kazi wa vitengo vya michezo na utamaduni katika ngazi za halmashauri nchini.

**197.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuunga mkono juhudi za kimataifa za kupambana na dawa na mbinu haramu michezoni *(anti-doping),* Wizara katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2024 imekuwa mwenyeji wa mkutano wa mwaka wa Kanda tano (V) Afrika kuhusu Mapambano ya Kuzuia Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni *(Antidoping)*. Mkutano huo ulifanyika tarehe 27 Septemba 2024 jijini Dar es Salaam, Tanzania ambapo jumla ya nchi 13 zilishiriki. Kupitia mkutano huo majadiliano na mikakati mbalimbali kuhusu kukabiliana na matumizi ya dawa na mbinu haramu michezoni iliwekewa mipango ya utekelezaji.

**198.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa timu ya Taifa ya soka inakuwa imara kwa ajili ya kujiandaa kwa mashindano ya AFCON 2027, mipango kadhaa imeandaliwa kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF). Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuwatumia wanamichezo wanaochezea nchi nyingine ambao wana asili ya Tanzania (Diaspora). Wachezaji hao hakika wameleta tija na hamasa katika timu yetu ya Taifa Stars. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuridhia kuwatumia vijana hao wa

diaspora katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. Mkakati mwingine ni kuandaa timu imara za Taifa kwa kuwa na timu tatu za vijana ambazo ni vijana chini ya miaka 17 (itakayotokana na mashindano ya UMISETA na UMITASHUMTA); vijana chini ya miaka 20 na vijana chini ya miaka 23 kutoka katika vilabu mbalimbali. Aidha, makocha wazoefu wataajiriwa na huduma za timu hizi zitasimamiwa kama programu maalumu. Kupitia mikakati hii tunaamini tutapata timu imara itakayotumika katika mashindano yajayo ya AFCON 2027 na mashindano mengine ya kimataifa.

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia imeratibu mashindano ya michezo ya shule za msingi na sekondari kitaifa za Afrika Mashariki (FEASSA) kwa mwaka 2024/25 yaliyofanyika kuanzia tarehe 16 hadi 26 Agosti 2024 Mbale nchini Uganda. Jumla ya washiriki 509 kutoka Tanzania walishiriki michezo hiyo ambapo wanafunzi walikuwa 423, na walimu na viongozi 86. Mashindano hayo kwa jumla yamekuwa na manufaa makubwa katika upatikanaji wa vipaji vya michezo mbalimbali hapa nchini. Fauka ya hayo, kwa sasa Wizara zinazohusika zipo katika maandalizi ya mashindano ya kitaifa ya UMISETA na UMITASHUMTA yanayotarajiwa kufanyika mwezi Juni 2025 mkoani Iringa. Michezo hii ni tanuri muhimu la kuibua vipaji kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nchini kote.

**200.** ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kujiimarisha zaidi katika Sekta ya Michezo nchi yetu imepata nafasi ya kuwa mwenyeji wa makao makuu ya Sekretarieti ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya 4, inayoundwa na mataifa ya Comoro, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Madagascar, Mauritius, Rwanda, Seychelles, Somalia, Sudani, Sudan Kusini, Tanzania na Uganda. Tumeiwezesha ofisi ya sekretarieti kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa na Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya 4. Katika kutekeleza majukumu haya, hadi kufikia mwezi Aprili 2025, tayari ofisi ya Makao Makuu ya Sekretarieti ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya 4, imeshaanzishwa jijini Dodoma, ikiwa imewezeshwa kuwa na watumishi, vitendea kazi na samani. Juhudi za kuiimarisha zaidi ofisi hii zinaendelea. Aidha, Sekretarieti ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya 4 imeweza kuratibu Mkutano wa kwanza wa Baraza la Ushauri la

Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya 4 uliofanyika kwa mafanikio tarehe 14-18 Oktoba 2024 jijini Dar es Salaam.

**201.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto za uendeshaji wa miundombinu ya michezo nchini, Wizara imeanza mchakato wa kuanzisha chombo maalumu cha usimamizi wa miundombinu ya michezo nchini *(Sports Infrastracture Management Agency - SIMA)*. Chombo hiki kitakuwa na mamlaka ya kusimamia uendeshaji, ukarabati na matunzo ya miundombinu yote ya michezo nchini. Hiyvo, ni matumaini yetu kwamba kuwapo kwa chombo hiki kutapunguza changamoto za usimamizi wa miundombinu na kutaongeza thamani ya miundombinu ya michezo nchini.

**3.2.4.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)**

**202.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kudhibiti aina zote za michezo ya ridhaa na kulipwa nchini kwa kushirikiana na wadau wa michezo vikiwamo Vyama na Mashirikisho ya Michezo; kusajili Vyama na Vilabu vya Michezo; kutoa Tuzo kwa Wanamichezo wanaofanya vizuri katika mashindano ya Kitaifa na Kimataifa; na kuamsha ari ya wananchi kupenda na kushiriki katika aina zote za michezo nchini.

**203.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuleta hamasa na mwamko kwa wananchi kushiriki katika maandalizi ya mashindano ya CHAN 2024 na AFCON 2027, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) iliratibu kongamano la wadau wa michezo kuhusu kushiriki katika maandalizi ya mashindano ya CHAN 2024 na AFCON 2027 lililofanyika tarehe 15 Januari 2025 jijini Dar es Salaam. Mgeni rasmi katika kongamano hilo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati. Mada kuu katika kongamano hilo ni maandalizi ya Tanzania kuwa mwenyeji katika mashindano ya CHAN 2024 pamoja na AFCON 2027.




*Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.) Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati akiwa kwenye picha ya pamoja na wadau mbalimbali wa michezo katika kongamano la wadau wa michezo kuelekea michuano ya CHAN na AFCON Januari 15 2025 jijini Dar es Salaam.*

**204.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia BMT imeendelea na uratibu wa matukio ya kimataifa ya michezo ambayo Timu za Taifa zimewezeshwa kushiriki katika mashindano mbalimbali. Michezo ambayo Timu za Taifa zimeshiriki ni pamoja na Michezo ya kufuzu Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025) na CHAN 2024; Mashindano ya Olimpiki yaliyofanyika tarehe 14 – 30 Julai 2024 nchini Ufaransa; Mashindano ya timu za Taifa za kuogelea ya Kanda ya Tatu maarufu kama *Africa Aquatics Zone III* yaliyofanyika nchini Burundi tarehe 22 - 24 Novemba 2024; Michezo iliyochezwa na timu ya Taifa ya mpira wa miguu ya wanawake chini ya umri wa miaka 17 (Serengeti Girls); na Michezo ya AFCON chini ya umri wa miaka 17 ambayo timu ya Taifa ya mpira wa miguu ya wanaume chini ya umri wa miaka 17 (Serengeti Boys) imefuzu. Michezo mingine ni fainali za Mataifa ya Afrika kwa Walemavu (AAFCON) iliyofanyika nchini Misri; na Michezo ya fainali za Mataifa ya Afrika (WAFCON) kwa wanawake itakayofanyika nchini Morocco kuanzia tarehe 05 – 26 Julai 2025 ambayo Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) imefuzu; na mashindano ya Dunia yaliyofanyika jijini Budapest, Hungary kuanzia tarehe 10 – 15 Desemba 2024 ambapo Timu ya Taifa ya Kuogelea ilishiriki, Timu ya Taifa ya Mpira wa miguu kwa

wanaume (Taifa Stars) katika mechi ya kufuzu kombe la Dunia iliyofanyika nchini Morocco.


*Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Mpira wa miguu Taifa Stars wakishangilia ushindi dhidi ya timu ya Taifa ya Guinea baada ya kufuzu kucheza mashindano ya AFCON yatakayofanyika nchini Morocco mwaka 2025.*

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa kwa kushirikiana na Ubalozi wa Ufaransa nchini limeendelea kutekeleza mpango wake wa mafunzo kwa walimu wa michezo wa shule za msingi na sekondari kupitia mradi wa michezo kwa jamii *(Community Sports Program)*. Mafunzo hayo yalitolewa kwa walimu wa michezo wa shule za msingi na sekondari 280 katika Halmashauri za Wilaya za Liwale 40, Ruangwa 60, Muheza 40, Manispaa ya Songea 60, Kwimba 40 na Bukombe 40. Mpango huo unalenga kuhakikisha kuwapo kwa walimu wa michezo wenye sifa stahiki katika ngazi za chini (Grassroot level).

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Baraza limetoa elimu ya usimamizi na utatuzi wa migogoro katika vyama na mashirikisho kwa viongozi 269 katika Halmashauri za Tabora viongozi 50, Shinyanga 50, Kakonko 52, Manispaa ya Kigoma 30, Manispaa ya Mpanda 41 pamoja na Manispaa ya Sumbawanga 46.

**207.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2024/25 Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika mashindano na michezo mbalimbali ambapo Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake (Twiga Stars) ilifuzu kucheza mashindano ya WAFCON yanayotarajiwa kufanyika mwezi Julai 2025 nchini Morocco. Aidha, timu yetu ya Taifa Stars imefuzu kucheza katika mashindano ya CHAN 2024 yatakayofanyika katika nchi tatu (3) za Tanzania, Kenya na Uganda. Timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 15 ilifanikiwa kuwa mabingwa wa mashindano ya mpira wa miguu kwa shule za Afrika kwa mara ya pili mfululuzo nchini Ghana. Timu ya wanawake ya Futsal imefanikiwa kutinga hatua ya fainali na kukata tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia Mwaka 2025 na Timu ya Taifa ya Kriketi chini ya miaka 19 imefuzu kucheza kombe la Dunia nchini Zimbabwe. Vilevile, Timu ya Taifa ya Wheelchair Tenis imefuzu kombe la Dunia nchini Uturuki, na Futsal wanawake wamefuzu kucheza kombe la Dunia nchini Ufilipino.


Pia, Klabu zetu za Simba, Yanga, Azam pamoja Coastal Union zilifanikiwa kushiriki mashindano makubwa Barani Afrika yaani Kombe la Shirikisho pamoja na kombe la Klabu Bingwa. Tunaendelea kuvipongeza vilabu vya Simba na Yanga kwa kuendelea kuiwakilisha nchi yetu katika mashindano makubwa barani Afrika, ambapo imewezesha ligi yetu kushika nafasi ya nne (4) kwa ubora, hii imekuwa chachu kwa vilabu vingine kufanya vizuri. Pongezi za kipekee ziende kwa klabu ya simba kufuzu kucheza fainali ya kombe la shirikisho Barani Afrika, ni imani yetu kwa mara ya kwanza klabu hii itakwenda kulitwaa kombe hili, **'Simba nguvu moja''.** Aidha, jitihada hizi zinatokana na hamasa ya goli la Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**208.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa kwa kushirikiana na Shirikisho la Ngumi za Wazi Tanzania (OBFT) iliendesha mafunzo ya kimataifa kwa waamuzi na majaji wa ngumi kutoka nchi 4 za Afrika ambapo waamuzi 26 walihudhuria, washiriki hao walitoka katika nchi za; Uganda 1; Kenya 8; Namibia 1 na Tanzania 16 walipatiwa mafunzo hayo ambayo yalifanyika kuanzia tarehe 6 hadi 10 Oktoba 2024 katika ukumbi wa Chuo cha Polisi (Kilwa Road) jijini Dar es Salaam. Vilevile, Baraza kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ngumi za

Kulipwa (TPBRC) liliendesha mafunzo kwa viongozi wa shirikisho, mabondia, mapromota pamoja na waamuzi nchini ikiwa na lengo la kuwaelemisha mabondia kujua haki za msingi katika mchezo wa ngumi (Ndondi) nchini ambapo jumla ya washiriki 120 walihudhuria. Mafunzo hayo yamewasaidia mabondia nchini kujua haki zao za msingi katika mikataba wanayoingia na mapromota.

**209.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa imeendelea kutoa elimu kwa umma kusajili Vyama/Mashirikisho na Vilabu vya Michezo. Baraza linahimiza usajili kutumia mfumo wa kidijiti, ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2025, jumla ya Vyama, Mashirikisho na Vilabu 132 vimesajiliwa. Aidha, Baraza linaendelea kuhamasisha jamii kusajili vyama na vilabu vya michezo nchini kwa njia ya usajili kwa mfumo wa kieletroniki (SARS), ili kutambulika na kurasimisha kazi zao.

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia kupitia BMT, imeratibu matamasha mawili (2) ya michezo kwa wanawake yaliyojulikana kama Ladies First na Tanzanite Women Sports Festival. Tamasha la Riadha kwa Wanawake "Juma Ikangaa Ladies First" liliratibiwa kwa kushirikiana na taasisi ya ushirikiano wa Kimataifa ya Japani (JICA) na kufanyika jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 23 - 24 Novemba 2024 ambapo jumla ya washiriki 149 walihudhuria. Tamasha hilo lilishirikisha wanariadha kutoka katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na Visiwani. Tamasha la kitaifa la michezo la wanawake (Tanzanite Women Sports Festival) lilifanyika jijini Arusha kuanzia tarehe 4 hadi 7 Machi 2025 ambapo viongozi wanawake walihudhuria. Lengo la tamasha hilo ni kuwajengea uelewa mpana kuhusu masuala mbalimbali ya michezo na uongozi, pamoja na kubadilishana uzoefu baina ya wanawake wa kada mbalimbali. Aidha, tamasha hilo lilitamatika kwa kuwapo kwa ligi ya wanawake iliyojumisha vilabu vya Yanga Princess, Simba Queens, JKT Queens pamoja na Fountain Gate Queens, ambapo bingwa wa kombe hilo alikuwa Yanga Princess. Jumla ya wanawake 342 walishiriki katika tamasha hilo.



*Wanariadha kutoka katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na Visiwani wakichuana katika msimu wa sita (6) wa mashindano ya riadha kwa wanawake "Juma Ikangaa Ladies First 2024" yaliyoratibiwa na BMT kwa kushirikina na Shirika la Maendeleo la Japan 'JICA' yaliyofanyika jijini Dar es Salaam katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanzia tarehe 23-24 Novemba 2024.*

**211.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia BMT imeendelea kusimamia utawala bora kwa vyama vya michezo kwa kuratibu vikao 35 vya vyama vya michezo kwa lengo la kujadili masuala ya maendeleo ya michezo. Vilevile, Baraza limefanikiwa kuratibu na kusimamia uchaguzi wa vyama vya michezo nchini. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 vyama na mashirikisho yafuatayo yamefanya uchaguzi wa Viongozi; Tanzania Olympians Association (TOA) ambao ulifanyika tarehe 10 Desemba 2024 mkoani Dodoma; Chama cha wanaolimpiki wa zamani na Tanzania Women Football Association (TWFA) uliofanyika mkoani Kilimanjaro tarehe 14 Septemba, 2024.

**212.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Aprili2025 Serikali kupitia BMT ilifuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Kamati za Michezo za Mikoa katika Mikoa ya Rukwa, Iringa, Njombe, Kigoma, Mbeya, Morogoro, Geita na Katavi. Ufuatiliaji huu ulilenga kufanya tathmini ya shughuli za uendeshaji wa michezo katika ngazi za mikoa. Maeneo yaliyozingatiwa ni pamoja na kuona uhai wa Kamati, utekelezaji wa shughuli za michezo, taarifa za mashindano katika ngazi za mikoa pamoja na utatuzi wa migogoro katika ngazi za mikoa. Katika vikao hivyo ilisisitizwa kuendelea kusimamia kwa

karibu utekelezaji wa shughuli za michezo katika ngazi za mikoa ikiwamo kuhamasisha ushiriki wa jamii katika michezo, kusimamia uendelezaji wa viwanja na miundombinu ya michezo, kuibua vipaji, na kusimamia vyama na vilabu vya michezo katika ngazi za mikoa na wilaya pamoja na kuhamasisha vyama na vilabu kulipa ada za mwaka na tozo mbalimbali.

**213.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutambua na kuibua vipaji vya wanamichezo kupitia vilabu mahiri na wanaofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, BMT iliratibu utoaji wa tuzo kwa wanamichezo waliofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kwa aina zote za michezo nchini. Kwa msimu wa mwaka 2023/2024 tuzo kwa wanamichezo waliofanya vizuri zilifanyika tarehe 23 Mei 2024 katika ukumbi wa *The Super Dome*, uliopo jijini Dar es Salaam ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tuzo hizi zilikuwa hazijatolewa kwa zaidi ya miaka 40 tangu Baraza la Michezo la Taifa lianzishwe. Aidha, kwa mwaka 2024/25 hafla ya utoaji wa tuzo inatarajiwa kufanyika mwezi Mei 2025 jijini Dar ss Salaam.

**214.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kunakuwa na miundombinu bora ya michezo kwa ajili uibuaji wa vipaji vya wanamichezo nchini, Baraza linatarajia kujenga kituo cha michezo katika kanda ya Kaskazini katika Mkoa wa Manyara. Kituo hicho kitajumuisha viwanja vya mpira wa miguu, mpira wa pete, kikapu, wavu, mpira wa mikono na eneo la kukimbilia kwa mchezo wa riadha (field and track). Viwanja hivi vitasaidia uibuaji na ukuzaji wa vipaji katika michezo.



*Mwonekano wa kituo cha michezo kitakachojengwa mkoani Manyara kitakapokamilika.*

**215.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Michezo la Taifa limeendelea kutoa vibali na idhini kwa timu na wachezaji kushiriki katika matukio mbalimbali ya michezo ya kimataifa. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya vibali 254 vimetolewa kwa matukio ya mbio za marathoni, mapambano ya ngumi za kulipwa, na matukio mengine ya michezo. Aidha, BMT imetoa vibali vya kazi kwa wachezaji na wataalamu wa michezo wa kigeni kutokana na maombi yaliyowasilishwa na vyama vya michezo husika kwa niaba ya vilabu na taasisi zinazoshiriki katika mashindano hayo.

**216.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia BMT imeendelea kuratibu maandalizi ya mashindano ya CHAN 2024 ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia mwezi Agosti 2025 katika nchi za Kenya, Uganda na Tanzania. Maandalizi haya ni pamoja na uratibu wa vikao vya Kamati kuu ya kitaifa ya maandalizi ya mashindano ya CHAN 2024 na AFCON 2027, Kamati ndogo pamoja na Sekretarieti ya Kamati za maandalizi ya CHAN 2024 na AFCON 2027. Vilevile, Serikali imeratibu ujio wa wakaguzi kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) ambao kwa vipindi tofauti wamefanya ukaguzi wa miundombinu ya michezo ambayo itatumika kwenye mashindano ya CHAN 2024 na AFCON 2025. Kuwapo kwa mashindano hayo katika nchi yetu kutafungua milango ya uchumi kwa sekta mbalimbali nchini na wananchi kwa ujumla.

### 3.2.4.3 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ni chuo pekee kinachotoa mafunzo ya elimu ya michezo kwa wataalamu wa michezo nchini. Chuo hiki kipo mkoani Mwanza katika Wilaya ya Kwimba. Jukumu kuu la chuo hiki ni kufundisha taaluma ya michezo, kufanya utafiti na kutoa ushauri kuhusu masuala ya maendeleo ya michezo.

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya imeendelea kudahili wanachuo katika masomo ya michezo. Katika juhudi hizo, Chuo kimefanikiwa kuongeza idadi ya wanachuo ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Chuo kimetoa mafunzo kwa wanachuo 312

ambapo wanafunzi wa Ngazi ya Nne ni 62, Ngazi ya Tano 122 na Ngazi ya Sita 128. Hii ni sawa na asilimia 100.9 ya lengo lililokusudiwa. Aidha, hili ni ongezeko la wanachuo 22 ukilinganisha na mwaka 2023/24 ambapo jumla ya wanachuo 290 walipatiwa mafunzo.

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25 Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimetoa mafunzo ya muda mfupi katika kituo chake cha Dar es Salaam, Makao Makuu ya Chuo Malya, mkoani Mwanza na Arusha. Hadi kufikia Aprili 2025 Chuo kilitoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki takribani 420, sawa na asilimia 140 ya lengo la kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau 300. Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na usimamizi wa miundombinu ya michezo, tiba katika michezo, uraibu wa dawa zilizopigwa marufuku katika michezo na huduma ya kwanza katika michezo. Aidha, mafunzo yalihusisha utawala na usimamizi wa miundombinu ya mpira wa miguu na utawala na usimamizi wa michezo katika taasisi na mashirika ya umma. Kadhalika, mafunzo ya michezo ya riadha, mpira wa mikono, mpira wa kikapu, mpira wa watu wenye uoni hafifu, mpira wa wavu na mpira wa miguu yalitolewa.

**220.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utoaji wa mafunzo kwa wanachuo, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kuendelea na ujenzi wa hosteli za wanachuo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, shughuli zilizofanyika katika ujenzi huo wa hosteli ni pamoja na; umaliziaji wa ujenzi wa kuta, uwekaji wa mifumo ya maji na umeme, uwekaji wa vigae, uwekaji wa madirisha na milango, upigaji wa plasta na kupaka rangi jengo.



*Mwonekano wa ujenzi wa hosteli za wanafunzi unaoendelea katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Hosteli hiyo itakuwa na jumla ya sakafu nne (4) itakapokamilika na itakuwa na uwezo wa kuchukua wanachuo 192.*



*Mwonekano wa hosteli ya Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya pindi itakapokamilika.*

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha michezo inaendeshwa kisasa zaidi Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na mbeba maono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na ujenzi wa Akademia ya Michezo ya kitaifa katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Hadi kufikia mwezi Aprili 2025 ujenzi huo umefikia asilimia 22.5. Kukamilika kwa ujenzi wa kituo hiki utakifanya kuwa kituo pekee cha uibuaji na ukuzaji wa vipaji katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

**222. *Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kituo kuchukua vijana walio katika mfumo rasmi wa elimu, kituo pia kitasaidia kutoa mafunzo kwa vijana wetu walioko katika mfumo usio rasmi wanaopaswa kuendelezwa katika michezo. Pia, kituo kitakuwa sehemu ya mafunzo kwa vitendo kwa wanachuo wanaosomea michezo, vilevile kitatumika kama kambi ya maandalizi kwa timu zitakazokuwa zinashiriki michezo ya kitaifa na kimataifa. Mradi huu utakapokamilika unakadiriwa kugharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 33 za Kitanzania.

### 3.2.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALIWATU

**223. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Wizara iliratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli mbalimbali za ofisi ikiwamo matengenezo ya magari, ununuzi wa mafuta ya magari, huduma za usafi na ulinzi, kulipa pango la ofisi, umeme na simu, na vitendea kazi mbalimbali vya ofisi ikiwamo samani za ofisi, magari na kompyuta. Pia, Wizara imeendelea kusimamia na kuwezesha upatikanaji wa stahili mbalimbali za watumishi yakiwamo malipo ya nauli za likizo, safari za kikazi na uhamisho.

**224. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushiriki wa watumishi katika kupanga na kutekeleza majukumu ya Wizara, mikutano miwili (2) ya Baraza la Wafanyakazi imefanyika. Pia, Wizara imeendelea kushiriki katika Sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani zilizofanyika Kitaifa jijini Arusha pamoja na kushiriki katika Michezo ya SHIMIWI iliyofanyika mkoani Morogoro.

**225. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Wizara inakuwa na rasilimaliwatu endelevu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake, Wizara imeajiri watumishi kumi (10) wa kada mbalimbali wakiwamo Maafisa Sheria wawili (2), Afisa Habari mmoja (1), Afisa Hesabu mmoja (1), Mafundi Sanifu watatu (3), Msaidizi wa Kumbukumbu mmoja (1), Mkutubi Msaidizi mmoja (1) na Dereva mmoja (1). Halikadhalika, Wizara imeendelea na programu za kuwajengea uwezo watumishi katika maeneo mbalimbali ili kuimarisha utendaji kazi wao ambapo watumishi 144 walishiriki

mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali na watumishi 14 walishiriki mafunzo ya muda mrefu.

**4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO**

**226.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2024/25, changamoto katika utekelezaji wa majukumu hazikosekani. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kama ifuatavyo:

(i) Kuwapo kwa kasi kubwa ya jamii yetu kuvamiwa na utamaduni wa kigeni ambayo ni hatari kwa jamii yetu kupoteza utamaduni na maadili yetu.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuelemisha jamii kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Mtanzania. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu matamasha mbalimbali ya utamaduni na sanaa kwa lengo la kutunza na kukuza utamaduni wetu.

(ii) Uelewa mdogo wa jamii hususan vijana kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kuenzi urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika na nafasi ya Tanzania kama kitovu cha harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika.

Wizara kupitia Kituo cha Programu ya Urithi wa Ukombozi imeendelea kutoa elimu kupitia makongamano, mitandao ya kijamii na kufanya maonesho mbalimbali ya kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kulinda urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

(iii) Kukosekana kwa mifumo madhubuti ya kidijiti ya kukuza Kiswahili, kama tafsiri za kompyuta na programu za lugha. Kadhalika, kuna ukosefu wa programu na zana za teknolojia ya kisasa zinazoendana na maendeleo ya Kiswahili.

Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali inatumia njia mpya na za kisasa zikiwamo programu za simu na mitandao ya

kijamii, kukuza matumizi ya Kiswahili. Pia, Serikali imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kidijiti kwa ajili ya uundaji wa machapisho ya Kiswahili. Mikakati mingine ni kuendeleza programu za Kiswahili za kidijiti, kama msamiati wa mtandaoni na programu za kujifunza Kiswahili. Kadhalika, BAKITA inashirikiana na wataalamu wa teknolojia ili kubuni mifumo ya kidijiti ya kusaidia kuchakata lugha, mathalani kongoo ya Kiswahili na programu za kompyuta za kutafsiri, kukalimani na kuhariri matini.

(iv) Uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa michezo katika kukuza uchumi na kutoa ajira hususan kwa vijana hali inayowafanya wazazi wengi kutowaruhusu watoto wao kushiriki katika michezo.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo Serikali inaendelea na utoaji wa elimu kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, mikutano mbalimbali, makongamano n.k., kwa lengo la kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa michezo.

## 5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2025/26 Wizara na Taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia maelekezo ya Hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2025/26; Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili 2021; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 - 2025); Mpango Mkakati wa Wizara (2021/22 - 2025/26); Malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030; na Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na maelekezo mbalimbali ya viongozi wakuu wa Serikali.

### 5.1 SEKTA YA HABARI

#### 5.1.1 IDARA YA HABARI - MAELEZO

**228.** ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara itaendelea na majukumu yake ya usimamizi wa Sekta ya Habari ili kuhakikisha inaendelea kukua na kuwa na mchango mkubwa kwa Taifa na kuhakikisha Watanzania wanapata taarifa sahihi na zilizochakatwa kwa weledi wa hali ya juu na waandishi wa habari wenye sifa.

**229.** ***Mheshimiwa Spika;*** Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari imeanzishwa na imeanza kutekeleza majukumu yake yakiwamo ya kusimamia maadili ya waandishi wa habari na weledi wa kitaaluma katika kuandika Habari. Aidha, Bodi inaendesha Mfuko wa Mafunzo kwa Waandishi wa Habari ambao unalenga kuwezesha mafunzo kwa waandishi wa habari, kusaidia uzalishaji wa maudhui ya ndani na pia kuwezesha tafiti katika masuala ya uandishi wa habari na mawasiliano kwa umma. Kwa hiyo, ili kuwezesha yote hayo ikiwamo uzalishaji wa maudhui ya ndani, Mfuko huu utaanza kuwasaidia waandishi wa habari kuwa na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika kutengeneza maudhui ya ndani.

**230.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO itaratibu na kuandaa mikutano 24 ya Msemaji Mkuu wa Serikali ili kuelezea masuala mbalimbali ya utekelezaji wa Serikali kuhusu miradi ya kimkakati, Sera na programu mbalimbali zinazotekelezwa; kuisemea Serikali kuhusu miradi mbalimbali inayotekelezwa; kukusanya, kuchakata na kusambaza habari na makala kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa Serikali; kuratibu na kufanya tathmini ya utoaji wa taarifa za Serikali kwa umma; kuratibu na kuandaa mikutano 60 ya taasisi kuongea na waandishi wa habari kuelezea mafanikio ya utekelezaji wa Serikali kupitia taasisi hizo; kuratibu Mkutano Mkuu wa Mwaka/Kikaokazi cha Maafisa Habari 500 wa Serikali; kuratibu mkutano wa mwaka wa Maendeleo ya Sekta ya Habari; kuchapisha leseni 30 za magazeti na majarida; kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano; kuchapisha nakala 10,000 za Jarida la NCHI YETU na nakala 1,000 za picha za

Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere na kuratibu vyombo vya habari na waandishi wa habari wa ndani na kutoka nje ya nchi katika matukio mbalimbali ya kitaifa na ziara za viongozi kutoka nje ya nchi.

**231.** ***Mheshimiwa Spika***; Wizara imeendelea na jukumu la uratibu wa Vitengo vya Mawasiliano Serikalini na ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika utoaji wa taarifa za Serikali, Wizara kupitia Idara ya HabariMAELEZO inashirikiana na Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kufanya tathmini ya Vitengo vya Mawasiliano katika Taasisi zote 571 za umma nchini. Lengo ni kufuatilia ufanisi wa Vitengo hivi, kutoa motisha kwa wanaofanya vizuri na hivyo kutoa ushindani kwa Vitengo. Hii itawaamsha wasiofanya vizuri kubadilika na kufanya vizuri.

### 5.1.2 SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)

**232.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26 majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya TBC eneo la Vikonje, Kata ya Mtumba jijini Dodoma; kuimarisha usikivu wa redio kwa kufunga mitambo ya masafa ya FM katika maeneo ya mpakani na yale yasiyo na usikivu au yenye usikivu hafifu; kuendelea kulipia gharama za uendeshaji wa mitambo (umeme, mafuta, vipuri na matengenezo); na kuendelea kulipia gharama za masafa (satelaiti na intaneti) ili kuwezesha matangazo ya redio, televisheni na mitandao ya kijamii kuwafikia wananchi muda wote.

**233.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu mengine ni kununua magari ya kurushia matangazo mbashara (OB Van) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu, 2025; kununua vitendea kazi ikiwamo magari, kamera, vinasa sauti, mitambo ya kuhariri picha na sauti, *fly away, drone na quantum* kwa ajili ya matangazo mbashara wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu, 2025; kukarabati na kufunga mifumo mipya ya studio katika OB Van ya Televisheni ili iweze kukidhi mahitaji ya kutangaza mpira pamoja na matukio ya Uchaguzi Mkuu, 2025; kuboresha miundombinu na mifumo ya utangazaji ya redio, televisheni na mitandao ya kijamii; kufunga na kuboresha

mifumo ya maktaba ya picha na sauti ili kuwezesha kuhamisha maudhui yaliyohifadhiwa katika mfumo wa analojia kwenda dijitali; kukamilisha tathmini ya ufungaji wa mitambo ya masafa mafupi na ya kati (*Short wave and Medium wave*) kwenye maeneo mahususi ya TBC yaliyotengwa na ITU kwa ajili ya shughuli za utangazaji, ambayo ni Iwambi (Mbeya), Njiro (Arusha), Kunduchi (Dar es Salaam), Mundemu (Dodoma), Mahembe (Kigoma), Songambele (Nachigwea), Pasiansi (Mwanza) na Bombambili (Songea) ambapo mitambo ya *Digital Radio Mondiale* (DRM) inatarajiwa kufungwa. Jukumu hili litakwenda sambamba na kuanzisha idhaa za redio na chaneli za televisheni za kimatifa (*External Services*) ili kuongeza ushawishi wa Tanzania katika ukanda wa SADC, Afrika na Ulimwenguni katika kuitangaza nchi kupitia Kiswahili na utamaduni wa Mtanzania kimataifa; kuimarisha chaneli za kimkakati za TBC (TBC Digital, TBC2, Tanzania Safari Channel na Bongo FM) kwa kununua vitendea kazi vya kisasa; na kuboresha maudhui kwa kutoa mafunzo kwa watumishi na kufunga mifumo ya kisasa ya kidijiti katika studio za TBC.

### 5.1.3 KAMPUNI YA MAGAZETI YA SERIKALI (TSN)

**234.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26 majukumu yaliyopangwa ni; kuchapa na kusambaza jumla ya nakala 5,198,387 za magazeti ikijumuisha Daily News: Nakala 3,824,670 na HabariLEO nakala 1,373,717; kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya kampuni; kukamilisha ufungaji wa mtambo wa uchapaji; kuhabarisha na kuelimisha umma kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani; kufuatilia madeni kwa wateja: Mashirika, Taasisi, Idara za Serikali na Sekta Binafsi; kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya fursa za uwekezaji; na kuimarisha matumizi sahihi ya TEHAMA katika uendeshaji na utoaji huduma.

### 5.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

### 5.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**235.** ***Mheshimiwa Spika***, malengo yaliyopangwa kutekelezwa ni kufanya utafiti wa urithi wa utamaduni usioshikika

pamoja na kuandaa Atlasi ya Lugha za Jamii na Atlasi ya Tamaduni Mbalimbali za Makabila ya Tanzania, kuhuisha Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997; kuratibu uandaaji wa mkakati wa kitaifa wa kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini; kuendesha Tamasha la Nne la Utamaduni la Kitaifa; kuratibu Matamasha ya utamaduni yanayoandaliwa na wadau; kuratibu ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa; kuratibu Maadhimisho ya Nne ya Kitaifa na Kikanda ya Siku ya Kiswahili Duniani pamoja na makongamano ya Kiswahili ya wadau na kuratibu kikaokazi cha Maafisa Utamaduni nchini.

### 5.2.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**236.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, limepanga kutekeleza majukumu mbalimbali ikijumuisha: Kuandaa Maadhimisho ya Tano ya Kitaifa na Kikanda ya Siku ya Kiswahili Duniani pamoja na makongamano ya Kiswahili ya wadau; kuandaa Kongamano la Pili la Kimataifa la Kiswahili nchini Ufaransa; kufanya usanifishaji mkubwa wa msamiati wa Kiswahili; kufanya utafiti unaolenga kuongeza maneno milioni 50 katika Kongoo ya Kiswahili ya Taifa; kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu; kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni; kutoa mafunzo ya msasa ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu kwa makundi maalumu; kuendesha mtihani wa kupima umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa wageni na kuendesha mafunzo ya Kiswahili kwa wageni. Mambo mengine yatakayotekelezwa ni pamoja na kufungua vituo vya kimkakati vya kufundisha Kiswahili kwa wageni ambavyo vitasimamaiwa moja kwa moja na waambata lugha kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; kuendesha mafunzo kwa wakalimani; kuandaa atlasi ya lahaja za Kiswahili na kusambaza *Kamusi ya Kiswahili kwa Shule za Msingi*.

### 5.2.3 KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA

**237.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika kimepanga kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwamo; kuratibu ujenzi wa kituo kikuu cha urithi wa ukombozi na kukarabati maeneo ya urithi wa ukombozi

wa Afrika yaliyomo nchini; kuratibu ziara kwenye maeneo yenye kumbukumbu za historia ya ukombozi wa Afrika kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa urithi wa ukombozi wa Afrika; kuratibu uandaaji na uchapishaji wa vitabu vya historia ya ukombozi, picha na vipeperushi kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu historia ya ukombozi wa Afika; kuratibu usimamizi na uendeshaji wa ofisi ya Kituo cha ukombozi wa Afrika; kuratibu na kuendesha kampeni na uhamasishaji wa umma kuhusu Urithi wa Ukombozi wa Afrika wakati wa matukio ya kumbukumbu (siku ya Afrika, siku ya ukombozi wa Kusini mwa Afrika); kutambua, kukusanya, kuhifadhi, kulinda na kuendeleza urithi wa ukombozi wa Afrika unaoonekana na usioonekana na rasilimali za kumbukumbu; na kufanya ziara kwenye nchi za Kusini mwa Afrika kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi wa urithi wa ukombozi wa Afrika na kubadilishana uzoefu.

## 5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

### 5.3.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali itahakikisha Sekta ya Sanaa na Ubunifu inasimamiwa vema na kuendelezwa katika ngazi ya kitaifa na kimataifa ili izalishe ajira zaidi, kuchangia katika uchumi wa wahusika na katika Pato la Taifa. Hivyo, ili kufikia azma hiyo, matamasha ya ndani na nje ya nchi na mafunzo mbalimbali yataendeshwa pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa za sanaa na ubunifu. Katika mwaka wa fedha 2025/26, malengo na majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 katika mikoa 10 ya Tanzania Bara; kuwezesha utayarishaji wa Mkakati wa Miaka 10 wa Maendeleo ya Sekta ya Sanaa Tanzania; kutathmini utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Idara ya Maendeleo ya Sanaa ambazo ni BASATA, COSOTA, Bodi ya Filamu Tanzania, TaSUBa na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

**239.** ***Mheshimiwa Spika.*** Majukumu mengine ni kuratibu matamasha 4 ya sanaa ya kitaifa na kimataifa; kuratibu

mashindano ya sanaa kwa vijana kupitia mashindano ya UMISSETA kwa shule za sekondari Tanzania, mashindano ya UMITASHUMTA kwa shule za msingi Tanzania, Taifa Cup na mashindano mengine; kuratibu shughuli za burudani wakati wa Maadhimisho ya Sherehe za Uhuru na Muungano na hafla nyingine za kitaifa na kimataifa; kuratibu shughuli za uhamasishaji kupitia sanaa kuelekea CHAN 2024 na AFCON 2027 kupitia shughuli za sanaa na burudani; kufanya utafiti kuhusu mchango wa sanaa na burudani katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania; kuratibu maandalizi ya ujenzi wa vituo vya sanaa katika mikoa 26 ya Tanzania Bara; kuendesha mkutano wa mwaka wa wadau wa sanaa Tanzania; na kuratibu, kulinda na kukuza sanaa ya kipekee ya Kitanzania ya ubunifu ikijumuisha mtindo wa Tingatinga, Muziki wa Singeli na Vinyago vya Kimakonde.

### 5.3.2 BODI YA FILAMU TANZANIA

**240.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu yatakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/26 ni: Kufanya mapitio ya Sheria ya Filamu pamoja na Kanuni zake ili kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya ukuaji na maendeleo ya shughuli za filamu na michezo ya kuigiza; kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika urasimishaji wa shughuli za filamu nchini kupitia mfumo wa wadau (AMIS); kukuza na kuendeleza vipaji vya filamu na michezo ya kuigiza kwa kuratibu Tamasha la Kitaifa la Utoaji wa Tuzo za Filamu; kuhamasisha uendeshaji wa matamasha mengine ya tuzo za filamu na michezo ya kuigiza pamoja na kuandaa na kuwezesha programu mbalimbali za mafunzo kwa wadau; kusimamia maudhui ya filamu kwa kuhakiki na kupanga katika madaraja filamu 200 pamoja na sehemu (episodes) 1,500 za tamthilia; kusimamia utayarishaji wa filamu kwa kuchakata maombi na kutoa vibali 300 vya utayarishaji wa filamu.

### 5.3.3 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**241.** ***Mheshimiwa Spika*****,** majukumu yatakayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2025/26 ni pamoja na kutafuta kiwanja cha kujenga *National Art Gallery*, jijini Dodoma na kufanya upembuzi yakinifu; kuhuisha muundo wa BASATA, kufanya mapitio ya

mchakato wa biashara *(business process review)* wa BASATA, kuandaa Atlasi ya Vyombo vya Muziki wa Kiasili kutoka kwenye makundi yote ya kikabila ya Tanzania, kuimarisha shughuli za utafiti kuhusu masuala yanayohusiana na maendeleo ya Sekta ya Sanaa nchini; kulinda maudhui ya utamaduni wa asili *(folklore expressions)* na kuratibu matukio na Tuzo za Muziki Tanzania ili kutambua mafanikio ya wasanii nchini.

### 5.3.4 OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa katika mwaka 2025/26 ni: kusimamia kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha katika makundi ya sanaa na uandishi; kupambana na uharamia wa kazi za wabunifu; kukusanya na kugawa mirabaha kwenye maeneo ambayo hakuna kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha; kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya hakimiliki; kushirikiana na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya Tanzania katika usimamizi wa hakimiliki; na kukamilisha uunganishaji wa mifumo ya kieletroniki kati ya COSOTA, BASATA na Bodi ya Filamu Tanzania ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wadau.

### 5.3.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa katika mwaka 2025/26 imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: kudahili wanachuo wa kozi ndefu wapatao 850 na 350 wa kozi fupi; ukamilishaji wa uandisi wa mitaala na kupata ithibati kutoka NACTVET; kutoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi 12 katika mambo ya sanaa na utamaduni; kufanya tafiti 3 katika maeneo ya sanaa na utamaduni; kutoa mafunzo maalumu ya uongozi wa sanaa na masoko kwa viongozi 30 wa sanaa; kuratibu upatikanaji wa Hati Miliki ya Viwanja vya Taasisi; kuratibu Tamasha la 44 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo; kuhuisha miongozo na kanuni za Taasisi zipatazo 6; na kutangaza Taasisi na bidhaa na huduma zake katika vyombo mbalimbali vya habari na katika mitandao ya kijamii. Kadhalika, kufuatia mabadiliko ya elimu Tanzania, Chuo kinaandaa mitaala mipya miwili ya Ualimu wa Muziki (*Music Education*) na Ualimu wa Sanaa za Ufundi (Visual Arts Education)

ili kuandaa walimu wa kufundisha masomo katika fani kuu ya elimu ya amali katika Sanaa Bunifu (Creative Arts).

### 5.3.6 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa katika mwaka 2025/2026 ni pamoja na kuendesha programu ya mafunzo ya urasimishaji wa kazi za utamaduni na sanaa ambapo wasanii 15,000 wanategemewa kufikiwa katika mikoa ya Kagera, Mara, Kigoma, Morogoro, Mwanza, Tabora, Kilimanjaro, Lindi, Mtwara, Mbeya, Songwe na Rukwa. Aidha, nguvu kubwa itawekezwa katika maeneo ya usimamizi wa miradi, utunzaji wa kumbukumbu na uwekaji wa akiba, biashara na familia, urasimishaji, mafao ya jamii, pamoja na uandishi wa maandiko ya mradi.

**245.** ***Mheshimiwa Spika***, wasanii watakaofuzu mafunzo hayo wataunganishwa na na taasisi/wadau wa sanaa kwa ajili ya kufanya mazoezi kwa vitendo, kuwaunganisha na wasanii waliofanikiwa katika maeneo husika ili waweze kulelewa na kujifunza mbinu mbalimbali za kibiashara na mwisho kuunganishwa na fursa za kiuchumi ikiwamo kuwezeshwa kupitia mikopo inayotolewa na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa.

**246.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa utawekeza Shilingi 3,600,000,000 kwa benki washirika ambapo kiasi hiki kitawezesha utoaji wa mikopo yenye thamani ya Shilingi 5,400,000,000 itakayowezesha wasanii 500 ikiwa ni wastani wa miradi 19 kwa kila mkoa na miradi hiyo inategemewa kuzalisha jumla ya ajira zisizopungua 75,537 zitakazowanufaisha wananchi 975,000 huku vipaumbele vikiwa ni makundi maalumU, mgawanyiko kisekta na mikoa.

**247.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko utatangaza huduma zake kupitia njia mbalimbali hasa katika maeneo ya pembezoni mwa miji ili ziweze kufahamika kwa wadau ambapo wananchi takribani milioni sita wanategemea kufikiwa. Aidha, miongoni mwa njia zitakazotumika ni pamoja na kuwakutanisha wadau wa utamaduni na sanaa kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na kutatua

changamoto za masoko kupitia Mkutano wa Tatu wa Mwaka wa Wadau wa Mfuko.

## 5.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

### 5.4.1 IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO

**248.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Michezo itatekeleza majukumu mbalimbali. Miongoni mwa majukumu hayo ni: kuratibu maandalizi ya michuano ya CHAN 2024 na AFCON 2027; kuratibu uanzishwaji wa chombo cha kupambana na dawa na mbinu haramu michezoni na utoaji elimu; kushiriki mikutano na makongamano ya kimataifa ya michezo; kuratibu kikaokazi cha kitaifa cha Maafisa Michezo; kuratibu utoaji wa huduma za kinga na tiba kwa wanamichezo; kuratibu michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI; kuratibu matukio ya kitaifa ya michezo ikiwamo michezo ya SHIMIWI na Mei Mosi; kuratibu michezo ya kimataifa ikiwamo michezo ya Jumuiya ya Madola; na kuandaa na kusimamia mwongozo wa viwango vya ubora wa miundombinu ya michezo nchini. Majukumu mengine ni kuendelea kuimarisha ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano ya kimataifa kwa kuwatumia diaspora; ujenzi na ufufuaji wa viwanja vya wazi vya michezo katika ngazi ya jamii; kuratibu shughuli za Sekretarieti ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV pamoja na kusimamia uanzishwaji wa chombo cha kusimamia miundombinu ya michezo nchini. Aidha, Wizara itaratibu miradi ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya michezo nchini, ikiwamo ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu Dodoma, ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu Arusha, ujenzi wa viwanja vya mazoezi na kupumzikia wananchi Dar es Salaam na Dodoma, ujenzi wa Arena ya Michezo na Sanaa Dar es Salaam na ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru n.k.

### 5.4.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**249.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuendelea kuwezesha na kuzigharimia Timu za Taifa 15 kushiriki mashindano mbalimbali

ya kimataifa; kuendelea kutoa mafunzo ya utaalamu wa michezo na usimamizi kwa wataalamu 150 ili kupata wataalamu wa michezo nchini; kuendelea kusajili vyama/mashirikisho na vilabu vya michezo vipatavyo 200; kuratibu matamasha mawili ya michezo ya wanawake; kuendelea kuhamasisha utawala bora katika vyama na mashirikisho ya michezo 48; kuratibu na kusimamia Mfumo wa Usajili wa Kidijiti (Online Registration); kuidhinisha vibali 180 vya matukio mbalimbali ya michezo; na kuendelea kutoa tuzo kwa wanamichezo bora kwa michezo yote inayochezwa Tanzania, kuendelea kufanya ufuatiliaji wa Kamati za Michezo ngazi za mikoa na wilaya ili kusimamia kikamilifu programu za kuinua na kuendeleza vipaji katika ngazi za chini.

### 5.4.3 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA

**250.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha michezo inaendeshwa kwa weledi mkubwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Chuo kimepanga kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanachuo wapatao 500; kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau wa michezo wapatao 640; kuongeza programu zinazotolewa Chuoni hapo kutoka programu tatu hadi sita ikiwamo programu ya uandishi wa habari za michezo, utalii katika michezo na elimu ya masoko ya bidhaa na huduma za michezo. Ongezeko la programu hizi litaakisi mabadiliko ya elimu Tanzania kwa kuandaa mitaala ya elimu ya amali katika masomo ya ualimu wa michezo (*physical education*) na ukocha wa michezo (*Sports coaching*). Aidha, Chuo kimekusudia kwa dhati kujenga uhusiano na vyuo vingine vya nje pamoja na kujenga mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia ili kuvutia udahili zaidi wa wanafunzi.

### 5.5 MIRADI YA MAENDELEO

**251.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi itakayotekelezwa na Wizara kwa mwaka 2025/26 inajumuisha Mradi wa Habari kwa Umma, Mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa TBC, Mradi wa Ufungaji wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji, Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, Ujenzi wa Jumba Changamani la Filamu (*Film Studio*), Mradi wa Kuimarisha BAKITA na Kukibidhaisha Kiswahili, Ujenzi wa

Akademia ya Michezo Malya, Ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Arusha na Dodoma, Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi (*Recreational Centre*), Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalumu za Michezo, Mfuko wa Maendeleo ya Michezo na Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

**252.** ***Mheshimiwa Spika;*** kupitia Mradi wa Habari kwa Umma, Wizara inatarajia kutangaza shughuli za Serikali kwa kuchukua taarifa za miradi ya maendeleo katika mikoa na halmashauri 184 na kuzitangaza kupitia vyombo vya habari pamoja na kuratibu mikutano ya Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi wao wa Halmashauri kuongea na vyombo vya habari kueleza kuhusu utekelezaji wa miradi. Wizara pia itaratibu ziara za Wahariri wa Vyombo vya Habari na Waandishi katika miradi mikubwa mitano ya kimkakati ili wapate fursa ya kuitangaza kupitia vyombo vyao vya habari kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wanakuwa na taarifa sahihi na za kina kuhusu utekelezaji wa Serikali yao.

**253.** ***Mheshimiwa Spika,*** sanjari na hilo, Wizara imepanga kutangaza utekelezaji wa miradi mikubwa 25 kwa kuandika makala, video na vipindi maalumu vya televisheni na kusambaza kupitia magazeti, majarida, televisheni, redio na mitandao ya kijamii. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara inatarajia kununua kiwanja eneo la Mwangaza Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Habari; kufanya upembuzi yakinifu wa eneo la ujenzi wa Kituo cha Habari na kutafuta mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo hicho katika eneo hilo. Jumla ya Shilingi 2,700,000,000 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa habari kwa umma.

**254.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa upanuzi wa TBC kwa mwaka 2025/26 umetengewa bajeti ya Shilingi 14,800,000,000. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kuimarisha usikivu wa redio kwa kufunga mitambo ya masafa ya FM maeneo ya mpakani na yale yasiyo na usikivu au yenye usikivu hafifu; kununua magari ya kurushia matangazo mbashara (OB Van) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu, 2025; kununua vitendea kazi ikiwamo

magari, kamera, vinasa sauti, mitambo ya kuhariri picha na sauti, *fly away, drone* na *quantum* kwa ajili ya matangazo mbashara wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu, 2025; kukarabati na kufunga mifumo mipya ya studio katika OB Van ya Televisheni ili iweze kukidhi mahitaji ya kutangaza mpira pamoja na matukio ya Uchaguzi Mkuu, 2025; kuboresha miundombinu na mifumo ya utangazaji ya redio, televisheni na mitandao ya kijamii; kufunga na kuboresha mifumo ya maktaba ya picha na sauti ili kuwezesha kuhamisha maudhui yaliyohifadhiwa katika mfumo wa analojia kwenda mfumo kidijiti; kukamilisha tathmini ya ufungaji wa mitambo ya masafa mafupi na ya kati kwa ajili ya kuitangaza nchi kimataifa; kuimarisha chaneli za kimkakati za TBC (TBC Digital, TBC2, Tanzania Safari Channel na Bongo FM) kwa kununua vitendea kazi vya kisasa; na kuboresha maudhui kwa kutoa mafunzo kwa watumishi na kufunga mifumo ya kisasa ya kidijiti katika studio za TBC.

**255.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa Ufungaji wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji kwa mwaka 2025/26 umetengewa bajeti ya Shilingi 14,000,000,000. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa jengo, ununuzi wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji, ununuzi wa malighafi za kiwandani, ununuzi wa vitendea kazi ikiwamo magari na ufungaji wa mtambo kwa ajili ya kuanza uendeshaji utakaokuwa na uwezo mkubwa wa kuchapa nakala 40,000 kwa saa na kuokoa zaidi ya asilimia 60 ya mapato ya ndani ya kampuni yanayotumika kuilipa kampuni binafsi kwa ajili ya shughuli ya uchapaji wa magazeti, vipeperushi, majarida, kalenda, daftari, mabango, vitabu, shajara, vitambulisho vya waandishi wa habari na kudarizi/kuchapa maandishi au picha kwenye nguo, vikombe na vifaa mbalimbali kulingana na mahitaji ya mteja.

**256.** ***Mheshimiwa Spika***, Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, katika mwaka wa fedha 2025/26 imetengewa jumla ya Shilingi 2,001,576,000. Shughuli zitakazotekelezwa ni: kutambua, kukusanya, kuhifadhi, kulinda na kuendeleza urithi wa ukombozi wa Afrika unaoshikika na usioshikika; kuratibu ujenzi wa Kituo Kikuu cha Kuhifadhi Urithi wa Ukombozi, kukarabati maeneo ya urithi wa ukombozi wa Afrika yaliyomo nchini; na kuratibu

uandaaji na uchapishaji wa vitabu vya historia ya ukombozi wa Afrika kwa lengo la kutoa elimu kwa umma.

**257.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, katika mwaka wa fedha 2025/26 mradi huu umepangiwa jumla ya Shilingi 4,000,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wadau wa utamaduni na sanaa; kuwajengea uwezo wasanii ili kurasimisha kazi zao pamoja na kuziendesha kibiashara na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi iliyowezeshwa kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili kubaini matokeo ya uwezeshwaji wa miradi hiyo kwa wasanii, Sekta ya Utamaduni na Sanaa na nchi kwa ujumla.

**258.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa ujenzi wa Jumba Changamani la Filamu (*Film Studio*) katika mwaka 2025/26 umetengewa bajeti ya Shilingi 1,000,000,000 ambapo shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: Upembuzi yakinifu wa mradi na kuanza ujenzi wa mradi. Lengo la Mradi huu ni kujenga miundombinu ya kisasa itakayowezesha utayarishaji wa filamu bora zenye ushindani. Aidha, utekelezaji wa Mradi huu unatokana na dhamira ya dhati aliyonayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukuza na kuendeleza sekta ya utamaduni, sanaa, na filamu nchini Tanzania. Katika ziara yake maalumu nchini Korea Kusini mnamo mwezi Julai 2024, akiwa ameambatana na wasanii mbalimbali, alifanya mikutano mbalimbali kwa ajili ya kujadili ushirikiano kati ya Tanzania na Korea Kusini katika nyanja mbalimbali za Sekta ya Sanaa ikiwamo filamu ambapo sasa zimezaa matunda mazuri kwa Taifa letu.

**259.** ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu umefanikiwa kujumuishwa kuwa moja ya miradi ya kipaumbele katika Mfuko wa Maendeleo ya Ushirikiano ya Kiuchumi (*Economic Development Cooperation Fund - EDCF*) baina ya Tanzania na Korea Kusini. Haya ni mafanikio makubwa, kwani itachochea ukuaji wa sekta ya filamu, kuhamasisha ubunifu na kutengeneza ajira kwa vijana wa Tanzania. Kiasi cha Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000) kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi ya

upembuzi yakinifu na kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii (*Environmental and Social Impact Assessment*).

**260.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kupitia Mradi wa Kuimarisha BAKITA na Kukibidhaisha Kiswahili limetengewa jumla ya Shilingi 3,400,000,000. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: Usanifishaji mkubwa; kuendeleza kongoo la Taifa; kupeleka Kiswahili kimataifa kwa kufungua vituo vya kufundisha Kiswahili kwa wageni katika nchi 10; kununua gari moja kwa ajili ya matumizi ya ofisi; kuboresha mfumo wa kufundishia Kiswahili (Swahili prime); kufanya ukarabati wa majengo ya Baraza; kupeleka Kiswahili kwa makundi maalumu ndani ya nchi (Wamasai na Wahadzabe); kujenga studio ya Baraza; kuratibu Maadhimisho ya Tano ya Siku ya Kiswahili Duniani (MASIKIDU); kuandika Kamusi ya Sheria; na kutoa mafunzo ya msasa ya ufananivu wa lugha ya alama ya Tanzania na alama za kimataifa kwa wakalimani wa lugha ya alama.

**261.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Arusha katika mwaka 2025/26 umetengewa Shilingi 193,096,682,000. Uwanja huu mara baada ya kukamilika utakuwa na uwezo wa kuchukua watu 32,000 ambapo ujenzi wake unajumuisha miundombinu ya eneo la kukimbilia riadha, viwanja vya mpira wa mikono, pete na netiboli. Mradi huu ni sehemu ya Maandalizi ya Tanzania kuwa mwenyeji wa AFCON 2027 kama uwanja wa mashindano. Aidha, uwanja huu utavutia watalii na mashabiki wa michezo kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi, na hivyo kuimarisha sekta ya utalii na kuongeza mapato. **262.** Mradi wa Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma, katika mwaka wa fedha 2025/26 umetengewa Shilingi 140,000,000,000. Mradi huu unajengwa katika eneo changamani la michezo, Nzuguni. Mara baada ya kukamilika utakuwa na uwezo wa kuchukua watu 32,500. Uwanja utajumuisha viwanja vya mpira wa mikono, pete, na netiboli. Aidha, Mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 hadi 2025.

**262.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi (*Recreational Centre*) katika

mwaka 2025/26 umetengewa Shilingi 8,000,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi kwa Dar es Salaam na Dodoma inayojumuisha miundombinu ya majengo ya utawala, viwanja vya mpira wa miguu, netiboli, pete, wavu, tenisi, vyumba vya kubadilishia nguo na eneo la mapumziko *(recreation)*; na kuanza ujenzi wa awamu ya pili kwa Dar es Salaam na Dodoma unaohusisha jiko, bwawa la kuogelea lenye hadhi ya Olimpiki, uzio na eneo la mapumziko.

**263. *Mheshimiwa Spika***, mradi wa Ujenzi wa *Sports and Arts Arena* katika mwaka 2025/26 umetengewa jumla ya Shilingi 450,000,000. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kupata mshauri elekezi na kufanya upembuzi yakinifu wa Mradi utakaohusisha michoro, gharama za ujenzi, utafiti wa athari za mazingira na andiko la biashara (*business plan*).

**264.** Mradi wa Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam katika mwaka 2025/26 umepangiwa jumla ya Shilingi 29,000,000,000. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuendelea na ukarabati mkubwa wa miundombinu ya Uwanja wa Uhuru ikiwamo kubadilisha viti chakavu na kuweka vipya eneo la watu mashuhuri (VIP), kuweka viti vipya eneo la watazamaji wa kawaida (u-shape), kubadilisha paa, kurekebisha mifumo ya maji, umeme, viyoyozi, vyoo na eneo la kuchezea (pitch). Aidha, shughuli zingine zitakazotekelezwa ni kuendelea na ukarabati kinga wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwamo utunzaji wa uwanja, miundombinu ya maji, umeme, mifumo ya zimamoto, kamera na kiyoyozi.

**265. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau wamiliki wa viwanja itakamilisha taratibu na kuanza ukarabati mkubwa wa viwanja vitano vya CCM kwa mujibu wa makubaliano ya pande mbili. Msingi wa ukarabati huu ni kuongeza miundombinu ya michezo nchini, kuimarisha vituo vya mazoezi, ubora wa ligi na hatimaye timu zetu za Taifa.

**266. *Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalumu za Michezo katika mwaka 2025/26 umepangiwa Shilingi 11,500,000,000. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuanza kwa

ukarabati wa miundombinu ya shule maalumu saba (7) za michezo ambapo ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya michezo katika shule hizo. Shule hizo ni pamoja na Dr. Damas Ndumbaro Sec School (Songea-Ruvuma), Kicheba Secondary School (Tanga), Ikwiriri Secondary School (Pwani), Babati Seconary School (Manyara), Mtwara Ufundi Secondary School (Mtwara), New-Kiomboi Secondary School (Singida), Kanono Se (KaragweKagera).

**267.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, katika mwaka 2025/2026 umetengewa jumla ya Shilingi 1,500,000,000. Serikali kupitia Mradi huu itaendelea na ujenzi wa miundombinu mipya ya Chuo ikiwamo nyumba za watumishi, bwalo la chakula, maabara, maktaba, jengo la utawala na madarasa; kukarabati nyumba kumi (10) za watumishi; kukarabati viwanja vya michezo saba (7) ambavyo ni mpira wa miguu viwili (2), netiboli kimoja (1), mpira wa mikono viwili (2) na mpira wa kikapu viwili (2); kuimarisha mifumo ya mawasiliano ya kidijiti; kuimarisha mifumo ya maji, umeme na ulinzi katika Chuo ; kujenga maabara mbili (2) za michezo, ofisi kuu ya Chuo ya ghorofa mbili (2), maktaba moja (1) yenye ghorofa mbili (2) ikiwa na kumbi mbili (2) za mihadhara, bwalo la chakula moja (1) pamoja na kununua samani za majengo hayo.

**268.** ***Mheshimiwa Spika***, Mradi wa Akademia ya Michezo katika Chuo cha Michezo Malya katika mwaka 2025/26 umetengewa jumla ya Shilingi 15,000,000,000. Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Akademia ikiwamo viwanja vya mpira wa miguu (3), netiboli (2), kikapu (2), mikono (2), wavu (2), madarasa, bwalo, jengo la utawala, hosteli na kuanza kwa ujenzi wa bwawa la kuogelea lenye hadhi ya olimpiki.

**269.** ***Mheshimiwa Spika,*** tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuitazama Sekta ya Michezo kwa jicho la pekee kabisa na kuendelea kutoa fedha katika miradi yenye lengo la kuinua michezo nchini.

**270. *Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Maendeleo ya Michezo katika mwaka 2024/25 umetengewa jumla ya Shilingi 12,000,000,000. Majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni kuwezesha timu za Taifa 20 kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa; kuratibu maandalizi ya mashindano ya CHAN 2024 na AFCON 2027; kujenga mfumo wa kielektroniki wa vibali kwa wachezaji na wataalamu wa kigeni katika michezo; ujenzi na ukamilishaji wa kituo cha michezo katika Mji wa Babati Mkoani Manyara; Ujenzi wa Ofisi za Baraza la Michezo la Taifa katika Jiji la Dodoma; kuwezesha Timu za Taifa kwa michezo ya vipaumbele ili zifanye vizuri katika mashindano ya kitaifa na kimataifa; kuratibu utoaji wa tuzo kwa wanamichezo waliofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa; na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa michezo 300 na viongozi 72 wa vyama na mashirikisho ya michezo nchini.

**271. *Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), katika mwaka 2025/26 umetengewa Shilingi 2,000,000,000. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kuboresha utoaji wa mafunzo; ujenzi wa studio ya kisasa ya kufundishia na kujifumzia; uandaaji wa mitaala ya Ualimu wa Muziki (*Music Education*) na Ualimu wa Sanaa za Ufundi (*Visual Arts Education*); ujenzi wa ukuta wa eneo la mabweni ya wanachuo; ukarabati wa majengo; uimarishaji wa mifumo ya TEHAMA; uimarishaji wa Tamasha la Kimataifa la Bagamoyo; uanzishaji wa redio na televisheni mtandaoni; na uimarishaji wa vituo vya mafunzo Songea na Dar es Salaam.

**272. *Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa katika mwaka 2025/26 umepangiwa Shilingi 1,000,000,000. Shughuli zitakazotekelezwa ni kufanya upembuzi yakinifu wa eneo; kuandaa andiko la kutafuta mbia wa kuandaa michoro na kujenga eneo lote; kumtafuta Msimamizi wa Mradi (Consultant); na kutekeleza Mradi wa Ujenzi kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na binasfi (PPP).

## 5.6 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI WATU

**274. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli za ofisi. Kwa mwaka 2025/26 shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli za ofisi ikiwamo matengenezo na mafuta ya magari, huduma za usafi na ulinzi, kulipa pango la ofisi, umeme na simu pamoja na ununuzi wa vitendea kazi mbalimbali na samani za ofisi.

**275. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na uratibu na kuwezesha mazoezi ya wafanyakazi wote wa Wizara kila wiki mara moja; kuwezesha upatikanaji wa stahili mbalimbali za wafanyakazi ikiwamo uhamisho, likizo, safari za kikazi n.k., na kuendesha vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi. Pia, Wizara itaendelea na kuratibu ushiriki wa Wizara katika sherehe za Mei Mosi, Siku ya Wanawake Duniani, Wiki ya Utumishi wa Umma na Michezo ya SHIMIWI; na kuratibu mafunzo, ajira na upandishwaji vyeo kwa watumishi.

## 6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

### 6.1 MAPATO

**276. *Mheshimiwa Spika***, mwaka 2025/26 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi Bilioni Moja, na Milioni Thelathini na Sita (Shilingi 1,036,000,000)**. Vyanzo vya mapato hayo ni Vitambulisho vya Waandishi wa Habari, Machapisho ya Picha, Mabango na Majarida, Usajili wa Magazeti, Ada ya Mwaka ya Magazeti, Viingilio katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru, Ada za Upangishaji na Matangazo katika Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam pamoja na Ada za Wanachuo kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Aidha, kwa upande wa Taasisi Kumi na Mbili (12) zilizo chini ya Wizara kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni **Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Mbili Tisini na Tano, Mia Moja Tisi na Mbili Elfu (Shilingi 40,295,192,000). *Kiambatisho Na.* 1** ni mchanganuo wa mapato yanayotarajiwa kukusanywa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2025/26.

## 6.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO

**277.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2025/26 Wizara imetengewa bajeti ya **Shilingi Bilioni Mia Tano Kumi na Tisa, Milioni Mia Sita Sitini, Sabini na Tatu Elfu** (**Shilingi 519,660,073,000).** Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi Bilioni Thelathini na Tatu, Milioni Mia Nne na Tatu Mia Nane Kumi na Tatu Elfu** (**Shilingi 33,403,813,000)**, Matumizi Mengineyo ni **Shilingi Bilioni Ishirini na Nane, Milioni Sitini na Tano, Mia Nne Sabini na Mbili Elfu (Shilingi 28,065,472,000)** na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Mia Nne Hamsini na Nane, Milioni Mia Moja Tisini Mia Saba Sabini na Nane Elfu (Shilingi 458,190,778,000)** ***Kiambatisho Na. 2*** kinaonesha mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Miradi ya Maendeleo.

## 7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2025/26

**278.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2025/26 naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2025/26 yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Tano Kumi na Tisa, Milioni Mia Sita Sitini, Sabini na Tatu Elfu (Shilingi 519,660,073,000).** Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi Bilioni Thelathini na Tatu, Milioni Mia Nne na Tatu Mia Nane Kumi na Tatu Elfu** (**Shilingi 33,403,813,000)**), Matumizi Mengineyo ni **Shilingi Bilioni Ishirini na Nane, Milioni Sitini na Tano, Mia Nne Sabini na Mbili Elfu (Shilingi 28,065,472,000)** na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Mia Nne Hamsini na Nane, Milioni Mia Moja Tisini Mia Saba Sabini na Nane Elfu (Shilingi 458,190,778,000).**

## 8.0 SHUKURANI NA HITIMISHO

**279.** ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2024/25 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali, taasisi za fedha, vyombo vya habari, taasisi za hiari

zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wasanii, wanamichezo, waandishi wa habari na wananchi kwa ujumla wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge.

**280.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa upande wa wadau siyo rahisi kuwataja wote kwa majina, nitawataja wachache nikianza na wadau wa ndani, ambao ni Kampuni za Azam Media; Multichoice Tanzania; Airtel Tanzania; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Benki ya NMB. Wengine ni Tanzania National Parks (TANAPA); Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (NCA); Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA); Benki ya CRDB; Benki ya NBC; Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF); na Makumbusho ya Taifa. Aidha, wadau wengine ni pamoja na Shirika la Bima la Taifa (NIC); Wakala wa Serikali Mtandao (eGA); Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC); Shirika la Culture and Development East Africa (CDEA); Taasisi ya Global Opportunity Youth Network (GOYN); Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); Kampuni ya Startimes; Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF); Vituo vya Redio vya Clouds Media Group, EFM; Wasafi na Crown Fm.

**281.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa upande wa wadau wa nje, naomba nianze na Balozi zote za Tanzania katika mataifa mbalimbali, Serikali ya Mji wa Busan nchini Korea ya Kusini; Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA); Bagamoyo Friendship Society (Ujerumani); Musicians for a Better Life (Ujerumani); Kituo cha Sanaa na Utamaduni cha Alliance Francaise; Wamiliki wa Kampuni za Emirates; Jamhuri ya Watu wa China; Umoja wa Ulaya; na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

**282.** ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba kumalizia hotuba yangu kwa kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maelekezo mahususi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla. Aidha, uwekezaji mkubwa uliofanyika chini ya uongozi wake katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo umeleta mageuzi chanya yanayogusa maisha ya Watanzania kwa namna ya kipekee sana.

**283.** ***Mheshimiwa Spika***, nawashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na ushauri katika kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Pia, namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo ya mara kwa mara yaliyowezesha kuboresha utendaji wa Wizara. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Doto Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati ambapo maelekezo yake yamekuwa na mchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**284.** ***Mheshimiwa Spika***, nitoe pongezi kwa viongozi wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa karibu katika kuhakikisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo unafanikiwa kwa ufanisi.

**285.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati kabisa nitumie fursa hii pia kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee kabisa niwashukuru Mheshimiwa Hamis Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Ndugu Gerson Msigwa Katibu Mkuu na Ndugu Methusela Ntonda, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo katika Wizara yangu, Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu katika maendeleo na taifa letu. Aidha, nawasihi tuendelee kushikamana, tushirikiane kwa karibu na tuendelee kuwa wabunifu katika kuhakikisha kuwa sekta tunazozisimamia zinachangia kikamilifu katika maendeleo ya taifa letu. "*Umoja wetu ni nguvu yetu, na kwa pamoja tunaweza kufanikisha makubwa zaidi*".

**286.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, nitumie fursa hii kuishukuru familia yangu, hususan mke wangu kipenzi Dkt. Amina Kabudi na watoto wetu wapendwa Dkt. Tumaini Mwendile Kabudi na Bw. Aidan Imani Kabudi. Ninyi mmekuwa nguzo imara ya faraja, matumaini na furaha kwangu. Mmenipa nguvu ya kuendelea

mbele kila siku, hata nyakati ambazo changamoto zimekuwa nyingi katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kazi. Kwa mapenzi yenu na uvumilivu wenu, nimeweza kutekeleza majukumu yangu kwa mafanikio.

**287.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mara nyingine niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilosa kwa kushirikiana nami katika kuwezesha maendeleo ya jimbo letu. Ushirikiano wenu na maoni yenu, ndivyo vilivyowezesha mafanikio tuliyonayo leo. Imekuwa miaka mitano (5) mizuri ya utendaji ulioacha alama kubwa kwa Jimbo la Kilosa na kwa unyenyekevu mkubwa nawaombeni tena muendelee kuweka imani yenu kwa Chama cha Mapinduzi nami Mbunge wenu. Nawaahidi sitowaangusha. Asanteni sana.

**288.** ***Mheshimiwa Spika*,** naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inapatikana kwenye Tovuti ya Wizara ambayo ni *www.michezo.go.tz.*

**289.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Waheshimiwa Wabunge ninamkabidhi sasa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge kuja kuchukua nafasi hii. *(Makofi)*

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee.

**MHE. MUSSA R. SIMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati

ninaomba kusoma Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96) kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hii ni matokeo ya shughuli za Kamati kwa kipindi cha tarehe 11 hadi 27 Machi, 2025 kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Sekta zilizo chini ya Kamati hii. Ninaomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulithibitishia Bunge kuwa, Muundo wa Taarifa hii umezingatia Masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kuhusu muundo wa Tarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa maelezo hayo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Bunge. Sehemu hizo ni:-

(i) Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla na kuonesha msingi, mbinu na wigo wa kazi ya Kamati katika kufanyia kazi makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hii.

(ii) Sehemu ya pili inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Wizara hii mwaka wa fedha 2024/2025 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iii) Sehemu ya tatu inabainisha maoni na ushauri wa Kamati na hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Nyongeza ya Nane chini ya Kanuni ya 137, imeweka masharti yanayofafanua jukumu la Kamati hii kufanyia kazi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6(7)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kinaipa Kamati hii jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge ilitaka makadirio haya yajadiliwe na Kamati kabla ya kuwasilishwa Bungeni leo. Ninaomba kulihakikishia Bunge hili kuwa masharti hayo yalitimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema asubuhi ya leo, taarifa hii imewekwa Mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 118(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na sasa, ninawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Bunge kama nilivyoeleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubainisha njia iliyotumiwa na Kamati kufanyia kazi hoja hii ni masharti ya Kanuni ya 142(a) ya Kanuni za Bunge. Madhumuni yake ni kuiwezesha Taarifa hii kuwa rejea madhubuti inayosaidia mjadala wa Bunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Kwa kufanya hivyo, Kamati imejenga msingi wa uadilifu uliozingatiwa ili kupata maoni na ushauri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbinu za uchambuzi zilijumuisha kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Uchambuzi wa majibu na mawasilisho ulifanyika kwa kufanya ulinganifu kimaudhui na wa hali halisi. Yote haya yamewezesha kupatikana kwa taarifa hii ambayo inabainisha maoni na ushauri wa kufanyiwa kazi katika hoja kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyofahamika, lengo la Taarifa hii ni kulipatia Bunge tathmini ya kina na yenye ushahidi kuhusu makadirio ya matumizi na mapato yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Madhumuni yake ni kuongoza mjadala, kuonesha uwajibikaji wa kibajeti na kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatengwa kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa na mahitaji halisi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Taarifa hii inagusa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Maudhui yake yanahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa Bunge lilipopitisha bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la maudhui ya Taarifa hii linagusa makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli, ulinganisho wa vipaumbele na matarajio ya wananchi na bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote nje ya maeneo niliyoyaeleza si sehemu ya taarifa hii. Sababu ya kufanya hivyo ni kuchunga masharti ya 71(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu mambo yasiyoruhusiwa. Jumla ya yote, wigo huo ni muhimu kwa taratibu bora za Bunge kujadili hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya jumla; kwa ujumla sehemu ya kwanza imeanza kwa ombi la kuwasilisha rasmi Taarifa hii katika majadiliano ya Bunge, kuonesha muundo wa Taarifa hii unaozingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge na kubainisha msingi wa Kamati kufanyia kazi makadirio ya Wizara hii. Kanuni zilizojenga msingi huu ni Kanuni ya 137 inayoweka masharti katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo inaonesha majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 118 inayohusu masharti ya makadirio haya kujadiliwa kwanza na Kamati kabla ya Bunge, Kamati kuweka Mezani taarifa mapema asubuhi kama ilivyofanyika na Kamati kuwasilisha rasmi wakati wa majadiliano

kama inavyofanyika sasa. Vilevile, Kanuni ya 142 inayotaka Taarifa yoyote ya Kamati kuwekwa katika sehemu kuu tatu ni msingi wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa makadirio ya mapato na matumizi. Sehemu hii imefafanua mambo makuu mawili: kwanza ni kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na pili ni uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika sehemu ya kwanza, maelezo yametolewa kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, sehemu hii imefafanua kuhusu uchambuzi wa makadirio ya maduhuli, uchambuzi wa makadirio ya bajeti na miradi ya maendeleo na uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Maelezo yaliyotolewa yameonesha kuwa sehemu ya ushauri uliotolewa unaendelea kufanyiwa kazi. Uzoefu wa mwaka wa fedha 2024/2025 umezingatiwa katika bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge umeendana na majukumu yaliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba maelezo kamili yanapatikana katika Taarifa ya Kamati. Baada ya uchambuzi, ninaomba kutoa maoni ya Kamati kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi. Maoni haya yanajenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Maoni haya ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokupatikana kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni jambo linaloweza kuathiri matarajio ya miradi iliyopangwa;

(ii) Kukosekana kwa mikakati ya kuboresha viwanja vya michezo nchini, kunafifisha uwezekano wa kuwa na viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya kitaifa na kimataifa, hali inayoongeza

mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa (*Benjamin Mkapa Stadium)*

(iii) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Arusha ni jambo linaloweza kufanikisha utekelezaji wa mradi huu kama ilivyokusudiwa hivyo, kuongeza chachu ya utalii na kuwa kituo muhimu katika Mashindano ya Mataifa ya Afrika *(AFCON)*.

(iv) Wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo za Hakimiliki kwa kuongeza vifaa vinavyotozwa Tozo hii hasa vya Kidijiti unahitaji kuboreshwa na kuongezwa;

(v) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji zipatikane kwa wakati, ili kutozuia ukamilishaji wa mradi wa ujenzi na ununuzi wa mitambo;

(vi) Upo umuhimu wa kufanyika kwa tathmini, uchunguzi na utafiti katika Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kuhusu utendaji kazi wa *TSN. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri. Kutokana na maoni yalivyoelezwa hapo juu, Kamati ilizingatia ipasavyo maoni hayo na kuyatumia katika msingi wa ushauri ufuataao:-

(i) Serikali iendelee kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio kwa Wizara hii;

(ii) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iandae mkakati wa kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya kitaifa na kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa *(Benjamin Mkapa Stadium);*

(iii) Serikali iendelee kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Arusha ili kufanikisha na kukamilisha utekelezaji wa mradi huu kama

ilivyokusudiwa na pia kuongeza chachu ya utalii na kuwa kituo muhimu katika Mashindano ya Mataifa ya Afrika *(AFCON);*

(iv) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iboreshe na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo za Hakimiliki kwa kuongeza vifaa vinavyotozwa Tozo hii hasa vya Kidijiti;

(v) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji zitolewe kabla ya tarehe Mosi Julai, 2025;

(vi) Serikali ifanye tathmini na utafiti kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kuhusu utendaji kazi wa *TSN* ili kuweza kujua ni sababu zipi zimesababisha jengo la kiwanda cha uchapaji kutokukamilika kwa wakati; na

(vii) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ikamilishe ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji ili kupunguza gharama ya uendeshaji na utunzaji wa mitambo katika maghala ya taasisi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Gerson Partinus Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Methusela Ntonda, pamoja na watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Singida Mjini kwa ushirikiano mkubwa walionipatia na kuhakikisha miradi mingi inapatikana katika Jimbo la Singida Mjini. Ninaomba tuendelee kuwa pamoja na maendeleo ya Jimbo la Singida Mjini yanahitaji umoja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninapenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongonzwa na Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Idelphonce Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika wakati wote tulipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96**) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Taarifa hii ni matokeo ya shughuli za Kamati kwa kipindi cha tarehe 11 hadi 27 Machi, 2025 kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na Matumizi kwa Sekta zilizo chini ya Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yote ya kamati iingie kwenye Hansard kama ilivyowasilishwa.**

### 1.1 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulithibitishia Bunge kuwa, Muundo wa Taarifa hii umezingati Masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, kuhusu muundo wa Tarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa maelezo hayo, Taarifa hii imegawanyika katika sehumu kuu tatu kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Bunge. Sehemu hizo ni:

(i) Sehemu ya **Kwanza** inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati katika kufanyia kazi makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hii.

(ii) Sehemu ya **Pili** inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Wizara hii Mwaka wa fedha 2024/2025 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Sehemu ya **Tatu** inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na hitimisho.

### 1.2 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati

#### 1.2.1 Msingi

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni mashartI ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Nyongeza ya Nane chini ya Kanuni ya 137, imeweka masharti yanayofafanua jukumu la Kamati hii kufanyia kazi Makadirio ya Mapato na Matumizi, Fungu 96.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 6 (7) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinaipa

Kamati hii jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge ilitaka makadirio haya yajadiliwe na Kamati kabla kuwasilishwa Bungeni leo. Naomba kulihakikishia Bunge hili kuwa masharti hayo yalitimizwa.

**Mheshimiwa Spika**, mapema asubuhi ya leo, taarifa hii imewekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (5) ya Kanuni za Bunge. Na sasa, nawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge kama nilivyoeleza hapo awali.

### 1.2.2 Mbinu na Njia Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** kubainisha njia iliyotumiwa na Kamati kufanyia kazi hoja hii ni masharti ya Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Bunge. Madhumuni yake ni kuiwezesha Taarifa kuwa rejea madhubuti, inayosaidia mjadala wa Bunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Kwa kufanya hivyo, Kamati inajenga msingi wa uadilifu uliozingatiwa ilikupata maoni na ushauri wake.

**Mheshimiwa Spika,** mbinu za uchambuzi zilijumuisha kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Uchambuzi wa majibu na mawasilisho ulifanyika kwa kufanya ulinganisho kimaudhui na hali halisi. Yote hayo yamewezesha kupatikana kwa taarifa hii ambayo inabainisha maoni na ushauri wa kufanyiwa kazi katika hoja kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

### 1.2.3 Wigo wa Kazi

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyofahamika, lengo la Taarifa hii ni kulipatia Bunge tathmini ya kina na yenye ushahidi kuhusu makadirio ya matumizi na mapato yaliyowasilishwa na Mtoa hoja. Madhumuni yake ni kuongoza mjadala, kuonesha uwajibikaji wa kibajeti na kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatengwa kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa na mahitaji halisi ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo, Taarifa hii inagusa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na

Makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Maudhui yake yanahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa Bunge lilipopitisha bajeti ya wizara hii. Eneo lingine la maudhui ya Taarifa hii linagusa makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli, ulinganisho wa vipaumbele na matarajio ya wananchi na bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** mambo yote nje ya maeneo niliyoyaeleza si sehemu ya taarifa hii. Sababu ya kufanya hivyo ni kuchunga masharti ya 71 (1) ya Kanuni za Bunge kuhusu mambo yasiyoruhusiwa. Jumla ya yote, wigo huo ni muhimu kwa taratibu bora za Bunge kujadili hoja ya Wizara hii.

### 1.3 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Sehemu ya Kwanza imeanza kwa ombi la kuiwasilisha rasmi Taarifa hii katika majadiliano ya Bunge, kuonesha muundo wa Taarifa hii unavyozingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge na kubainisha msingi wa Kamati kufanyia kazi makadirio ya Wizara hii. Kanuni zilizojenga msingi huo ni Kanuni ya 137 inayoweka masharti katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge ambayo inaonesha majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** nyingine ni Kanuni ya 118 inayohusu masharti ya makadilirio haya kujadiliwa kwanza na Kamati kabla ya Bunge, Kamati kuweka mezani taarifa mapema asubuhi kama ilivyofanyika na Kamati kuwasilisha rasmi wakati wa majadiliano kama inavyofanyika sasa. Vilevile, Kanuni ya 142 inayotaka Taarifa yoyote ya Kamati kuwekwa katika sehemu kuu tatu ni msingi wa Taarifa hii.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI

### 2.1 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii imefafanua mambo makuu mawili: Kwanza ni kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na pili ni uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika sehemu ya kwanza, maelezo yametolewa kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utekelezaji wa majukumu na mipango ya wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, sehemu hii imefafanua kuhusu uchambuzi wa makadirio ya maduhuli, uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo na uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Maelezo yaliyotolewa yameonesha kuwa sehemu ya ushauri uliotolewa unaendelea kufanyiwa kazi, uzoefu wa mwaka wa fedha 2024/2025 umezingatiwa katika bajeti kwa mwaka 2025/2026 na upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge umeendana na majukumu yaliyopangwa.

**Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba maelezo kamili yanapatikana katika taarifa ya Kamati**.

**SEHEMU YA TATU**

## 3.0 MAONI, USHAURI NA HITIMISHO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi, naomba kutoa maoni ya Kamati kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi. Maoni haya yanajenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokupatikana kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni jambo linaloweza kuathiri matarajio ya miradi iliyopangwa;

(ii) Kukosekana kwa mikakati ya kuboresha viwanja vya michezo nchini, kunafifisha uwezekano wa kuwa na viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya kitaifa na kimataifa, hali inayoongeza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamini Mkapa (*Benjamini Mkapa Stadium)*.

(iii) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Arusha ni jambo linaloweza kufanikisha utekelezaji wa mradi huu kama ilivyokusudiwa. Hivyo, kuongeza chachu ya utalii na kuwa kituo muhimu katika Mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON).

(iv) Wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo za Hakimiliki kwa kuongeza vifaa vinavyotozwa Tozo hii hasa vya Kidijitali unahitaji kuboreshwa na kuongezwa;

(v) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji zipatikane kwa wakati, ili kutozuia ukamilikaji wa mradi wa ujenzi na ununuzi wa mitambo;

(vi) Upo umuhimu wa kufanyika kwa tathmini, uchunguzi na utafiti kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu utendaji kazi wa TSN.

### 3.3 Ushauri

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na maoni yalivyoelezwa hapo juu, Kamati ilizingatia ipasavyo maoni hayo na kuyatumia kama msingi wa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iendelee kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio kwa Wizara hii.

(ii) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iandae mikakati ya kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya kitaifa na kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamini Mkapa *(Benjamini Mkapa Stadium)*.

(iii) Serikali iendelee kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Arusha ili kufanikisha na kukamilisha utekelezaji wa mradi huu kama ilivyokusudiwa na pia kuongeza chachu ya utalii na kuwa kituo muhimu katika Mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON).

(iv) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iboreshe na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo za Hakimiliki kwa kuongeza vifaa vinavyotozwa Tozo hii hasa vya Kidijitali.

(v) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji zitolewe kabla ya tarehe 01 Julai, 2025;

(vi) Serikali ifanye tathmini, utafiti kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu utendaji kazi wa TSN ili kuweza kujua ni sababu zipi? zimesababisha jengo la kiwanda cha uchapaji kutokukamilika kwa wakati.

(vii) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ikamilishe ujenzi wa Jengo la Kiwanda cha Uchapaji ili kupunguza gharama za uendeshaji na utunzaji wa mitambo katika maghala ya Taasisi nyingine.

### 3.4 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru – Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb),

Naibu Waziri - Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndg. Gerson Partinus Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Methusera Ntonda, pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongonzwa na Katibu wa Bunge *Ndg. Baraka Idephonce. Leonard,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Husna Juma Sekiboko, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU,**
**UTAMADUNI NA MICHEZO**
07 Mei, 2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhani Sima, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii kwa niaba ya Mwenyekiti kwa kusoma kwa ufasaha mkubwa sana Taarifa ya Kamati, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na tutaanza uchangiaji asubuhi hii. Tutaanza na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko atafuatia Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza kabisa kwenye Wizara hii muhimu katika kuleta furaha, amani, upendo na mshikamano wa Taifa letu. Kabla sijaweka mchango wangu nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapinduzi makubwa aliyoyafanya katika Sekta ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tutakuwa mashahidi kwamba ni katika kipindi cha miaka michache tu (miaka mitatu, minne) nchi yetu sasa imekuwa na *identity* (utambulisho). Nchi yetu sasa inafahamika kwa namna ilivyo; kwa nini? Kwa sababu ya mapinduzi makubwa kwenye Sekta ya Michezo na mapinduzi makubwa kwenye Sekta ya Sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukisikiliza nyimbo zinazopigwa hapa Tanzania, ukiangalia maigizo na filamu zinazofanyika Tanzania ni tofauti kabisa kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuweka fedha, kuunga mkono shughuli zinazofanywa na wasanii na wanamichezo nchini. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu. Nimekuwa kwenye hii sekta tangu nimeingia kwenye Bunge hili huu ni mwaka wa tano. Kila bajeti ambayo imeletwa mbele ya Kamati yetu tumeona namna ambavyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akiongeza fedha mwaka hadi mwaka kuhakikisha kwamba anawaunga mkono Wasanii na Wanamichezo na mwisho wa siku tunakwenda katika ile Tanzania tunayoitamani kuiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea ninaomba niseme jambo moja. Mheshimiwa Waziri, Profesa Kabudi wakati ameteuliwa kuwa Waziri (na yeye huwa analisema kwenye majukwaa lakini na hapa nirudie). Wakati ameteuliwa kuwa Waziri mimi binafsi niliamini ni mtu ambaye anatumika zaidi kwenye *hard power* sikutegemea kama ni mzuri kiasi hiki kwenye *soft power. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninataka nikiri mbele ya Bunge lako Tukufu kwa muda ambao tumefanyakazi na Mheshimiwa Profesa Kabudi tumeona kwamba kweli Mheshimiwa Profesa Kabudi ana-*fit* kwenye *hard power* na *soft power.* Tunampongeza sana na tunamtakia utekelezaji mzuri sana wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu na kaka yangu Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Mwinjuma maarufu kwa jina la Mwana *FA*. Waheshimiwa Wabunge, ninadhani wanafahamu tupo pamoja kwenye hii nchi siku zote, wameshakuwepo Naibu Mawaziri wa Michezo kadha wa kadha kwenye nchi hii lakini Mwana *FA* yupo peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hayo kwa sababu gani? Mwana *FA* siyo tu kwamba ni mtumishi, ni msomi, ni Mbunge lakini ni mwanamichezo kindakindaki. Tumemuona akiahangaika na sekta ya michezo kila uchao siyo Simba au Yanga, siyo Taifa *Stars* au Twiga *Stars.* Kila sehemu tunamwona Naibu Waziri anahangaika kutafuta matokeo kwenye sekta aliyopewa kuisimamia. Nitumie fursa hii kumpongeza sana Mwana *FA*, kazi yake ni nzuri na sisi tuliopo nyuma yake tunakuunga mkono na tunaona namna gani ambavyo tunaweza tukafaidi katika Sekta hii ya Michezo kwa miaka ijayo, kama utaendelea kuwa katika dawati hilo. Tunakupongeza na tunakutakia kila la heri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefanya kazi na hii sekta na sasa ninafanya nayo kama Mwenyekiti. Hii Wizara kipindi cha nyuma wengi walikuwa wanaamini ni mlango wa kutokea, yaani ukipelekwa kwenye Wizara ya Michezo baada ya muda kidogo kazi yako imekwisha, lakini ninataka nikuhakikishie kwa timu ya wataalam Wakuu wa Taasisi waliopo kwenye sekta hii ya michezo kwa sasa, hakika sasa umekuwa mlango wa kuingilia na siyo mlango wa kutoka tena. Kazi inayofanyika tunaiona kwa macho tukilinganisha na miaka ya nyuma, tunaona matokeo ya wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawapatia mifano, leo Tanzania katika mwaka mmoja tu wa utekelezaji wa bajeti tumeanza ujenzi

wa viwanja vitatu vikubwa, jambo ambalo halikuwahi kutokea. Tumejenga Uwanja wa Benjamin Mkapa *years and years* huko nyuma lakini leo Dkt. Samia Suluhu Hassan anapeleka fedha *billions of moneys.* Kiwanja cha Arusha peke yake zaidi ya bilioni 200, ukarabati wa Benjamin Mkapa zaidi ya bilioni 35. Ujenzi wa Uwanja wa Dodoma peke yake zaidi ya bilioni 300. Hii inadhihirisha kwamba, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kwa dhati kuwekeza kwenye michezo kuhakikisha kwamba Tanzania inapata *identity.* Tunakwenda kutambulika kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumeshuhudia michuano ya *indoor football* iliyochezwa na timu za mabinti Afrika kwa ajili ya kufuzu kwenda kwenye Michuano ya Kimataifa ya Kidunia. Timu yetu ambayo imepata kufanya mazoezi kwa mwezi mmoja tu, imekwenda mpaka hatua ya fainali na ilikuwa chupuchupu wangechukua kombe. Hii, maana yake ni kwamba tunapiga hatua kubwa sana kwenye Sekta ya Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya hayo yote kupiga hatua kubwa kwenye michezo, sanaa, filamu na kila eneo maana yake ni kwamba, tunakuwa na Taifa lenye furaha. Leo asubuhi mmeona wenyewe wakati wametambulishwa hapa viongozi wa vilabu, soka na *TFF* makofi yalikuwa mengi. Hii inadhihirisha kwamba Tanzania tunapenda michezo na kuwekeza kwenye michezo siyo jambo la kawaida kwa sasa ni jambo la msingi na lazima liwekewe dhati katika bajeti, mipango na uendelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme jambo moja. Tanzania ni nchi ambayo ina amani. Amani iliyopo imejengwa kwa muda mrefu, lakini inalindwa kwa namna nyingi. Moja ya eneo muhimu ambalo linailinda amani yetu ni kuendeleza na kuwekeza kwenye michezo. Watu wakiwa na nafasi ya kucheza, kufurahi na kuburudika wanapata fursa ya kupunguza *stress,* msongo wa mawazo na mwisho wa siku tunakuwa na Taifa lenye furaha hatimaye tunakuwa tunaendeleza amani na mshikamano uliopo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana kwa kunipatia fursa, lakini ninataka nikuhakikishie kwamba, kazi ambayo ameifanya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika miaka mitatu ambayo tumeishuhudia kwa macho haijapata kutokea. Tupitishe bajeti, kazi hiyo ikaendelezwe na mwisho wa siku tuweze kufika katika Tanzania yenye utambulisho wake ndani ya dunia yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati hii inayohusiana na masuala ya sanaa na michezo. Tunakushukuru sana kwa mchango wako na kwa kufungua dimba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mheshimiwa Husna Sekiboko Wabunge wote watakaochangia wamepewa dakika saba, hakutakuwa na nyongeza ya muda, tunaomba tuji-*align* katika utaratibu huo.

Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, tafadhali.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, vilevile tumpongeze Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira ya dhati anayoionesha kupenda michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo niendelee kumpongeza Baba yangu Mheshimiwa Waziri Kabudi, watoto wa Mjini tunasema *homeboy,* sasa hivi singeli anacheza na kukesha anakesha kama *CNN*. Kwa hiyo, *alhamdulillah* wanasema ukienda Chile fanana na Watu wa Chile, hongora sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninapenda kumpongeza ndugu yangu huyu ni msanii wangu niliachiwa anaitwa Mwana *FA*, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma. Hii Wizara ina Naibu Waziri anapambana kwa ajili ya sanaa pia. Tumeona mfano wa ile Samia *Festival* ya juzi, Jukwaa la Kimataifa na kila kitu kimekaa

vizuri. Hatuna cha kusema zaidi ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuenda kuibadilisha hii Wizara ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze vilevile mtani wangu ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Michezo na pia ni Msemaji Mkuu wa Serikali, hongera sana na tunaona, tulisimama hapa na Kamati tukipambana bajeti ipande, leo hii tukizungumzia Wizara ya Michezo unaona Wizara bora kabisa na hata bajeti imepanda, imesimama. Tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, piga makofi kwa Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuende kwenye soka. Mimi ni mpenzi wa mpira wa miguu, hata wakati Naibu Spika anatambulisha Viongozi wa Simba na Yanga pale, kilichoonekana Wabunge wanapenda soka. Kinachoendelea kwenye soka la nyumbani, kwanza niipongeze *TFF* kwa ujumla wake kwa kile wanachokifanya kwenye soka letu la Afrika Mashariki nzima, sisi tunaongoa Tanzania. Ninaipongeza pia Bodi ya Ligi Tanzania tunafanya vizuri na tunakwenda ku-*compete* na timu kama za Morocco na wapi huko tunaonekana tuna klabu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuwe wawazi wote hapa, Simba na Yanga haiwezi kufungwa na timu yoyote ya nchi hii kuna nini? Wanasema '*yamshillajabar illa jarda'* punda haendi bila bakora. Viongozi wa *TFF* na Bodi ya Ligi waache kudekeza Simba na Yanga. Acheni kutengeneza utaratibu ambao tunaona kabisa kama hawa wanabebwa wengine hawabebwi, waache! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe wawazi, mimi ni Simba, tunaona juzi wenzetu walikuwa wanacheza pale Zanzibar, wakiwa hawachezi hapa utasikia Yanga kampiga mtu tano na Simba kampiga mtu saba. Wakitoka nje ya hapa, jini katoka mganga hoi. Yaani wanashinda kwa shida, kuna siasa mnafanya kwenye mpira, siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ligi ya Italy imepoteza heshima yake kwa sababu ya hiki ambacho leo hii tunakileta Tanzania. Hiki tunachokileta…

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza kumshukuru mchangiaji kwa mchango mzuri anaouchangia. Ninaomba nimpatie taarifa kwamba hili alilolisema ni muhimu sana na ndiyo sababu timu ya Taifa ya Tanzania Bara ina muda mrefu sana imeshindwa kuifunga timu ya Taifa ya Zanzibar. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taletale, unaipokea taarifa?

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nilikuwa nawaza dakika saba ulizonipa ni ndogo. Tuongee ukweli, hakuna watu wanafanya vizuri wameikuza na kuiheshimisha ligi yetu kama Viongozi wa Bodi wa Ligi ya sasa. Hakuna watu wameweza kukuza mpira wa nchi hii kama Kiongozi wa *TFF, Brother* yangu Karia hongera sana, lakini pole kwa kumpoteza mama yako, lakini leo hii fuateni sheria, haina huruma. Mtu anakurupuka amevaa tai yake hatuchezi *khaa!* Viongozi wanajua sheria, wasimamie sheria, ndiyo itakayotubeba, kama wanashindwa kufuata sheria tunakwenda kuua soka ambalo watu wote humu ndani tunapenda mpira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya nirudi kwenye mchezo wa ngumi. Ninapotokea starehe yetu kubwa ni mchezo wa ngumi. Vijana wangu wa pale kwenye Kata ya Kiloka niliwapelekea *gloves* na kadhalika nikijua ngumi sasa hivi ni biashara. Ametoka muungwana mmoja huko alipotoka amekwenda kuishtaki Azam badala yake leo hii ngumi hazichezwi, hakuna ngumi. Ametoka tu kijana mmoja anatokea Tanga anaitwa Mafia ameandaa vijana wake, wanaenda kimungumungu ili wafike, leo hii hakuna mchezo wa ngumi. Kwenye hili Mheshimiwa Waziri ninaondoka na shilingi yako kama

hatokuja na utaratibu wa kutuambia, vijana wetu wanaocheza ngumi hatima yao ipo wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amempa Waziri kitengo cha habari ana *TBC, one of the biggest media* kwetu Tanzania aweke nguvu pale basi au atuambie huyu muungwana ambaye leo hii ameweza kuzuia michezo ya ngumi isichezwe, mimi nina mpiganaji wangu bora pale Morogoro Ndugu Twaha Kiduku ana-*struggle* leo hii, Azam wamefunga milango, sasa tujiulize wale vijana wanakwenda wapi? Wanataka kuongeza wakabaji mtaani? Kwa nini tunashindwa kuwasaidia hawa watu? Hili ni jukumu la nani kama siyo Wizara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitakuwa kipaumbele kwa kushika shilingi kama Mheshimiwa Waziri au Ndugu yangu Mwana *FA* hajaja na kauli ya nini hatma ya wacheza ngumi nchini tutaiona. Tusimuachie Mafia peke yake hatoweza tutamuumiza yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, Mheshimiwa Waziri hapa amezungumza kuhusu Mfuko wa Wasanii, ninamwona pale mwanangu Barnaba, hongera baba. Mfuko wa Sanaa, huu Mfuko Mheshimiwa Rais ameleta fedha kwa wasanii hawa, lakini Wizara wameibadilisha hii fedha wameipeleka benki, inadaiwa benki. Kwa hiyo, tukienda kukopa mkopo una sura ya kibenki, yale maono ya Mheshimiwa Rais siyo tena hayo, maono hayo ni ya kwao wao. Wizara warudishe maono ya Mheshimiwa Rais, anataka wasanii wafaidike, wao wametoa hizo hela wamezirudisha benki, wasanii wakienda kukopa mpaka wawe na nyumba, wana nyumba wale, wamewapa nyumba tangu lini? Hamna msanii mwenye nyumba hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Taletale tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, tunakushukuru kwa mchango wako. Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, atafuata Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa ya kuchangia katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia fursa hii. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii. Amekuwa karibu sana na wanahabari, wanautamaduni na wanamichezo kwa ujumla wao, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizo ziende sambamba kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake, wamefanya kazi nzuri sana na ninaona hii Wizara ipo ndani ya damu. Siyo mara moja ama mara mbili Mheshimiwa Waziri nimeona akirekebisha lugha kwamba tutumie hivi badala ya hivi. Pia, Naibu Waziri nimemuona siyo mara moja wala mara mbili akipiga mistari kutusherehesha, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni katika sehemu ya sanaa au utamaduni. Kuna makusanyo yanayoingia kutoka kwenye kanda tupu *(blank tape levy)*. Hizi fedha huwa zinapelekwa *COSOTA* kwa ajili ya sekta mbalimbali za sanaa na maendeleo ya wasanii. Wanufaika hadi sasa inaonekana ni sanaa za maonesho, watu wa filamu na watu wa muziki, lakini sijaona mpaka sasa hivi sanaa za ufundi wanafaidika vipi na fedha zile. Kwa hiyo, ni vizuri watuambie sanaa za ufundi na wao wananufaika vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunaingia katika michuano ya *AFCON* hapa nchini, ningependa pia kujua BASATA mmejipangaje kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali wabunifu kama wachoraji, wafinyanzi na watengeneza viungo kama vile Zanziba*r spices*, watengeneza mapambo ili waweze kuonesha na kuuza bidhaa zao kwa kutangaza nchi na pia kujipatia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiria kwamba katika kipindi hiki basi ni vizuri wakae nao wawape mbinu, michakato ya kufanya pia wawaandalie hata lugha rahisi za biashara, kwa sababu wanaokuja siyo wote wanaojua Kiswahili. Sasa, wawaandalie angalau mafunzo mafupi kwa ajili ya lugha za baisahara na wawaandalie wakalimani. *AFCON* inayokuja wajasiriamali wabunifu wanataka wafanye biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala lingine la usajili wa wasanii. BASATA wanakusanya ada na kodi nyingi kuliko *TRA*. Msanii binafsi akiimba mwenyewe peke yake anaenda kuambiwa hilo ni kosa la jinai lazima akajisajili. Huko kwenye kujisajili anaambiwa alipe fedha, msanii mchanga hela anatoa wapi? Kuna tozo wanatoa, tozo hiyo hiyo yule msanii ambaye ameshakua wanamweka sawa na msanii mchanga, sasa hawa wachanga watakua lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna malipo ambayo wanayafanya mtu anasema kuna tamasha langu nitafanya nchi nzima, BASATA ndiyo wanajua nchi nzima ina mikoa mingapi, lakini akija Dar es Salaam akilipa akienda Mwanza anaanza utaratibu mpya, akienda Mbeya mwingine akienda Mtwara mwingine, akienda Zanzibar pia, msanii huyo huyo fedha yake mpaka waichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi sijajua BASATA walishawasaidia nini wasanii. Wasanii wana makosa mbalimbali wameyafanya sijasikia BASATA wanatoa Mwanasheria wa kwenda kumsaidia msaniii. Pia, BASATA haohao sijaona msanii katengeneza nyimbo yake anataka kurekodi hana fedha, wakasema sisi tumepitia nyimbo yako, tumeipenda, tunakupa hizi nenda karekodi, sijaona, lakini fedha zao wanakusanya! Wakija hapa watuambie kitu gani ambacho wanawasaidia wasanii siyo tu kukusanya ada na fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wanawafungia wasaniii bila hata kuwahoji, kwa sababu wanawaacha wanaingia gharama kubwa, wanatengeneza video zao tayari wanamaliza, ikitoka wananchi tumeshapenda wimbo tunataka kurukaruka, tunaambiwa imefungiwa. Halafu yule mwenyewe hawamwiti

wakamwambia wamemfungia kwa sababu zipi na hawampi nafasi ya kujieleza, pia hawaangalii gharama alizotumia kutengeneza hizo *video*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilipenda kuzungumzia suala la Vazi la Taifa na Mdundo wa Taifa, linakera. Zaidi ya miaka 10 tunazungumza hayo hayo, kwa hiyo hata sasa hivi tukiongea ni kama vile tunampigia gitaa mbuzi. Ninaomba kabla ya hiyo shilingi sijafanya kampeni ya kumnyang'anya basi atakapokuja atupatie jibu la Vazi la Taifa na Mdundo wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilitaka nizungumzie kuhusu Tuzo ya Kalamu ya Mama Samia. Nichukue nafasi hii kuwapongeza waandaji wote *TAMWA* na *TCRA*. Hapa tumepata funzo kubwa sana na ndiyo maana siku zote ninasema mama akifanya kitu basi kafanya kwa wote. *TAMWA* ni Waandishi wa Habari Wanawake, lakini tumeona tuzo wamepewa mpaka wanaume. Hongereni sana *TAMWA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCRA* nao wameshiriki wameonesha jinsi gani kwamba hizi Taasisi za Serikali zinashuka kwa wananchi na hawa wananchi wanajua kwamba wapo pamoja na wao. Nishukuru Wizara zote zilizotoa ahadi, ninaomba ahadi hizi zikatekelezwe maana nyingi zimeongewa hapa tumezisikia. Kubwa zaidi katika mwono wangu, katika zile zawadi sijaona watu wa picha za *video* na kwenye magazeti na nini, kwa sababu zile nazo pia ni habari. Mtoto mdogo hajui kusoma, hajui kuandika, lakini akitazama picha anakwambia huyu ni Mama Samia. Waangalie na wao jinsi gani watu wa picha za video nao wanaweza kuwapa tuzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ninaomba hawa BASATA wakae na wasanii wao. Wasanii ni kioo cha jamii, tunakaa tunawaangalia, tuna wapenzi wao, tuna rafiki zao ambao tunapenda kuwafuatilia. Kinapofika kipindi wasanii wanaanza kugombana, kudhalilishana, kutukanana, kukashifiana, pale hawataki umaarufu, ule siyo umaarufu, umaarufu hauji kwa hivyo. Wafanye kazi, sisi tutawapa umaarufu, tunajua umaarufu wao; hawana sababu ya kutukanana. BASATA wakae nao wawaeleze

mafunzo mbalimbali ya uelewa juu ya mila, desturi, tamaduni, malezi na makuzi ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa haipendezi mtu binafsi na demu wake wanaachana wenyewe, matangazo yanakuja huku. Unamzibia mwenzio riziki asiolewe tena, jamani au asioe tena! Siyo vizuri. BASATA semeni nao wasanii wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niseme kwamba, kwa kuwa, Wizara imejipanga vizuri kwa bajeti hii ya mwaka wa fedha 2025/2026. Nimeiangalia mikakati waliyoiweka; na kwa kuwa, Mawaziri ninyi ni wasikivu na waelewa na wako tayari kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kazi zake kuhusu Wizara hii, niko tayari kuunga mkono hoja. Ninaunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Malembeka. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. *(Makofi)*

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa hii nafasi asubuhi ya leo. Kwanza kabisa ninachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyosaidia na kuhakikisha Wizara hii inafanya kazi zake kwa sekta zote, ikiwemo michezo, utamaduni, sanaa, pamoja na Lugha yetu ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa juhudi zake anazofanya katika kuhakikisha Wizara yake inafanikiwa kwa asilimia kubwa, ikiwemo kuwa mtetezi mkubwa wa Lugha ya Kiswahili. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, hapa upele umepata mkunaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wote katika Wizara hii. Wanafanya kazi sambamba kuhakikisha Wizara yao inafanikiwa katika sekta zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, ninapenda pia, kuwapongeza Wizara wakiongozwa na

Mheshimiwa Waziri katika kuhakikisha kwamba, ushirikiano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar unakuwa wa pamoja katika ushirikishwaji wa masuala yote ya kupeana elimu, uzoefu na kujengeana uwezo. Tunawashukuru na tunawaomba waendelee kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana kwa makongamano yanayofanyika ya Kimataifa na Kitaifa katika kukuza utamaduni wetu na kuueneza, pamoja na kueneza Kiswahili duniani. Pamoja na hilo, ninapenda kuongezea kwamba, katika kuhakikisha tunaeneza utamaduni wetu tutumie sana ngoma zetu za asili na vionjo vyetu vya asili. Kama Zanzibar kule Taarabu Asilia ndiyo inatakiwa itangazwe na siyo hii Taarabu ya sasa hivi. Ninaona hapo nimeshaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, ninawapongeza sana kwa kongamano lililofanyika kule Havana Cuba, pamoja na Kamusi zile za Kiswahili kwa Kihispania na Kihispania kwa Kiswahili, ninawapongeza sana. Kazi hii iendelee, ili Kiswalihi kiendelee kukua duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kuwapongeza na kuwashukuru waasisi wetu waliofanya Taifa letu Lugha ya Kiswahili iwe Lugha ya Taifa, lakini leo imekuwa si Lugha ya Taifa, imekuwa ni Lugha ya Dunia. Tuendelee kuwaombea dua na maisha mazuri huko waliko peponi. Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika balozi zetu tunafundisha Kiswahili, lakini pia, ninaongezea, tufundishe na utamaduni wetu wa asili. Kwa mfano, *South Korea,* ndugu yetu Tunu Mayemba anajitahidi sana kufundisha Kiswahili, lakini anaeneza Utamaduni wa Mtanzania kule *South Korea*. Anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kwenye Bodi ya Baraza la Kiswahili. Bodi ya Baraza la Kiswahili ina wajumbe sita na mmoja kutoka Zanzibar. Ninaona sasa kuwepo na umuhimu wa kuongeza idadi ya wajumbe kutoka upande wa pili wa Muungano ili kuleta ile hamasa zaidi ya Lugha yetu ya Kiswahili

kwa sababu, sasa hivi Kiswahili kimekuwa ni Lugha ya Afrika na ni Lugha ya Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wazo kwa Wizara hii, kama watashirikiana na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba, wanafunzi wanaokuja Tanzania kusoma basi wapate ile, kama *orientation,* ambayo watakuwa na Mafunzo ya Kiswahili kwa muda wa miezi mitatu mpaka sita ili kukitangaza zaidi Kiswahili. Pia, kuongeza mapato ndani ya nchi kwa hao wanafunzi wanaokuja kujifunza masomo mengine ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, tumeona kwenye bajeti kutakuwa na mapitio na kuongeza baadhi ya maneno mbalimbali ya Kiswahili. Ushauri wangu ni kwamba, tuendelee kufuata utaratibu katika kuongeza haya maneno na istilahi mpya za Kiswahili. Kwa sababu, kuna maneno tayari yamo kwenye Lahaja za Kiswahili na inasemekana kwamba, Lahaja za Lugha ya Kiswahili, kama lile neno lipo, basi lisitafutwe neno jipya kwa sababu, maneno yale tayari yapo na yanatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa mfano wa neno "Guruguru". Guruguru nimeambiwa ni ngurumo, lakini neno ngurumo lipo! Sasa kwa nini tena tunatafuta haya mambo ya maguruguru kuingiza kwenye Kiswahili wakati guruguru tayari ni mdudu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujitahidi lugha yetu iwe nyepesi, inayoweza kuzungumzika, inayoweza kusomesheka, inayoweza kutafsirika kwa watu wanaotaka kujifunza Kiswahili. Tukiendelea tu kujaza maneno, maneno, maneno, kwa sababu, tunayakataa maneno ya kigeni! Lugha zote zinatohoa maneno kutoka lugha nyingine. Mfano, kwa sasa kuna vitu vinavumbuliwa, sasa hivi hilo neno tutalipata wapi wakati kile kitu ni kipya na kimevumbuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kutoa mfano, nikichangia bajeti hii, mara nyingi ninatoa mfano kwenye Lugha yetu ya Kiswahili jinsi tulivyotohoa maneno kutoka lugha mbalimbali, Kihindi, Kiarabu, Kifaransa, Kiingereza na Lugha nyingine. Ninataka kutoa mfano mwingine leo kwa lugha nyingine, kwa nchi nyingine

walivyotohoa maneno tuone kwamba, hakuna haja ya kubadilisha maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kwenye Lugha ya Kingereza, kuna neno "*bus*", Kifaransa "*bus*", lakini ki-Mauritius ni "*bis*", ki-Komoro ni "*bis*", lakini kwa maana ya basi. Ninakuja neno "*train*"; Kifaransa "*tra*", lakini ki-Mauritius *train,* wametohoa wanaita vilevile *train*, wametumia kwa Kiingereza. Neno "*tablet*" Kingereza, "*tablete*" Kifaransa, *tablet* ki-Mauritius. Ninakuja neno '*tea*', *tea* kwa maana ya *tea* kwa lugha tatu; Kingereza, Kifaransa na ki-Mauritius. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini "*television*" Kingereza, "*television*" Kifaransa, "*television*" ki-Mauritius. "*Doctor*" Kingereza, "*Docteur*" Kifaransa, "*doctor*" ki-Mauritius, mmetumia hapa! Tuone kwamba, kutohoa lugha za kigeni ni kawaida katika lugha katika dunia yetu. Kwa hivyo, tusiwe tunaongeza maneno magumu, mazito, yasiyoweza kutamkika, yasiyoweza kutafsirika, lugha itakuwa ngumu, lugha haitikuwa nyepesi, tutakimbiwa. Watu watakwenda kutafuta wataalam wenye lugha nyepesi, ili waweze kujifunza kuongea tu na kubadilishana maneno na mawazo kwa sababu, siyo watu wote wanakwenda kufanya mitihani; kama wataingia darasani wafanye mitihani, maneno magumu. Watu wanataka kujua kuzungumza Kiswahili, kuelewana na kufahamiana. Ninafikiri nimeeleweka *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kupongeza juhudi mbalimbali zinazofanywa katika kuwajengea uwezo wataalam wetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, muda wako ulishakwisha, lakini kwa uzito wa hoja nilikuachia dakika mbili. *(Makofi)*

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili ni ajira, tuendelee kuhamasisha vijana wetu na Wizara itenge kitengo au watu maalum wa kuwasaidia vijana wetu wa Tanzania namna ya kuzitafuta hizi fursa za ajira. Kwa sababu,

wengi hawana upeo na uelewa mkubwa wa kujua hizi fursa za ajira, matokeo yake nchi ni nyingine na nchi jirani wanazipata wao wakati vijana wetu wana uwezo zaidi kuliko hao wanaokwenda kufundisha na kuwa wakalimani. Ninaomba tuwasaidie, tuweke kitengo au watu maalum wa kuwasaidia vijana wetu. Mwisho, ninawapongeza Wizara kwa andiko la kuomba kujengewa Kituo cha Utamaduni na Mambo ya Kiafrika, *UNESCO*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Muda wako ulishaisha.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninadhani Mheshimiwa Profesa Kabudi utam-*consult* baadaye Mheshimiwa Khadija, ili kutekeleza huu ushauri wake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninamkaribisha sasa Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, wajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Ninampongeza sana rafiki yangu Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii. Siku nilipoona uteuzi wake niliamini kabisa kwamba, anaenda kurekebisha mambo yote kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake anazofanya katika kuinua michezo nchini kwetu. Ninamuomba Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa iliyofanywa na Simba; mimi ni Mwanayanga, lakini kwa kazi kubwa iliyofanywa na Simba wanastahili na wao kupewa ndege, ili waende kwenye fainali huko Morocco. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimewaona viongozi wa Bodi ya Ligi na nimemwona Rais wa *TFF,* ninampongeza sana. Nimemwona Rais Mstaafu, Bwana Tenga; ninadhani Bwana Tenga ni mtu wa kuigwa sana kwenye hii Tasnia ya Michezo. Kwa

kweli, ni kiongozi ambaye alifanya kazi yake vizuri na akastaafu na bado wanamtumia, lakini ni mtu anayeheshimika sana kwenye Tasnia ya Michezo. Sasa ninadhani na wale walioko kwenye madaraka waige mfano wa jinsi gani Mzee Tenga aliongoza michezo yetu hapa Tanzania, vinginevyo watamaliza vipindi vyao halafu watakuwa ma-oya-oya huko mtaani, hawaeleweki na hawaheshimiki kwa kazi walizozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuuliza kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kabudi, Waziri, na nilikuona, kutokana na mgogoro uliopo kwenye timu zetu hizi kubwa mbili, nilimwona alitoka saa nne usiku kwenye kikao. Baada ya kutoka mle shaah! Mpaka leo hatujajua kilichotokea kule. Ninatanguliza maneno haya, ili uyajue, leo nitashika Shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpira wa Simba na Yanga. Timu ya Simba na Yanga kwenye nchi hii ndiyo burudani pekee iliyobaki kwa watu wote. Sasa wanatambua kabisa ipo migogoro, lakini hata kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Profesa Kabudi sijaona mahali ambapo anataja. Ikiwa Rais mwenyewe anafadhili mpaka anatoa hela zake mfukoni kuwapa vijana hamasa, halafu wanaona huu mchezo tuendelee kusikia tu ngonjera za huyu na huyu! Ninamtangulizia kabisa shilingi Mzee Profesa Kabudi, ninaondoka nayo. Kama hatakuja na taarifa sahihi, alichokisikia akieleze hili ndilo Bunge la wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa tunasikia mitandaoni na wewe mwenzetu aliyeteuliwa kwenda kutuwakilisha amesikia sirini, halafu analeta taarifa tumpitishie bajeti, tunaacha kuelewa kinachoendelea. Sisi tukirudi huko majimboni kwetu na sisi tuwe tena watu wa mitandao? Leo kama hatatoa taarifa sahihi nitashika Shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamini Simba hawana makosa, Yanga hawana makosa, lakini kinachoendelea, nani anayetakiwa kutueleza taarifa sahihi? Tunaona kama mchezo, eeh! Kesi imeenda *CAS*, imerudi *CAS* imekuja huku, kabla hajamsikiliza mlalamikaji anatangaza mechi, anacheza Bodi ya Ligi, inacheza Yanga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kujua, Mheshimiwa Profesa Kabudi yeye aliendа, alisikiliza pande zote mbili, Simba na Yanga. Sitaki kusema Yanga ina makosa wala Simba ina makosa, Waziri aliyesikiliza atupe majibu sisi Wabunge, ili tukawaeleze watu wetu. Michezo ni furaha, Simba na Yanga ni *part* ya maisha ya kuburudisha Watanzania. Kwa hiyo, akija bila maneno, leo nitamzingua Mheshimiwa Profesa Kabudi, lazima aje na taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania tumepata heshima ya kuandaa *AFCON*, halafu dunia yote itaangalia *AFCON* imeandaliwa Tanzania. Halafu tunakuwa na viongozi wahuni tu, wanaamua wanavyotaka, hatuwezi kwenda kwa *design* hiyo. Hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote tunaweza kuwa Marais wa *TFF*, wote humu tunaweza kuwa Viongozi wa Bodi ya Ligi. Hata mimi ninaweza kuteuliwa, lazima niwe wazi, siyo tu kama tumempa mtu kuongoza familia yake. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, kuliko kulitia aibu Taifa hili tunakokwenda kwenye michezo yetu, ni lazima aje na taarifa Bunge tufahamu. Asipokuja nayo, leo nitaondoka na Shilingi. Mimi ni Daktari, yeye ni Profesa. kwa hiyo, Mzee ajiandae na yeye mwenyewe amenipandisha kuniita Profesa, ananiita Profesa. Kwa hiyo, leo nitamzingua kiprofesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie, nishauri; Bodi ya Ligi isiongozwe na *TFF*, iwe *independence,* Wazungu wanasema ijitegemee. Tunaona...

**MBUNGE FULANI:** *(Hapa hakusikika vizuri)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** …hivyo hivyo! *independent,* hivyo hivyo. Tunaona sasa inapokea maelekezo tu kutoka kwenye *TFF*. Kwa hiyo, ninaomba sana tuache na tuunde Bodi ya Ligi inayojitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwenye Mfuko wa Wasanii; nimewaona rafiki zangu wasanii. Unajua tatizo huko Serikalini huwa wanakurupuka, hawajui biashara, tuna mipango

mizuri ya pesa, lakini biashara hawaifahamu. Tukitoa mawazo, mimi nimeshiriki sana kuzitafuta zile pesa wasaniii wanajua, ukifika muda wa pesa wanakurupuka na shule. Sasa, hili ndiyo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Wasanii, pesa alizotoa Dkt. Mama Samia, leo tukiuliza kuna shilingi ngapi au waliowakopesha wamerudisha shilingi ngapi? Wako hapa! Kuchukua hela leo na wengine kuoa, kununua magari, starehe, wengine zimewaua na kuwaua! Badala ya kuwapa watu wanaoandaa filamu, wanaoandaa muziki, ma-*producer,* wanaenda kuwapa watu wanaoonekana kwenye *TV* kwa kuangalia *shape!* Hii haifai! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa yote imeisha. Wako hapa, tuwaulize; halafu tunaanza kuwasingizia masharti yamekuwa magumu mpaka walete hati. Hakuna pesa inatoka kirahisi, pesa lazima iwe na masharti ili tupate marejesho. Hatuwapi hela ya kwenda kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kuwapa watu wanaoandaa filamu, msanii anayeonekana kwenye *TV* wengi wao wanamalizana na ma-*producer*, analipwa *cash* yake anaondoka. Badala ya kuwapa wale waandaaji wa muziki, kuwapa waandaaji wanaoandaa filamu, wanaenda kuwapa watu wanaoonekana kwenye *TV*. Waziri aniambie kwenye taarifa yake, zile shilingi milioni 50, milioni 40 tulizotoa, aje na majibu, wangapi wamerudisha? Hata mmoja na anazifanyia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukakague biashara zao, wote wamenunua *Kluger,* wamenunua *Alphard*, zimeisha zote hamna hata mia. Sasa wangetuchukua tukawashauri, tuliozoea maisha ya kitaa, leo hii tungekuwa na wasanii mabilionea. Kwa sababu, ukimwezesha mwandaaji ni sawa umemwezesha yule anayeonekana kwenye *TV*. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa, akija hapa aje na majibu yanayoeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais na ninaendelea kuwaombea Simba wakafanye vizuri. Unapoenda kuiwakilisha nchi kwenye fainali sisi wote

tunaungana, kama Taifa moja. Serikali iangalie ndege na kama kuna nafasi, ninaomba *lift* kabisa, ninatanguliza, nikashangilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Profesa Kabudi, yeye ni mzee, mwalimu mbobevu wa Kitivo cha Sheria, nina imani anaweza kurekebisha hii Wizara. Ninajua yeye ni Mwalimu mzuri, sidhani kama ata-*fail*. Aki-*fail*, kama kuna kitu kinamsumbua mimi nipo, ninaweza kumshauri bila malipo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami leo niweze kuchangia katika Taarifa hii ya Bajeti au Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo. Awali ya yote ninapenda nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa jitihada kubwa anazofanya na uwekezaji mkubwa anaoufanya katika Sekta ya Michezo, Utamaduni na Sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mzee Wangu, Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi. Kwa kweli, anaiongoza vizuri Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa anaoupata kutoka kwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Katibu Mkuu Ndugu Gerson Msigwa, pamoja na Naibu Katibu Mkuu Methusela. Pia, ninazipongeza taasisi zote zinazosimamia michezo yetu na sanaa na utamaduni, pamoja na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwa kazi kubwa inayoifanya katika kuboresha tasnia zote ambazo ziko chini ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninapenda nichangie upande wa michezo. Hoja ya kwanza kwa kweli, ninapenda kama nilivyosema hapo mwanzo, nimempongeza Mheshimiwa Rais na kwa kweli, Rais wetu anastahili pongezi. Kwa sababu ku-*host CHAN* Mwaka 2024, *AFCON* Mwaka 2027, kuwa na timu ambazo

zinafanya vizuri za Mpira wa Miguu, *Under 17*, *Under 20*, kwenye *Golf*, kwenye *Cricket*, kwenye *Women's Football* ya Afrika kwa kweli, ni hatua kubwa ambayo imefikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina pendekezo; kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wetu ameshirikishwa katika kutoa tuzo mbalimbali kwa wasanii, wanamichezo na wadau wengine wa tasnia ambazo ziko chini ya Wizara hii, mzee wangu Mheshimiwa Profesa Kabudi, ninafikiri tuandae tuzo kwa Mheshimiwa Rais pia, katika kumtia moyo kuendelea kuzisimamia tasnia hizi na kuhakikisha uwekezaji mkubwa unakuwepo katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuipongeza Klabu ya Simba, ambayo imefikia hatua ya kucheza Fainali ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Sanasana ninampongeza pia, ndugu Mo Dewji kwa uwekezaji mkubwa ambao amekuwa akiufanya katika Klabu ya Simba na hivyo kuiwezesha kushika nafasi ya nne kwa ubora Barani Afrika katika Vilabu vya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya Simba yamelifikisha Taifa letu kuwa na ligi namba nne, msukumo mkubwa umetoka Simba na mapinduzi makubwa katika soka la nchi hii yametokea Simba kutokana na uwekezaji wa Mo Dewji. Siwalazimishi wana-Simba wajenge sanamu kule *Mo Arena* Bunju wala pale kwenye *club* yao ya Msimbazi, lakini nafikiri wanaweza wakafanya jambo hata kumpa tuzo Mheshimiwa Dewji, ninasema Mheshimiwa kwa sababu alishawahi kuwa Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo, siku ya tarehe 8 Machi tulitarajia kwamba kungekuwa na mechi ya lingi kuu, mechi namba 184. Mechi hii ilifutwa lakini baada ya kufutwa jana tumepata taarifa kwamba imepangiwa kuchezwa tarehe 15 mwezi Juni. Hata hivyo nisikitike kusema, kwamba mamlaka zetu za mchezo wa mpira wa miguu hazijatutendea haki, kwa sababu hawajatupa taarifa yoyote kwamba kilitokea nini mpaka kupelekea mechi ile isichezwe siku ya tarehe 8; lakini pia hatujapewa taarifa ni hatua gani zimechukuliwa kwa wote waliohusika na mechi ile kutokuchezwa tarehe 8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri, pamoja na kutangaza tarehe 15 mechi itachezwa mwezi Juni tunatakiwa tufahamu nini kilitokea na hatua gani zimechukuliwa. Hii itapelekea kuhakikisha kwamba matukio yasiyokuwa na afya katika mchezo wa mpira wa miguu hayatokei tena siku zijazo na ninataka nikwambie, kwamba timu zetu za Simba na Yanga ni timu maarufu sana Afrika Mashariki na Kati. Kuna wakati fulani nilisafiri kwenda Bujumbura nikafika mtaa mmoja unaitwa Buyenzi, siku hiyo mechi ya Simba na Yanga ilikuwa inachezwa, timu moja ikafunga goli, mtaa wote ulishangilia utafikiri upo Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Kwa hiyo ni timu zenye hadhi kubwa na mambo yetu yanatakiwa yaende kikubwa kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ninapenda kulizungumza ni kuhusu taasisi simamizi ya viwanja. Niiombe Wizara yetu ya Sanaa, Utamaduni, Habari na Michezo iteue watu makini kwenye hii taasisi ili hivi viwanja vyetu viweze kusimamiwa vizuri. Serikali imetenga fedha nyingi na inakarabati kwa kutumia fedha nyingi na kujenga viwanja. Ukienda pale Benjamini Mkapa ukarabati unaendelea, ukienda kule Zanzibar Kizimkazi matengenezo ya uwanja yanaendelea na viwanja vingine ambavyo vitatumika kwa ajili ya mashindano mbalimbali ikiwemo mashindano ya *AFCON* mwaka 2027. Kwa hiyo ninaomba hii taasisi simamizi iteuliwe watu madhubuti; sio kama wale ambao wametuletea aibu siku ile ya mechi ya Simba na Al Masry, uwanja ukawa hauchezeki, mpira haunogi kabisa pale uwanjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia hata siku ile ya tarehe 7 inadaiwa kwamba kulikuwa na watu wameingia wanazuia watu wengine kufanya mazoezi na kadhalika, lakini *TFF* nao katika vile viwanja ambavyo vinatumika kwa ajili ya mchezo wa mpira wa miguu kwa ligi mbalimbali ambazo zinatambuliwa na *TFF* watoe mafunzo kwa hawa watendaji watakaopatikana kwa taasisi hii simamizi; watoe mafunzo kuhusu zile kanuni za mchezo wetu wa mpira wa miguu na michezo mingine. Wapewe mafunzo ya kutosha ili kuhakikisha kwamba basi hivyo viwanja vinasimamiwa vizuri ili fedha nyingi ambazo zimewekezwa katika viwanja hivyo ziweze kuleta tija na ufanisi kwa michezo yetu yote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Kisangi

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye wizara hii. Kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhamasisha michezo ya Tanzania. Wote tumeshuhudia goli la mama, jinsi gani Mheshimiwa Rais alikuwa anazihamasisha timu zetu katika kuwapa motisha washilingi kadhaa katika timu zetu ili wale wachezaji wetu wapate *morale* ya kuweza kuwakilisha nchi yetu. Hayo tumeyaona matunda yake, tumeona matunda yake kwa timu za Yanga na Simba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niwapongeze timu ya Simba kwa kuingia fainali katika Kombe kubwa la Shirikisho. Pia niwapongeze timu ya Yanga kwa hatua waliyofikia. Asiyekubali ushindi si mshindani. Yanga imejikubali, sasa kwa pamoja tuungane twendeni tukawaunge mkono wenzetu Watanzania wenzetu wana *Simba Sports Club* warudi hapa na kombe hili la shirikisho. Huo ndio uzalendo na ndio Utanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nimpongeze Mheshimiwa Waziri Profesa Kabudi, Naibu Waziri na Katibu wake Mkuu Msigwa, amefanya kazi kubwa sana Katibu Mkuu huyo, hakuna sehemu ambayo hakanyagi. Mheshimiwa Waziri amefanya kazi kubwa sana sana sana sana; lakini Naibu Waziri. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuweka ile timu pale, kuna mzee mmoja na kijana mmoja; timu kali kweli kweli. Ukiunganisha maarifa yale ya kijana na ya yule mzee pale Profesa basi nina imani mambo yanaenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mimi utajikita katika Wilaya yangu ya Temeke. Wilaya ya Temeke ilipata fursa kubwa ya kupata Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru. Uwanja ule wa Uhuru ndio uwanja ambao mwaka 1961 Uhuru wa Tanzania ulipatikana katika Uwanja ule wa Uhuru. Ni uwanja

wenye kumbukumbu kubwa na wenye historia kubwa ya uhuru ambao upo Temeke. Kama haitoshi niishukuru Serikali wameweza kujenga tena uwanja mkubwa kuupanua Uwanja wa Mkapa. Huko kwa Mkapa kwa kweli ni uwanja mkubwa na upo katika Wilaya ya Temeke. Hiyo kwa wana Temeke na kwa Watanzania ni tunu kubwa sana kwetu, ni tunu ya wana Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu; niombe sasa, kulikuwa na mashindano ya UMITASHUMTA, UMISHUMTA na michezo mingine mingi tu, Uwanja wa Uhuru ulikuwa unachachuka kwa michezo hiyo na michezo mingine ya kijeshi; lakini sasa naona hivyo vitu havipatikani, kwa nini, kumetokea nini? Ile michezo ilipokuwa inakuja pale kwenye Uwanja wa Uhuru kama ile michezo ya vijana, wanafunzi wanatoka katika mikoa mbalimbali wanakuja pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Dar es Salaam kuwa jiji, tumepewa ni jiji la kiuchumi bado na sisi ni mkoa kama mkoa mwingine. Tunaomba yale mashindano yaje. Wakati mashindano yale yanakuja pale sisi kama Wanatemeke ndiyo faida yetu, Wajasiriamali, mama lishe na wale wauza vinywaji; wote wanaozunguka kwenye uwanja ule na wengine wote wanaotoka pembezoni kote kwa Dar es Salaam wanafaidika na ile biashara; ndiyo sababu uwanja ule ukawa ni tunu na ni faida kwa Wanatemeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna lile gawio ambalo kama michezo inachezwa pale, wanacheza timu kubwa kubwa na mapato yanapatikana kwa wingi, gawio lile linatakiwa liletwe pale kwenye Halmashauri ya Temeke ili tuangalie nini tunataka kufanya kwa wakati huo. Hata hivyo, utakuta hilo gawio linakwenda maeneo maeneo tu. Sasa sisi faida yetu pale kama Wanatemeke ni nini? Kufagia takataka? Haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima niombe Serikali, kwamba ipange utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba kile kidogo kitakachopatikana katika michezo ile basi na Wanatemeke nao wapate walau kidogo, angalau kuboresha kwenye huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale michezo ikichezwa ikitokea mmoja ameumia atakimbizwa Hospitali ya Temeke, akitokea mwingine ameumia atakimbizwa muhimbili. Basi waangalie namna watakavyokwenda kusaidia angalau kitengo cha mifupa pale Temeke au kitengo cha mifupa kile cha Moi; angalau kukiongezea vitu yaani changamoto zao kidogokidogo ili na sisi tuone tumefaidika kutokana na mechi zinazoendeshwa katika uwanja wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiungana na mwenzangu kwenye Kiswahili, hapa yeye amezungumzia lahaja za Kiswahili, mimi nitazungumzia ushairi wa Kiswahili. Wapo washairi na wapo walioienzi lugha hii ya Kiswahili kwa kutunga mashahiri, kama marehemu Shaban Robert. Sisi wazee wa zamani tumemsoma vizuri sana Shabani Robert kwenye mashairi yake yule "Amina umejitenga, kufa umetangulia. Ile hali kama huwa umeifumba baada ya kuchanua, nakuombea kwa mola mema kukufanyia". Hayo mambo yalitukaa kwenye akili sisi tuliosoma wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona pia kitabu cha Wakati Ukuta, Peni na Mlamba, tumemwona mtunzi. Je, watunzi hao tunawaenzi kwa kiasi gani katika kuendeleza Kiswahili cha nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Profesa, wapo maprofesa wengine ambao mimi siwajui ambao wamekienzi Kiswahili. Hata Dkt. mdogo Nyambari Nyangwine, hakuna mwanafunzi wa Dar es Salaam ambaye hakukutana na kitabu cha Nyambari Nyangwine. Yeye yule alitusaidia sana katika kukidadavua Kiswahili sisi ambao hatuwezi kusoma sana. Alijaribu kukidadavua Kiswahili kutoka kwenye Kiswahili fasihi na kuwafundisha wanafunzi. Naye tumevisoma na hakuna mwanafunzi ambaye alishindwa kufaulu Kiswahili *form four* kama hakupita kwa Nyambari Nyangwine, lazima tumsifu kwa kile alichokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye kuenzi wazee; ninaona, ndiyo baada ya uhuru pale kwenye picha ya Bismini kuna picha ya askari *monument* na tumeona kuna maeneo kadhaa kuna picha za Baba wa Taifa. Sasa, Tanzania inakwenda

kuingia katika historia mpya ya kupata Rais mwanamke wa kwanza, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Je, histori ya Tanzania imejipanga vipi katika kuhakikisha tunamwachia alama mama huyu? Tumwekee mnara. Kwa sababu kwenye Kiswahili au *cultural heritage* ina-*include monument* ambazo zinatakiwa zitengenezwe sanamu mbalimbali, picha kubwa na minara ya kihistoria ili kuwaenzi hawa watu. Pamoja na marais wengi ambao wamepita hapa, lakini sisi tunaomba huyu mwana mama wa kipekee tumuenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka vile vile nimpongeze leo kwa mara nyingine tena Mbunge wa Rufiji kwa jinsi ambavyo ameweza kumuenzi mama, Bibi Titi Mohammed Mandangwa. Ndugu zangu Bibi Titi Mohammed Mandangwa leo anaenziwa kule Rufiji lakini alipigania uhuru wa nchi hii. Sisi wa Rufiji wenzie tunafurahi na tunaona jinsi gani na tunampongeza sana Mbunge huyo wa Rufiji, tunamwombea kwa Mungu, *Inshallah,* amrudishe ili lile tamasha liendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Bibi Titi Mohammed alirudi tena aliishi Temeke Ngarambe, lakini alikuwa na wadogo zake katika kutetea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa...

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie. Alikuwa na ndugu zake Bibi Asha Ngoma, Mwamvua Mrisho, Mama Dezi, Bibi Sitti Kilungo ambaye ni Mama Mtemvu na Tatu Ligawike. Akinamama hawa wote kwa pamoja....

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa hatuna muda....

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** ... walitetea uhuru wa nchi hii...

**MWENYEKITI:** Hatuna muda naomba uhitimishe...

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** ... na tunawakumbuka Wanatemeke na tunawashukuru sana kwa mchango wao. Ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, wajiandae Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu na Mheshimiwa Esther Edwin Malleko.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara hii ya muhimu sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Profesa Kabudi pamoja na timu yake yote; Naibu Waziri na timu yake yote kwenye wizara kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, wanaendelea kuifanya kwenye wizara hii na kwa kuaminiwa kuendesha wizara hii pana na ya muhimu sana. Profesa Kabudi ni mwalimu wa wengi ikiwa ni pamoja na mimi ninayezungumza hapa, ni mbobezi sana kwenye Sekta ya Sheria; lakini pia *CV* yako kwenye Sekta ya Habari ni kubwa. Ninaamini kabisa kwamba akisaidiwa na Naibu Waziri kijana ambaye kazi ipo kwenye damu yake basi tutapasua anga na tutakwenda vizuri. Mungu awaongoze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amefanya uwekezaji mkubwa katika Sekta hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hata tunavyoona sekta binafsi kuna watu wengi wafanyabiashara wakubwa ambao wameingiza mitaji yao hapo sio kwa sababu nyingine, wanavutwa na wanakuwa na imani kwa kuona kwamba Mheshimiwa Rais mwenyewe yupo mstari wa mbele katika hili. Kwa hiyo mafanikio yote haya yanatokana na yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana nami kwamba, masuala haya ya utamaduni, sanaa na michezo ambayo yapo *associated* na mambo ya burudani, kwa miaka mingi na hasa katika mila zetu za Kiafrika, kwa Kiswahili cha leo yamekuwa yakichukuliwa poa tu, kwamba ni mambo ya ziada ziada. Wasanii wanaburudisha watu baada ya kazi, wanaburudisha watu wakiwa kazini ili kuwapa hamasa na maeneo mengine mengine.

Haikuonekana kama ni jambo ambalo linaweza kuwa na *impact* kwenye uchumi na ndiyo maana hata wasanii wa zamani kama Mzee wetu Morris Nyunyusa, akina Mwinamila, akina Mbaraka Mwinshehe, hata baadhi ya wacheza mpira maarufu hata kustaafu kwao hakukuwa kuzuri sana kwa sababu hawakuweza kuenziwa ipasavyo kutokana na historia, labda na mila, kwamba sanaa ni kitu ambacho ni cha ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa imedhihirika kwamba sanaa ndio *soft power* ya nchi na kila kitu sasa hivi kinakwenda *softly* na wana mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi na katika kui-*brand* nchi na kujenga taswira ya nchi kwa dunia nzima. Kwa hiyo basi, upo umuhimu mkubwa wa Serikali ikiwakilishwa na Wizara hii kuhakikisha kwamba inaweka mifumo mizuri zaidi ya kisheria na kitaasisi ili kuwalinda wasanii, kuwalea na kuwawezesha hasa katika maeneo ya mitaji na elimu ya kazi yao ili sasa waweze kufanya kazi yao vizuri. Kwa maneno mengine tunahitaji uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Afrika Magharibi wamejitahidi sana kuwekeza kwenye eneo hili mapema sana; na ndiyo maana hata ukienda nje wasanii na wanamichezo wengi waliyobobea wanatoka huko Afrika magharibi. Hata fedha za *remittances* wanazorudisha nyumbani kwa kufanya kazi hizi nje wenzetu kule wanapata fedha nyingi sana. Tazama sisi kwetu kwa mfano kijana wetu Mbwana Samatta jinsi ambavyo anatuwakilisha vizuri na nina hakika kuwa kuna kipato ambacho kinachorudi nchini. Tunahitaji kuwa nao wengi na hatuwezi kuwa nao wengi ikiwa hatutawekeza vizuri na kwa nguvu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo malalamiko kwa wasanii wadogo wadogo, kwamba, wenzetu wa BASATA wamekuwa viranja zaidi kuliko walezi. Ile Sheria Namba 23 ya Mwaka 1984 pamoja na kanuni zake imewapa mamlaka ambayo wasanii wadogo wanaona kwamba yanatumika zaidi kama fimbo kuliko kuwalea. Kosa dogo sana lina faini kubwa na mengine yanapelekwa kuwa makosa ya jinai na hata kuwaharibia rekodi zao hawa wasanii. Badala ya kwamba mengine yawe ni ya kupewa elimu tu; mtu anaanza kufanya michezo yake hapa kwa kutumia makopo yake ya pale nyumbani, anatakiwa kuelimishwa

na kuendelezwa na si kupewa kosa la jinai kwa vile eti hajajisajili. Huwezi kuanza kukimbia kabla hujatembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunachoomba ni kwamba BASATA itengeneze vyanzo vingine vya mapato, isitegemee sana hizi faini na tozo na kadhalika. Kazi yao ni kubwa wana uwezo mkubwa sana wa kupata mapato wakiwa bado wanaendelea kuwalea hawa wasanii wadogo ili waweze kukua na kufikia *level* ambazo kwa kweli tunazihitaji. Hilo linahitaji tu mfumo wa kitaasisi na marekebisho ya sheria na kanuni zile zitengenezwe vizuri ili ziwasaidie hawa vijana waweze kukua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa michezo, hasa mpira wa miguu; tunaipongeza sana sana Serikali, Mheshimiwa Rais kwa kweli amekuwa *champion*. Ninaungana kabisa na wenzangu waliotangulia, Mheshimiwa Ndulane na dada yangu Mariam Kisangi; kwamba kwa kweli ipo haja ya Mheshimiwa Rais kupewa tuzo kama mwanamichezo, kama mwanasanaa na kama mwanautamaduni namba moja. Ipo haja kabisa ya kufikiria namna ya kufanya hivyo kwa namna nzuri kwa sababu amefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Jimbo langu la Mwanga, jiografia ya Mkoa wa Kilimanjaro Wilaya za Same na Mwanga zinabeba 60% ya Mkoa wa Kilimanjaro; lakini ukiangalia wilaya hizi mbili zimekuwa nyuma sana katika upande wa mambo ya kuwasaidia kukuza michezo; kwa mfano viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mwanga Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga imefanya kazi nzuri sana. Imejenga uwanja ambao una *fence* na una *pitch* nzuri na jukwaa moja. Mheshimiwa Rais wa *TFF*, ndugu yangu Wallece Karia, nimtaje hapa kwa shukurani sana, kwamba alikuja kufunga ligi yangu, ligi ya *Tadayo Cup* na aliuona ule uwanja ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba, ninaomba aje Mwanga baada ya bajeti hii ili autazame ule uwanja. Nimwombe sana, kwamba kwa haraka atafute fedha kidogo ili tuurekebishe ule uwanja, tuuwekee majani haya ya kisasa ili hata mazoezi ya *AFCON* yafanyike pale

pia. Sehemu hii ya Mkoa wa Kilimanjaro ya 60% ipate nayo *cake* hii ya *AFCON* na burudani nyingine ambazo zitaendana na hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mwanga na Wilaya ya Same zipo mahali pazuri na hasa pale kwangu Mwanga hata wanaotaka kwenda kupanda Mlima Kilimanjaro wanaweza wakaja wakafanya mazoezi ya kupanda mlimani. Sekta binafsi imeitikia vizuri kuna hoteli na maeneo ya kukaa. Kwa hiyo, nina-*encourage* sana Mheshimiwa Waziri karibu Mwanga uje uone lakini utafsiri namna ya kuhuisha ule uwanja kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, atafuata Mheshimiwa Jesca, lakini kabla hajaanza ninaomba nimpishe kwanza Mheshimiwa Naibu Spika.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaomba kuchangia katika Wizara yetu hii ya Utamaduni. Niwapongeze kwa ajili ya mafanikio ambayo yamefanyika katika Wizara hii. Kwa ajili ya maslahi ya muda nitaomba niendee moja kwa moja kwenye hoja zangu tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza itakuwa katika kuendeleza sana katika nchi yetu ikiwepo umuhimu wa viwanja tunaomba sana Wizara hii iweke msisitizo kwenye kusimamia masuala ya viwanja vya michezo nchini. Kuna mwamko mkubwa wa watu kufanya michezo lakini ukiingia kwenye viwanja vyetu vingi bado havipo kwenye menejimenti ya kuweza kuruhusu watu kufanya michezo ukiwepo Uwanja wetu wa Taifa. Tunaomba sana hii tabia ya kwamba Uwanja wa Taifa umefungiwa inaonekana hatuna menejimenti nzuri sana katika kuendesha ule uwanja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni hivyo itafutwe menejimenti ya uhakika kama ni vipi basi waweze kuona wanaongea vipi na sekta binafsi kuona namna gani tunafanya menejimenti, lakini kushirikiana na wale ambao wana viwanja katika Taifa letu ili kuona viwanja vile vinakuwa *active* kwa ajili ya ku-*accommodate* michezo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Iringa tuna Uwanja wa Samora pia mna maandalizi ya *AFCON* sasa. Tuna uwanja mzuri sana na lile ni lango la utalii Kusini. Tunawaomba kwa kuwa Kamati imetoa mapendekezo kwamba waangalie na viwanja vingine wanavyoweza kuviendeleza, basi tunawakaribisha sana Iringa na watu wakija pale wataweza kutembelea vivutio mbalimbali vya Mikoa 10 ya Nyanda za Juu Kusini ikiwepo *Ruaha National Park*. Sisi tumejiandaa vizuri uwanja wa ndege upo tayari, ndege kubwa zinatua pale vyakula vipo vya kila aina na ambavyo huwezi kuvipata sehemu nyingine katika Tanzania. Kwa hiyo, karibuni sana Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka niliongelee ni kuhusiana na masuala ya utamaduni na kabla sijaenda utamaduni, ninaomba niongelee Kiswahili. Mheshimiwa Khadija ameongea, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri umesema hatuwezi kukikuza Kiswahili bila kuangalia changamoto tatu: kubagaza, kubananga na kufubaza Kiswahili, lakini inaonesha kabisa kwamba katika ufubazaji huo, ubanangaji huo na ubagazaji huo inawezekana hata kabisa hata Baraza letu la BAKITA linabagaza kwa kutupa maneno magumu magumu ambayo hatuyaelewi. Yaani unaamua kutengeneza neno, kwa mfano, kishikwambi yaani mpaka mtu aje alewe apate *coordination* ya hilo neno na kile kinachoongelewa inachukua muda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuja kuongelea maneno mengi kwa mfano; humu kuna maneno mengi wameyatumia, ‘kongoo’ vitu kama hivi yaani unakuta ni vigumu. Mheshimiwa Khadija ameelezea vizuri sana, wakati kuna maneno mazuri au laini tu. Kwa mfano, unaniambia Akili Mnemba, hasa mimi nikianza kuanza kutafuta lile neno mnemba na *correlation* ya *artificial* silipati. Kwa nini, usiniambie Akili Bandia, kirahisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana uwepo mjadala wa Kitaifa kukubaliana kama singeli itakuwa ndiyo mchezo au utamaduni wa Taifa letu kwa nyimbo zake, maneno yake, uvaaji wake na uchezaji wake. Je, tutakubaliana? Kwa kuwa ni suala la Kitaifa basi ni vizuri tukubaliane kwa pamoja tunakubaliana kwa pamoja, tunakubaliana singeli ndiyo ituwakilishe Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilituma kitu fulani kwenye *group* la Wabunge jinsi michezo ile inavyochezwa wakati mwingine; kama Wizara ndiyo wasimamizi basi mwone namna ya kudhibiti na nidhamu maneno yanayotamkwa na uchezaji wake. Nilituma juzi kitu ambacho siyo kizuri kwenye *group,* lakini watu wamebanwa na utamaduni wana mihemko, wanacheza hiyo singeli wapo uchi, wananing'inia kwenye daladala wanacheza uchi, lakini wakienda kucheza, kwenye kuvaa kwenye matamasha mbalimbali wanavaa nguo nyingine ambazo zinaonesha kabisa. Sasa tukubaliane kama tunakubaliana kama Watanzania ile ndio *representation* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni suala la Kitaifa tusikubaliane kirahisi wamesema watafanya Tamasha la Kitaifa la Utamaduni huko ndiko wakatoe namna gani Watanzania watakuwa *represented…*

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumpa taarifa Mzungumzaji kwamba hatujaona Kamati iliyokaa kupitisha singeli kama ndiyo ngoma inayowakilisha Tanzania. ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, haichezwi kwenye daladala na hicho ulichokiona wala sicho, umeona kitu kingine na wala hawavui nguo. Ni mchezo ambao unaburudisha na hasa kwa watu wa Pwani. Kwa hiyo, haya mambo uliyoyaona, sitaki

kutaja ni nani, kwa sababu sitaki kuwa *implicated,* lakini singeli haina kabisa mambo hayo na muda wako umekwisha vilevile.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kiti chako ni kikubwa sana, sasa siwezi kusema chochote kwenye hilo.

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha vilevile.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *opinion* yako, lakini kwa kuwa nilikuwa nimepewa taarifa, ninaomba niikubali taarifa Mheshimiwa Taska Mbogo, lakini ya kwako ibaki imeelea hivyohivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tukubaliane tutafute mjadala wa Kitaifa kukubaliana kama singeli itatu-*represent*. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Malleko, jiandae Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Nianze moja kwa moja kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa ndiye mwanamichezo namba moja Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nimpongeze Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu Waziri bila kumsahau Katibu Mkuu, Ndugu yangu Gerson Msigwa pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda ninaomba niende moja kwa moja kwenye zile mada zangu ambazo nitachangia siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali ione ni namna gani inaweza kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa mtiririko ulio sahihi ili tuweze kukamilisha vile vitu ambavyo

tumejipangia hasa hasa kwenye Wizara. Ninasema hivyo kwa sababu gani wakati tunafanya ziara ya Kamati tuliweza kutembelea maeneo mbalimbali, lakini pamoja na hayo tuliweza kwenda kwenye kiwanda au Kampuni ya Magazeti ya Serikali. Pale tunaona fedha zimetolewa kwa ajili ya kujenga jengo, lakini hazikwenda kwa mtiririko unaotakiwa. Kwa hiyo, jengo halijakamilika, lakini vifaa tayari vimekwishanunuliwa ina maana kwamba mashine zote zimenunuliwa na zimewekwa kwenye maghala ya taasisi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapoteza fedha nyingi sana kwanza hii mitambo imekaa zaidi ya miaka miwili chini inaenda kuharibika lakini siyo hivyo tu, pamoja na mitambo hii kuharibika, pia fedha inatumika nyingi kwa ajili ya kukodisha maghala yale. Pamoja na hayo, Serikali inaingia hasara, kwa mwaka mmoja katika uchapishaji Serikali inatoa zaidi ya shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya kuchapisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo ni nyingi sana zingeweza kutumika kufanya mambo mengine, lakini kwa sababu mitambo imenunuliwa na jengo halijamalizika. Kwa hiyo, kazi inashindwa kuendelea. Tunaishauri Serikali ione ni namna gani fedha zitatolewa kwa mtiririko ili ile Kampuni jengo lao liweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, niendelee kuipongeza Wizara kwa kazi inayoifanya, lakini ione ni namna gani itaandaa mikakati ya kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya michezo au mashindano, kwa sababu kwa sasa uwanja unaotumika ni Uwanja wa Mkapa pekee yake na tunajua 2027 tunakwenda kwenye mashindano ya *AFCON*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuipongeze Serikali kwa kuamua kujenga Uwanja wa Arusha pamoja na Dodoma lakini hapohapo niendelee kuishauri Serikali kwa sababu pale Kilimanjaro tuna Uwanja wa *Memorial* ione namna gani itaenda kuujenga ule uwanja ili wale wanaocheza kwenye Viwanja vya Arusha waweze kwenda kufanya mazoezi kwenye Kiwanja hicho cha Moshi kwa sababu ni karibu na Arusha. Tuna uwanja wa ndege, na tuna hoteli za kitalii za kutosha. Jambo hili liweze kufanyiwa kazi ili na sisi

Kilimanjaro tuweze kupata nafuu hiyo katika uwanja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wazungumzaji wengi wamezungumza katika jambo hili na mimi ninaomba niunge mkono kwamba je, tumekubali kwamba singeli ndiyo itakuwa inawakilisha Tanzania kwenye jambo la muziki? Kwa nini, tunasema hivyo? Singeli ni muziki mzuri, lakini basi tuangalie je, unakidhi maudhui ya Kitanzania? Kwa sababu wote tunaona mara nyingi nyimbo zinazoimbwa zimebeba maneno ambayo hayaendani na maudhui ya Kitanzania. Kwa hiyo, tuone ni namna gani tunaweza kufanya jambo hili likawa linaleta heshima na kulinda hadhi ya Watanzania hasa wanawake wanadhalilishwa sana kwenye ile michezo wanayocheza kwenye hizo singeli, haipendezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ninaomba kuishauri *BASATA* iangalie ni namna gani inaweza kuendelea kuibua vipaji vya wasanii hasa vijana ili kuongeza hamasa kwa vijana wetu, lakini pia kuongeza ajira na kipato kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo ninataka kuishauri Serikali iangalie ni namna gani itapunguza ile hela ya kiingilio pamoja na ada kwa sababu bado ni fedha nyingi sana na vijana wetu hawa ndio kwanza wanajitafuta, hawawezi kulipa fedha zote hizo. Nia ni njema sana kulinda haki zao, lakini ni namna gani basi tuweze kuwasaidia vijana hawa na wao waweze kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hata leo kikundi kikienda kuimba kwenye ngoma kama kuna uchaguzi au kuna matamasha yoyote kuna vile vikundi vidogovidogo vya akinamama vinaenda kuimba na wao wanapaswa wajisajili na kulipa hizi hela bado wanajitafuta, hawajaweza kuwa na fedha za kutosha kufanya vitu kama hivi. Kwa hiyo, tunaomba kuishauri Serikali ni namna gani iangalie jambo hili ili tuweze kuwasaidia hawa ndugu zetu waweze na wao kupata ajira na kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia hapo, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa nina tangazo la wageni. Wageni Waliokaa Jukwaa la Spika: Wageni wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, hawa ni Wafanyakazi wa Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Kilosa; Viongozi wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Wadau wa Habari *(TAGCO, YOUTU, UTPC, TAMWA, UNIQUE, MISA - TAN, OJACUT), Tanzania Blogger Network (TADIO);* Watangazaji na Waandishi wa Habari wa *TBC* Waliopewa Tuzo za Umahiri; na Wadau wa Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo Wadau wa Utamaduni wa Kiswahili; Taasisi za Fedha za *NBC, CRDB* na *NMB;* Kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha *TASUBA*; Viongozi wa Mashirikisho ya Vilabu na Wadau wa Michezo Nchini; Wachezaji na Makocha wa Timu ya Taifa ya *Cricket*; Viongozi Watendaji wa Vyama Mashirika na Vikundi vya Sanaa ikiwemo Filamu na Utamaduni; Viongozi na Asasi za Kiraia zinazojihusisha na Shughuli za Sanaa; Wadau wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa; Viongozi na Wasanii wa Muziki; Wasanii wa Tamthili ya ya Juakali, Kombolela, Saluni ya Mama Kimbo, na Zahanati ya Kijiji pamoja na Wasanii wengine wa Filamu. Karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Nami nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa uwasilishaji mzuri. Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji kwenye sekta ya michezo na sekta zote ambazo zipo chini ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, goli la mama limechangia sana hamasa kwenye mpira wa miguu, lakini vilevile uwekezaji kwenye ujenzi wa Chuo cha Malya, ujenzi wa Uwanja wa Mpira kule

Arusha na mipango ya kujenga Uwanja wa Mpira hapa Dodoma ni sehemu ya uwekezaji ambao utahamasisha na kuimarisha sana michezo hasa mpira wa miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nimeisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona nikumbushe baadhi ya mipango ambayo ilikuwepo hapo katikati kama miaka mitatu, miaka minne iliyopita ambayo haijatekelezwa na Serikali. Kulikuwa na mpango wa kununua angalau mpira mmoja kila kijiji, mpira mmoja kila shule, mpira mmoja kila mtaa; jezi seti moja kila kijiji, jezi seti moja kila mtaa angalau hiyo ingehamasisha sana. Hata hivyo, viwanja vya kiijiji, viwanja vya mtaa vilikuwa ni vya muhimu sana; uwekezaji mdogo sana unahitajika hasa eneo tu la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili wa hizi timu zetu, hivi kweli yangu kutoka Kitunda, timu yangu kutoka Kiloli, timu ipate usajili Dar es Salaam, kwa nini, Mamlaka ya Usajili isiende kwenye Halmashauri ya Wilaya? Timu za mpira wa miguu ziwe zinasajiliwa kama ambavyo wajasiriamali wanavyosajili vikundi vya ujasiriamali. Hiyo ingeboresha sana kupata timu ambazo zimesajiliwa katika wilaya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kukumbusha mambo machache kuhusu historia ya mpira. Kama isingekuwa Ligi ya Dar es Salaam kuanzishwa mwaka 1929 kusingekuwa na maendeleo mazuri ya mpira wa miguu Tanzania; na kama kusingekuwa na Vita Vikuu vya Pili vya Dunia ambavyo vilisababisha Serikali ya Kikoloni ikaziondoa timu za majeshi na timu za Taasisi za Serikali kwenye Ligi, basi timu za Simba na Yanga zisingekuwa na umaarufu zilizo nao leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana kukumbuka hiyo historia, lakini timu ya kwanza ya wananchi au timu ya kwanza ya kiraia kucheza Ligi ya Dar es Salaam ilikuwa *Cosmopolitan*. Kwa hiyo, ni muhimu sana kukumbuka kwamba Timu ya Cosmopolitan ni timu kogwe kuliko timu za Simba ya Yanga na lazima kuipa Timu ya *Cosmopolitan* heshima. Mamlaka za Mpira wa Miguu Dar es Salaam zisaidie hii timu ya *Cosmo* angalau iweze kupanda daraja ili iweze kutoa ushindani kwa Simba na Yanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, …

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, anasema tuipe heshima Timu ya *Cosmo,* ninaomba atusaidie Mheshimiwa kwamba, hiyo timu ipo wapi mpaka sasa hivi? Ahsante!

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Timu hii ya *cosmopolitan* ipo kwenye Jimbo lako na sasa hivi inashiriki Ligi Daraja la Tatu. Kwa hiyo, ni muhimu sana kijana wangu aelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo makubwa sana kwenye michezo hasa kwenye mpira wa miguu. Tatizo la kwanza, kuna tatizo la kukosekana kwa uadilifu kwenye mpira wa miguu watu wanajali zaidi mapenzi ya Simba na Yanga bila kujali maendeleo ya mpira wa miguu. Tatizo la timu kucheza chini ya kiwango kwenye ligi ninaomba Serikali na Mamlaka za Mpira wa Miguu ziliangalie sana hilo jambo, yaani timu inaamua kucheza chini ya kiwango kwa sababu inacheza na timu fulani. Sasa kuna kuwa na mapatano ya aina gani? Inatakiwa uchunguzi ufanyike ili kubaini tatizo hilo na kulitafutia ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la kuahirishwa Mechi ya Simba na Yanga, Mamlaka za Mpira zilisema zinafanya uchunguzi, lakini tangu ziseme zinafanya uchunguzi mpaka leo taarifa ya uchunguzi haijatolewa hadharani, halafu inaibuka ratiba tu ya Ligi kuendelea bila taarifa ile, Watanzania wanakuwa hawajatendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, Sheria 17 za soka, zimekuwa zikilegezwa katika baadhi ya mechi. Kuna matatizo makubwa ya ma-*referees* wengine wanapewa adhabu kila siku. Ninaomba sana Mamlaka za Mpira wa Miguu zisimamiwe vizuri ili

zisimamie Ligi yetu vizuri na iwe bora kweli kweli siyo bora kwenye karatasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, niipongeze sana *Simba Sport Club,* timu ya Simba imeiletea sana sifa nchini. Mwaka 1974 isingekuwa penati Timu ya *Mahalla Ghazl El Kubra* ilikuwa imeshatolewa mashindanoni, Simba iliingia Nusu Fainali ya Klabu Bigwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1993 Simba iliingia Fainali ya Kombe la *CAF* ambalo ni kabla ya kuunganishwa makombe mawili Kombe la *CAF* na Kombe la Washindi ambalo sasa hivi ndio Kombe la Shirikisho na mwaka huu imeingia Kombe la Shirikisho. *Simba Sport Club* imekuwa ni nembo kubwa ya soka la Kimataifa la Tanzania, ni muhimu sana kila mtu aunge mkono maendeleo ya soka Tanzania, kupitia timu hizi za Simba na Yanga. Ahsante sana. Ninakushukuru Sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Tarimo, Mheshimiwa Swalle, Mheshimiwa Nusrat, Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid na Mheshimiwa Gulamali.

Ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 Jioni.

*(Saa 6.59 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Priscus Tarimo, ajiandae Mheshimiwa Swalle, ajiandae Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, tena wa kwanza kabisa mchana huu. Nichukue nafasi ya kipekee kabisa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri ambaye ni mchezaji wangu ndiyo mambo yanavyokwenda, ni *captain* wake wa *basketball,* lakini pia Katibu Mkuu pamoja na timu nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina *section* mbili; kwanza nina maombi ambayo nimeshayawasilisha *formally,* lakini ni vizuri yawe *registered* hapa. Kwenye hili suala la *AFCON.* Sisi Moshi Mjini ndiyo tumeshikana na Arusha na inajengwa *stadium* kwa ajili ya michezo yenyewe. Sasa viwanja vya mazoezi kwa kudodosa nasikia vinatakiwa vijengwe kama vitano,

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimeleta ombi hili *formally*, nilishamwomba Mheshimiwa Waziri aliyepita alipokuja kwenye Kili-*Marathon* mwaka 2024, lakini nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa sasa mwaka huu 2025 tukaenda kulitembelea eneo la *Memorial* ambalo lina hekta 50, kuwaomba sasa ili kugawanya haya manufaa ya michezo au manufaa ya *AFCON* basi na Moshi Mjini ambapo ni kilomita 75/80 hivi kutoka pale Arusha, lakini iwe pia ni mwanzo wa kuboresha michezo kwenye Mkoa wa Kilimanjaro hasa pale Moshi Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili la kwanza ni ombi pale *Memorial Stadium,* lakini pia kwa sababu tuna *facility* zote, *hotel* za kitalii zipo za kutosha kwenye Mkoa wa Kilimanjaro, tuna uwanja wa ndege ni karibu, lakini ukivuka tu barabara kuna uwanja wa gofu, kwa hiyo, ninaomba hilo ombi la kwanza kwamba, katika vile viwanja kwa ajili ya mazoezi basi watuangalie sana pale *Moshi Mjini – King George Memorial Stadium.*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni uwanja wa kwanza wa gofu Tanzania ni *Moshi Club*, ambao upo Moshi Mjini. Huu uwanja ulijengwa tangu mwaka 1920. Nilikuwa naomba na hili, najua Wizara wameshaanza kuangalia namna ya kuboresha na kuhakikisha kwamba unalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwaomba kwa sababu Mheshimiwa Waziri wewe ni *encyclopedia* inayotembea. Sasa uwanja wa kwanza wa gofu ni ule wa Moshi Club wa mwaka 1920. Ni vizuri uangaliwe kwa upekee yaani tusiachie tu *members,* hata wakiwa wachache wakishindwa ku-*maintain* ushindwe kuendelea kutunzwa. Ni mashimo 18, ni uwanja mkubwa upo *located* sehemu nzuri, kwa hiyo, ninaomba pia hilo mlipokee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la tatu, nilishalileta tena huko nyuma kwamba, ni vizuri tuhakikishe sasa hii michezo tunaisogeza yote kwa pamoja. Riadha Tanzania hatujawahi kuwa nyuma sana, tumeshaonekana sana hasa kwenye *marathon*; na hata juzi Boston Marathon tuliwakilishwa vizuri sana na Simbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilishaleta ombi kwamba ni vizuri tuangalie sehemu za kujenga zile kambi za wanariadha kama ilivyo ile *Iten* kule *Kenya Home of Champions.* Kule West Kilimanjaro kwa sababu wanapenda sehemu ya *high altitude* ni sehemu nzuri sana ya kutuingizia kipato. Pia kwa sababu tukishakuwa na zile kambi tunaweza tukawapa sekta binafsi wakaja wakajenga, maeneo ambayo ni *suitable.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule West Kilimanjaro ni eneo zuri, lakini pia maeneo ya Karatu, na *Rift Valley* lote ambayo ni maeneo ya *high attitude,* unaweka ile kambi hata kujenga hayo

mabweni tusijenge kwa sababu watu wanavyokuja wanalipa *fee*, ila watu waende wanalipa halafu wana-*train*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kenya ipo hiyo *Iten* tunaweza kwenda kuitembelea halafu tukapata namna ya kukuza huu mchezo wa riadha. Kwa upande mwingine tukawa tunaingiza kipato kwa watu kuja ku-*train* kule. Kwa hiyo, kambi za riadha *West* Kilimanjaro na maeneo yote ya *Rift Valley*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishaongelea sana suala la kuunganisha michezo na utalii na hili linahitaji juhudi za makusudi kwamba ni lazima tuangalie namna ya kuviunganisha ili viweke tija. Kwa hiyo, sababu ya muda, napenda kuendelea kushauri sana tuangalie namna ya kuviunganisha hata kwa kutumia *desk* la michezo pale kwenye Wizara ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, ni mchango wangu huo. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Swalle, jiandae Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Ninaomba nianze kuungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ambaye ni mwanamichezo namba moja wa nchi yetu kwa sababu kwa mpango wake mzuri wa sekta hii ya michezo ameinua sana michezo nchini. Hongera sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ninajisikia fahari sana kuchangia wizara hii ambayo inaongozwa na mwalimu wangu mahiri sana Mheshimiwa Profesa Kabudi ambaye amenifundisha katika fani ya sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hongera sana kwa Profesa kwa uteuzi huu, jambo ambalo sikujua ukiwa mwalimu, sikujua pia kama wewe ni bingwa wa singeli. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri, ndugu yetu Mheshimiwa Mwinjuma kwa kazi nzuri, ninakushukuru sana na wewe ni mtu rahimu sana, ni mtu

muungwana sana. Kwa kweli wananchi wa Muheza walipata Mbunge mahiri ahsante sana. Nimshukuru Mheshimiwa Msigwa pamoja na Naibu wake kwenye Wizara hii ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nichangie maeneo machache mchana huu. Nianze na jambo la kwanza ni kuhusu mikopo kwa wasanii na hapa niwasemee mahususi wananchi wangu wa Jimbo la Lupembe na wananchi wa Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri alikuja Jimbo la Lupembe kufunga Swalle *Cup* mwaka 2023, alishuhudia wingi wa vijana wenye vipaji vya muziki, vipaji vya michezo. Kule Jimbo la Lupembe tunao vijana wengi wenye vipaji vya muziki na michezo. Tunao vijana kama akina Buki Boy kutoka pale Madeke, lakini Manisaiso, tunao akina *B2K* kutoka pale Makambako, akina Mack Ford kutoka Makete ambaye ameimba wimbo maarufu sana wanasimama na mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao vijana kama wakina *Masai the don*, kaimba wimbo maarufu sana, unaitwa mama mitano tena. Hao vijana wamealikwa mpaka Ikulu kwenye hafla kwa ajili ya Sanaa. Kwenye mpango huu wa mikopo ninaomba, mikopo hii isilenge watu wakubwa tu, iwalenge pia na vijana hawa chipukizi ili wapate mikopo hii waweze kuinuka pia katika sanaa yao ya muziki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nichangie pia kuhusu viwanja vya michezo. Nimeona kwenye bajeti ya awamu hii, wana mpango wa kujenga viwanja mbalimbali ndani ya mikoa na ndani ya halmashauri. Sisi Mkoa wa Njombe ni eneo muhimu sana kwa kuwekeza kwenye michezo. Wasiojua sisi Mkoa wa Njombe tumewahi kutoa wachezaji mahiri katika nchi hii na hasa katika Jimbo la Lupembe. Wasiojua, Fred Mbuna katokea Jimbo la Lupembe ninakozaliwa mimi na amekuwa mchezaji mzuri kwa timu ya Yanga, lakini pia tumekuwa na mchezaji Nico Nyagawa kafanya vizuri sana kwenye Simba mpaka leo yupo. Hawa ni *icon* ya Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mkoa wa Njombe kwenye mpango huu muukumbuke kuupatia uwanja wa mpira kwa heshima ya hawa wachezaji na wananchi wa Njombe. Jimbo la Lupembe tunalo eneo kubwa, mkitaja maeneo Lupembe yapo ya kutosha. Tunavyo viwanja vingi tu pale Mtwango, Nyombo, Kidege, Wanginyi. Mnaweza kuchagua kati yake mkajenga uwanja mzuri sana kule Njombe kwa ajili ya michezo ya vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine pia nataka nichangie hapa leo kwa mchana huu, ni kuhusu ligi za Waheshimiwa Wabunge. Kumekuwa na ligi nyingi za Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yao, Wabunge wamekuwa wakitumia fedha nyingi sana kwa ajili ya hii michezo. Ninaomba Wizara hii i-*coordinate* hii michezo ya Wabunge, itambue Wabunge kama ni wadau kwenye hii michezo ili iwasaidie ufundi pale panapobidi, lakini pia kufuatilia hii michezo ili iwe sehemu ya kukuza michezo ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ninaomba niseme hapa. Nimeona pia huu mpango wa kuanzisha taasisi ya kusimamia miundombinu ya michezo, hili ni jambo kubwa sana Mheshimiwa Waziri. Miundombinu mingi sasa hivi kama umetazama, tumeanza kutia aibu, kucheza mpira kwenye viwanja vilivyojaa maji, kuwa na viwanja vitu vimeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini taasisi hii ya kusimamia miundombinu ninaomba ianze mapema, ianze kusimamia viwanja vya michezo. Hii itatusaidia kuwa na uhakika wa viwanja vyetu kwenye sehemu ya ulinzi pamoja pia na usalama wa viwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kuchangia kidogo. Kuna jambo moja Mheshimiwa Waziri ambalo pia wengi wamesema sana humu ndani tangu asubuhi, ni kuhusu mchezo wa Simba na Yanga. Jambo hili limeleta taharuki kubwa isiyokuwa na sababu, tumemwona Mheshimiwa Waziri akienda kwenye kikao, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, walipotoka hawakusema jambo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Ligi naiheshimu sana, Mheshimiwa Rais wa *TFF* namheshimu sana, wanafanya kazi kubwa sana, lakini kuna shida gani kutuambia maamuzi waliyofikia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kwa mujibu wa Kanuni zetu, suala hilo unalolizungumzia lipo kwenye shauri la kisheria, katika ngazi ya maamuzi. Kwa hiyo, nikuombe usizungumzie masuala hayo ndani ya Bunge na kulihusisha Bunge na masuala ya kisheria na kulitia Bunge katika migogoro. *TFF* na vilabu wana kanuni zao, wanatawaliwa na mamlaka zao za *CAF* na za *FIFA*. Endelea.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea maelekezo ya kiti na siwezi kupingana nayo, ninaheshimu. Nilichotaka niseme tu ni kwamba, kwa sababu kuna hisia za mashabiki wa Tanzania tunaomba vyombo vyetu vya vilabu waheshimu sana hisia za mashabiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuacha haya mambo kwenye giza bila kuwa na ufafanuzi, nani kakosea, nani kapatia, hii sio sawasawa kwa sababu mpira sio mpira wa busara, ni mpira wa sheria, mwenye kadi nyekundu, kadi nyekundu, mwenye njano kadi ya njano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat, jiandae Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Nimpongeze mwanautamaduni, Sanaa na michezo nambari moja Tanzania, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameonesha utayari kwenye ku-*support* utamaduni, Sanaa na michezo kama ambavyo jina la Wizara lilivyo na shughuli zake wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemwona mara kadhaa akienda kwenye matamasha mbalimbali yanayohusiana na masuala ya utamaduni, Sanaa na michezo. *Flow* ya fedha pia

kuelekea kwenye Wizara hii ni tofauti kulikoni miaka mingine yoyote ya nyuma tukiangalia *flow* ya fedha watu ambao wanafuatilia mwenendo wa bajeti kwa mwaka baada ya mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua ni kwa sababu pia kuna msukumo mkubwa wa *AFCON* na ninajua pia hata wakiuliza katika *lobbying* tunamfahamu ni miongoni mwa *lobbyist* namba moja kwenye mambo mbalimbali ya kidunia na kikanda kwa maana ya Africa. Ninafikiri hata sababu mojawapo ya kuleta *AFCON* Tanzania ni pamoja na ushawishi wake kwenye nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia wasaidizi wake Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Serikali kwa sababu wanakimbizana kutuhakikishia kwamba nchi inaenda kwenye masuala ya utamaduni, sanaa na michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Wizara nimewapongeza hapo lakini ninajua kuwa Wabunge wengi wameshajadili, wameshazungumza pia kuhusiana na mienendo ya vilabu vyetu kwa mfano kwa upande wa Simba na Yanga na vilabu vingine *of course* kwa sababu kuna vilabu lazima vijue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze na niwaombe sana muendelee kuwa waadilifu kwa sababu sisi tunaamini Serikali ndiyo *balancing*. Kila watu ni mashabaki kwenye vilabu vyao vya Simba au Yanga ama Azam na timu nyingine, lakini Serikali ndiyo *balancing*. Kwa hiyo, tuwaombe waendelee kuwa waadilifu kwenye eneo hilo, mnajua kila mtu anajua wajibu wake na majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya uchache wa muda nitajielekeza kwenye hoja moja tu mradi namba 6505, ujenzi wa kiwanda na ununuzi wa mitambo ya uchapaji wa magazeti ya Serikali *TSN*. Ukifuatilia taarifa ya Kamati wameshauri baadhi ya vitu ambapo pia vinaweza vikashtua watu kwa nini tumeshauri kwamba Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali aende akapitie pale *TSN* aone kuna changamoto gani ambazo

zilitokea, lakini nitaeleza kwa ufupi sana ili waelewe kwa nini tumesema kwamba waende wakakague, tuna wasiwasi kuna kitu hakipo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mradi una maeneo mawili. Kuna upande wa ujenzi wa kiwanda, eneo la pili ni ununuzi wa mitambo na vifaa kwa ajili ya kuendesha mradi wote wa *TSN*. Kwa hiyo, upande wa kwanza kwenye ujenzi, tarehe 7 Juni, 2023, *TSN* ilisaini mkataba na Kampuni ya *Group Six International* ambayo ilipewa kazi ya kujenga hilo jengo ambalo ndilo kiwanda tunachokizungumza ilikuwa na takribani bilioni 3.8. Malengo na mkataba ulikuwa unaeleza kwamba ndani ya miezi sita wawe wameshamaliza kujenga jengo yaani *structure* iwepo ili kiwanda cha *TSN* kianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka ninavyozungumza, kwa hiyo ukiangalia hapo hesabu kuanzia Juni ilitakiwa Novemba wakabidhi jengo, lakini mpaka ninapozungumza jengo halijakamilika na halijafika 50% na kamati tumeenda kukagua, bado kuna changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho kimetushtua sana ni kwa sababu mwenyewe kwenye maisha yangu tu hata ya ujenzi sijawahi kuona na kila mtu hapa anajenga tunafahamu, huwezi kununua *furniture* kabla haujamaliza kujenga, lakini *TSN* wamenunua mitambo, ambalo eneo la pili, nilisema ni ununuzi wa mitambo, wameshanunua mitambo 78% jengo halijafika 50%. Mitambo tunayozungumza hapa sasa hivi, wamekodi godauni, limewekwa pale wanawasha *AC full time* kwa mwaka wanalipa milioni 45 kwa ajili ya kupuliza ile mitambo isiharibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo mitambo imeshafika, mradi unasema kununua mitambo saba, wameshaleta saba, mitano imeshakombolewa bandarini lakini miwili bado ipo bandarini. Tunapozungumza, bandarini kuna mitambo ya shilingi bilioni 6.9, hatujui ina hali gani kwa sababu hatukufika bandarini kukagua mitambo ambayo ipo bandarini, mashine zile za uchapaji ambayo ipo pale ambayo ni mitambo mitano na imegharimu 15.3 bilioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wameiweka pale kwenye godauni. Kuna gharama za uendeshaji wa kutunza hilo eneo, kuna gharama za kodi tunalipa na hii kununua mitambo ilikuwa 2022, pamoja na kwamba ninajua ile ni *special order*. Kwa hiyo, ile mitambo ilitengenezwa kwa ajili ya ku-*feed* mahitaji ya kiwanda chetu. Ninajua kwamba ilibidi watoe *pre*, ndiyo maana tumesaini 2022 halafu imeanza kuletwa mpaka sasa hivi 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijawahi kuona hiki kitu, ndiyo maana tunaomba *CAG* akaangalie pale. Tunajua kuna mambo yanaendelea na yule mama pale ana mwaka sasa hivi, yeye kabla hata hajaingia yule Mkurugenzi Mtendaji wa pale *TSN* hayo mambo yalishafanyika huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijui kama hii Serikali ipo namna gani, kwa sababu, kwanza unaweza ukashangaa kwamba mitambo ipo pale ni mitambo ya Serikali na Serikali ni moja hii hii. Kwa nini, hii mitambo badala ya kuiweka pale kutumia gharama kuilinda na kuihifadhi ili isiharibike, kwa nini wasingeweka kwenye *entity* nyingine ya Serikali ambayo inafanya *printing? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hii *TSN* tunapozungumza ndiyo tulisema tutengeneze kiwanda cha uchapaji ili hata kulinda nyaraka za Serikali zisiwe zinachapishwa kwenye makampuni binafsi. *TSN* bado inatumia makampuni binafsi kuendesha shughuli zao za ki-*media,* kiuandishi na kiuchapaji, wanalipa makampuni ku-*print* taarifa zao. Maana yake tunapoteza pesa, tukiweka hiki kiwanda tuna uwezo wa kuokoa 60% ya gharama za uchapaji wa taarifa zinazozalishwa kwenye magazeti ambayo yapo *TSN*, magazeti ya Serikali tunayafahamu *Daily News* na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua tulishazungumza pia kwenye Kamati, tuwaombe sana Wizara, tunaomba waokoe kwa sababu hizi ni fedha tunazozungumza ni fedha za Watanzania. Hizi *figures* nimetaja kwa sababu ununuzi wa mitambo peke yake ni bilioni *23 full.* Kwenye ujenzi inakwenda bilioni tano kwa sababu kuna *part* ya kwanza ya ujenzi na *part* ya pili ya kuweka *infrastructure* za maji na umeme. Kila akitokea Waziri mpya

anapelekwa pale kwenda kukagua lile jengo limebaki pale *white elephant.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kiti chako na viongozi ambao wanatusikiliza, hebu tumieni busara. Pelekeni *flow* ya hela iwe nzuri pale, mWende mkamalize lile jengo. Malizeni lile jengo ili ile mitambo ianze kutumika. Kama haiwezekani, basi pelekeni kwenye *entity* nyingine ya Serikali ambayo inafanya *printing* ili ile mitambo ikatumike kwa sababu hizo fedha ni za walipakodi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongea hivi kwa uchungu sana, kwa sababu tumeenda pale kuona. Kwa hiyo, nilitaka nizungumze hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia cha mwisho nawapongeza sana *TFF* kwa sababu tulienda kukagua *one of the sports academies* (vituo vya michezo) viwili; kimoja kipo Tanga na kingine kipo Kigamboni. Tumeona vijana wadogo wa *under fifteen* waliopita pale wameshinda kwenye michezo ya *under fifteen* mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba pia Serikali iendelee kuona umuhimu wa kuanzisha *sports academies* kwa sababu pia tuna miaka miwili kwenda kwenye *AFCON*. Pengine itasaidia kukuza vipaji na pengine hata sisi watu wa Ikungi tunaweza tukapata *sports academy* na pengine tunaweza tukapata pia kiwanja cha riadha, kwa sababu unajua sisi watu wa Singida tunakimbiza upepo sana, ndiyo maana mnaona hata Alphonce Simbu ameshinda kwenye Mashindano ya Boston juzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono Hoja ya Kamati.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Rashid Abdalla, ajiandae Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata fursa hii. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya katika Sekta ya Michezo na kuhakikisha kwamba viwanja kwa ajili ya *AFCON* vinatayarishwa. Tunajua kuna Viwanja vya Dodoma, Arusha na baadhi ya viwanja vingi ambavyo vinafanyiwa ukarabati. Tunamshukuru sana kwa kazi hii kubwa ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunampongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Kabudi pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba Wizara hii inafanya majukumu yake kama ambavyo wamejipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nianzie kwenye Kombe la Muungano. Kombe hili tuliliacha miaka mingi , lakini ni miaka miwili sasa Serikali zetu hizi mbili kupitia Wizara ya Habari na Michezo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na ile Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zimelirudisha tena kombe hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawakumbusha hawa Waheshimiwa Mawaziri kwamba kombe hili lina hadhi kubwa sana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ni vyema kwamba mashindano haya yasishirikishe tu timu nne kutoka Bara na timu nne kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuige wenzetu ambao wanafanya mashindano hayo ikiwemo *Spain*. Kuna Kombe La Mfalme linashirikisha timu nyingi. Halikadhalika Afrika Kusini na Misri, wote wana mashindano hayo, ukiacha ligi kuu ambazo zinaendeshwa nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika katika jambo hili, zawadi ambazo zinatolewa ni ndogo. Kwa mfano, juzi tumeshuhudia kule Timu ya *Dar es Salaam Young African* ikichukua kombe lile na zawadi ya shilingi milioni 50 kwa kuifunga Timu ya JKU ya Zanzibar. Kwa kweli kwa hadhi ya kombe hili, namwomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Mheshimiwa Waziri Tabia wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kombe hili liwe na zawadi kubwa ambayo inafika hata shilingi milioni 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar kuna mashindano wanachezesha yanaitwa Yamle Yamle *Cup*. Mashindano haya huanza kwa timu zaidi ya 80, lakini fainali yake inakuwa ni fainali moja kubwa sana na ya kibabe ambapo mara zote mgeni rasmi huwa ni Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na zawadi kubwa nazo huwa zinatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, kwenye Mashindano ya Yamle Yamle, naomba Mheshimiwa Waziri azungumze na viongozi wake akiwemo Mheshimiwa Rais Karia. Hili jambo la kufuta haya mambo ya Ndondo *Cup*, siyo jambo zuri sana kwa sababu jambo hili la hizi Ndondo *Cup*, mashindano kama yale ya Yamle Yamle ndiyo ambayo yanawafanya wachezaji wetu wa Tanzania kukuza vipaji vyao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona mfano kwamba, asubuhi hapa nilikuwa ninampa taarifa Mheshimiwa Taletale kwamba, ile Zanzibar timu zao kuwa imara, kuwa zinafanya vizuri, hazifungwi mabao matano na manne; ule ni uimara wa *ZFF* jinsi ambavyo inasimamia ile ligi vizuri. Hakuna mabao matano, hakuna mabao manne au sita. Hamna habari ile. Wala hausikii wachezaji kugombana na waamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, timu ni gharama na mashindano ni gharama. Timu zinagharamika, ufadhili upo sawa, lakini haitoshelezi kuziendesha timu. Kwa hiyo, naiomba *TFF*, jambo la kusimamia ligi kwa uadilifu ni jambo muhimu sana na litatupeleka mbele sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Zanzibar kuna wachezaji zaidi ya 50 ambao wako huku Tanzania Bara wanacheza kwenye vilabu mbalimbali vya Ligi Kuu ya Tanzania Bara. Yote hii ni kwa nini? Ni kwa sababu wameonekana katika mashindano mbalimbali ambayo yanachezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, namwomba Mheshimiwa Waziri kitu kimoja pia kwamba, kuna ruzuku ambayo inatoka *CAF* na *FIFA*, ambayo kwa makubaliano yao *TFF* na *ZFF* wamekubaliana kwamba kila mwezi wawapatie wale *ZFF* shilingi milioni tano. Kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha sana. Leo tuko

Mei lakini hakuna hata senti iliyopelekwa *ZFF*. Kadhalika, kuna mwaka 2024, nadhani kuna miezi kadhaa ile fedha nayo bado haijaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TFF* wale *ZFF* ni ndugu zenu na Karia yupo anasikia. Wawasaidie ile elfu tano tano ili nao wakuze lile suala la michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye *AFCON*, Zanzibar ni lazima tumpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kurekebisha miundombinu ya viwanja vya michezo. Tunashukuru kwamba hata Ligi Kuu ya *NBC* kuna baadhi ya mechi zinachezwa kwenye Uwanja wa Amani *Complex*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumeshuhudia vilevile kwenye hili Kombe la Muungano kwamba mashindano yale yamefanyika katika Uwanja wa Gombani, uwanja ambao una hadhi ya kuchezwa *AFCON.*

Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo ikikupendeza hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na mashindano yanakuja Tanzania, ni vyema ule Uwanja wa Amani na Gombani ukatumika kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenyewe anayesimamia michezo hapa *TFF,* Rais Karia, ambaye '*r*' yake ni ndogo, alikwenda Zanzibar kushiriki kwenye yale mashindano na alikwenda kukagua baadhi ya viwanja. Kwa hiyo, namhakikishia kwamba kuna viwanja vingi vya timu kufanya mazoezi, viwanja *standard* na viwanja vinavyokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashukuru kwa kunipatia muda huu na ninasema, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia

kwenye hii Wizara ya Michezo. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye sekta hii ya michezo. Hongera sana Mheshimiwa Rais. Kazi kubwa imeonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uteuzi wa nafasi ya hii Wizara, maana yake ni Mheshimiwa Waziri ambaye ni mbobevu kwenye masuala ya kisheria.

Hongera sana Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi kwa kuteuliwa na kuongoza. Watanzania wanakutegemea na wanakuona kwamba upo kwenye nafasi sahihi kwa sababu umeingia, unafahamu sheria na kanuni, huwezi kuburuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, napenda kuipongeza Serikali kwa uwekezaji kwenye viwanja. Kuna ujenzi kule wa Kiwanja cha Arusha, ujenzi wa Kiwanja Dodoma na ujenzi wa viwanja mbalimbali na maboresho kwenye Kiwanja cha Taifa cha Dar es Salaam. Hongera sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa Mheshimiwa Waziri akikumbuke na Kiwanja cha Ali Hassan Mwinyi pale Tabora, tupate kiwanja bora cha kisasa. Wazungumze na *partnership* CCM ili kuona ni namna gani wanaweza kukiboresha, kwani kuna fedha nyingi. Kama unavyotambua, Tabora ni Mkoa wa kimkakati na Tabora tunahitaji kukuza viwango vya wanamichezo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalopenda kuzungumza, kama ambavyo unafahamu, tumeweza kuona namna gani ambavyo tunashiriki michezo yetu. Ligi yetu inakua na inavutia sehemu mbalimbali duniani. Leo natumia nafasi hii kuwapongeza Azam kwa uwekezaji mkubwa katika ligi ya Tanzania. Hongera sana kwa Azam, wamefanya kazi kubwa na amewekeza fedha nyingi. Watanzania wanaona, dunia inaona, na wachezaji wanavutika kutokana na fedha alizowekeza kwenye ligi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri. Tumeweza kuona Ligi Kuu ya Uingereza inayoongozwa na bodi ya ligi ambayo inaitwa *EPL.* Pia *Federation* ya Uingereza ina Ligi yao ya *FA*. Hizi ni ligi mbili na bodi ya ligi ya Uingereza inasimamia kila kitu na masuala mazima ya Ligi Kuu ya Uingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Ligi Kuu ya *Spain* inaongozwa na bodi ya ligi. Pale *Spain* kuna bodi ya ligi inaitwa *LaLiga* inasimamia masuala mazima ya michezo katika Ligi ya *Spain*. Pia, *federation* ina ligi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Tanzania, nampongeza Mheshimiwa Leodegar Chila Tenga kwa kuanzisha bodi ya ligi ndani ya Idara ya *TFF* na imekuwa nzuri. Toka ilivyoanzishwa mwaka 2008 ilikuwa imeanzishwa ikiwa chini ya Idara ya *TFF* lakini malengo yalikuwa baadaye ije ijitegemee kama zilivyo Bodi ya Ligi ya Uingereza na Bodi ya Ligi ya *Spain*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa bodi yetu bado iko chini ya *TFF*. Tunaomba Mheshimiwa Waziri aiboreshe bodi hii, iwe *independent* na ijitegemee. Tumeona bodi ambayo haijisimamii; asubuhi inatoa matamko haya, jioni inatoa matamko haya. Hii inaonesha nyuma ya pazia bodi inasukumwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri bodi hii ijisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu Ligi Kuu ya Uingereza inasimamiwa na Bodi ya Ligi Kuu ya...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali…

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Naam!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali, wewe ni Mbunge mzoefu. Usiliingize Bunge kujadili vitu ambavyo bado havijafika rasmi…

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, vitu gani?

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya 81 inakataza kujadili au kutuhumu mtu au chombo ambacho hakina nafasi ya kuja kujitetea wakati wewe unasema… *(Makofi)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali!

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya 84. Ukikataa maelekezo ya Kiti au Spika, unashtakiwa kwa kanuni kwa kosa la kukosa nidhamu…*(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Ukipinga Kanuni ya 84 unakwenda 85, ndiyo mbaya kabisa, hata Ubunge hutagombea. Usituhumu chombo chochote… *(Kicheko)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Ninakuomba, mimi nakusaidia tu. Kuna kesi ilitokea hapa ya Mheshimiwa mmoja mkubwa na Mbunge humu ndani kuzungumza vitu ambavyo unatoa maamuzi na unalalamikia maamuzi yaliyofanywa. Wewe hukuwa sehemu ya hicho kikao, na mimi kwa kukaa hapa naweza nikaingizwa kwenye kesi yako. Punguza munkari, changia mambo ambayo una uhakika nayo. Endelea.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muda wangu ulindwe. Nazungumzia muundo wa bodi zetu za ligi zilivyoanzishwa. Ukienda Uingereza kuna bodi ya ligi inayojitegemea inaitwa *EPL*… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali!

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda *Spain* kuna bodi ya ligi inayojitegemea… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali, haya makofi hayatakusaidia… *(Kicheko)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sizungumzii huko. Nazungumzia jinsi…

**NAIBU SPIKA:** Utakapopelekwa kwenye kikao cha nidhamu haya makofi hayatakusaidia. Hawa wote watakutazama tu. Unapuuza maelekezo ya Kiti, unalalamikia maamuzi ambayo siyo sehemu yetu hapa. Endelea. *(Makofi)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea maelekezo, lakini silalamiki. Nazungumzia muundo wa bodi za ligi duniani… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Umezungumzia bodi hii inatoa…

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumzia Bodi ya Ligi ya Uingereza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali, umezungumzia bodi hii asubuhi inasema hivi, jioni inasema hivi. Ndiyo ulivyosema. *It is recorded*.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Ligi ya Uingereza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali, muda wako umekwisha, kaa chini. *(Makofi/Kicheko)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa maendeleo makubwa ya michezo na sanaa ikiwemo ongezeko kubwa katika ukuaji uchumi na mchango katika pato la Taifa na pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa Kimataifa *(national competitiveness)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na majirani zetu Kenya na Uganda, kwa maandalizi ya kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika *(AFCON 2027)* ambayo yataanza Juni, 2027. Mafanikio mazuri yamefikiwa katika ujenzi na uboreshaji wa viwanja, viwanja vipya vilivyopangwa kujengwa Arusha na Dodoma na pia viwanja vya Zanzibar na Mwanza ikiwemo kuboresha viwanja vya Benjamin Mkapa, Uhuru vya Dar es Salaam na *Aman Stadium* na Gombani vya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maandalizi mazuri ya kuboresha viwanja vya kufanyia mazoezi na kuna maandalizi mazuri ya mahoteli, hospitali na miundombinu ya barabara na mawasiliano na vifaa vingine kwa ajili ya kuandaa michuano ya *CHAN 2025* na *AFCON 2027*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kuchukulia michuano ya *CHAN 2025* na *AFCON 2027,* kuwa ni fursa muhimu za kuijenga Tanzania vizuri zaidi katika ramani ya dunia na hususan fursa za kiuchumi ikiwemo utalii. Ninapendekeza taasisi hasa za utalii, kuchangamkia fursa hii kwa kuwekeza vivutio zaidi na kuhakikisha tunakuwa na sehemu kubwa ya soko na biashara zitakazozalishwa na michuano hii ya *CHAN 2025* na *AFCON 2027*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yote panapojengwa na kuboresha viwanja vitavyotumiwa na mashindano haya, iendane na kuboresha miundombinu ya barabara, maji, umeme,

mawasiliano na hata huduma za mahoteli, migahawa, biashara mbalimbali na hata sehemu za burudani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza wanamichezo wote kwa kufanya vizuri katika mashindano ya Kimataifa. Kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hamasa na msukumo alioweka katika michezo yote na hasa mafanikio makubwa ya timu zetu za Yanga na Simba katika mashindano ya Kombe la Shirikisho *(CAF Confederation Cup)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza Klabu ya Simba kwa kujiwekea rekodi ya kuingia fainali za ya Kombe la Shirikisho *(CAF Confederation Cup)*. Kutokana na hamasa ya Mheshimiwa Rais, Klabu za Yanga na Simba zimeandika historia na kuipa nchi yetu heshima kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inastahili pongezi kwa mkakati wake katika kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha ushiriki wa timu za Taifa na vilabu katika michezo na michuano mbalimbali ya Kimataifa na kikanda. Kama sehemu ya mkakati huo, Wizara iweke msukumo zaidi wa kuhamasisha kujenga, kukarabati na kuboresha miundombinu ya viwanja vya michezo hususan vya mpira wa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vingi vya mikoani vipo katika hali mbaya na kwa kiasi kikubwa ni sehemu ya changamoto katika maendeleo ya michezo nchini. Michezo na sanaa ni muhimu sana katika kujenga sura na sifa ya Taifa letu *(Nation brand)*. Hivyo ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha inaweka umuhimu mkubwa wa ushiriki wa timu zetu za Taifa na kuwepo kwa mkakati wa Kitaifa wa kuhakikisha timu zetu za Taifa na vilabu zinafanya vizuri kwenye mashindano ya kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati huu katika michezo na sanaa ni nguzo muhimu katika kutekeleza Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026. Serikali itenge bajeti ya kutosha kuhakisha tija katika ushiriki wetu katika mashindano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuboresha miundombinu ya viwanja, Wizara ijikite katika kuibua vipaji mbalimbali vya michezo na sanaa kwa kuimarisha ushirikiano na Wizara nyingine hususan Elimu na TAMISEMI. Pamoja na kutokuwepo kwa miundombinu rafiki, mikoa mingi imekuwa inatoa wachezaji wenye vipaji vikubwa katika mpira wa miguu, riadha na hata sanaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika muda sasa wa kuwepo kwa mkakati wa kuibua na kuendeleza vipaji hivyo ambavyo vimekuwa vinaonekana kikanda zaidi kama vile riadha kwa Mikoa ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Mikoa ya Kati. Pia kwa upande wa mpira wa miguu kumekuwepo na mikoa kadhaa ya vipaji vikubwa, na huko ndiyo Serikali iweke msukumo zaidi wa kuibua na kuendeleza hivyo vipaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwa wasanii, kuna mikoa imekuwa inatoa idadi kubwa ya vipaji kwenye uigizaji, uimbaji ikiwemo nyimbo za Injili ambazo zinapata umaarufu sana duniani. Kutokana na vipaji vingi vya michezo hususan mpira wa miguu na riadha, napendekeza Shule ya Sekondari Santilya ya Wilaya ya Mbeya iongezwe kwenye orodha ya shule teule za michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa Kiswahili, kuwa lugha rasmi Kimataifa, napendekeza uwekezaji zaidi katika kuitangaza na pia kuwezesha ulimwengu kujua kuwa mizizi na ustawi wa Kiswahili ni Tanzania pekee na wengine wanaigiza kwetu. Serikali iendelee kuchukua hatua zaidi ya kukistawisha Kiswahili katika Mataifa mengine Barani Afrika na kwingineko kwa kushirikisha vyuo vikuu hapa nchini na vyuo vikuu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake mbalimbali katika Taifa letu, hususan ustawi wa kijamii kisiasa, kiuchumi, amani, kidiplomasia na mshikamano. Hali hii imetuweka nchi yetu kuwa kisima cha amani mbele ya Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wote wa Jimbo la Mbulu Mjini kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025, Mwenyezi Mungu ambariki pamoja na Serikali yake nzima ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Prof. John Mwaluko Kabudi, Waziri wa Wizara, Naibu Waziri Mwinjuma na watendaji wote wa Wizara hii kupitia hotuba ya mapendekezo ya maombi ya mapato na matumizi 2025/2026 kama ilivyowasilishwa mbele ya Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wajumbe wote wa Kamati kupitia taarifa yao waliyowasilisha mbele ya Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo hayo mawili ya Wizara na Kamati. Kwanza, Serikali iandae kalenda/ratiba ya michezo kupitia Kamati za michezo ambazo Mwenyekiti wa Wilaya ni Katibu Tawala na Mkoa ni Katibu Tawala wa Mkoa kuunganisha na ngazi ya Taifa ili kubaini na kutangaza vipaji kwa vijana wetu walioko ngazi za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Kamati za Michezo za Wilaya na Mikoa hazina majukumu kabisa na mipango kazi inayoonesha muundo wake, majukumu, hali inayopelekea wanamichezo wengi vijijini kucheza kama burudani wakati kuna vipaji vingi vya michezo katika makundi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendeleza miundombinu ya viwanja vya michezo kwa ajili ya mashindano ya *AFCON*. Hatua hiyo ni kubwa sana kwa Taifa letu, hivyo basi, tuendelee kujenga miundombinu hiyo ya michezo katika ngazi za mikoa na wilaya kama vile uwanja wa michezo wa *Mwalimu Nyerere Stadium* ulioko Wilaya

ya Mbulu, Mkoani Manyara ambao ulitumiwa na timu kutoka mikoa ya Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, basi tunaiomba Serikali yetu itafute fedha za kukarabati uwanja ule. Kwa kweli hali ya hewa ya Wilaya ya Mbulu ni nzuri sana kwa michezo, na tuna hazina nyingi za vijana wenye vipaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba sana Serikali yetu ijitahidi kupeleka fedha zinazoombwa kwenye bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa kuwa sekta ya michezo nchini itachochea ajira kwa kundi kubwa la vijana wengi walioko mitaaani ambao Mwenyezi Mungu amewajalia vipaji vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, na ninaomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Naibu wake Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Katibu Mkuu Ndugu Gerson Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Methusela Mtonda, wataalamu wa Wizara na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa kazi nzuri wanayofanya kuboresha utendaji katika sekta hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita kwenye umuhimu wa kuwekeza katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza nchini Tanzania. Filamu na michezo ya kuigiza huweza kutumika katika jamii kuelezea tamaduni zetu, kuibua hisia fulani kwenye jamii, kutoa elimu za kimaadili, burudani na kujiingizia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu huo, tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza kama zitachukuliwa kwa umakini mkubwa, zinaweza kuwa chanzo bora na muhimu katika kulijenga Taifa letu na zinaweza kutumika kama jukwaa la mafunzo la kuchochea mijadala nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii inaweza kuwa kichocheo kikubwa kwenye kukuza uchumi wa Taifa letu na mtu mmoja mmoja. Kwa mfano, filamu ya *The Royal Tour* iliyotengenezwa kuonesha vivutio vya utalii katika Taifa letu imekuwa mkombozi katika sekta ya utalii hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wa tasnia hii, miaka ya hivi karibuni tumekumbana na wimbi kubwa la kushuka kwa tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza hapa nchini Tanzania ukilinganisha na nchi kama Nigeria na *South Africa* ambao wapo vizuri sana kwenye tasnia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kudidimia kwa tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza hapa nchini, wananchi wengi wa Tanzania wameishia kupata burudani kutoka kwa wasanii wa nchi nyingine kama Nigeria na Afrika Kusini. Kwa mfano, Watanzania wengi hupenda kufuatilia kipindi cha tamthilia cha wasanii wa Afrika Kusini kinachorushwa na *Azam TV*. Upenzi wao unatokana na umakini wao na kuigiza mambo ya misisimko, mafunzo na ya kipekee katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiuhalisia, tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza hapa nchini bado ipo nyuma sana na Serikali yetu ni kama imeipa kisogo na kugeukia michezo wa mpira wa miguu ambao hauhitaji sana teknolojia za kisasa. Hivyo basi, kutokana na ukosefu wa ajira hapa nchini, ni vyema Serikali ikaja na mkakati wa kuhamasisha vijana kuchangamkia fursa zilizopo katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi wa wasanii waliong'ara hapa nchini ni pamoja na Stephen Kanumba, Ramadhani Mkieti (Sharo Milionea) na wengine wengi. Taifa letu likiwa na mipango madhubuti, tunaweza kukuza tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza na kufikia kiwango kizuri na kuzalisha wasanii wakubwa na maarufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hili kwa sababu katika nchi yetu, tumebarikiwa kuwa na wahitimu wengi waliosomea tasnia ya sanaa na utamaduni ikiwepo masuala ya filamu na michezo. Kama wasomi wetu hawa watatumika vizuri, baada ya

kumaliza masomo yao, watasaidia sana kuendeleza hii sanaa waliyosomea na kulipatia faida Taifa na wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla na kiwango kikubwa, waigizaji wetu wengi wamekuwa wanatumia lugha ya Kiswahili kwenye kutengenezea filamu na kuigiza hapa nchini. Filamu hizi zinapendwa sana katika nchi za Afrika Mashariki kutokana na kuwa zinatumia lugha adhimu ya Kiswahili. Nje ya jumuiya ya Kiswahili, filamu hizi hazina soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati muafaka sasa kujiongeza na kuzalisha filamu kwa kutumia lugha za Kiingereza kama wanavyofanya nchini nyingine za Afrika zikiwemo Kenya na Nigeria ambapo kwenye tasnia zao za filamu na michezo ya kuigiza hutumia lugha ya Kiingereza na kuchanganya na Kiswahili au lugha ya kienyeji kidogo na kufanya filamu hizo kupata soko la ndani na la Kimataifa. Kwenye haya Mataifa, Kiingereza kinatumika kama lugha ya biashara Kimataifa ili kupata soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu, napendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Serikali iwekeze kikamilifu kwenye Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Tanzania ili waweze kuandaa, kuratibu na kuendesha warsha, vikao, mijadala na mafunzo ya kujenga uwezo kwa wadau wa filamu hapa Tanzania. Pia uwezeshaji huo utawasaidia kutafuta fursa katika sekta na kuziwekeza kwa wadau na kuratibu uibuaji vipaji kupitia michezo ya kuigiza na filamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ili kuiendeleza sekta ya filamu, Serikali kwa kushirikiana na wadau wanapaswa kulisaidia Shirikisho la Filamu Tanzania ili kuwawezesha watayarishaji na wasanii kupata mafunzo ya kitaalamu kwa njia ya warsha na semina ili kuongeza uwezo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Serikali ifanye uwekezaji wa kimkakati katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza. Hii ni pamoja na kujenga studio za kisasa za uzalishaji wa filamu na zenye ubora. Miundombinu ya filamu hapa ni duni sana. Wasanii

wetu wapewe fursa ya kutumia studio hizi hata kwa kuchangia gharama kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Serikali ije na ajenda mahsusi ya Kitaifa kuhusu tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza itakayowahusisha wadau wote ikilenga kujenga uzalendo na kuifufua tasnia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Serikali iwekeze nguvu kuingiza nchini teknolojia mpya kwenye tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza kwa kuweka mazingira rafiki ya kikodi. Teknolojia hizi ziletwe kutoka kwenye Mataifa yaliyo mbele zaidi kimaendeleo katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Serikali iwekeze kimkakati kwenye kuandaa wataalamu mahiri wa kutayarishaji na kuunda filamu na michezo ya kuigiza. Wataalamu hawa wawe na ubobezi katika ubunifu, matumizi ya lugha (Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu) na matumizi ya vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya upungufu wa wataalamu hasa katika lugha ni changamoto inayoturudisha nyuma zaidi katika tasnia ya filamu nchini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wadau wa ndani au Kimataifa hutazama zaidi lugha ili kupata ujumbe ulioko kwenye filamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, Serikali iendelee kuboresha sera, sheria pamoja na kanuni za kusimamia filamu na michezo ya kuigiza Tanzania Ili ziwanufaishe wasanii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kushauri kwamba ni vyema wasanii wetu wakajikita zaidi katika kuzalisha filamu zinazotoa elimu kwenye changamoto zinazosumbua Taifa na ulimwengu kwa ujumla kama zile zinazogusa hisia za watu. Kwa mfano, filamu zinazohusu utekaji wa watoto, ubaguzi wa rangi na jinsia, udhalilishaji wa akina mama, watoto na akina baba, na fursa mbalimbali zilizopo hapa nchini. Ni vyema filamu na michezo ya kuigiza kutoka kwa wasanii wetu ziwe na maudhui ya heshima na ya kuijenga jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja iliyoko Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyoinua michezo nchini kwa uhamasishaji wake uliokwenda sambamba na utoaji wa fedha zilizoleta mabadiliko chanya katika sekta ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na *management* nzima ya Wizara kwa kazi kubwa na nzuri ambayo Wizara imefanya katika kuinua michezo na kuleta hamasa kubwa kwa wasanii, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua nchi yetu itakuwa mwenyeji wa mashindano ya *AFCON 2027*. Mpango wa Wizara ni kuwa na viwanja vitano vitakavyotumika katika mashindano ya *AFCON*. Mbali na ujenzi wa viwanja vipya hivyo vitano, moja ya viwanja ambavyo vilikusudiwa kutumika katika michezo hiyo, ni pamoja na uwanja wa CCM Kirumba ambao ulitakiwa kufanyiwa ukarabati mkubwa ili utumike aidha, kwa mazoezi au kwenye mashindano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Wizara iko kimya kuhusiana na ukarabati wa uwanja huo. Napenda kujua suala hili limefikia wapi? Naomba utekelezaji wa suala la ukarabati ufanyike mapema ili uwanja huo utumike katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naunga mkono uanzishwaji wa mamlaka/taasisi itakayosimamia viwanja vya michezo nchini. Nashauri taasisi hiyo itakapoundwa isihusishe viongozi wa michezo, bali ijitegemee kabisa ili kuepuka mwingiliano wa kiutendaji ili kuleta tija katika utendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni kutaka kujua suala la maandalizi ya kuwa na vazi la Taifa imefikia wapi? Kama imeshindikana tufahamishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho japo siyo kwa umuhimu Serikali iangalie kwa mapana tamaduni zetu. Kumekuwepo na utamaduni usiokidhi au unaokiuka maadili ya Kitanzania. Ngoma zinazochezwa sasa hususan Ukanda wa Pwani zaidi sana Dar es Salaam, wanakiuka sana maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, Wizara itupie macho tamaduni hizi ambazo zinaaibisha sana na kukiuka maadili ya Mtanzania. Hivi karibuni baadhi ya wasanii hao walikwenda Kenya na kujinasibu kuwa huo ulikuwa ndiyo utamaduni wa Mtanzania. Yaliyojiri baada ya onyesho lao, ni aibu kwetu kama Watanzaniaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka ya uhai na kutuwezesha kukutana hapa jioni hii ya leo kujadili Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa ya moyo wangu, namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini mimi na wenzangu kwenye Wizara hii ambao tunaongozwa na Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi kwa sasa na kuendelea kutuunga mkono na kuonesha kwamba yeye ni mwanamichezo namba moja kwa kuhakikisha tunayafanyia kazi maono yake kwa kuwezeshwa na mkono wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais na ninamwahidi kwamba nitaendelea kuwa mtiifu kwake na kwa nchi hii na nitaendelea kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na akili

zangu zote ili kuhakikisha tunayatekeleza maono yake kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nawashukuru wenzangu kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo wakiongozwa na Prof. Kabudi kwa ualimu na maelekezo ya mara kwa mara ambayo yanafanya tuendelee kuifanya kazi hii ya wananchi wa Tanzania ambao walikiamini Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi wa 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika nakushukuru wewe kwa niaba ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya dada yangu Mheshimiwa Husna Sekiboko kwa miongozo na maelekezo yanayofanya tuweze kuifanya kazi yetu kwa ushirikiano mkubwa ambao wanatupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru familia yangu, mke wangu na watoto wangu pamoja na wananchi wenzangu wa Muheza kwa kuendelea kuniunga mkono, kuni-*support*, kunivumilia na kunitia moyo hata pale mambo yanapokuwa magumu. Nawashukuru sana na ninawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutolea ufafanuzi hoja kadhaa za Waheshimiwa Wabunge ambazo zimetolewa toka asubuhi ya leo kabla sijamwacha Mheshimiwa Prof. Kabudi kuja kuhitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo hoja kadhaa, na sina uhakika kama muda utanitosha, lakini nitakapoishia ndiyo hapo nitakapokuwa nimejaaliwa. Jambo la kwanza, ni ile hoja kuhusiana na Muziki wa Singeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge kadhaa hapa wameongea toka asubuhi na wameonesha hisia nyingi kuelezea jinsi ambavyo kuna sintofahamu kati ya Singeli kuwa mziki wa Taifa, lakini hali kadhalika maudhui ambayo yanabebwa kwenye aina hii ya muziki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, hakuna mtu yeyote aliyesema mahali popote kwamba tunataka kuufanya Singeli kuwa muziki wa Taifa. Kilichotokea ni kwamba Singeli kama muziki ambao umetoka mtaani, umejipigania wenyewe na umejipambania wenyewe, ukifanywa na vijana wadogo ambao wametengeneza ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Kwa muda mrefu tuliona kwamba muziki huu umeshika na unakubalika katika maeneo mengi ikiwemo nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimewahi kwenda kwenye Maonesho ya Singeli nje ya nchi na muziki huu umekuwa unafanya vizuri sana. Sasa ukweli ni kwamba hakuna mtu yeyote kutoka sehemu nyingine yoyote duniani anayeweza kuja kudai kwamba Singeli ina asili ya kutoka nchini kwao. Kwa hiyo, kimsingi Singeli ina asili ya kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichofanya tulikuwa tunajaribu kuwasaidia hawa vijana ambao wamejitengenezea ajira na wamejitoa mtaani kwenye kufanya mambo ya ovyo ili kuhakikisha tunawasaidia kuu-*brand*, kuu-*package* na kuu-*promote* muziki huu. Pia, wakati tunafanya hivyo tuwasaidie pia kuu-*sanitize* (kuusafisha) muziki wa Singeli. Hiyo ndiyo ajenda yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uhuni ambao unasemwa uko katika Singeli, ninaamini nikiongea kama mwanamuziki; najua kwamba uhuni uko katika miziki yote na vijana hawa wanahitaji maelekezo na siyo kususwa kama ambavyo tumekuwa tunasema kwa ukali.

Mheshimiwa Naibu Spika, siamini kama kuna Mheshimiwa Mbunge yeyote anataka tuwatelekeze vijana hawa au anataka kuua Muziki wa Singeli, lakini ninachojua ni kwamba wanataka tujaribu kuusafisha muziki huu ili uweze kuwa utambulisho mzuri kwa Taifa letu huku ukiwa unabeba maudhui yanayoweza kuuzika ndani na nje ya mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote walioongea kwa hisia sana akiwemo dada yangu Mheshimiwa Esther Malleko kwamba,

watupe nafasi tuwasaidie vijana hawa kusafisha muziki huu na muziki huu utakuwa wenye matumaini makubwa hapo mbeleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sasa hivi muziki wa Singeli ndiyo unafanya vizuri hata kwenye mikutano yetu ya kampeni. Kwa hiyo, unafurahiwa na watu wengi na ni jukumu letu kuuelekeza badala ya kuususa na kuunyoshea vidole.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Esther Malleko na wengine wote ambao walisema kwa ukali kuhusiana na muziki wa Singeli, watupatie nafasi ya kufanya hili na sisi tunawahakikishia tutawaongoza vijana hawa na muziki huu utakuwa safi, unaoburudisha badala ya kupotosha maudhui na kupotosha jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili alilisema Mheshimiwa Hamisi Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki. Lenyewe lilikuwa linahusiana na kadhia ambayo Kampuni ya Azam imeingia baada ya kusimamishwa kuonesha kipindi chake cha vitasa, kipindi ambacho kilikuwa kinaonesha mchezo wa ngumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema ukweli mimi binafsi ni mpenzi mkubwa wa mchezo wa ngumi, nami nimecheza ngumi. Azam baada ya kuingia na kufanya udhamini, kwenye mchezo wa ngumi walikuwa wanabadilisha maisha ya vijana wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchezo wa ngumi unachezwa sana uswahilini, unachezwa na vijana wenye hali duni za maisha na ni mchezo hatari kusema ukweli. Baada ya Azam kuingia, wakaubadilishia hadhi. Maeneo ambayo mchezo huu ulikuwa unafanyika yakawa yenye hadhi kubwa, lakini pia mapato ambayo mabondia (wapiganaji) walikuwa wanayaingiza yakawa yameongezeka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea ni kwamba, kuna bondia mmoja wa zamani akaenda Mahakamani akashtaki kwamba Azam wamechukua *idea* yake ya kuonesha kipindi cha aina hii na akaiomba Mahakama kwanza alipwe fidia na Azam wazuiwe kuonesha mchezo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafikiri *proceedings* za kesi wengine tuliziona na hazikuwa nzuri sana kwa upande wa Azam kiasi kwamba Azam kweli wakazuiwa kuonesha mchezo ule japokuwa wamekata rufaa na kesi yao sasa iko kwenye Mahakama Kuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri pamoja Naibu Waziri, usizungumze jambo ambalo liko Mahakamani, zungumza *topic*, maudhui unaweza, lakini usizungumzie kesi ambayo iko wapi, wamefikia hatua gani? Ndiyo kanuni zetu, na Kanuni ya 84 ukikataa maelekezo ya Spika, ina adhabu yake. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea. Jambo lingine lilisemwa na Mheshimiwa Malembeka kuhusiana na msaada ambao wasanii wanaupata kupitia Baraza la Sanaa la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Malembeka, ule upolisi ambao Baraza la Sanaa la Taifa lilikuwa likiufanya huko nyuma umesimama sasa hivi. Baraza la Sanaa la Taifa linafanya shughuli yake kama walezi wa wasanii badala ya kuwa Polisi. Sasa hivi tumekuwa tukifanya mijadala mingi na wasanii na hata wasanii hawajisikii vibaya na hawapati uwoga wanapopata wito wa kuitwa BASATA, kwa sababu wanajua ni majadiliano na maelekezano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampa shukrani za dhati Dkt. Kedmon Mapana kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Baraza la Sanaa la Taifa. Kimsingi BASATA haiwezi kuwalipia wasanii, kuwatengenezea nyimbo zao na kuwatengenezea video, lakini linachofanya ni mambo mbalimbali ikiwemo kuwapa msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 2024 pekee yake wasanii zaidi ya 20 wamepata msaada wa kisheria kutoka BASATA, wasanii zaidi ya 100 wamepata kazi, matamasha na maonesho mbalimbali ndani ya nchi kupitia BASATA. Maonyesho zaidi ya 200 ya nje ya nchi yamepatikana kwa wasanii wa nchi hii kwenda kutumbuiza kupitia BASATA, hili la upolisi limekwisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ada ambazo wasanii wanatakiwa kulipwa zimeshushwa kutoka shilingi 40,000 mpaka shilingi 20,000 kwa mwaka mzima kuanzia mwezi Julai, mwaka huu 2025. Hata zile za kutozwa mara mbili, kwamba kuna tozo ya Halmashauri na tozo ya BASATA na zenyewe zinakwenda kukoma mwezi Julai, mwaka huu, 2025 kwa sababu BASATA imeanzisha Mfumo wake unaitwa *AMIS* ambao unakwenda kusomana na Mfumo wa TAUSI, na tozo hizi zitakuwa zinakatwa mara moja ili kuwapunguzia kadhia na usumbufu mwingi wasanii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwelezee Mheshimiwa Malembeka ya kwamba, BASATA inafanya kazi yake ya ulezi kama inavyotakiwa kuwa, na mahali popote ambapo wasanii wanakuwa na mkwamo wa aina yoyote BASATA imekuwa ni kimbilio lao kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni la Mheshimiwa Babu Tale ambaye alilisema kuhusiana na fedha za Mfuko wa Utamaduni, mikopo yake kutolewa kupitia benki. Mwanzoni wakati Mfuko wa Sanaa na Utamaduni unaanza, fedha hizi zilikuwa zinatolewa na mfuko moja kwa moja. Idadi ya mikopo ambayo ili-*default*, ambayo haikurudishwa ilikuwa ni zaidi ya 80% ya fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mfuko huu kufanyiwa marekebisho na kupelekwa benki, mikopo hii ikaanza kutolewa benki. Sasa hivi hakuna mkopo hata mmoja ambao haujarudishwa. Hii inaonekana kabisa jinsi ambavyo mfuko huu umekuwa na ufanisi wa hali ya juu baada ya kupelekwa kutolewa mikopo hii kwenye mabenki kinyume na ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili jambo halijafanywa kwa ajili ya kuwakomoa wasanii, limefanywa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatolewa na zinarudi ili kuwanufaisha wasanii wengi zaidi. Halikadhalika, ni fursa ya wasanii kujirasimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukilifanya jambo hili kwa juhudi kuwa zaidi, kwa sababu miongoni mwa kazi za Mfuko

huu pamoja na kukopesha, hali kadhalika ni mafunzo na ruzuku. Tumekuwa tukihakikisha wasanii wengi zaidi wananufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Swalle, hata wale wasanii wake wa Lupembe aliowataja hapa, wana nafasi ya kunufaika na Mfuko huu. Ni kufanya maombi na maombi hayafanywi, siyo lazima hata aende kwenye mfuko, yanafanywa kwa njia ya mtandao, na sisi tutaangalia namna ambavyo tunaweza kuwafikia na wasanii wa Lupembe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kengele ya pili, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiwezesha Wizara yangu kwa bajeti ya kutekeleza majukumu ambayo yamepangwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, hususan maandalizi ya *AFCON* ambayo yatapelekea uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji huu ni mbegu na chachu ya mabadiliko makubwa kuelekea kujenga uchumi, ajira na mapato kupitia sekta hii bunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha hotuba yangu katika Bunge lako Tukufu. Pia nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Husna Sekiboko, kwa ushauri, maoni na maelekezo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Sekta za Habari, Utamaduni,

Sanaa na Michezo. Aidha, nawashukuru na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na kuchangia hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 15 ambapo kati ya hao 14 wamechangia kwa kuzungumza na Mheshimiwa mmoja amechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nitoe ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, majibu ya hoja zote kwa kina yatawasilishwa kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa Sekta ya Habari, nieleze kwamba, kwa kushirikiana na wadau wa habari Wizara imeendelea kulinda na kuuenzi uhuru wa habari na hii imefanya Tanzania kuendelea kutambulika na dunia katika kuuenzi uhuru huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitatu, Tanzania imepanda kwa nafasi 48 katika viwango wa uhuru wa habari duniani kutoka nafasi ya 143 mwaka 2023 hadi kufikia nafasi ya 95 mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa mujibu wa ripoti ya *Reporters Without Boulders*, ambapo katika ripoti ya mwaka 2024 Tanzania ilipanda kutoka nafasi ya 143 hadi nafasi ya 97 na katika ripoti ya mwaka huu iliyotoka wiki jana tarehe 2 Mei, 2025, Tanzania imepanda nafasi mbili kutoka 97 hadi 95. Hii ni ishara kwamba uhuru wa habari hapa Tanzania unazidi kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pamoja na hayo yote, Tanzania imeendelea kuwa kinara wa waandishi wake nguli wa habari wanaoshikilia nafasi za juu katika Vyama vya Kihabari Kikanda. Waandishi hao ni Deodatus Balile ambaye ni Rais wa Jukwaa la Wahariri Afrika Mashariki, Ndugu Kajubi Mkangaja ni Mwenyekiti wa Baraza la Habari Afrika Mashariki na Ndugu Ernest Sungura, ni Mwenyekiti wa Mabaraza Huru ya Habari Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu tunategemea kuwa na Mkutano wa Kimataifa wa Mabara Huru ya Habari Duniani, unaotarajiwa kufanyika Mkoani Arusha mwezi Julai mwaka huu. Ninawashukuru wote waliochangia katika hotuba yetu, na kama nilivyosema, majibu mengine mtayapata kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hili la *TSN* (Shirika la Magazeti ya Serikali). Hali hiyo imeanza kubadilika kwa sababu ya mtiririko wa fedha kwa mwaka 2023/2024 zilitengwa shilingi bilioni 10, lakini zilitoka shilingi milioni 270 pekee, katika mwaka 2024/2025 zilitengwa shilingi bilioni tano na zilitoka zote shilingi bilioni tano. Katika mapitio ya bajeti, kulionekana umuhimu wa kuongezewa fedha shilingi 4,800,000,000 katika mradi huu. Tayari kwa miezi minne iliyopita Serikali imetoa shilingi bilioni 2.3, hivyo kufanya jumla ya fedha zilizotolewa mwaka huu 2024/2025 kuwa shilingi bilioni 7.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kwa usimamizi na mtiririko wa fedha unaondelea sasa, mradi umefikia asilimia 57.9 na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2025. Wizara inapokea ushauri wote unaotolewa na Wabunge lakini ninawahakikishia kwamba hali ya *TSN* inazidi kubadilika na tunaamini kutokana na huu mtiririko wa fedha hali itakuwa bora zaidi, lakini lolote ambalo litatusaidia kufanya hali hiyo ikamilike kwa haraka sisi tutaliunga mkono na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye mkakati wa ajira za Kiswahili kwa vijana wetu, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, alilieleza vizuri. Nieleze tu kwamba, Wizara inaendelea kutekeleza fursa za ajira za Kiswahili kwa vijana ikiwemo, ujenzi wa shule ya Kiswahili na Stadi za Kiafrika itakayotoa fursa za ajira kwa vijana, kufungua vituo mbalimbali vya kufundishia Kiswahili kwa wageni kupitia Balozi za Tanzania nje ya nchi na vituo nje ya Balozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia BAKITA imeendelea kuendesha mafunzo ya msasa kwa taaluma mbalimbali za Kiswahili mfano, ukalimani, tafsiri, uhariri na ufundishaji Kiswahili kwa wageni hasa vijana ili waweze kutumia fursa za ukalimani katika mikutano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mchango wa Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi kuhusu kuwaenzi wazee na waandishi wa mashairi ambao wamesaidia kukuza na kuendeleza Kiswahili na miongoni mwao ni Ndugu Shaaban Robert, Prof. Penina Muhando na Ndugu Nyambari Nyangwine, tunapokea maoni yake ya kuwaenzi wataalam wa mashairi na watu wenye mchango katika kukuza na kuendeleza Kiswahili. Ni jambo lenye tija ambalo limekuwa likifanywa na BAKITA na imeshatoa tuzo mbalimbali kwa Waandishi wakiwemo hayati Shaaban Robert, Prof. Penina Muhando, Prof. Massamba, Mzee Amiri Soud Andanenga na wengineo wengi. Tuzo zinaendelea kutolewa na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine naye atafikiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa shule zetu pia kurudisha kwa kasi kabisa ushairi wetu wa ngonjera, ambazo zilikuwa zinahamasisha vijana kuwa wabobevu katika lugha ya Kiswahili fasihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu ametoa ushauri mzuri, kwamba BAKITA iepuke kutengeneza maneno magumu mathalani Kishikwambi, Akili Mnemba ambayo yanahusisha vitu na hali halisi. Maoni yakeo yamepokelewa, ni vyema mchakato wa kuunda maneno uwe wa maneno ya kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza maneno hutafutwa kwenye lahaja za Kiswahili na tunazo nyingi tu. Napenda kuwapongeza BAKIZA kwa kutoa Kamusi ya Kiswahili cha lahaja ya Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba, na tumewahimiza waendelee kutoa Kiswahili katika lahaja ya Kimvita, lahaja ya Kipate, lahaja ya Kiamu, lahaja ya Kiungwana ambayo inazungumzwa Congo, lahaja ya Kiswahili ambacho kinazungumzwa Madagascar na lahaja ya Kiswahili ambacho kinazungumzwa Comoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kufanya maneno ya utohozi na yapo mengi tu katika Kiswahili kutoka kwenye Kiarabu, Kiajemi, Kireno na Kijerumani. Nataka kusema kwamba utohozi tu unaweza pia ukakifanya Kiswahili kupoteza uhalisia wake, lakini pia tunachukua ushauri wa Prof. Wole Soyinka, ambaye kwa mara

ya kwanza mwaka 1976 ndiye aliyesema Kiswahili kiwe Lugha ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Prof. Wole Soyinka naye alishauri kwamba ili Kiswahili kiwe lugha ya Afrika, kianze kuchukua maneno kutoka lugha nyingine za Afrika ili baada ya hapo Waafrika wote wawe na lugha ambayo inawaunganisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutajitahidi kutumia maneno kutoka kwenye lugha zetu na lahaja zetu badala ya kuunda maneno kwenye maabara za lugha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la singeli. Kwanza nashukuru sana mjadala huu ambao umekuwepo kwa muda mrefu, tuliamua kukaa kimya ili Watanzania waseme. Watanzania tunasahau sisi ndio Taifa katika Bara la Afrika lenye tofauti kubwa za utamaduni, tofauti kubwa za lugha kuliko Taifa lolote katika Bara la Afrika. Sisi tuna utofauti mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao utamaduni wa Wabantu, Wakushi, Wakhoisan na *Afroasiatic*, lakini kinachotufanya Watanzania tujione ni wamoja ni juhudi za Baba wa Taifa kutuunganisha kuwa Taifa moja. Nje ya hapo, sisi tuna tofauti kubwa kuliko nchi yoyote ya Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ndiyo pekee yetu tuna makundi matano ya lugha, pamoja na lugha za watu waliokuja baadaye wa *Afroasiatic* ambao ni Wairaqw, Wambugu, lakini tuna watu wenye lugha ya asili ya kale katika Bara la Afrika Wahdzabe. Kwa hiyo, tuna tofauti kubwa sana ya Utamaduni. Ukitaka kulijua hilo, leta jambo lolote la utamaduni, hapo ndipo utakapojua tofauti ya Watanzania na tutahangaika na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, Serikali haiwezi kuja na wimbo mmoja, haiwezi kuja na chakula kimoja, haiwezi kuja na nguo moja ikijua kuna uanuai *(diversity)* huo. Wakati mwingine imetufanya tukimbilie nyimbo za Kwaito, kwa sababu haina mwenyewe, kuliko nyimbo zetu wenyewe kwa sababu tunaona ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Baba wa Taifa, kwani asingefanya hivyo, Tanzania hii ingekuwa haikaliki. Kwa sababu tuna tofauti kubwa katika mavazi, katika chakula, katika vionjo na pia vinachochewa na imani za dini. Kwa hiyo, tushukuru tuko Taifa moja. Maana yake ni nini? Ni lazima tutekeleze *4R* katika kujadili muziki wa Singeli, *4R* za Rais Samia Suluhu Hassan za ustahimilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Singeli kwa sasa imekuwa ni moja kati ya Miziki ya Tanzania kama ilivyo kwa miziki ya dansi, taarabu, kwaya, Bongo Fleva na miziki mingine. Tunachokifanya kwenye Singeli, wala siyo kuipeleka duniani. Singeli tayari imeshakwenda duniani kwenye matamasha ya Ubelgiji na haichezwi kama hizo ambazo mnaziona, ambazo Naibu Spika amenisaidia, imekwenda kwenye Tamasha la Primavera, Spain; Tamasha la *CORA Festival,* Ufaransa; Tamasha la *Munich*; Tamasha la *Dusseldorf;* na tamasha ambalo ashakum siyo matusi Nyegenyege, Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tarehe 26 Aprili, 2025, kwenye Tamasha la *Samia Serengeti Music Festival* ambalo mgeni wa Heshima alikuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dogo Paten pamoja na Zuchu, walicheza Singeli ambayo iliwafanya watu wachangamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, yako mambo ambayo ni ya upotofu wa maadili na hiyo siyo kwa Singeli tu, iwe ni muziki wa Injili, iwe ni muziki wa dansi, iwe ni muziki wowote, utakapokuwa na mambo ambayo siyo ya maadili, Wizara itachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama muziki wa Injili utakuwa ni wa kunengua utachukuliwa hatua; kama muziki wa kawaida utakuwa hauendi na maadili utachukuliwa hatua; kwa hiyo, tusichanganye vionjo vya wachezaji na aina ya muziki.

Mheshimiwa Naibu Spika, yakumbukeni maneno ya Yesu Kristo katika Biblia walipompelekea kahaba akasema, "yule ambaye hajawahi kufanya hayo, awe wa kwanza wa kumtupia huyo jiwe." Wote waliangalia chini na kuchora chini ya miguu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwasaidie vijana hawa kuusafisha muziki huo ambao tayari umeshakwenda duniani. Hatutavumilia aina yoyote ya muziki unaotweza wanawake, wala kuwashushia hadhi, uwe ni wa aina yoyote ile, lakini Singeli imepiga hatua,

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyosemwa, Singeli tunayoizungumza ya kwenye video na nimeletewa hiyo sijui ya Nairobi, ya wapi, hao ni vijana waendelee kuombewa, waendelee kuaswa, waendelee kuonywa. Kama alivyosema Yesu, nimekuja kwa wagonjwa, mimi ni tabibu, na siyo kwa walio wazima. Ninyi wote ambao mmeokoka endeleeni kuwaombea hao watu, na imbeni tabibu wa kweli ni Yesu Kristo au Mtume Mohamadi *(S.A.W.)* ili wawe na heshima katika aina zote za miziki na aina yoyote ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la mustakabali wa mchezo wa kati ya Simba na Yanga. Umeeleza wazi, kwa mujibu wa Sheria za *FIFA*, Wizara au Serikali haiwezi kuingilia suala hilo. Suala la Ligi inasimamiwa na *TFF*, linasimamiwa na bodi ya ligi na Kanuni haziruhusu Serikali kuingilia mambo hayo, kwa sababu ukifanya hivyo, *FIFA* itaifungia Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa ndugu yangu Mheshimiwa Swalle na Wanasheria wengine, hilo jambo ni *sub judice* na kwa sababu ni *sub judice* siwezi kulisema. Nikilisema nitakuwa nimefanya makosa ya Padri kutoa maungamo. Kwa hiyo, tunaendelea na juhudi mbalimbali na mazungumzo yetu yaligusa kuhusu kuboresha mchezo wa mpira katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii tena kuwashukuru Wabunge wote waliotoa maoni ya kwamba Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan apewe tuzo kwa kufanya maendeleo ya michezo. Hakika Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa ni hidaya ya Taifa letu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa ni hiba ya Taifa letu katika eneo la Sanaa na Michezo, nami naunga mkono kabisa wazo hilo la Wabunge la kuwa na aina maalumu ya tuzo kwa Mheshimiwa Rais kwa kutambua mchango wake mkubwa katika Sekta hii ya Michezo, Sanaa, Utamaduni na Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya viwanja, niwahakikishie kabisa ndugu yangu Mheshimiwa Priscus Tarimo wa Moshi Mjini kwamba tutatuma wataalam kuja kuangalia suala la Kiwanja cha Moshi. Ndugu yangu alikuwa hapa Mheshimiwa Joseph Tadayo, ninaona ametoka Mbunge wa Mwanga na ninajua ni kwa nini ametoka. Kama mlivyosikia tangazo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumefikwa na msiba mkubwa wa kuondokewa na Mzee Cleopa David Msuya, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alikuwa Waziri Mkuu wakati wa Mwalimu, alikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara na Waziri wa Fedha. Ni mzee ambaye ametoa mchango mkubwa wa Taifa. Kwa hiyo, ndiyo maana yeye hayupo hapa, naye namhakikishia nitakwenda Mwanga kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimhakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Edwin Swalle, nitafika Lupembe, Njombe ili kuona eneo hilo na tuone na wataalam ni jinsi gani pia tutaboresha Uwanja wa Lupembe, Njombe. Ipo sababu kubwa sana ya mimi kufika Lupembe, Njombe, kwa sababu Mama yangu mkubwa nilikokulia aliolewa na Luchangiro kutoka Lupembe. Kwa hiyo nitakwenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha kwa kueleza kwamba baada ya mafanikio makubwa ya timu ya Simba na sasa inaingia kwenye mchezo wa kwanza wa Fainali ya Kombe la Shirikisho linaloandaliwa na *CAF* ambapo Klabu ya Simba inakwenda Morocco kupambana na Klabu ya RS Berkane, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya maamuzi ya kutoa ndege itakayoipeleka Klabu ya Simba nchini Morocco kwa ajili ya mchezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYETITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

## KITABU CHA PILI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*.....................Sh. 8,657,935,500

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina Mshahara wa Mheshimiwa Waziri na nina majina hapa nimeletewa, Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Timu yetu ya Bunge imekuwa ikienda nje, kwenye magari yake inaandika *Visit Tanzania* na timu zetu za Simba na Yanga zimekuwa zikitumia jezi zimeandikwa *Visit Tanzania.* wakati tunaandika *Visit Tanzania,* tunategemea wageni kutoka nje ya nchi, kwa maana ya watalii wa michezo na watalii wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya mchezo wowote ule Tanzania tuna-*attract* wageni kutoka nje na maana yake ni kwamba, wageni hawa wanaingia gharama za kuja Tanzania wakiamini kwamba, Tanzania ni nchi salama na kwamba, kulingana na matangazo ya *Visit Tanzania* wanakuja kuona burudani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ndiyo mmiliki wa Viwanja vya Michezo, kama Benjamin Mkapa, na sasa hivi inajenga viwanja vingine vikubwa Tanzania. Kwa mujibu wa taarifa ambayo ilisababisha kuahirishwa kwa mpira wa Simba na Yanga, moja ya sababu, ilikuwa ni usalama kwenye Kiwanja cha Serikali. Taarifa ilisema ni usalama, kulingana na Taarifa ya Bodi ya Ligi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri atuthibitishie kwamba, taarifa za usalama zilizosababisha Watanzania kula hasara Siku ya Mechi ya Simba na Yanga zilikuwa zimetolewa na chombo gani cha usalama? Ambacho kilisababisha Watanzania wale hasara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama majibu yake hayataridhisha, nitashika Shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ulikuwa unakwenda vizuri, mradi umeingiza vilabu viwili ambavyo ndivyo *conflicted,* hoja yako bado ipo Mahakamani.

Mheshimiwa Musukuma. Mheshimiwa Kanyasu kaa chini. Mheshimiwa Kanyasu, *please* kaa chini.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo tu, jambo ambalo tunalizungumza...

**MWENYEKITI:** Umetolea mfano kitu ambacho kina-*pend* maamuzi ya Mahakama.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nakuelewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu!

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo dogo tu. Kazi yangu ni kuishauri Serikali, ndiyo iliyonileta humu ndani. Kama hilo haliwezekani, sina sababu ya kukaa humu. Jambo la Simba na Yanga lilikuwa *tribunal,* halikuwa Mahakamani na kama *tribunal* inaweza ikazuia kujadili jambo kwenye chombo...

**MWENYEKITI:** *Tribunal* nayo ipo kisheria, maana yake si ni Mahakama!

Mheshimiwa Kanyasu unajua vitu vingine humu ndani msifikiri kama Kiti kinafanya vitu makusudi. Imetokea kwa Mheshimiwa Gulamali kachanganya vitu viwili. Kachanganya Kanuni ya 81 na Kanuni ya 71 na tumeyazungumza sana haya mambo. Jambo lako vilevile bado linangoja hukumu ya Mahakama, hilo la kwanza. La pili, suala la usalama, una-eco kama vile sasa unatahadharisha nchi na dunia zisije Tanzania, kitu...

Mheshimiwa aah, Mimi ndiyo nasema, Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo ni kasheshe. Nakushukuru, naomba utuongoze vizuri, tunaweza kukukosea adabu, lakini hatuna historia hizo. Naomba utuongoze vizuri kwa sababu, ni masuala ya kiroho na kimoyo, utuwie radhi pale tutakapokosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano kwenye nchi zinazotuzunguka, kwa mfano nchi ya Congo, kwenye ligi yao Lupopo na Mazembe leo ni mwaka wa pili Serikali imezuia hiyo dabi haichezwi. Ligi ya *South Africa* vilevile, Kaizer Chiefs na wao hawachezi, yaani mpaka Serikali iliingilia kuwakutanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga msingi wa hoja yangu, unatukataza tusizungumze Simba na Yanga, nilitaka atuambie, baada ya hili suala kutokea, tulimwona Mheshimiwa Waziri Prof. Kabudi ameenda na Mheshimiwa Naibu wake kule kwenye kikao. Sasa, kama hatuwezi kulijadili, yeye Mheshimiwa Kabudi aliende kama nani kule? Ni mchezaji au ni Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunayemwuliza ni Mheshimiwa Waziri, ambaye sio suala gumu kutuambia tu kwamba, pengine Serikali inalifanyia kazi kuwakutanisha, lakini tunakoelekea sasa kwamba, ikitokea...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, ahsante sana. Wewe wala sikupeleki Mahakamani, hilo siyo suala la sera, kaa chini.

Mheshimiwa Taletale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kulingana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri na kulingana na mwongozo wako, nimeamua kuachia Shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili na mimi nisiende Mahakamani.

**MWENYEKITI:** Katibu tuendelee.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*......................Sh. 8,657,935,500
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……….Sh. 713,296,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*.................Sh. 961,485,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*…Sh. 524,147,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*……Sh. 487,834,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*….……………….......Sh. 416,749,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*……………….........Sh. 536,938,000
Kifungu 1008 – *Legal Service Unit*……......................Sh. 365,171,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*……………………………….......Sh. 416,895,000
Kifungu 6001 – *Culture Development Division*………………………………...Sh. 3,242,538,000
Kifungu 6004 – *Sports Development*……………...Sh. 4,932,996,500
Kifungu 6005 – *Arts Development Division*……....Sh. 11,316,275,000
Kifungu 7003 – *Information Services*……………...Sh. 28,897,025,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| | |
|---|---|
| Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*………..Sh. | 2,742,530,000 |
| Kifungu 6001 – *Culture Development Division*…..Sh. | 5,401,576,000 |
| Kifungu 6004 – *Sports Development*……….……..Sh. | 410,546,682,000 |
| Kifungu 6005 – *Arts Development Division*...........Sh. | 8,000,000,000 |
| Kifungu 7003 – *Information Services*……………......Sh. | 31,500,000,000 |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 (3) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Kamati yako ya Ufundi, Makatibu Wakuu, wataalamu na viongozi wengine ambao wapo katika Wizara yako na taasisi ambazo unaziongoza.

Waheshimiwa Wabunge niwashukuru kwa michango mizuri, michango yenye afya, yenye majibu, yenye afya, majibu sahihi kabisa. Nakushuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ulivyoweka mambo sawa na kujua utaratibu hasa wa kazi, hongera sana kwa kazi zako. Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe hongera sana kwa shughuli unayofanya.

Baada ya maneno haya, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho Saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.11 Jioni, Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 8 Mei, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*